# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI

### Kikao cha Nne – Tarehe 2 Februari, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Karibuni tena kwenye Kikao chetu cha Nne leo, Mkutano wa Kumi. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. FLATEI G. MASSAY- K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante Sana Mwenyekiti. Tunaendelea. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 40

### Hitaji la Kuboresha Zahanati ya Kalenga

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Zahanati ya Kalenga iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa haikidhi mahitaji halisi ya wakazi wa vijiji vinavyoizunguka.

Je, ni lini Serikali itaboresha zahanati hiyo kwa kujenga vyumba vya ziada na mahitaji mengine ya msingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati ya Kalenga ilijengwa zaidi ya miaka 40 iliyopita. Kutokana na ongezeko la watu, kwa sasa zahanati hii imekuwa ikitoa huduma kwa wananchi ambao wamekuwa wengi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Hata hivyo, Halmashauri haiwezi kuongeza majengo kwenye eneo la zahanati hii, kwani tayari imezungukwa na makazi ya watu, hivyo hakuna nafasi ya kuongeza majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hiyo, baadhi ya vijiji vilivyokuwa vinapata huduma kwenye zahanati hii, vimejengewa zahanati ambayo ni zahanati ya Mangalali iliyofunguliwa mwezi Februari, 2017. Zahanati hii imesaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika zahanati ya Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, juhudi zinafanyika kwa kuhamasisha ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Jirani ya Mlanda. Ujenzi huu unafanyika kwa nguvu za wananchi na upo katika hatua za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri katika mpango wa bajeti wa mwaka 2018/2019 imetenga kiasi cha shilingi milioni 54 ili kufanikisha ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Mlanda. Kituo hicho kitakapokamilika, kwa kiasi kikubwa kitapunguza msongamano wa wagonjwa katika Zahanati ya Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuziagiza Halmashauri zote nchini kutenga maeneo ya kutosha kwa ajili ya Taasisi za Umma kama vile shule, vituo vya kutolea huduma za afya na Ofisi za Vijiji, Mitaa, Kata na kuhakikisha maeneo haya yanapimwa na kupatiwa Hati Miliki ili kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza siku za usoni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamwindi.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Zahanati ya Mangalali imefunguliwa Februari. Zahanati hii ipo katika Kata ya Ulanda na katika vijiji ambavyo bado vinaendelea kupata huduma kutoka kwenye Zahanati ya Kalenga ni Kijiji cha Makongati ambacho kutoka pale Zahanati ya Kalenga pana kilometa karibu 15, lakini pia Zahanati ya Kalenga ipo jirani kabisa na Makumbusho ya Chifu Mkwawa, lakini pia iko karibu kabisa na Barabara Kuu iendayo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, kwa kuwa mpango wa Serikali ni kila Kata kuwa na Kituo cha Afya, je, Serikali iko tayari kuunga mkono jitihada za wananchi wa Kalenga walio tayari kutoa eneo lao na sehemu ya nguvu kazi kwa ajili ya kupatiwa Kituo cha Afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWNEYEKITI:** Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeelezea jinsi ambavyo hakuna uwezekano wa kuongeza majengo katika Zahanati ya Kalenga kutokana na eneo lile kwamba lina makazi na tayari yameshapimwa kiasi kwamba uwezekano wa kutoa *compensation* Halmashauri haina uwezo huo.

Mhesimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niungane na Mbunge kwa kumpongeza kwa jinsi ambavyo anapigania suala la kuhakikisha wananchi wanapata afya iliyo bora, lakini pia na Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Mgimwa kwa jitihada zake. Kwa taarifa nilizopata ni kwamba mpaka sasa hivi ameshachangia mabati 100 na mifuko 80 ya saruji ili kuhakikisha kwamba Kituo cha Afya kinajengwa Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Vituo vya Afya vingi vinajengwa ili kupunguza msongamano ambao unajitokeza katika

Hospitali ya Mkoa wa Iringa kwani kutoka Kalenga kwenda Iringa ni kilometa 15 na pale kuna lami kiasi kwamba wananchi wana *option* ya kwenda hata kule, lakini lengo ni kuhakikisha kwamba wanapata huduma kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi halafu Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lushoto lina Kituo cha Afya kimoja tu, lakini kwa juhudi za wananchi wamejitahidi kujenga Vituo vya Afya viwili, ambapo kituo cha kwanza kipo Ngwelo, Kituo cha pili kipo Gare. Je, nini kauli ya Serikali juu ya kumalizia vituo vile vya afya ili wananchi waweze kupata huduma wasiende mbali kufuata huduma za afya?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake Mheshimiwa Shekilindi anasema tayari wameshajenga Vituo vya Afya viwili, lakini kwa bahati mbaya hajafafanua vimejengwa *to what extent?* Kama vimekamilika au la! Maana kama vimekamilika, kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba huduma inapatikana kwa kupeleka Waganga pamoja na Wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba Vituo vya Afya vyote vinakamilika na viweze kutoa huduma ambayo tunakusudia na hasa upasuaji wa dharura kwa akina mama na watoto. Kwa hiyo, naamini baada ya kujua *status* ya hivyo Vituo vya Afya ambavyo vimejengwa kwake, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba inachangia ili huduma hiyo ambayo tumeikusudia, iweze kutolewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Chalinze Wilayani Mdaula, kuna zahanati ambayo wananchi kwa nguvu zao wamekuwa wanaijenga tangu mwaka 2012. Wamejenga, wameweka plasta, wameweka madirisha, lakini bado wanasuasua kwa sababu uchumi siyo mzuri. Sasa swali langu kwa Serikali, ni lini sasa Serikali itaongeza nguvu ya Serikali kuwasaidia wananchi ile zahanati imalizike kusudi wananchi waweze kupata mahali pa kwenda kupata tiba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), majibu. Ooh, Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Naibu Waziri wangu kwa ufafanuzi mzuri wa maswali yote ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunafahamu Mdaula na maeneo mengine kuna changamoto, wananchi wamefanya juhudi kubwa na ndiyo maana azma ya Serikali yetu ni kuhakikisha kwamba tunaunga mkono juhudi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, sasa hivi tunafanya uwezeshaji wa kuangalia jinsi gani tutafanya kuhakikisha maboma yote yaliyojengwa katika Halmashauri zetu tunayakamilisha. Tutatumia takribani shilingi bilioni 69 ambapo jambo hili maeneo ya Mdaula pale, hasa Halmashauri ya Chalinze tutawaelekeza wahakikishe katika umaliziaji wa maboma hayo, ile Zahanati ya Mdaula iweze kutengewa fedha katika hizo fedha ambazo tutazitoa kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo lile wanapata huduma za afya, kama azma ya Serikali ilivyokusudia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini na linaelekezwa kwa Ofisi hiyo hiyo ya Rais, (TAMISEMI). Mheshimiwa Maftaha.

Na. 41

**Kuvunjwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)***

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Je, kuvunjwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* kuna faida gani kwa wakazi wa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, maarufu kama mashine ya Kusini, kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilivunja Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* tarehe 15 Mei, 2017 kutokana na muingiliano wa kimamlaka kati yake na Manispaa ya Dodoma ambapo licha ya kuongeza gharama za uendeshaji, ulisababisha migogoro mingi ya kiuendeshaji, ikiwemo vyanzo vya mapato na migogoro ya ardhi, hali iliyosababisha kupungua kwa kasi ya maendeleo ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuvunjwa *CDA* wananchi wamepata faida nyingi ikiwa ni pamoja na kupungua kwa gharama za uendeshaji ambazo zilibebwa na wananchi kupitia kodi, kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa kazi, kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri ambayo matumizi yake huamuliwa na Wawakilishi wa wananchi (Madiwani), kuongezeka kwa idadi ya watumishi, majengo, maabara na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo limewezesha kuongeza ufanisi wa Manispaa katika kuwahudumia wananchi.

Aidha, ubadilishaji wa mikataba ya upangishaji *(Ground Lease Agreements)* za miaka 33 iliyokuwa ikitolewa na *CDA* kwa kuwapatia wananchi Hatimiliki za miaka 99 umehamasisha uwekezaji katika kuendeleza kwa kasi zaidi Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kifupi cha kuanzia Mei hadi Desemba, 2017 wananchi wamebadilisha jumla ya mikataba 19,000 kati ya 65,000 iliyotolewa na *CDA* kuwa kwenye mfumo mpya wa Hatimiliki za miaka 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida hizo, Manispaa ya Dodoma inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo madeni na migogoro iliyorithiwa kutoka *CDA.* Manispaa inakabiliana na changamoto hizo kwa kuimarisha makusanyo na kuimarisha usimamizi katika sekta ya ardhi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa Wakazi wa Dodoma wakiwemo Wabunge na Taasisi mbalimbali za Kiserikali kwamba ili waweze kupata huduma ya ardhi Manispaa ya Dodoma, basi kuna mzunguko mkubwa sana na mlolongo mkubwa sana.

Je, Serikali ipo tayari hivi sasa kufanya uchunguzi maalum na kuchukua hatua kwa kuwa, sasa Manispaa ya Dodoma ni Mji Mkuu kwamba tunahitaji huduma hizi ziende kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, zipo Taasisi za Serikali ambazo zinahamia Dodoma hivi sasa, zinataka kujenga ofisi zao hapa Dodoma, lakini bado kumekuwa na urasimu mkubwa sana taasisi hizo kupewa ardhi pale Manispaa.

Je, Serikali ipo tayari hivi sasa kuweka utaratibu maalum ili Taasisi hizi za Kiserikali ama Taasisi za Umma ziweze kupewa maeneo ya kuweza kujenga ofisi zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma na ndiyo maana wakazi wa Kusini wanamwita mashine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlundikano wa kazi uliokuwepo katika kipindi hiki cha awali cha utekelezaji wa majukumu mapya ya kuunganisha majukumu ya iliyokuwa Manispaa ya Dodoma na ile iliyokuwa *CDA* ndio umefanya kuwe na baadhi ya malalmiko katika hatua za awali za utekelezaji wa kazi, kwa sababu kulikuwa na migogoro mingi sana ya viwanja, mahitaji ya kubadilisha mikataba mingi sana na hapo hapo kuna mahitaji ya kuendelea kupima maeneo mapya. Kwa hiyo, haya matatizo ambayo Mheshimiwa Maftaha ameyataja ni matatizo ya mpito tu ambayo yatarekebishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, hadi sasa Manispaa imepima viwanja 1,288 na ambavyo tayari hati zake zimetayarishwa. Maeneo ambayo ni Mji Maalum wa Serikali yamepimwa viwanja 147, ikiwemo Ikulu, Wizara zote zimepatiwa hati na vilevile taasisi za umma na viwanja vya mabalozi 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nakuonesha hati ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni hii hapa, tayari imepatikana na ipo

Ofisini. Wizara zote zina hati kama hii. Taasisi zote za umma ambazo zinahitaji ardhi, waende Manispaa pale watapewa hati zao ambazo zitawawezesha kupata maeneo ya kuweza kujenga ofisi zao haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika maeneo ya Nala wamepima viwanja 922 na kiwanja cha michezo cha Nzuguni kimepimwa, kile ambacho tulipata msaada kutoka Morocco na viwanja 218 katika maeneo mengine.

Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wanakaribishwa waombe viwanja Manispaa na mimi kama msimamizi wa Manispaa hiyo, nawaahidi kwamba watakuwa wamepata hati kabla ya mwisho wa mwezi huu wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo limepimwa viwanja vya Serikali ni hili hapa na naweza nikalionyesha Waheshimiwa Wabunge waweze kuliona. Kazi imefanyika vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Dodoma sasa hivi ni Makao Makuu ya nchi na Manispaa wameongezewa jukumu lingine la ardhi ambalo lilikuwa la *CDA,* lakini kuna upungufu mkubwa wa vitendea kazi pale Manispaa hasa ile Idara ya Ardhi pamoja na watendaji ni wachache kiasi kwamba ukienda pale bado kuna watu wengi wanakaa kwenye foleni kwa muda mrefu.

Serikali sasa kwa kutambua kwamba Dodoma ni Makao Makuu, imejipangaje kuhakikisha kwamba Manispaa ya Dodoma inawezeshwa kwa vitendea kazi, miundombinu pamoja na watendaji wa kutosha ili wafanye kazi kwa weledi na kwa haraka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupata nguvu kazi ya kutosha kutoka kwenye ile iliyokuwa *CDA,* ni kweli kwamba bado kuna mahitaji ya watumishi na baadhi ya vitendea kazi na hivyo vinafanyiwa kazi mpaka mwezi wa sita, matatizo mengi yatakuwa yamekamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Suleiman Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene na linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 42

**Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Mambali – Itobo – Kahama kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Barabara ya kuanzia Tabora - Mabali – Bukene – Itobo hadi Kahama ni muhmu sana kwa shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa Jimbo la Bukene na barabara hii ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Je, ni lini barabara hii yenye urefu wa kilometa 149 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Tabora – Mambali - Itobo yenye urefu wa kilometa 115 ni sehemu ya mradi wa barabara ya Tabora – Mambali - Itobo hadi Kagongwa Wilayani Kahama yenye urefu wa kilometa 180, inayounganisha Wilaya ya Tabora, Nzega na Kahama. Kwa sasa barabara hii inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa kazi hiyo ulisainiwa tarehe 14 Septemba, 2017 na ni wa miezi 15. Kazi hii inafanywa na Mhandisi Mshauri *M/s Nimeta Consult* kwa gharama ya shilingi milioni 789.205. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 608 zimeshatolewa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii utaanza baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli huyu mshauri yuko *site* na kazi hii inaendelea, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa sababu barabara hii ilivyo sasa katika Miji ya Bukene na Itobo inapita katikati ya miji na kwa mfano Bukene ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami tutalazimika kuvunja Kituo cha Afya, jengo la Polisi, tanki kubwa la maji, ma-*godown* makubwa na kuvunja nyumba nyingi tu cha wananchi.

Je, Serikali itakuwa tayari kutoa kauli itakayoondoa hofu na itakayofanya kuepusha fidia kubwa kwamba usanifu huu ujumuishe kuichepusha barabara hii katika miji ya Bukene na Itobo ili isipite katikati ya Miji ya Bukene na Itobo ili kuondoa kwanza fidia kubwa ambayo itatokea baada ya kuvunja taasisi nyingi hizi na nyumba nyingi za wananchi?

Je, Serikali iko tayari kutoa kauli ili wananchi wa Bukene na Itobo wawe hawana hofu kwamba barabara hii itachepushwa pembeni ya miji hii na kuondoa gharama zote hizi ambazo zitajitokeza?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia sana hii barabara ambayo inatoka Tabora - Mambali kuja Itobo. Niseme tu kwamba upo utaratibu kwa upande wa Serikali wa kuangalia hizi gharama wakati tukisanifu hizi barabara. Kwa hiyo, niseme kwamba tutazingatia ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo jambo geni kwa sababu zoezi hili tumelifanya katika Mji wa Nzega, kuna mchepuo; tumefanya katika Mji wa Urambo, kuna mchepuo; lakini pia tumezingatia tulivyosanifu barabara ya kule Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikutoe wasiwasi na niwatoe wasiwasi wananchi wa Bukene kwamba tutazingatia wakati tunakamilisha zoezi la usanifu wa barabara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank, naanza na Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** *Okay*.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Changamoto za

Jimbo la Bukene zinafanana na changamoto za Jimbo la Karagwe. Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuweka mpango wa kuweka lami barabara ya kuanzia Karagwe kwenda Benako - Ngara na barabara ya kuanzia Karagwe kwenda Murongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango hii mizuri ya Serikali wananchi wanaoishi katika barabara hizi wamesubiri fidia kwa muda mrefu, je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wa Karagwe wanaopakana na barabara ya Karagwe - Benako na Mugakorongo - Murongo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amefuatilia sana barabara za Karagwe na anafahamu kwamba ziko barabara nyingi ambazo zinaunganisha nchi yetu na nchi ya jirani ambazo ziko kwenye mpango wa ujenzi wa lami. Hii ni pamoja na juhudi zake Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana na na sisi kama Serikali tunaendelea kushirikiana naye kuhakikisha kwamba wananchi wa Karagwe wanapata huduma hii ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili suala la fidia, tunategemea tutakapopata fedha tutaweza kulipa mara moja. Kwa hiyo, namuomba tu Mheshimiwa Mbunge labda baada ya kikao hiki tuwasiliane ili tuzungumze ofisini tuweze kuona hatua gani tumefikia ili aweze pia kuwapa taarifa wananchi wa Karagwe juhudi ambazo tumefikia upande wa Serikali. Kwa hiyo, tuonane tutalizungumza suala hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tumeanzisha Wakala wa Barabara *(TARURA)* katika Mkoa wa Songwe na Wilaya ya Momba hakuna barabara yoyote ambayo inajengwa sasa hivi kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018, je, kazi hii ya *TARURA* itaanza kutekelezwa lini na hasa barabara ya kutoka Kakozi - Ndalambo kuelekea Kapele? Barabara ni mbaya sana na sasa haipitiki. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na kama tunavyofahamu, ni kwamba tarehe 7 Julai, 2017 ndiyo Wakala huu umeanza kufanya kazi rasmi katika mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao. Huu ni Wakala mpya na lengo lake ni kuhakikisha kwamba zile kazi zilizokuwa zinafanywa na Halmashauri zetu, sasa zitafanywa na Wakala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mwezi uliopita nilikuwa na kikao na Watendaji wote wa *TARURA* wa Nyanda za Juu Kusini pale Mjini Mbeya na kuwapa maelekezo mbalimbali, lakini zoezi hilo lilikuwa limekamilisha semina na maelekezo mbalimbali kwa wataalam wote wa *TARURA* nchi nzima. Baada ya kufanya *zone* zote nne, tulianza Bagamoyo tukaenda Tanga, tukaenda Mwanza na tukamalizia kule Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakala huu sasa uko katika mchakato wa *stage* mbalimbali. Ndiyo maana wale wanafahamu mikoa mbalimbali hivi sasa. Sasa kandarasi zinaanza kutoa mikataba kwa wakandarasi wa aina mbalimbali na mingine kutokana na zile bajeti zake zilizopita ziko kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba mchakato huu unaenda na maeneo yote ya Tunduma na mikoa yote hivi sasa itashughulikiwa kwa kadri kandarasi hizo zilizotangazwa. Naomba niwahakikishie kwamba katika hili hatutakuwa na masihara katika usimamizi hasa wa ukandarasi utakaofanyika kule *site,* lengo letu ni kwamba Halmashauri zipate barabara bora kwa lengo kubwa la kuwasaidia wananchi wetu.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 43

**Ukosefu wa Mawasiliano ya Simu Kisiwani Pemba**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Baadhi ya maeneo katika Kisiwa cha Pemba yamekuwa na tatizo la kukosa mawasiliano ya simu kwa mitandao ya Tigo, Airtel na Zantel hali ambayo imekuwa ikisabbisha usumbufu.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa vile tatizo hili ni la muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano *Engineer* Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote

na watoa huduma za mawasiliano kuhakikisha kuwa huduma bora za mawasilino nchini zinawafikia wananchi wote kwa kuhakikisha inatatua changamoto mbalimbali za kiufundi na kiutendaji. Kwa mujibu wa takwimu za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Kisiwani Pemba kuna jumla ya minara saba ya Airtel, minara tisa ya Tigo, minara tisa ya Vodacom, minara 24 ya Halotel na minara 47 ya Zantel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, minara hiyo imejengwa katika Kata zifuatazo: Kata za Kisiwa Panza, Muambe, Kangani, Stahabu, Kengeja, Jombwe, Kendwa, Mtambile, Ng'ombeni, Uweleni, Mtangani, Chambani, Ukutini, Ngwachani, Chumbageni, Mizingani, Kilindi, Pujini, Mvumoni, Kibokoni, Mgogoni, Kichungwani, Wara, Tibirinzi, Mkoroshoni, Ndagoni, Michungwani, Ngw'ambwa, Ziwani, Ole, Kiuyu Minungwini, Mtambwe Kusini, Piki, Mtambwe Kaskazini, Pandani, Limbani, Jadida, Utaani, Selem, Finya, Wingwi, Kinyasini, Junguni, Gando, Chimba, Kojani, Chwale, Konde, Makangale, Tumbe Magharibi, Kiuyu Mbuyuni na Kata ya Majenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu hizi, tunaamini kuwa Kisiwa cha Pemba kinapata huduma nzuri ya mawasiliano kutoka kwa watoa huduma. Hata hivyo, kulingana na jiografia ya Pemba, baadhi ya maeneo yanaweza kupata shida ya kupata huduma kwa uhakika na mfuko utawasiliana na watoa huduma wakiwemo Zantel, Airtel, Tigo, Halotel na Vodacom ili kuona ni jinsi gani maeneo yote yenye changamoto hizi yanapata huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ana majina ya vijiji hivyo vyenye shida ya mawasiliano, anikabidhi ili tuvifanyie kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutupatia taarifa hizi na pia naomba nimhakikishie kwamba Wizara yangu itaendelea kufanyia kazi changamoto za Mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwemo Pemba.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maida.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mheshimiwa Waziri kujibu swali hili na kunihakikishia/kukiri kwamba yapo baadhi ya maeneo Kisiwani Pemba ambayo yanapata shida ya mawasiliano, hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la mawasiliano Kisiwani Pemba katika maeneo ya Makangale, Kipange, Tumbe Kiungoni, Mtambwe, Gando na maeneo mengine yaliyopo Kaskazini na Kusini Pemba na kupelekea wananchi wa mikoa hiyo kupata usumbufu wa mawasiliano hasa katika kipindi cha dharura...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa, uliza swali.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali kupitia Wizara hii inawaambia nini tena wananchi kuhusu kutatua changamoto hii ambayo imekuwa ikiwaletea shida muda mrefu na wakati mwingine wananchi hulazima kupanda kwenye miti mirefu kutafuta mawasiliano? *(Makofi)*

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuongozana na wataalamu wake kwenda Pemba kutafuta maeneo na vijiji mbalimbali kuweka minara ili kuwatatulia matatizo wananchi wa Pemba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba kuna uwezekano pamoja na Kata nyingi nilizozitaja kwamba zina mawasiliano,

kuna sehemu nyingine baadhi ya vijiji havina mawasiliano kutokana na jiografia ya Pemba ikiwemo Matangale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge aniorodheshee majina ya vijiji vyote ambavyo mpaka sasa hivi havipati mawasiliano ili tuwatume watu wetu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote watembelee sehemu ile ili kuweza kuleta mawasiliano kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ya nchi yetu wananchi wanawasiliana. Napenda nichukue nafasi hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba mpaka sasa hivi kwa takwimu tulizonazo kutoka Mfuko wa Mawasiliano wa Wote Watanzania asilimia 94 wanawasiliana. Kwa hiyo, asilimia sita iliyobakia inawezekana ni baadhi ya vijiji ambavyo amezungumza Mheshimiwa Mbunge; na ninamkaribisha Ofisini aje atuletee majina ya vijiji ambavyo hawawasiliani ili tuweze kutatua changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kwa ruhusa yako, mimi niko tayari kuongozana naye mpaka Pemba ili tuweze kwenda kuangalia hizo sehemu ambazo zina changamoto. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zuberi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwamoto na mwisho Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nipate kuuliza swali la nyongeza.

Matatizo ya mawasiliano katika Halimashauri ya Wilaya ya Liwale na Wilaya nzima ile ni makubwa sana na ujio wa Kampuni ya Halotel pamoja na *TTCL* tuliona kwamba inaweza kuwa kama mkombozi kwa ajili ya mawasiliano katika Halmashauri ile. Kwa bahati mbaya zaidi, miradi ambayo ilikuwa tayari wananchi wametoa maeneo yao kwa

ajili ya kujenga minara katika Kata za Mirui, Ngongowele, Mpigamiti, Mkutano, Ndapata na Igombe na Mtunguni miradi ile yote imesimama hatuwaoni tena wale Halotel...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali juu ya kukwama kwa miradi hii katika hizo Kata nilizozitaja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya sehemu ambazo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na watoa huduma za mawasiliano wameendelea kupata changamoto mbalimbali katika kutekeleza miradi ya kuweka mawasiliano kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumeendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali katika sehemu mbalimbali kuhakikisha kwamba mawasiliano yanawafikia wananchi kwa wakati. Kwa hiyo, namwakikishia Mheshimiwa Kuchauka kwamba hiyo miradi ambayo imekwama tunaifahamu na tunaifuatilia tutahakikisha kabla ya mwisho wa mwezi wa Juni, 2018 tutawatembelea sehemu hizo ili watu waweze kuwasiliana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ni Wilaya ambayo ina matatizo makubwa sana ya miundombinu na kupelekea usafiri wa magari usiwepo, kwa hiyo, mawasiliano pekee tuliyokuwa tunategemea, ni simu.

Sasa kuna vijiji ambavyo havina kabisa mawasiliano na hivyo kupelekea watu kupata shida na hata kupoteza maisha. Kwa mfano, Masisiwe, Ilambo, Magana, Mdaila, Kising'a, Masege na Uruti, hakuna kabisa. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu unawaambiaje watu wa Kilolo?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* Serikali ilitambua kata zenye uhitaji wa mawasiliano 443.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kata hizo, tayari tumeshapeleka huduma za mawasiliano kupitia mkataba wa Serikali ya Viatel, ambao ndiyo wanatoa huduma za Halotel 391. Pia mtambue kwamba Kata 75 ambazo zina vijiji 154 zinatakiwa ziongezwe kwa ajili ya kufikishia mawasiliano itakapofika Juni, 2018 .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja kati ya kata hizo na vijiji alivyovitaja, vitakuwemo kwenye mpango wa kupelekewa huduma za simu itakapofika Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Venance Mwamoto, kama ana mashaka niko tayari kwenda naye Jimboni kwake kwa ajili ya kuendelea kuhakikisha kwamba wananchi wa Kilolo ambako bahati nzuri nimeshafika, tena zaidi nilifika kwenye kijiji chake cha Masege, wanapata huduma ya mawasiliano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Omari Kigua kwa kifupi.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mawasiliano katika Kisiwa cha Pemba ni sawa kabisa na Wilaya ya Kilindi, baadhi ya maeneo hayana mawasiliano kabisa. Nini kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu wananchi wa Kata ya Saunyi, Kata ya Loane na baadhi ya maeneo ya Kata ya Kimbya ambao hawana mawasiliano kabisa katika Wilaya yangu ya Kilindi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejikita kupeleka mawasiliano sehemu zote ambazo hazina mawasiliano kabisa. Tunapata changamoto kwa baadhi ya vijiji ambavyo vina mawasiliano, lakini wananchi wanataka kutafuta mawasiliano ya ziada. Katika maeneo hayo, mipango ipo, lakini siyo ya haraka.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mgumba nafahamu kwenye Kata ya pili uliyoitaja baada ya Saunyi, kuna mawasiliano ya aina moja na wananchi wanataka mawasiliano ya aina nyingine. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuwasiliana na watoa huduma za mawasiliano, watakapoona kuna faida kwao, watapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumejikita kupeleka vile vijiji ambavyo wale watoa huduma lazima tuwashawishi kupeleka huduma za mawasiliano. Sile sehemu ambazo hakuna mawasiliano kabisa, hizo ndiyo tumejikita kama Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo hilo, wanawasiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndani ya vijiji hivi ambavyo nimevitaja, kama sehemu mojawapo ambako vinasomeka, tutahakikisha tunapeleka mawasiliano ili wananchi wa Tanzania wote wawasiliane.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni, mshauriane lakini kwa sauti ya chini. Waheshimiwa nawaombeni sana, naomba utulivu Bungeni. Ahsanteni.

Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Madini.

Na. 44

**Serikali Kujenga Kiwanda cha Kuchakata Madini ya *Tanzanite* Manyara**

**MHE. ESTER A. MAHAWE** aliuliza:-

Madini ya *Tanzanite* yanachimbwa Mkoani Manyara katika Wilaya ya Simanjiro, lakini madini hayo huchakatwa na kuuzwa Mkoani Arusha hali inayosababisha wananchi wa Manyara kutofaidika kiuchumi.

(a) Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu kujenga kiwanda cha kuchakata madini hayo Mkoani Manyara?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeshachangiwa na madini haya katika mapato ya Mkoa wa Manyara?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa madini ya *Tanzanite* yananufaisha wananchi wa Simanjiro, Serikali imetoa tamko la kutaka shughuli zote zinazohusu madini ya *Tanzanite* ikiwemo uendeshaji wa minada na ujenzi wa

viwanda vya uchakataji wa madini hayo zifanyike katika eneo la Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imetenga eneo katika Kijiji cha Naisinyai, Mererani ili kuwa eneo maalum kiuchumi kwa ajili uanzishaji wa viwanda vya uchakataji *(Economic Processing Zone - EPZ)* ili kuvutia uwekezaji katika eneo hilo kwa kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji. Hivyo Wizara itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa viwanda vya kuchakata madini ya *Tanzanite* kujenga viwanda katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo kwa vitendo, Wizara ya Madini imepata kiwanja katika eneo la *EPZ* ili kujenga Kituo cha Umahiri *(Center of Excellence),* sehemu ya jengo hilo itakuwa na taasisi mbalimbali zinazosimamia shughuli za madini ili kutoa huduma kwa wafanyabiashara wa madini ya *Tanzanite* kwa haraka *(One Stop Centre).* Pia baadhi ya ofisi katika jengo hilo litatumika kutoa huduma za uthaminishaji wa madini na kuendesha minada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017 madini ya *Tanzanite* yamechangia kiasi cha shilingi 140,954,229.37 kutokana na kodi ya tozo ya huduma *(Service Levy)* inayotozwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, manufaa mengine yaliyopatikana kwa Wilaya ni pamoja na fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kutokana na kuwepo kwa migodi katika eneo husika na huduma za jamii zinazotolewa na mgodi ambapo mgodi umetoa ajira kwa wafanyakazi 674 ambapo asilimia 93 ya walioajiriwa ni Watanzania na asilimia saba iliyobaki ni wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya waajiriwa hao, asilimia 21.81 ya wafanyakazi wameajiriwa katika vijiji kutoka vijiji vinavyozunguka mgodi vya Naisinyai na Mererani. Katika kipindi hicho mgodi wa *Tanzanite One* umefanikiwa

kuchangia jumla ya dola za Kimarekani 429,664 katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii ukilenga kuimarisha mahusiano na jamii zinazozunguka mgodi pamoja na kuchangia maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Huduma hizi zinahusisha masuala ya elimu, afya, lishe, ujenzi na sanaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba uniruhusu nimshukuru sana na kumpongeza Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuamua kujenga ukuta katika eneo lote ambalo *Tanzanite* inachimbwa katika Mkoa wa Manyara hususan eneo la Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niruhusu nimshukuru na kumpongeza sana Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Job Ndugai ambaye alimua kwa dhati kabisa kuunda Kamati Maalum kwa ajili ya kuchunguza upotevu wa fedha kupitia madini hayo ya *Tanzanite* yanayopatikana peke yake duniani eneo la Simanjiro.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kumekuwa na upotevu wa pesa kwa sababu wageni wanaotoka nje wanaokuja kununua *Tanzanite* hawalipi *VAT,* lakini wazawa waliopo pale eneo la Simanjiro, ama Arusha na Manyara wao ndio wanaolipa *VAT*. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro unaohusiana na mitobozano hususan kwa wachimbaji wadogo wadogo katika eneo hilo la Mererani, ni nini sasa kauli ya Serikali ili kuzuia migogoro hiyo isiyo ya lazima? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu,

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linalohusiana na *VAT,* kwa kawaida *VAT* huwa hatozwi mtu mgeni. Vilevile ni kweli kabisa kwamba katika mnada huu, wageni walikuwa wanunua *Tanzanite* kwenye mnada bila kutozwa *VAT,* lakini kwa wale wenyeji walikuwa wanatozwa *VAT.* Mfano ukienda sehemu nyingine ni kwamba *VAT* unatozwa kule unakonunua bidhaa, kisha unaenda kurudishiwa kwenye kituo cha ndege *(airport).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi kama Serikali tunaangalia namna mpya ya kuhakikisha kwamba katika mnada ule, watu wote wanaonunua *Tanzanite,* sasa hivi tutaanza kuwatoza kodi ya *VAT* halafu mgeni aende akarudishiwe kule *airport.* Huo ndiyo msimamo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la pili, kuhusu mitobozano. Ni kwamba mitobozano ni mgogoro wa muda mrefu pale Mererani na kuna kamati nyingi zimeundwa kuhakikisha kwamba wanakwenda wanatatua tatizo la mitobozano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba sasa hivi Umoja wa Wachimbaji wa *Tanzanite* pale pale Mererani wameweka mkakati wa namna wa kutatua mgogoro wa mitobozano. Kuna mkakati wameutengeneza na wamekubaliana kwa pamoja. Kwa hiyo, mkakati huo, ambao tuna hakika kwamba tukiufuata na utataribu ambao wameuweka mgogoro wa mitobozano utakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la

nyongeza. Kwa kuwa mbali na madini ya *Tanzanite* kuwa chanzo cha mapato kikubwa kwa wafanyabiashara wa mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara, lakini pia kuna madini ya aina ya Rubi yanapatikana katika Kijiji cha Mundarara, Wilayani Longido Mkoani Arusha.

Ningependa kujua Serikali, inajipanga vipi ili madini haya aina ya Rubi iweze kuwanufaisha wananchi wa Longido? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru na ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kutetea wachimbaji wadogo wadogo Mkoani Arusha na kazi nzuri anayoifanya na wananchi wa Arusha wanaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini ya Rubi yanapatikana katika Kijiji cha Mundarara katika Wilaya ya Longido Mkoani Arusha. Madini hayo yanapatikana na eneo hilo kwa pembeni yake kuna leseni ya mtu anayeitwa Mheshimiwa Mareale. Sasa hivi ni kwamba kuna wachimbaji wadogo wanavamia eneo lile. Sisi kama Serikali tunawapenda wachimbaji wadogo, lakini tunataka wafuate taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokitizama sasa hivi ni kwamba lile eneo ambalo ni la mtu ambaye anayelimiliki na haliendelezi, tutaangalia namna bora ambayo tunaweza tukawatafutia wale wachimbaji wadogo waweze kuchimba na tuwatambue na wachimbe katika vikundi ili tuweze kuwatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanapochimba, basi tuweze kama Serikali kupata kodi zetu pale, tupate mrahaba pale, Halmashauri ya Longido ineemeke na Serikali kwa ujumla ineemeke na zile fedha tupeleke kwa wananchi

wengine ambao wako nje na maeneo ya uchimbaji, waweze kuneemeka kupata huduma za maji, barabara na huduma za afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge na linaelekezwa kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Na. 45

**Mradi wa Maji ya Kutoa Mto Kagera**

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

(a) Je, lini mradi wa maji ya kutoka Mto Kagera utaanza kuhudumia wananchi wa Kyaka na Bunazi?

(b) Je, mradi huo utagharimu kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba *(BUWASA)* imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Kagera kwenda kwenye Miji ya Kyaka na Bunazi. Kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni za ujenzi inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama halisi za utekelezaji wa mradi huo zitajulikana ifikapo mwezi Septemba, 2018 baada ya kukamilika kwa usanifu unaoendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kamala.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukiangalia majibu yaliyotolewa ni kwamba upembuzi unaendelea na gharama halisi zitajulikana Septemba.

Sasa hii inanipa wasiwasi kidogo kwa sababu kipindi hicho bajeti itakuwa imepitishwa, sasa wananchi wa Jimbo la Nkenge wawe na uhakika upi kwamba ni kweli mradi huu utaanza kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, tufuatane twende katika Wilaya ya Misenyi tuweze kupokea na kuona changamoto mbalimbali tunazokumbananazo katika utekelezaji wa miradi ya maji. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Balozi kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya katika kuwatetea wananchi wake waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata maji, na sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa wananchi wake katika kuhakikisha wanapata maji, siyo maji tu, ni kwa maana ya maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahikikishie wananchi wa Mheshimiwa Dkt. Kamala kwamba sisi katika bajeti yetu kwa kuwa tumeshakuwa na upembuzi, inatupa *estimation cost* ya kuwaweka katika suala zima la bajeti ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la kwenda kufanya ziara, nipo tayari kwenda kutembelea, siyo kwenda kuona tu katika hali ya kwenda kutatua matatizo ya maji katika Jimbo lake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Waitara wa mwisho Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mto Kagera, pamoja na Mto Ruvugu ni mito ambayo ikitumiwa vizuri inaweza kuondoa kero ya maji kwa Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Geita; na kwa kuwa tayari mwaka 2017 Mheshimiwa Rais alipokuja Jimbo la Ngara wananchi wa Jimbo la Ngara kupitia Mbunge wao tulimwomba kuanzisha mradi huu mkubwa wa maji kwa ajili ya kutatua kero ya maji Wilaya za Ngara, Biharamulo, Karagwe, Bukombe, Mbogwe na Chato kwa kutumia fursa ya kijiografia Wilaya ya Ngara.

Ni lini mradi huu sasa utaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu ili kuondoa kero kwa wananchi wa Mkoa wa Geita na Kagera? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Ooh, Waziri mwenyewe, Mheshimiwa *Engineer* Isack.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi lililoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Kamala linahusu pia Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ambapo huyu mkandarasi ambaye anamalizia usanifu wa kina, anahusisha miji sita kama alivyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunarajia kwamba kwa vile tayari upembuzi yakinifu tunao, tunamalizia usanifu

wa kina, tunarajia kupanga bajeti kwenye mwaka ujao wa fedha na kuanzia mwezi wa tisa tutaanza kutangaza tenda ambayo itahusha pia na Mji wa Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie pamoja na wananchi wako wa Ngara kwamba tunatekeleza hiyo miradi ili uweze kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba Bunge lililopita niliwaomba kwamba Kata ya Msongola ina matawi tisa na ina maji kwenye visima vitatu katika mitaa mitatu tu. Kata ya Zingiziwa, Chanika, Buyuni na Pugu, hazina maji. Mvua ikinyesha ndiyo wananchi wanachota maji yale wanatumia.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, ni kwa nini Mawaziri hawa wamekataa kuja Ukonga kuongea, hata kuwapelekea akina mama wenye shida ya maji pale na wanakaa Dar es Salaam?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyolieleza Bunge, kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha tayari tumeshakamilisha miradi miwili na tuna maji ya kutosha zaidi ya lita milioni 510 ambayo ni maji toshelevu. Kinachoendelea sasa hivi, tulikuwa tunahitaji dola milioni 100 ili tuweze kukamilisha usambazaji katika eneo lote la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani na awali tulipata dola milioni 32 mradi ambao sasa utakamilika tarehe 15 Februari, 2018 lakini tumepata tena dola milioni 45

kutoka Benki ya Dunia. Tunarajia kutangaza tenda mwezi huu wa pili; tunaendelea, itakuwa imebaki fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka maeneo yote ya Zingiziwa unayoyazungumza tutahakikisha kwamba maji yanafika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutuletea maji Segerea, lakini nilitaka nimuulize Waziri, pamoja na kwamba tunapata maji asilimia 70, lakini kumekuwa na matatizo ya Kata kama Bonyokwa, Kipawa pamoja na Kiwalani na Minazi Mirefu. Sasa Serikali ina mpango gani kwa hizi Kata zilizobaki kuziletea maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii, lakini kubwa napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mbunge wa Segerea kwa namna anavyowatetea wananchi wake. Moja ni Mbunge shapu ambaye alishafika ofisini kwetu katika kuhakikisha kwamba tunaenda kufanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam katika Jimbo la Segerea. Sisi mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwapatia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari baada ya Bunge kwenda kuongea na wananchi wa Segerea katika kufanya mpango wa haraka ili wananchi wake waweze kupata maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mbunge wa Mlimba. Linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 46

**Uhaba wa Maji Safi na Salama Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Jimbo la Mlimba lina mito mikubwa inayotiririka mwaka mzima kwa miaka mingi, lakini Jimbo limekuwa na tatizo kubwa la kupata maji safi na salama.

(a) Je, ni lini Serikali itatumia uwepo wa mito hiyo kama fursa ya kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Mlimba hasa Mji Mdogo wa Mlimba?

(b) Je, ni lini Serikali itatumia uwepo wa mito hiyo kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwajiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Jimbo la Mlimba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeanza kutumia fursa ya mito iliyopo katika Jimbo la Mlimba kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Jimbo hilo. Mpaka sasa kuna miradi minne ya Tanganyika Masagati, Chita/Ching'anda, Mngeta/Mchombe na Mkangawalo/ Kidete/Itongowa. Vyanzo vyake ni mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali imepanga kujenga mradi wa maji Mbingu/Vigaeni ambao chanzo chake ni Mto Ifumbo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero imepanga kufanya usanifu wa kupeleka maji katika Kata ya Mlimba kwa kutumia Mito ya Mgugwe na Mpanga, kwa sasa mji mdogo wa Mlimba unapata huduma ya maji kupitia visima virefu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo *(USAID)* ilifanya upembuzi yakinifu katika Bonde la Mto Kilombero ikiwemo maeneo ya Jimbo la Mlimba kwa ajili ya kubainisha maeneo ya kujenga skimu za umwailiaji na mabwawa ambapo takribani hekta 43,000 zilibainishwa. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya uendelezaji maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi.

Swali (a) kwa kuwa hapa ukiangalia tu haraka haraka kwenye jibu (a) unakuta kwamba kuna kazi kubwa inaendelea, lakini naomba hii kazi ukaone kwa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii Mlimba aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sasa inatumia maji ya kisima, kweli kuna kisima kimoja na hicho kisima kwa vile Mji wa Mlimba unakua kwa kasi na ni Makao Makuu ya Wilaya ya Tazara, yaani kwa wiki mara hii, moja, ndiyo maji tunapata. Kwa hiyo, naomba ukaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu sasa, kwa kuwa anasema kuna huu mradi ambao utakuja kufanyiwa upembuzi yakinifu kupata maji Mto wa Mgugwe na Mpanga, na kwa kuwa eneo la Mlimba lina vyanzo vingi vya mito, je, Serikali iko tayari kwenye huu mradi wa Mlimba kutumia maji ya Mpanga na Mgugwe kuingiza katika bajeti ya Serikali mwaka huu wa fedha ili wananchi wa Mlimba wapate maji safi na salama? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia masuala ya Masagati, ni Kata ya Masagati; na hapa sitapoteza muda kusema mambo mengi, ninaomba sasa uje Mlimba maana umetoa ahadi nyingi sana hapa na

Waheshimiwa Mawaziri wengi wakija wanaishia Ifakara badala kwenda Jimbo la Mlimba...

**MWENYEKITI:** Swali *please!* Swali.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki tukimaliza Bunge naomba Mheshimiwa Naibu Waziri twende Mlimba akaone hali halisi maana sasa hivi muda hautoshi kusimulia, ili akija hapa anapojibu maswali aone kama anajibu hali halisi kutokana na hilo Jimbo la Mlimba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukimwona mzee wa matobozano analia, ujue kuna jambo Mlimba. Kwa hiyo, mimi kama Naibu Waziri nipo tayari kwenda Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwa kuwa kuna changamoto kubwa sana Mlimba kwa ruhusa yako, namwomba Mheshimiwa Susan tuweze kukutana baada ya Bunge ili tuweze kuangalia namna pekee ya kuweza kuwasaidia wananchi wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tatizo lililopo Mlimba linafanana kabisa na tatizo la ukosefu maji safi na salama lililopo katika Mkoa wa Katavi. Serikali iko tayari kutumia maji ya Mto Mpanda, Mto Manga, Mto Katuma ili wakazi wa Kata ya Mwamkulu, Kakese pamoja na Kasokola wapate maji safi na salama hususani katika suala la kilimo katika Mkoa wa Katavi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Isack.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatekeleza miradi mingi ya visima katika Mkoa wa Katavi na tayari tumetumia mito iliyopo kupeleka maji katika Mji wa Mpanda na sasa hivi tunaelekea kuwa na asilimia zaidi 70 ya maji safi na salama katika Mji wa Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshapokea andiko na tunalifanyia kazi ili tuweze kumaliza tatizo la maji kabisa katika Mkoa wa Katavi kwa kuchukua maji kutoka katika Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi kunakikisha mikoa yote inapata maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Ester Mmasi wa mwisho.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufanya ziara katika Halmashauri ya Mbeya na katika ziara yake tuliahidi kuwa mradi wa Iwindi wananchi wangeanza kupata maji kabla ya Desemba mwaka 2017, je, ni lini mradi wa maji kwa Vijiji vya Izumbwe, Iwindi, Mwashiwawala na Mbalizi utakamilika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu. Lini mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Mbalizi, Mzee Njeza kwa kazi kubwa anayoifanya katika suala zima la kuhakikisha wananchi wake wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa nilishafanya ziara kule lakini ipo changamoto baadhi yetu wataalam kushindwa kusimamia miradi. Moja, nataka nimhakikishie tu, katika hali niliyoiona nipo tayari kushirikiana naye lakini pia na watalaam

wetu kwenda katika kusukuma miradi ile ili wananchi wake waweze kupata maji kwa wakati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bwawa la Nyumba ya Mungu kwenda Wilaya ya Same na Mwanga ni mradi ambao ulipaswa uwe katika hatua za mwisho za utekelezaji, lakini mpaka ninapoongea leo mradi huu umeonekana kutokufikia hata asilimia 40 ya utekelezaji wake.

Je, Serikali imejipangaje katika kuwakwamua wakazi wa Wilaya ya Same na Mwanga na *especially* wanawake wote na wapiga kura wangu wa Wilaya ya Same na Mwanga? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer* Isack.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Same/Mwanga kutokutoa maji kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu, mkandarasi wa kwanza yuko asilimia 75, mkandarasi wa pili tayari anafika asilimia 30 na kazi inaendelea. Sasa hivi *tank* kubwa la Mlima wa Kiverenge linajengwa ambapo *tank* hilo likishakamilika, sasa maji yatakwenda Mji wa Mwanga na Same; na kazi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya miezi sita wananchi wa Same na Mwanga wataanza kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dotto Gimbi Masaba, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 47

**Kufuta Ushuru wa Matrekta ya Kilimo**

**MHE. GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Zaidi ya 70% ya Watanzania, uchumi wao unategemea kilimo.

Je, kwa nini Serikali isifute ushuru wa matrekta kuanzia matano hadi kumi kwa kila kijiji nchini kwa ajili ya kilimo ili kuwawezesha wananchi kuondokana na kilimo cha mkono?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 6(1) Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Sheria ya Kodi ya *VAT* ya mwaka 2014, kimebainisha misamaha ya kodi kwenye vifaa mbalimbali vya kilimo. Mojawapo ya vifaa vya kilimo vilivyosamehewa kodi ni matrekta, mashine za kuvunia *(combine harvester),* vifaa vya umwagiliaji, dawa za kuulia wadudu waharibifu wa mazao, vipuri vya matrekta na kadhalika. Hivyo basi, kwa mujibu wa jedwali hili, matrekta pamoja na vipuri vyake hayatozwi kodi na ushuru wa forodha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gimbi.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Watanzania zaidi ya asilimia 65 wanategemea kilimo cha mikono; na kwa kuwa kilimo kimechangia asilimia 29.1 sawa na dola za Kimarekani bilioni 13.74 kwenye pato la Taifa yaani *GDP* ya mwaka 2016/2017...

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuondoa kodi na tozo zote kwa zana za kilimo hasa matrekta pasipo kuwepo na ukomo kama ilivyo kwa sasa? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wengi Tanzania wana matamanio ya kupata matrekta kwa wingi, je, Serikali haioni kwamba inatakiwa ihamasishe kupata viwanda vya kuunganisha matrekta ili wananchi walio wengi waweze kuyanunua kwa wingi ili kuweza kuboresha kilimo cha kisasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu ni shahidi, katika kipindi cha mwaka huu wa 2017/2018 Serikali kwa kutambua umuhimu wa wakulima na mchango wao mkubwa kwenye pato la Taifa, iliondoa kodi na tozo mbalimbali ambazo zilikuwa zinamsumbua mkulima na hii ni dhamira njema ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa kodi hizi ni mchakato wa kisheria na Serikali ya Awamu ya Tano tumekuwa tukimsikia Mheshimiwa Rais wetu akisema, yuko tayari kabisa yeye na Serikali yake kuhakikisha kodi zote zile ambazo ni sumbufu kwa wakulima zinaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza 2017/2018 kuondoa zaidi ya kodi 15 kwa wakulima wetu na tunaendelea na mchakato sasa wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018/2019. Dhamira ya Serikali ni njema tu tutaendelea kutekeleza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kutoka kwenye ukomo huo, Serikali inatambua. Tuliweka ili kuangalia mazingira ya ufanyaji kazi, tunaendelea kulishughulikia na litakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili kuhusiana na viwanda vya kuunganisha matrekta, naamini Mheshimiwa Waziri wa Viwanda yuko hapa na amekuwa akisema vizuri. Tayari tuna kiwanda pale Kibaha cha kuunganisha matreta, tumeanza kutekeleza dhamira ya Serikali ili kuhakikisha kilimo chetu kinaongeza uchangiaji wake katika pato letu la Taifa na kuwawezesha Watanzania walio wengi katika shughuli hii muhimu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani. Aida!

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata pembejeo za kutosha na wanapata masoko ya uhakika, jambo ambalo Serikali hii imeshindwa kutimiza wajibu wake.

Swali langu, Serikali ina mkakati gani wa kuandaa masoko ya uhakika badala ya taabu ambazo wanazipata wananchi wetu na kupata umaskini unaosababishwa na Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikanushe kwa herufi kubwa kwamba Serikali imeshindwa kutengeneza mazingira kwa ajili ya watu wetu. Hiyo ni uongo kabisa na ndiyo maana suala la *commodity market* kama Wizara tunaendelea kulisimamia na limefika hatua nzuri kuhakikisha sasa wakulima wetu, wafanyabishara wetu wanauza mazao yao katika soko ambalo limeandaliwa kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme na ndiyo maana hata zao la korosho limenyanyuka na linakimbia, hii ni kwa sababu ya jitihada za Serikali yetu kuhakikisha wakulima wetu na wafanyabiashara wetu wanaweza kufikiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa nimeomba swali namba 45.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Tunaendelea.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Kwa bahati mbaya muda wa swali hilo umepita.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pia naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa ambayo inaendelea kuwafanyia wakulima wetu. Nitakuwa na swali ndogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa wakulima wetu wengi *especially* Mkoa wangu wa Iringa wamekosa mwongozo na baadhi hawana uelewa ni kitu gani wanatakiwa kufanya ili bidhaa zao ziweze kufika kwenye Soko la Kimataifa, sasa Serikali iko tayari kuwa na Kitengo Maalum ambacho kitakuwa kinafanya kazi usiku na mchana, siyo tu kwa kutafuta masoko, bali kwa kutoa taarifa kwenye mikoa yetu juu ya hali ya masoko ya bidhaa ambazo wanazalisha? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Tweve kwa swali zuri.

Kuanzia mwaka 2017 maelekezo ya Serikali ni kwamba Shirika la *TanTrade* lina jukumu la kuhakikisha kwamba

linatafuta masoko ya mazao na bidhaa zote za Tanzania na lina wajibu wa kuhakikisha linatengeneza mtandao kupitia Halmashauri za Wilaya kwamba waweze ku-*identify* wakulima wana nini na masoko yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tulionao sasa ni kwamba Wizara yangu kwa kushirkiana na Wizara ya Kilimo na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Biashara ngazi ya Wilaya watakuwa waki-*link* na *TanTrade* na hizi Wizara za kisekta katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata masoko ya mazao yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa *Engineer* Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini na linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Fedha na Mipango.

Na. 48

**Mazao Kuchangia Pato la Taifa**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Je, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ni mazao yapi yaliongoza katika kuchangia Pato la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa, mchango wa mazao ya kilimo, misitu na uvuvi katika pato la Taifa kwa kipindi cha miaka mitano iliopita ulikuwa ni asilimia 31.1 mwaka 2012; asilimia 25.0 mwaka 2013; asilimia 24.5 mwaka 2014; asilimia 23.5 mwaka 2015 na asilimia 26.4 mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yaliyoongoza katika mauzo kwenye soko la nje na kuchangia kwa sehemu kubwa katika pato la Taifa ni tumbaku, korosho, kahawa, pamba na chai. Fedha za kigeni zilizopatikana kutokana na mauzo ya mazao hayo ni dola za Kimarekani milioni 956.8 mwaka 2012, dola za Kimarekani milioni 868.9 mwaka 2013, dola za Kimarekani milioni 808.8 mwaka 2014, dola za Kimarekani milioni 793.4 mwaka 2015 na dola za Kimarekani milioni 895.5 mwaka 2016.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Makani.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza majibu mazuri ya Serikali kwa swali hili. Lakini pamoja na pongezi zangu hizo naomba kuwasilisha maswali yangu mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza takwimu zilizosomwa kwa ufupi zinaonesha kwamba kwa wastani uchangiaji wa mazao katika sekta ndogo hizo za kilimo, misitu na uvuvi ni 26.1%. Lakini pia wastani wa fedha za kigeni katika miaka hiyo mitano ni dola za Kimarekani milioni 864.68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Taifa letu limepanda treni ya mwendo kasi inaitwa viwanda kwa ajili ya kukamilisha safari yake kuelekea uchumi wa kati inaonekana wazi kabisa, ushahidi upo unaoonesha kabisa juu ya umuhimu wa sekta hii ya kilimo, lakini mahususi kabisa mazao yale matano yaliyotajwa yaani tumbaku, korosho, kahawa, pamba na chai.

Mheshimiwa Mwenyeki, sasa maswali yangu ya nyongeza yatajikita zaidi kwa korosho kwa leo na nikisema kwamba swali la kwanza, kwa kuwa sasa tunataka mazao haya yachangie zaidi uchumi na kuongeza kasi hiyo yakufikia malengo ya Taifa ya kiuchumi. Je, Serikali inajipanga namna gani kuondoa vikwazo, kuondoa hali yoyote ile ambayo inawafanya wakulima washindwe kuzalisha zaidi? Kwa mfano kwa sasa hivi kule Tunduru wananchi wanapata matatizo ya upatikanaji...

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. ENG. RAMO MATALA MAKANI:** Ndiyo, Serikali itaboresha namna gani utaratibu wa kibenki, unaowafanya Wananchi wa Wilaya ya Tunduru wapate shida katika kupata fedha zao baada ya kuuza mazao ya korosho miezi kadhaa iliyopita waondokane na misururu mirefu lakini pia na kusafiri kilometa nyingi zinafikia 120 na kukaa Makao Makuu ya Wilaya kwa siku mbili mpaka tatu? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili linausiana na suala la pembejeo, upande wa pembejeo ningependa kuzungumzia ubora wa pembejeo zenyewe, lakini pia ningependa kuzungumzia upatikanaji kwa wakati wa pembejeo zenyewe, lakini pia bei ya pembejeo zenyewe. Kwa ujumla Serikali inajipanga namna gani katika kuhakikisha kwamba wananchi hawa wa Tunduru hasa wa zao la korosho, ni wa mazao yote lakini hususani wa zao la korosho kwa leo ili waweze kupata pembejeo hasa mbolea na madawa ya kuweza kuboresha, kilimo na hasa mazao ya ya korosho upande wa *sulphur?*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaifahamu changamoto hiyo ya wananchi wetu na hasa wakulima wetu wa kule Tunduru kwenda kupanga foleni katika mabenki yetu na hili hata Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda tarehe 10 Januari aliwasiliana na mimi akiwa Masasi, akiwa kwenye foleni na wananchi hao kwa ajili ya kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba kama ambavyo nimekuwa nikiliambia Bunge lako Tukufu kuanzia mwaka 1991 tuliingia katika soko uria kuhusu sekta ya kifedha na mabenki nchini. Lakini pia, mabenki yetu kwenda kufungua matawi maeneo mbalimbali huwa inahitaji kuangalia nguvu ya soko *(demand and supply)* katika hilo, maana na wao ni wafanyabiashara wanahitaji kupata faida wanapofungua matawi yao.

Ninafahamu kuhusu wakulima wetu wa korosho kule Tunduru na Mtwara kwa ujumla na Wilaya zake na zao hili ni la msimu kwa hiyo kunakuwa na wateja wa msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya kama Wizara ya Fedha kwa sasa ni kuongea na mabenki yetu kuona jinsi gani watafikisha huduma za mawakala *(Agent Banking)* au waweze kutumia *Mobile Banking* katika kuwahudumia Wananchi wetu wa maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili Serikali inatambua umuhimu wa mazao yote kwa ujumla na *particular* mazao haya matano niliyoyasema na ndiyo maana Serikali mwaka 2013 ilikuja na *Regulatory Authority* ambayo ni *TFRA* inayoshughulika na pembejeo za wakulima wetu. Tunaendelea kuimarisha wakala huu ili uweze kufanya kazi nzuri kuhakikisha wananchi wetu wanapata pembejeo wanazozihitaji hasa katika ubora na bei ambayo wanaweza kuihimili kuinunua.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ahsante Mwenyekiti na Mtemi wa Wanyantuzu kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa dhamira ya Serikali ya kuanzisha benki ya kilimo, ni kwa ajili ya kuinua sekta ya kilimo na kuwasaidia wakulima kwa ujumla ambao ndiyo sekta hiyo ndiyo inayochangia katika ajira pamoja na pato la Taifa. Tunajua, Benki ya Kilimo ....

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo naenda Benki ya Kilimo ina mtaji wa Bilioni 60, ili kufikia malengo ya kuwasaidia wakulima ilikuwa inapaswa kuwa na Bilioni 800, Serikali mkaji-*commit* kwa kila mwaka kwa miaka minane kupeleka bilioni 100, 100 lakini mpaka hivi tunavyoongea hamjapeleka.

Je, ni lini Serikali sasa mtapeleka fedha hizo kwenye Benki ya Kilimo, ili wakulima wanufaike na benki hiyo na kuhakikisha wanachanigia zaidi katika pato la Taifa na Sekta ya Kilimo kwa ujumla?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jana tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema vizuri sana kuhusu Benki ya Kilimo. Kwa hiyo, na Mheshimiwa Ester alikuwepo naamini anakumbuka na Bunge lako Tukufu linakumbuka kwamba dhamira ya Serikali yetu ni kuhakikisha kwanza tunaimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba nikope maneno yako uliyoyasema jana; "Kwamba tayari tuko mchakato unaelekea mwisho wa kuhakikisha menejimenti inakaa vizuri ili pesa ya Serikali inayoingizwa kwenye benki hiyo iweze kufanya kazi vizuri na waweze kuwafikia wakulima wetu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikumbushe Bunge lako Tukufu, nimekuwa nikisema benki hii sasa pamoja na ukakasi uliopo kwenye menejimenti lakini tayari walishaanza mchakato wa kufungua matawi kwenye kanda sita ndani ya Tanzania, hii ikiwa ni dhamira ile ya dhati ya Serikali yetu yakuhakikisha benki hii inawafikia wakulima kule walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yetu ni ya dhati na ndiyo maana tumechukua pesa kutoka *African Development Bank* na kuzipeleka benki ya Kilimo. Kwa hiyo, hii bilioni moja, moja kwa miaka nane inayosemwa mbona hatuongelei hizi pesa za *African Development Bank*. Hizi ni pesa za Serikali pia na ndiyo maana tumepeleka ili kuiwezesha benki yetu iweze kuhudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 49

**Kuwezesha SIDO Kufikia Malengo**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua kama Serikali ya viwanda na kuna Shirika la Serikali lililoanzishwa kwa ajili ya kuanzisha na kuimarisha Viwanda Vidogo Vidogo vya *SIDO* .

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali imeliwezesha Shirika hilo katika kufikia malengo yake na malengo ya Serikali kwa Tanzania ya viwanda?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Shirika hilo linakuwa na matawi katika kila Wilaya tofauti na sasa kuwa na Ofisi katika ngazi za Mikoa tu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuliwezesha Shirika la *SIDO* kutoa huduma za kujenga uwezo kwa wajasiriamali kupitia programu za mafunzo, ushauri, teknolojia, masoko na utoaji wa mitaji. Katika kufanikisha hilo Serikali imekuwa ikiimarisha bajeti za *SIDO* kila mwaka na kwa mwaka wa fedha 2018/2018 *SIDO* ilitengewa shilingi bilioni 14.2 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu

ya viwanda na kuongeza mtaji kwenye mfuko wa *NEDF*. Kati ya fedha hizo Serikali imekwishatoa shilingi bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Ofisi na *Industrial Sheds* katika mikoa ya Simiyu, Geita, Kagera kwa hatua ya kwanza na utaratibu unakamilika kwa hatua ya pili katika mikoa ya Mtwara, Manyara, Dodoma na Katavi.

Pia Serikali kwa kushirikiana na wabia na maendeleo ikiwemo Serikali ya Japan kupitia *JICA*, Serikali ya Canada kupitia *CESO* na Serikali ya India zimeendelea kuipatia *SIDO* uwezo ikiwemo kuanzisha vituo vya viatamizi vya kuonyesha na kufundishia teknolojia mbalimbali, kuendesha makongano ya wanaviwanda vidogo nchini na kushirikiana na *SIDO* kutambua mahitaji halisi ya wajasiriamali na kuwasaidia kuongeza tija katika shughuli za uzalishaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira yetu kuwa karibu na wananchi katika dhama hizi za kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda kwani viwanda vidogo na vya kati ni muhimu katika kujenga uchumi ulio jumuishi. Kutokana na ufinyu wa bajeti kwa sasa tunahudumia ngazi ya kata mpaka Wilaya kwa kupitia Halmashauri za Wilaya.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kumekuwa na Mamlaka nyingi za usimamizi na uwezeshaji katika mipango ya Serikali hasa katika suala hili la la viwanda.

(a) Je, Serikali kupitia *SIDO* ina mkakati gani wa kuunganisha mipango hii na hiyo mipango ikaunganishwa na rasilimali watu wanaozalishwa katika vyuo vyetu vya Ufundi hapa nchini?

(b) Sera na usimamizi wa kodi ni mambo muhimu sana katika kufanikisha suala la viwanda. Je, ulipwaji na utozwaji wa kodi unaofanywa na mamlaka husika hapa

nchini, umezingatia vipi suala hili ili kutokuhathiri sekta hii changa ambayo inakua?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Injinia Stella Manyanya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, niseme tu kwamba katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ni kwamba suala hili ni mtambuka na linafanywa na wadau mbalimbali na sekta nyingi na hivyo hata usimamizi ulikuwa umepangwa zaidi kulingana na uhalisia wa eneo ambao usimamizi wake unahitajika ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwenye suala la madawa na vyakula, tunazungumzia masuala ya kiafya. Kwa hiyo, unaangalia kwamba kulikuwa na kuangalia mamlaka hiyo ya usimamizi itakuwa imeweza kufanya kazi zake vizuri na kuondoa vikwazo kwa kiasi gani kama itakuwa imekaa katika eneo hilo. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikiendelea kufanyia kazi suala hilo ili kuona namna bora zaidi ya hizi mamlaka za usimamizi zinavyoweza kuunganishwa ili kuweza kuleta tija zaidi katika uchumi huu wa maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, kwa suala ambalo ni la *SIDO* kuwa yeye sasa kama muunganishaji. Kimsingi *SIDO* haifanyi kazi peke yake, mfano tu kwamba kwa mfano katika Mkoa wako wa Manyara ukiangalia katika suala la uendelezaji wa zao la vitunguu swaumu, pale tayari kuna wadau wengi ambao wamehusika *MIVAP* ambao kulikuwa na jengo pale lakini pia katika *chain* ya kuongeza thamani, ukienda Magugu kuna *SNV* wanaoshirikiana na *SIDO* katika uongezaji thamani katika eneo la mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika na katika eneo la Hanang, vilevile kuna suala la kuangalia menejimenti ya kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Kwa hiyo, kimsingi ni kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wadau wote wanaunganika pamoja na kila mtu kuweka

*intervention* katika eneo linalohusika ili kuweza kupata tija katika uendelezaji wa wajasiriamali na viwanda kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tunaendelea, Wizara hiyo hiyo, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Rashidi Mohamed Chuachua Mbunge wa ...

Na. 50

**Kiwanda cha Korosho Masasi**

**MHE. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiahidi kusimamia Sera ya Viwanda ili Tanzania iwe na uchumi wa kati, lakini hakuna jitihada za wazi za kufufua viwanda vya korosho ili kuongeza thamani halisi ya zao hilo na kutengeneza ajira.

(a) Je, ni lini Serikali itahakikisha Kiwanda cha Korosho cha Masasi kinafanya kazi?

(b) Kwa kuwa utaratibu wa ununuzi wa korosho hauruhusu viwanda kununua korosho kutoka kwa wakulima; je, ni lini Serikali itafungua mlango ili kukuza viwanda hivyo ili vipate fursa ya kununua malighafi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Korosho cha Masasi ni moja ya viwanda vilivyobinafsishwa na kuuzwa kwa Kampuni ya *BUCCO Investments Holdings Limited* ambayo ilishindwa kukiendesha kutokana na benki ya *CRDB* kuzuia mali za kiwanda baada ya kiwanda kushindwa kurejesha

mkopo waliokopa. Hatimaye kiwanda kiliuzwa na *CRDB* kwa Kampuni ya *Micronix Export Trading Co. Ltd.*, kwa njia ya mnada. Kwa kuwa *BUCCO* hawakuridhika na utaratibu uliotumika kuuza kiwanda hicho, walifungua kesi mahakamani na kuishtaki benki ya *CRDB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kesi iliyopo mahakamani uendelezaji wa kiwanda hicho umeshindikana hadi hapo mahakama itakapotoa uamuzi wa kesi husika. Serikali inaandaa mazungumzo na wadau wa viwanda vyote ambavyo vina kesi mahakamani kikiwemo Kiwanda cha Korosho Masasi ili kuharakisha utatuzi wa migogoro iliyopo na hatimaye kuwezesha uwekezaji kuendelea ili vianze uzalishaji haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijakataza viwanda kununua korosho kutoka kwa wakulima, bali imekataza ununuzi wa korosho kufanyika kiholela kutoka kwa wakulima. Kwa kuwa lengo ni kusimamia maslahi ya wakulima na wadau wengine wa zao la korosho, Serikali ilianzisha utaratibu wa kuuza korosho kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo huo haulengi kuvififisha viwanda bali kuwanufaisha wakulima na wadau wengine ikiwa ni pamoja na wenye viwanda. Kutokana na mfumo huo, korosho zilizohifadhiwa kwenye maghala huweza kutumika kama malighafi ya viwanda kwa mwaka mzima. Aidha, wakulima wanafaidika na bei shindani na udhibiti katika ubora wa korosho unakuwa ni wa uhakika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chuachua.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na swali langu. Lakini ukweli kwamba kuna shida ya kupatikana kwa malighafi ya korosho kwa viwanda vyetu vidogo vidogo vya ndani uko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ili kuweza kuingia kwenye mnada wa korosho unahitaji kuweka *bond* ya zaidi ya shilingi milioni 100 ili kuweza kupata kupata korosho,

jambo ambalo wajasiriamali wetu wadogo wadogo ambao wana viwanda vidogo vidogo wanashindwa kulimudu.

Sasa ni lini Serikali itaona haja ya kuhakikisha kwamba utaratibu mzuri tulionao unaendelea, lakini pia inatangeneza utaratibu wa kuhakikisha kwamba wajasiriamali wenye viwanda vidogo vidogo nao wanapata fursa ya kununua korosho kwa ajili ya kuzichakata? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kuona kwamba na yeye anaunga mkono mfumo unaoendelea sasa, ni lengo la Serikali kuona kwamba wadau wote ambao wanashiriki katika mnyororo mzima wa thamani ya korosho wananufaika. Na kwa hali hiyo basi, niseme tu kwamba baada ya kuona manufaa makubwa ya mfumo huu, lakini pia baada ya kupata changamoto kwa wadau wengine kama ambavyo unavyoeleza. Serikali itakaa pamoja na wadau kuangalia namna bora zaidi ya kuhakikisha kwamba hivi viwanda vidogo navyo vinafanya shughuli zake bila kuathirika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masala atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Katika moja ya masharti ya mkataba uliosainiwa kati ya Kampuni ya *Sunshine* na wamiliki wa ghala la *Lindi Pharmacy* ambayo kilikuwa Kiwanda cha Korosho Wilayani Nachingwea ilikuwa ni kuanza kufanya kazi Septemba, 2017. Lakini mpaka sasa ninapozungumza kiwanda kile hakijaanza kufanya kazi, naomba kupata majibu ya Serikali juu hatma ya kiwanda cha korosho Nachingwea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya nini hatma ya kiwanda hicho.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia na niseme tu kwamba lengo letu ni kuhakikisha kwamba Mikataba inayokuwa imeingiwa inafanya kazi yake inavyostahili. Lakini kwa sababu suala hili limekuwa ni *very specific* kwa Kiwanda cha *Sunshine* na mimi maishani mwangu sipendi kutoa majibu ya kukurupuka au ya uongo, nitalifanyia kazi na nitakuletea taarifa inayostahili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia swali la mwisho.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante viwanda vyote ambavyo vilibinafsishwa kwa maana viendelee kubangua korosho sasa hivi vimegeuka maghala tofauti na mikataba iliyoingiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juhudi gani Serikali hasa Wizara ya Viwanda na Biashara inasimamia kuhakikisha kwamba vinaendelea kuwa viwanda na sio maghala ya korosho kwa sababu vibali vya kufanya maghala vinatolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Lini wataacha kuwapa vibali ya kufanya maghala na wafanye viwanda?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri mwenyewe Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji lini mtaacha kutoa vibali?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Ghasia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juhudi gani, kama swali la msingi ilivyoelezwa Kiwanda hiki cha Masasi kimekwama kwa sababu ya shauri lililopo mahakamani. Lakini katika mfumo huo kuna viwanda vingine vipo mahakamani, katika sekta ya korosho ninavyo viwanda ambavyo nimehakikisha mwenyewe wamiliki wake wameshaanza kutengeneza mipango ya kuviendeleza ikiwemo kuleta mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitambo nimeiona mwenyewe kuanzia hivi vya Kibaha mpaka vya Liwale *one,* kwa hiyo juhudi zinafanyika kuendelea kuwafuatilia hawa wawekezaji ili waweze kuvirudisha katika njia ya kufanya kazi viwanda hivi, ikiwa ni pamoja na kutafuta mitaji, kwa hiyo, juhudi hizi za kuhakikisha vinafanya kazi tutahakikisha zinaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi na linaulizwa kwa Waziri wa Nishati.

Na. 51

**Uchimbaji wa Mafuta na Gesi katika Vijiji vya Kipenyo na Mtimbira**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* iliingia mkataba wa utafiti wa uchimbaji wa gesi na mafuta na Kampuni ya Mafuta ya Swala *(SOGTP).* Katika utekelezaji wa mpango huo wamegundua kuwepo kwa wingi mafuta ya petroli na gesi katika vijiji vya Kipenyo na Mtimbira Wilayani Malinyi katika Mkoa wa Morogoro.

(a) Je, ni lini uchimbaji wa visima na uvunaji wa mafuta utaanza rasmi katika maeneo hayo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatayarishia wananchi wa maeneo hayo ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza baina yao na Serikali kama vile gesi ya Mtwara?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mafuta katika kitalu cha Kilosa – Kilombero unafanywa na Kampuni ya *Swala Oil Gas Tanzania* ulianza mwezi Februari, 2012. Utafiti huo ulianza baada ya kusainiwa kwa Mkataba wautafutaji kati ya Serikali kupitia *TPDC* na Swala mwezi Februari, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo limeainishwa kwa ajili ya uchimbaji wa kisima hicho lipo katika Kijiji cha Ipera Asilia katika Hifadhi Tengefu ya Bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisima hicho kinatarajiwa kuanza kuchimbwa mwezi Septemba, 2018 kutegemea matokeo ya utafiti huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TPDC* imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi wa maeneo kunakofanyika utafiti huo. Tarehe 06 hadi 17 Februari, 2017 *TPDC* kwa kushirikiana na Kampuni ya Swala ilitoa elimu ya masuala ya gesi na mafuta katika maeneo ya Halmashauri ya Mji huo ikiwa Mji Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Wilaya za Kilombero pamoja na Malinyi. Aidha, wananchi wa Kata ya Mtimbira, Njiwa pamoja na Kitete katika maeneo vijiji vya Mtimbira, Kipenyo, Ipera Asilia na Warama pia walipata elimu ya hifadhi ya mazingira pamoja na manufaa ya mradi huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mponda maswali.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na vilevile naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na dhamira yao ya dhati kabisa kufanya mradi huo ukamilike. Nina maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, uchimbaji wa kisima cha mradi huu,ulipangwa kufanyika mwaka 2016 na tafiti zilifanyika ikabainika kuna mafuta ya kutosha kupata mafuta ya kuendesha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kwa utaratibu ambao wameuwekeza ukiritimba umezidi mno

umesababisha mpaka sasa hivi mkataba kati ya mwekezaji kampuni ya Swala ya Kitanzania na *TPDC* bado haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni lini sasa mtakamilisha mkataba huu ili mradi huo wa uchimbaji wa haya mafuta uanze kwa sababu haraka haraka tu pale itaajiri wananchi karibuni 500 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nakubali mmetoa elimu lakini mafundisho tuliyopata Mtwara mnaelekea huko huko, elimu mnayo toa mnafanya visemina na mikutano, watu wachache sana wanahusishwa, eneo lengwa tarafa nzima ya Mtimbira lina wakazi karibu 75,000, hizo semina sijui mtaendeshaje nawashauri na baadaye nauliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumieni *media*, tumieni vyombo vya habari ambavyo vitaweza kusambaza taarifa na habari haraka sana kuliko hizo semina mnazofanya. Katika maeneo yetu kuna redio za jamii mbili…

**MWENYEKITI:** Swali sasa, swali, swali, swali!

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Nakwenda huko Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Muda Mheshimiwa.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** ...redio FM Ulanga, je, Serikali mpo tayari kutumia redio hizo za jamii ili kuelimisha jamii katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla ya kujibu maswali napenda nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mponda anavyofuatilia utekelezwaji wa mradi huu. Mradi utakapoanza kutelezwa

utaajiri watanzania takribani 200 hadi 300, Kwa hiyo, Mheshimiwa Mponda hongera sana kwa kufuatilia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali lake la kwanza nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba mkataba ulishasainiwa tangu mwezi Februari, 2012 kwa hiyo, kilichobaki ni uekelezaji wa kufanya *drilling* kwa maana ya uchimbaji na ugunduzi wa mafuta, na katika eneo hilo Mheshimiwa Mponda mafuta yanayotarajiwa kuchimbwa katika eneo hilo yanafikia milioni 180 hadi milioni 200. Kwa hiyo, ni mtaji mkubwa na utakuwa na manufaa kwa wananchi wako na watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa uchimbaji utaanza, kama ambavyo nimeleeza kama ambavyo nimeleleza kwenye hilo la msingi kwamba kinachosubiriwa ni kupata kibali cha mazingira kutoka *NEMC* na wenzetu *NEMC* wanalifanyia kazi pamoja na Mamlaka ya *TAWA* yaani Hifadhi ya Mamlaka ya Wanyamapori, wametuhakikishia kwamba kuja kufika mwezi Julai vibali vimepatikana na mwezi Septemba uchimbaji utaanza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili kuhusiana na elimu, kwa kweli niwapongeze sana *TPDC* na Swala wametoa elimu katika mkoa mzima wa Morogoro sasa takribani ya watu 350 wamepewa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumepeleka elimu pia katika vijiji vingi, ikiwemo kijiji cha Mheshimiwa Dkt. Mponda, Ipera, Kipenyo, Mtimbira lakini pamoja na maeneo ya Mnazini pamoja na vijiji vingine anavyovijua Mheshimiwa Mbunge na maeneo mengine ya Kijiji cha Kitete na kata zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, takribani ya wananchi 350 walipata elimu, lakini tutaendelea na kutoa elimu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri. Lakini kuhusu vyombo vya habari tumeshaanza kutumia *TBC* na nimechukua ushauri wake kwamba chombo cha *FM media* cha Ulanga nacho tutazingatia tutakipa kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda siyo rafiki tunaendelea, swali linalofuta linaulizwa na Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini linaelekezwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Na. 52

**Kujenga Mahakama ya Mwanzo Mkomazi**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Miongoni mwa Mahakama za Mwanzo ambazo Serikali iliahidi na kuamua kuzijenga ni pamoja na Mahakama ya Mwanzo Mkomazi.

Je, ni lini Mahakama ya Mwanzo Mkomazi itajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niba ya Waziri wa Katibu na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo ya Mkomazi ni moja ya Mahakama zilizo kwenye mpango wa ukarabati na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo nchini. Hivyo, kwa mujibu wa mpango huo Mahakama ya Mwanzo Mkomazi imepangwa kujengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. STEPHEN HILARY NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza kwa ruksa yako naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kunipa shilingi bilioni moja kwa ajili ya vituo viwili vya Afya, Kata ya Mkumbala na Kituo cha Afya Bungu, Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka 2012 Mahakama hii iliahidiwa kwamba itajengwa, mwaka 2014 iliahidiwa itajengwa, mwaka 2015 iliahidiwa itajengwa, sasa nataka tamko la Serikali mwaka 2020 ni kweli kituo hiki au Mahakama hii ya Mwanzo itajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ilijenga Mahakama ya Mwanzo ya kisasa zaidi pale Magoma katika Tarafa ya Magoma, na nikajitahidi nikakarabati Mahakama moja katika Tarafa ya Bungu, lakini Mahakama hizi mpaka zaidi ya miaka saba hazijafunguliwa.

Sasa naomba Serikali iniambie ni nini sababu zinazuia Mahakama hizi zisifunguliwe wakati wananchi wanapata shida sana kutolewa umbali wa kilometa 30 kwenda kufuata Mahakama sehemu nyingine? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kuanza kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada kubwa anazozifanya katika kuhakikisha kwamba huduma hii ya Mahakama inawafikia wananchi wake kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lakle la kwanza la nyongeza, nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mwaka wa fedha wa mwaka 2019/2020 Mahakama hii ya Mwanzo itajengwa na nimuondolee hofu kwa sababu hivi sasa, kupitia Wizara tunashirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi na Baraza la Nyumba la Taifa na sasa tuna mfumo mzuri wa ujengaji wa Mahakama kutumia teknolojia ya *moladi* ambayo inafanya kazi kukamilika kwa muda mfupi na ukuta kuwa imara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hiyo itafanyika na hivi sasa navyozungumza. Tunayo miradi takribani 39 nchi nzima

ambayo inatekelezwa na kufikia mwaka wa fedha 2018/2019 tutakuwa tumekamisha Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mkoa takribani 70. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni ahadi ya Serikali na jambo hili litatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu Mahakama ya Magoma ambayo tayari ukarabati na ujenzi umefanyika lakini mpaka leo haijafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumuagiza Mtendaji wa Mahakama wa Mkoa wa Tanga kuhakikisha kwamba anafuatilia na kutupatia taarifa na sisi tutakwenda kufuatilia na tutampatia majibu Mheshimiwa Mbunge, lakini nataka nimuahidi tu kwamba kama hakuna vikwazo vingine vyovyote basi tutahakikisha kwamba Mahakama hii inafanya kazi na wananchi wa Tarafa ya Magoma wanapata huduma hii stahiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo linaulizwa kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 53

**Tozo nyingi kwenye Zao la Tumbaku**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Zao la tumbaku lina tozo nyingi ambazo ni mzigo kwa wakulima.

(a) Je, ni lini Serikali itapunguza tozo hizo?

(b) Je, kama itapunguza, itaanza kupunguza tozo ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto mbalimbali katika uzalishaji wa mazao ya biashara nchini ikiwemo zao la tumbaku. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo ada na tozo mbalimbali zinazotozwa kwa wakulima na wadau wengine wanaojishughulisha na mnyororo wa thamani wa zao hilo ambazo zimekuwa na athari katika mapato ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 imefuta, ada na tozo zipatazo 80 kati ya tozo na ada 139 zilizokuwa zinatozwa katika mazao ya kilimo nchini ambazo zilibainika kutokuwa na tija kwa wakulima. Kutokana na maamuzi hayo kwenye tasnia ya tumbaku, jumla ya tozo 10 zilifutwa na tozo mbili zilipunguzwa viwango na tasnia ya kahawa jumla ya tozo 17 zilifutwa na tozo moja ilipunguzwa kiwango, tasnia ya sukari jumla tozo 16 zilifutwa, tasnia ya pamba tozo mbili zilifutwa, tasnia ya korosho tozo mbili zilifutwa, tasnia ya mbegu tozo saba zilifutwa, tasnia ya mbolea tozo tatu zilifutwa na tozo moja ilipunguzwa kiwango. Aidha, tozo 20 zilikuwa zinatozwa na Vyama vya Ushirika katika ngazi mbalimbali nazo zilifutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha ya tozo ambazo zilitamkwa kufutwa katika tasnia ya tumbaku kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2017/2018 ni pamoja na mchango kwa Chama cha Ushirika cha Msingi kiasi cha USD 0.072 kwa kilo na mchango wa Chama cha Ushirika cha Mkoa kiasi cha USD 0.030 kwa kilo.

Hata hivyo, baada ya majadiliano ya wadau katika tasnia ya tumbaku, tozo hizo zilirejeshwa kutokana na umuhimu wake katika kuwezesha usimamizi unaofanywa na Vyama vya Ushirika katika tasnia ya tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mukhtadha huo, ada na tozo zilifutwa katika tasnia ya tumbaku ni pamoja na ada ya fomu ya maombi ya leseni za kununua tumbaku, ada ya leseni ya kununua tumbaku kavu, ada ya leseni ya kuuza tumbaku nje ya nchi, ada ya leseni ya kununua tumbaku mbichi kiwandani, tozo ya leseni ya kununua tumbaku mbichi kwa kila Wilaya, tozo ya Baraza la Tumbaku *(Tobacco Council)* na tozo ya dhamana ya Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya mikopo.

Aidha, mpango wa Serikali ni kuhakikisha tozo na ada mbalimbali ambazo ni kero kwa wakulima wa tumbaku zinafutwa na kubakia zile ambazo zina mahusiano na uendelezaji wa zao husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, kwanza niipongeze Serikali kwa mwaka wa fedha tuliopo kwa kuweza kupunguza hizo tozo 10 ambazo sasa zinaweza kusaidia kwa kiasi fulani wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi tozo zilizopunguzwa tozo tano zinahusiana na makampuni ambayo hayaja washawishi katika kuboresha bei ya ununuzi wa tumbaku, na tukizingatia kwamba wanaendelea kushusha kiwango cha kununua toka tani 60,000 mpaka tani 55,000 na imepelekea wakulima wanazalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na tumbaku ya ziada ambayo ilizalishwa na ikapelekea Serikali kuwa na maongezi na makampuni bei ya dola 1.25 kwa *grade* ya juu. Lakini kwa sasa hivi tunavyozungumza wananunua tumbaku hiyo mpaka senti 64 kwa kilo. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wakulima wa tumbaku wanafaidika katika suala la bei kuliko na matatizo ambayo yametokea mwaka jana na tumbaku imekuwa sasa hivi inanunuliwa kwenye *grade* ambayo iko ya chini kwa kukaa muda mrefu kupata unyevu nyevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali la pili, Chama cha Wakulima wa Tumbaku Mkoa wa Katavi *(RATCO)* kutokana na masawazisho ya bei ya pembejeo ilipelekea kuwa na madeni ya zaidi kudai vyama vingine/mikoa mingine zaidi ya dola 400,000 na ambazo kuna vyama vingine vimekufa na vingine bado viko hai.

Sasa Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa tumbaku wa Mkoa wa Katavi ili waweze kulipwa madeni yao kutokana na masawazisho ya bei ya pembejeo ambayo ilitokana na usafirishaji wa hizo pembejeo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili ya nyongeza na ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbogo kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia sana katika zao zima hili la tumbaku na jinsi wakulima wanavyopata shida katika eneo lake la Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake ya (a) na (b) naomba nijibu; la kwanza naomba niseme tu kwamba kwa upande wa wakulima wa tumbaku zao la tumbaku, kunakuwa na makubaliano ya bei za kuzalisha kila mwaka, kwa mfano sasa hivi tuko katika mwaka wa 2018 unakuta kwamba tangu Septemba, 2017 wakulima hao walikuwa wameshajadiliana ni bei gani watazalisha kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mfano mwaka huu, tayari tutakapokuwa tunazalisha lile zao la tumbaku, tumeshajua ni shilingi ngapi wale wakulima watanunua. Lakini nikija katika swali lake la bei, kuhusu bei ya zao la tumbaku kwa maana amezungumzia dola 1.25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa wakulima wote wa tumbaku kwamba kwanza wazalishe

tumbaku kwa kiwango cha ubora, lakini vilevile ninaomba ntoe siku saba kwa Mrajisi wangu kutokana na lile deni ambalo anasema wananchi wakulima wa Katavi wamekuwa wakiwadai kutokana na mambo ya *WETCO* hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ninachotaka kusema yale siyo madeni, wakulima wa tumbaku wana tabia ya kufidiana na kuchangiana katika zao la tumbaku bila kujali eneo, bila kujali umbali, bila kujali bei. Lakini kwa sababu ya Mheshimiwa Mbunge ameli-*raise* hili na mimi ninampa Mrajisi siku saba awe ameshashughulikia kuhakikisha kwamba wananchi wa Katavi wanapata haki yao ya malipo yao.

**MWENYEKITI:** Asante. Mheshimiwa Haonga, muda mnaangalia muda. Nakupa tu Haonga basi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwaka jana Serikali ilipunguza tozo 17 kutoka kwenye zao la kahawa. Lakini kwa bahati mbaya sana tozo 17 hizi hazimgusi mkulima wa zao la kahawa moja kwa moja na hivyo haijamletea mkulima unafuu hata kidogo.

Je, Serikali sasa iko tayari kupitia upya tozo zile ambazo zitamgusa mkulima moja kwa moja ambazo ni kero na iweze kuzipunguza? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi, kero zinazomgusa moja kwa moja mkulima wa tumbaku.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimezungumzia kwamba Serikali imepunguza au imetoa tozo 80 zaidi ya tozo 139 katika msimu huu wa fedha wa bajeti ya mwaka 2017/2018 zao la kahawa likiwemo. Sisi kama Serikali tunasema zao la kahawa na lenyewe ni mojawapo ya mazao mkakati ya biashara kwa nchi yetu na tumezingatia sana kuhakikisha kwamba tunaendelea kupunguza tozo katika zao la kahawa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Asante tunaendelea na swali letu la mwisho kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud Mbunge wa Viti Maalum linaelekezwa kwa wizara hiyo hiyo ya Kilimo.

Na. 54

**Mahitaji ya Viuwadudu kwa Wakulima wa Pamba**

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukidhi mahitaji ya viuwadudu kwa wakulima wa pamba?

**MWENYEKITI:** Linahusu pamba eeh, sikufahamu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, linahusu pamba. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa viuwadudu katika kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mazao nchini.

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2017/2018 wakulima wameitikia kwa vitendo azma ya Serikali ya kuimarisha kilimo cha pamba nchini kwa kuongeza eneo linalolimwa pamba kutoka wastani wa ekari 1,000,000 hadi wastani wa ekari 3,000,000. Kutokana na mwitikio huo, hadi tarehe 22 Desemba, 2017 jumla ya ekari 1,500,000 zilikuwa zimelimwa na kupandwa zao la pamba na kwa kuhitaji chupa zile (*acrepacks*) 4,500,000 za viuwadudu. Hata hivyo, kwa kuwa mvua zinaendelea kunyesha wakulima wameendelea kuhakikisha kwamba zao hili linafanyika na vilevile suala la viuatilifu linafanikiwa. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nawapongeza Wizara kwa juhudi zao za kuwasaidia wakulima wetu. Pamoja na majibu yaliyojitosheleza suala langu, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wamehamasika sana kulima kilimo cha pamba, nauliza Serikali ni kwa nini haioni umuhimu wa kuanzisha soko huria la uzalishaji wa mbegu bora ili kumrahisishia na kumpa unafuu mkulima wa pamba na kuachia kampuni moja tu ya Quton ambayo inazalisha mbegu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na majibu ya Serikali, pamba imehamasika sana na kwa wastani tani 600,000 itazalishwa na itakuwa sokoni. Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha pamba yote iliyozalishwa inanunuliwa ili kuwaondolea usumbufu wakulima wa pamba?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Khadija Aboud kwa maswali yake mawili ya nyongeza na vilevile kuwa makini katika kufuatilia kilimo ambacho ni mojawapo ya zao la mikakati kilimo cha zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake ya msingi (a)na (b) swali la (a) amezungumzia kuhusu Kampuni ya Quton ambayo ndio imekuwa iki-*dominate* katika kufanya biashara hii ya pamba.

Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Kampuni hii ya Quton ilikuwa imeshinda *tender,* lakini katika kushinda *tender* yenyewe ilikuwa inafanya tu *...ginnery* na kwa maana ya kwamba ilikuwa inafanya mbegu zile za

kunyonyoa tu halafu inapeleka kwa *ginners*. Sasa baada ya Serikali kuona mapungufu hayo ikawa imefuta ile *tender* na ikaamua kuweka soko huria kwa *ginners* ili wao waweze kuwa wanafanya biashara moja kwa moja na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wakulima wote wa zao la pamba ambalo ni zao la kimkakati kwamba kuanzia sasa hivi zao la pamba litakuwa linafanyika katika soko huria bila kujali kwamba ni nani anafanya hiyo biashara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, katika kuitikia wito wa Serikali wananchi wa mikoa ya Mwanza, Simiyu katika majimbo mbalimbali ikiwemo na Jimbo la Bariadi, Misungwi, Sumve pamba imelimwa kwa wingi sana.

Swali langu Mheshimiwa Waziri, endapo wanunuzi wa pamba watashindwa kuinunua pamba yote kwa sababu pamba imelimwa kwa wingi sana msimu huu. Je, Serikali imejipangaje kuwanusuru wakulima hawa ambao wameitikia wito wa Serikali wa kulima Pamba kwa wingi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa kifupi.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali naomba niwaambie wakulima wote wa zao la pamba kwamba tulishakutana na wadau wote wanaolima zao la pamba. Tulishakutana pia na mabenki yote kuhakikisha kwamba pia yale mabenki yanatoa mikopo kwa wafanyabiasha ili waweze pia kutoa mbegu na ukizingatia pia kwamba katika kile Kitalu cha Igunga ambacho kinatoa mbegu bora kabisa ile ya UKM 08 kwamba wakulima wanapata mbegu kwa wingi na vilevile wakulima hao na wafanyabiashara wanapata mikopo kutoka benki ili kuweza kuhakikisha kwamba zao la pamba linazalishwa kwa ufanisi na kwa ubora, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru. Nilikuwa namuomba *Chief Whip* wa Serikali aangalie tu uwezekano katika ukiona haya majibu ya Serikali utaona *improvement* Wizara nyingi yameanza kuwa mafupi lakini hizi kama Wizara tatu unayaona kabisa wangeweza kuyafupisha tu na *messsage* ikafika kwa wananchi. Nifanye sahisho wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omari Kigua alimtaja kama Ndugu au Mheshimiwa Mgumba. Ili tuweke *record* vizuri sahihi aliyekuwa anajibiwa aliyeuliza swali la nyongeza ni Mheshimiwa Omari Kigua.

Sasa nije kwa matangazo ya wageni tulionao kwa siku ya leo. Wageni tulionao waliopo kwenye Jukwaa la Spika ni wageni kumi wa Mheshimiwa Charles Mwijage Mbunge na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambao ni watendaji wa Wizara hiyo wakiongozwa na Profesa Elisante Ole Gabriel, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, karibuni sana, ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni saba wa Mheshimiwa Salum Khamis ambao ni Wanafunzi Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* Tawi la Mwanza wakiongozwa na Rais wa chuo hicho Ndugu Peter Benjamin. Karibuni, ahsanteni sana, karibuni sana. Mwanza ni kwema. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine maalum kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango hawa ni watoto wake, mabinti zake wawili Samira Kachwamba ambaye ni *first born* wake na Nadia Ali Kijaji. Sasa hawa amewaleta Bungeni hapa waone jinsi tunavyofanya kazi, lakini kwa sababu gani wamefanya vizuri sana katika mitihani yao ya kidato cha nne. *(Makofi)*

Kwa hiyo, karibuni sana mama yetu ndio anatusaidia sana Bungeni hapa, mmeona anavyojibu maswali vizuri kabisa. Na ninyi mfuate nyayo zake na muende zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Nakuja kwa matangazo ya waliokuja kwa ajili ya mafunzo, tunao wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Mzumbe kilichopo Mkoani Morogoro. Wako wapi? Wanafunzi, nadhani wapo sehemu nyingine. *(Makofi)*

Tuna wauguzi 46 wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati chini ya Chama cha Wauguzi Tanzania *(Tanzania National Nurses Association – TANNA)* wakiongozwa na Mwenyekiti wao Dkt. Elionora Lyimo. Watakuwa kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Matangazo mengine ya kazi zetu lakini na mambo muhimu. Nianze na la Dkt. Rashid Chuachua, Mbunge wa Masasi anawatangazia Wabunge wanajumuia ya Kiislam kukutana katika Ukumbi wa *dispensary* mpya mara tu baada ya kipindi cha maswali hiki.

Lakini pia na Mheshimiwa Flatei ana mgeni wake kutoka Mbulu ambaye ni Kaka John Harmi, mdau wa maendeleo katika maeneo yetu ya huko Mbulu. *(Makofi)*

Tangazo la semina, Waheshimiwa Wabunge nawatangazia kwamba kesho Jumamosi tarehe 3 Februari kutakuwa na semina kuhusu shughuli zinazofanywa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)*. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa nne asubuhi.

Aidha, semina kwa Wabunge wote kuhusu masuala ya afya ya moyo ambayo ilikuwa ifanyike siku ya Jumapili tarehe 4 Februari sasa itafanyika siku ya Jumatano wiki ijayo tarehe 7 Februari kuanzia saa 7:30 mchana hadi saa 10:30 alasiri. Hilo ndio badiliko ilikuwa ifanyike Jumapili sasa itafanyika Jumatano, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hizo. Hayo ndio matangazo yaliyonifikia hapa kwa leo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taja jina lako.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Amina Mollel.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mussa mbarouk.

**MWENYEKITI:** Polepole mimi siyo *computer.*

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Amesema pole pole.

**MWENYEKITI:** Amina Mollel, Mussa Mbarouk.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MWENYEKITI:** Tumemaliza huku, Dkt. Kikwembe

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Gekul Pauline.

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limekuwa likijitokeza humu Bungeni mara kwa mara na jambo lenyewe ni suala la swali la Mbunge linaposhindwa kujibiwa vizuri, lakini Mbunge mwingine haruhusiwi kuomba Mwongozo kwa sababu tu hilo suala limeulizwa na Mbunge mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia Kanuni sikuona kanuni yoyote ambayo inamzuia Mbunge kuhoji hilo swali. Sasa naomba mwongozo wako kwa sababu Mawaziri wanapojibu maswali naamini wanajibu kwa ajili ya Kitaifa kwa ajili ya kila Mbunge na sio kwa Mbunge Pauline tu najibiwa. Kama ni suala la mazao ni kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limejitokeza siku ya leo wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida kwamba hakuna Watanzania

ambao wameingia kwenye dimbwi la umaskini kwa mazao yao kwa Serikali kukosesha mazao yao soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu ya Serikali nafikiri siyo sahihi kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Manyara ambao wanalima mbaazi mpaka leo wameshindwa kuingia mashambani kulima kwa sababu mbaazi zao hawajazivuna na wameshindwa kukodi matrekta kwa ajili ya kulima kwa msimu huu, wameshindwa kupeleka watoto wao shule kwa sababu hakuna soko la zao la mbaazi. Halafu Serikali inajibu inasema hakuna Mtanzania aliyeingia kwenye dimbwi la umaskini.

Naomba Mwongozo wako ni kwa nini Serikali inatoa majibu ya uongo kiasi hiki kwa Wabunge wakati wananchi wetu mpaka leo hawajui hatma yao? Naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa namna ambavyo Waheshimiwa mara nyingi ni jambo ambalo limekuwa likijitokeza toka nimeingia humu Bungeni ambapo inakuwa Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa wanauliza maswali wanaopata nafasi za kuuliza maswali na kupata majibu baada ya majibu ya nyongeza, maswali ya pili wamekuwa akiomba kwamba tunaomba tuongozane na Mheshimiwa Waziri Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako nitake kujua wajibu wa Mawaziri, je, ni kuombwa na Wabunge kwenda kuzungukia majimbo ama ni wajibu wao kuzunguka nchi nzima kujua masuala na matatizo ya wananchi. Imekuwa ikijitokeza hata Waheshimiwa Mawaziri wanapokwenda majimboni ama mikoani kutembelea ziara zao wamekuwa ni wageni wa Wakuu wa Mikoa na ma-*DC* na Wakurugenzi na si wageni wa... na hata Mbunge ukiwa Jimboni wamekuwa wakipita na misululu ya magari na

wananchi wakiwaona badala ya kusimama na kujibu hoja na kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Mheshimiwa wangu namheshimu sana Mheshimiwa Kalemani, amepita kutoka Inyonga, akapita Kavuu saa mbili usiku sawa sikatai, ndivyo alivyopangiwa na Serikali, lakini wakumbuke wao ni Wabunge na wamechaguliwa na wananchi na wananchi na wanaenda kusikiliza kero za wananchi, hawaendi kumsikiliza Mkuu wa Mkoa wala *DC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mwongozo wako, kwa nini wanapokuja kule wasije moja kwa moja. Hili hajalifanya Mheshimiwa Kalemani tu, amelifanya Mheshimiwa Mpina na karibu Waheshimiwa wote kwa kweli na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, alikuja Jimboni kwangu akakagua mradi wa zahanati baada ya kuitwa na Mheshimiwa Mstaafu Waziri Mizengo Pinda alipokuwa mapumzikoni nyumbani kwake, mimi nikiwa Jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wa kazi na wajibu wa Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, nimesimama kwa kanuni ya 68(7) kwa kuokoa muda sitoisoma lakini niongezee alipomaliza dada yangu kwa sababu yanafanana kidogo. Nipo hivi Waheshimiwa Mawaziri wanajitahidi sana kujibu maswali hapa, lakini kwa hilo wanalosema kwamba tukimaliza Bunge hili tuongozane, sasa Bunge likiisha unapopiga simu Waziri hapokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kitu kimoja, Mawaziri wetu kabla Bunge hili halijakwisha, kila Waziri hapa atoe orodha yake kwamba ataongozana na Mbunge yupi wa mwanzo mpaka wa mwisho. Hii ni kwa sababu imekuwa sasa wanatudanganya. Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako katika hilo, Mawaziri watayarishe orodha za ziara zao kwa

Mbunge wa mwanzo mpaka wa mwisho atakayeongozana nae, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel Amina.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kupata Mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ramo Matala Makani kuhusiana na ni mazao gani ambayo yameongeza au yanaongeza pato la Taifa, korosho ilikuwa ni mojawapo ya zao ambalo linaongeza pato la Taifa. Hivi karibuni kumekuwepo na taarifa kwamba korosho ya Tanzania imegundulika kuwa na mawe/mchanga na kama inavyofahamika ni kwamba ubora wa korosho ya Tanzania ni mzuri na ndio maana pengine ikawa chanzo cha kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wangu ni kwamba kama taarifa hizi ni za kweli basi wahusika ni dhahiri kabisa kwamba wanaihujumu nchi.

Mimi nilikuwa naomba mwongozo wako kwa sababu kama ilivyojionesha kwamba korosho inaongeza pato la Taifa kwa nchi hii na kama kweli, na tumeshuhudia katika vyombo vya habari, baadhi ya vifurushi vya michanga ambavyo vimegundulika katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kauli ya Serikali kwamba ni hatua gani zimechukuliwa ili kubaini kama ni kweli korosho yetu imegundulika kuwa na mawe au mchanga. Na kwa sababu kama ni kweli ni uhujumu uchumi, ni hatua gani wahusika watachukuliwa na ikiwa ni pamoja na kupitia kuangalia mazao mengine ambayo tumekuwa tukiyauza na yanaingiza pato kwa Taifa ili basi tusije kupatikana na kasoro hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yako naomba majibu ya Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khenani Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kipindi nauliza swali langu la nyongeza namba 47, Naibu Waziri wa Fedha amejibu tena akasema tena najibu kwa herufi kubwa kwamba suala hilo ni la uongo juu wananchi kupata umaskini kwa kutopata soko la uhakika juu ya mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa, bei ya sasa ya gunia la mahindi ni shilingi 27,000 na wateja hakuna na wakati huo wamenunua pembejeo kwa bei kubwa. Yeye anasimama hapa anatoa majibu ya Serikali, wananchi hawa ambao wanatakiwa leo waendelee na kilimo kingine wameshindwa kununua pembejeo kwa sababu gunia leo ni shilingi 27,000. Leo majibu ya Serikali yanasema ni uongo tena anasema kwa herufi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mwongozo wako, kati ya mimi na yeye nani ni muongo na kama yeye ndio muongo aombe radhi kwa sababu wananchi walikuwa wanamsikiliza na mpaka sasa wana hali mbali. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, nasimama kwa kanuni ya 68(7) kuhusiana na jambo lililotokea hapa Bungeni leo, naomba Mwongozo wako suala hili linahusiana na usalama hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi viti tunavyokalia vingi ni vibovu na vingine licha ya kwamba vinatatuka lakini vingine vinang'oka, hivi ninavyoongea pale nyuma anapokaa Mheshimiwa Obama hakuna kiti, hicho kiti nimebinuka nacho mimi, kama ingekuwa sio mazoezi labda sasa hivi kisogo changu sijui ningekuwa naongeaje au namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale sasa hivi kiti kimoja kipo chini na nimeanguka nacho mimi. Sasa sijui naomba Mwongozo wako, hivi viti vinafanyiwa matengenezo wakati gani hasa kwa kuangalia usalama wa Wabunge, wengine ni watu wazima humu wakiteguka nyonga sijui itakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maombi yenu ya Miongozo/Mwongozo. Nianze na Mheshimiwa Gekul, nirudie niliyosema majuzi; uamuzi wa Spika ukishatolewa unatufunga sote na kama Mbunge haridhiki na uamuzi huo, taratibu zipo na kanuni zinaruhusu. Kanuni ya 5(4) inakuruhusu wewe kuwasilisha malalamiko ili suala hilo liangaliwe maana ni la kikanuni. Lakini sisi hatuwezi tukasimama hapa na kuanza kuhoji maamuzi yaliyochukuliwa na Spika kutuongoza humu.

Waheshimiwa Wabunge, anayeweza akasema jibu lililotolewa na Serikali kwa swali la msingi au la nyongeza halikufikia kiwango alichotegemea, hakuridhika nalo, yeye ndio anayeruhusiwa sasa kuyasemea. Wengine ambao tumepata bahati kuuliza maswali ya nyongeza Mwongozo umeshatolewa hatuwezi kulalamikia unapopata majibu ambayo wewe hukuridhika nayo, lakini aliyeuliza yeye karidhika. Nadhani tuelewane katika hilo na litakuwa limekaa vizuri tu. Lakini kwa yale ambayo yanagusa hali halisi ya wananchi, hii Serikali ipo inayachukua haya na wataona namna ya kuyashughulikia.

Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, je, Waziri anaweza akaongozana na mimi baada ya kikao hiki? Ukiniuliza kama kanuni zinakataza, kanuni hazikatazi, ni ombi analitoa humu Bungeni na sote tumo humu Bungeni kwa kutegemea nafasi sasa ya huyu anayeombwa na mara nyingi huwa wanasema Serikali tukimaliza shughuli za Bunge sisi tutakuwa na wewe *site.*

Lakini nilivyomuelewa Mheshimiwa Kikwembe amekwenda mbali zaidi, kwamba hivi Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri hayo sio majukumu yao, lazima wakaribishwe? Maana wao majukumu yao ni kutembea nchi nzima kuona hali halisi ya utekelezaji wa Ilani ya CCM katika maeneo tunakotoka.

Sasa hilo sote tunajua ndio jukumu lao la msingi, wanapopata nafasi kwa ratiba zao ndio wanapaswa wayafanye hayo basi sio *by invitation*, sio kwa kukaribishwa. Inapotokea kwamba kuna ahadi ilitolewa Bungeni na aliyeomba akakubali nadhani itakuwa sio uungwana ulitoa ahadi yako Bungeni na nikaamini mimi kama Mbunge kwamba tutakupokea uje halafu usionekane. Sasa hayo ni ya kwetu.

Nadhani yale ambayo yanaweza yakaumiza baadhi yetu ni pale ambapo Mbunge wa Jimbo wewe unakwenda kwenye Jimbo hilo hata kama ulikaribishwa na mwingine bila hata kuwajulisha. Mimi nadhani Serikali ikiweka utaratibu mzuri katika hili wala hakuna tatizo. Hii ni kwasababu Mbunge wa eneo hilo na yeye atambulike apewe heshima yake kwamba yeye ndio yupo pale. Sasa yale mengine ni ya ziada tu, mimi nadhani huo ndio mwongozo wangu kwa hilo. Mheshimiwa Mbarouk aliingizia hapo hapo lakini yote ni heri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amina Mollel, ndio yale majibu aliyopewa Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani na Naibu Waziri wa Fedha, yamejitosheleza kwa maana ya alivyouliza. Sasa kama nilivyokuelewa wewe huu mtindo wa kutaka kuongeza *speed governor* ujipatie pesa nyingi, kuweka mawe/mchanga kwenye zao la korosho zinazouzwa nje au kwenye zao lolote ambalo tunauza nje, mimi nadhani Serikali kama limetokea wanaweza wakalisemea hili. Nadhani ndio alikuwa anaelekea huko, lisemewe maana lina athari kubwa sana kwa *export* zetu. Limetuumiza kwenye pamba tulipojidai ujanja huo kwamba tunaibiwa sana kwenye mizani ile na sisi tukasema tutawafanyia ujanja huo tukawa tunaongeza maji na mchanga mle ndani, lakini inapoenda nje ndio

maeneo mengi yalikataa kupokea pamba kutoka Tanzania kwa sababu ya michezo hiyo. Sasa Serikali itasema kama kweli kwenye zao la korosho tumeanza mchezo mbaya huu, nadhani ni hatarisho. Yawezekana labda linafanywa kusudi kutuharibia soko lazima Serikali mlione hilo, huo ndio Mwongozo wangu, naiachia Serikali watalisemea.

Mheshimiwa Aida, majibu yangu ni hayo hayo, kama wewe hukuridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe uliza swali lako tu kwenye eneo hilo *specific question* ambayo ita-*deal* na hali ya umaskini wa Watanzania kama unavyoiona wewe, utajibiwa vizuri tu.

Sasa Mheshimiwa Emanuel, nadhani tulichukue hili na jirani yangu ninayekaa naye pale kiti chake mara nyingi amesema sana, sasa wewe umepata tukio limetokea humu Bungeni bahati nzuri tu wewe mwana-*sport* umejua namna ya kujikinga usifike chini. Lakini ukweli ni kwamba tulichukue hili tuone Katibu wa Bunge anaweza kufanya nini kwa hali hii iliyopo. Sote tunajua itategemea na hali halisi ya fedha lakini usalama wetu ni muhimu sana sana kwa suala hili.

Mimi nadhani ndio hayo niliyoombwa niyatolee mwongozo, yeah! Nimemamaliza ni hayo. Baada ya kusema, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017**

**MWENYEKITI**: Ahsante taarifa hizi zitawasilishwa moja baada ya nyingine, mara baada ya pale ndiyo tutazichangia. Tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba taarifa yote iingie kwenye *Hansard* kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Bajeti na kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kuanzia mwezi Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka kuhusu masuala mbalimbali yaliyotekelezwa na Kamati katika kipindi husika. Aidha, kupitia taarifa hii nitaeleza kuhusu uchambuzi wa hali ya uchumi na utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Desemba, 2017 na mwelekeo hadi Juni 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Bunge lako Tukufu, kwa mara ya kwanza Kamati ya Bajeti inawasilisha taarifa ya mwaka ambayo pia imebeba maudhui ya uchambuzi wa taarifa iliyowasilishwa Bungeni jana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ni utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 56 cha Sheria ya Bajeti ambacho pamoja na kutoa fursa kwa Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha taarifa husika kinaipa Bunge mamlaka ya kujadili taarifa hiyo. Hivyo Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kujadili Taarifa hii pamoja na Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango iliyowasilishwa jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii pia kuwapongeza wajumbe watatu kutoka Kamati hii, kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kushika wadhifa wa Naibu Waziri katika Wizara mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe hao ni Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ambaye alikuwa pia Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na ameteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa niaba ya Kamati napenda kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2017, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015 kama ilivyorejewa mwaka 2017, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Sera za Kodi, Sheria za Fedha pamoja na sheria nyingine, taratibu na miongozo mbalimbali iliyopo inayohusiana na masuala ya fedha, kodi na bajeti katika kutekeleza shughuli hizo. Kamati ilikutana na Serikali, taasisi, mashirika, sekta binafsi pamoja na wadau wengine ili kupokea taarifa mbalimbali ambazo Kamati ilizitumia wakati wa kutekeleza majukumu yake na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zifuatazo ni kazi zilizotekelezwa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2017:-

(a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017.

(b) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2016/2017.

(c) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya

Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Bunge.

(d) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo visivyo vya kodi.

(e) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

(f) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2017.

(g) Kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao.

(h) Kupitia na kujadili kuhusu mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na hatimaye kutoa maoni na ushauri wake.

(i) Kufanya uchambuzi kuhusu sera za kodi, sera za kifedha na sera za kiuhasibu zinazopendekezwa na Serikali.

(j) Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti.

(k) Kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge.

(l) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ingependa kuwatambua wadau wa masuala ya bajeti na uchumi

ambao wameshirikiana na Kamati kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake kwenye kipindi husika: -

(a) Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Benki Kuu ya Tanzania *(BOT),* Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(NAOT),* Ofisi ya Msajili wa Hazina *(Treasury Register),* Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana *(CMSA).*

(b) Sekta Binafsi, chini ya umoja wao wa *Tanzania Private Sector Foundation* ambao Kamati ilikutana nao mara kadhaa kupata maoni yao kuhusu hatua na utekelezaji wa kodi nchini.

(c) Shirikisho la Watoa Huduma za Utalii nchini ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia Sekta ya Utalii.

(d) Umoja wa Watoa Huduma za Simu nchini ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta ya mawasiliano.

(e) Umoja wa Wenye Mabenki nchini ambao walijadiliana na Kamati kuhusu masuala kadhaa ya kibenki na namna bora ya Serikali kupata mapato ya Serikali kupitia njia mbalimbali za kibenki.

(f) Umoja wa watoa huduma za Bima nchini ambao walishauriana na Kamati kuhusu uwezekano wa kupanua huduma za bima hususani katika shughuli za bima ya uchimbaji wa gesi na madini.

(g) Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC)* kujadili Taarifa kuhusu masuala ya usimamizi na uwekezaji katika biashara na masuala yanayohusu sera na sheria mbalimbali zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yao.

(h) Asasi ya Kiraia inayojihusisha na masuala ya Deni la Taifa na Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza na

kuwashukuru wadau na taasisi zote zilizoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake mbalimbali. Aidha, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake thabiti wa kufanya majadiliano ya mara kwa mara na sekta binafsi, yenye lengo la kuimarisha uhusiano na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara. Majadiliano hayo yatakuwa na tija endapo yatakuwa na matokeo chanya na yataimarisha sekta binafsi kama *engine* ya ukuaji wa uchumi na kuipatia Serikali mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyojitokeza katika shughuli ambazo nimezieleza za kutekeleza majukumu ya Kamati yote yanapatikana katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi chote ambacho Kamati ilikutana na Serikali na hata katika taarifa zake ambazo Kamati imeziwasilisha katika Bunge lako Tukufu iliendelea kuishauri na kutoa maoni mbalimbali yanayohusu uchumi na bajeti.

Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2017, Kamati ilitoa maoni na mapendekeo kuhusu masuala mengi, baadhi ya masuala hayo ni yafuatayo:-

Kwa Kuwa, Bunge limepewa mamlaka la kujadili na kupitisha utaratibu wa kukusanya mapato ya Serikali kupitia Sheria ya Fedha kila mwaka;

Na Kwa Kuwa, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Sheria ya Fedha iliyotungwa iliruhusu Serikali kurekebisha viwango vya kodi kwa kuongeza, kuondoa ama kusamehe kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali na baadhi ya maeneo kwenye Sheria hiyo, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wake;

Hivyo Basi, Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha inatekeleza Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 kama ilivyopitishwa na Bunge hususan katika maeneo yafuatayo:-

(i) Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348, Serikali ihakikishe mfumo ya kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato

ya Wizara na Taasisi za Serikali unakamilishwa ili makusanyo yote ya Serikali yapitie katika mfumo huo kama sheria inavyoelekeza.

(ii) Sheria ya Kodi ya Majengo Sura ya 289, Serikali ihakikishe inakamilisha mfumo wa *PTMS (Property Tax Management System)* na kuunganisha *Geographical Information System* unaotumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika utambuzi wa majengo na mabango ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi hizo.

Kwa Kuwa Deni la Taifa ni himilivu kwa mujibu wa maelezo ya Serikali na kwamba fedha nyingi zinazokopwa na Serikali ni kwa ajilii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

Na Kwa Kuwa, Serikali haijakamilisha zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni ili kuongeza uwezo zaidi wa Serikali kukopa kutoka katika vyanzo nafuu;

Hivyo Basi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha ukopaji na ulipaji wa deni hilo hauathiri ugharamiaji wa bajeti ya Serikali kwa kila mwaka wa fedha. Pia Serikali ikamilishe zoezi la tathmini ya nchi kukopa na kulipa madeni. Aidha, Serikali iendelee kufanya majadiliano na taasisi, nchi na Benki ya Dunia ambao wanaidai nchi kwa madhumuni ya kupata masharti nafuu katika ulipaji wa Deni la Taifa *(Debt Reprofiling)* kama walivyofanya wenzetu wa Kenya na Malawi. *(Makofi)*

Kwa Kuwa, hivi karibuni sekta ya benki, hasa Benki za Jamii *(Community Banks)* zimekumbwa na msukosuko hasa baada ya benki tatu kuwekwa chini ya uangalizi na benki tano kufungiwa kati ya Benki 12.

Na Kwa Kuwa, moja ya tatizo kubwa liliokumba benki hizo ni usimamizi mbovu wa Bodi za Mabenki hayo;

Hivyo Basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki Kuu kuanzisha Kitengo Maalum chini ya Idara ya Usimamizi wa Mabenki ili kitengo hicho kiwe na jukumu la kuhakikisha

kwamba bodi za mabenki ya jamii zinaendeshwa kwa weledi na ufanisi na kuzisaidia kutoa ushauri wa kitaalamu.

Kwa Kuwa, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018 umeainisha viapumbele mbalimbali ambavyo Serikali imelenga kutekeleza katika kipindi hicho ambavyo ni kukuza uchumi wa viwanda, uendelezaji wa miundombinu, maji, elimu na afya;

Na Kwa Kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mpango huo unahitaji ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara;

Hivyo Basi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka fedha kwa wakati kugharamia miradi hiyo na kushirikisha sekta binafsi katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ili Serikali ibaki na jukumu la kutekeleza miradi ya maendeleo yenye lengo la kutoa huduma zaidi kama vile afya, usambazaji maji na utoaji wa elimu;

Kwa Kuwa, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka haikuainisha utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati;

Na Kwa Kuwa, miradi hiyo ina manufaa makubwa kitaifa kama ujenzi wa reli ya *standard gauge (SGR)*, Mradi wa Makaa ya Mawe ya Linganga na Mchuchuma, ujenzi wa gati Na.13 na Na.14 pamoja na ujenzi wa maeneo maalumu ya mauzo ya nje;

Hivyo Basi, Kamati inaishauri Serikali kusimamia ipasavyo utekelezaji wa miradi hiyo muhimu pamoja na kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo Bungeni na kwa wananchi kwa ujumla.

Kwa Kuwa, Serikali bado inahitaji kuongeza ukusanyaji wa mapato hasa ya ndani kuptia vyanzo mbalimbali;

Na Kwa Kuwa, Bunge kupitia Sheria ya Fedha mwaka

2017/2018 ilifanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 ili kutoa fursa kwa Serikali kuwatambua wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi kwa kuongeza watozwa kodi wapya *(broaden tax base);*

Hivyo Basi, Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali kuhakikisha inaongeza kasi katika zoezi la urasimishaji wa biashara na shughuli ndogondogo za kiuchumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mapato na kudhibiti mapato hayo;

Kwa Kuwa, mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ni muhimu katika kuimarisha sekta binafsi ya ndani na kuvutia uwekezaji kutoka nje na hata ndani, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali;

Na Kwa Kuwa, Kamati imefurahishwa na muongozo uliotolewa na TAMISEMI kwa ajili ya kuboresha utoaji wa vibali vya ujenzi katika Halmashauri na Wizara ya Ardhi kwa kuanzisha mfumo wa kielectroniki wa utoaji wa hati na hivyo kuondoa zile kero ambazo zilikuwa zinagusa katika maeneo hayo;

Hivyo Basi, Kamati inazitaka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuandaa mkakati madhubuti wa kutanzua vikwazo vinavyoathiri mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara. Mikakati hiyo izingatie fursa zilizopo mfano matumizi ya eneo la kijiografia na wingi wa rasilimali zilizopo. Hatua hii itasaidia kukuza uchumi haraka, kuongeza ajira, kupanua wigo wa mapato na kuondoa umaskini.

Kwa Kuwa, mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilihamisha ukusanyaji wa kodi ya majengo kutoka Serikali za Mitaa na kupeleka Serikali Kuu *(TRA)* kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji;

Na Kwa Kuwa, Kamati ilikubaliana na pendekezo hili kwa makubaliano kwamba chanzo hiki cha mapato ni cha Serikali za Mitaa na fedha zitarejeshwa kwa ajili ya

kugharamia miradi ya maendeleo iliyopangwa. Hata hivyo, utaratibu ulivyo hivi sasa unazitaka Halmashauri kuwasilisha mahitaji yao Hazina ndipo warejeshewe fedha hizo kulingana na mahitaji.

Hivyo Basi, Kamati imeona kuwa utaratibu huu unaleta ugumu kwa Halmashauri kutofautisha fedha zinazotokana na kodi ya majengo na ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hivyo, Kamati inapendekeza Serikali itafute utaratibu rahisi wa kuzirejesha fedha hizo Halmashauri ili zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Kwa kuwa, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka, miongoni mwa mafungu yaliyoombewa fedha nje ya Bajeti ni Bodi ya Korosho kiasi cha shilingi bilioni 10;

Na Kwa Kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Korosho Namba 203, *(The Cashewnut Industry Act, (Cap.203))* Kifungu cha 17A (1)(a) na (b) vimeainisha kwamba asilimia 35 ya makusanyo ya ushuru wa masafirisho ya korosho ghafi nje ya nchi, yatapelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na asilimia 65 itapelekwa Bodi ya Korosho kwa ajili ya kuendeleza tasnia hiyo;

Hivyo Basi, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuweka kifungu *(sub-vote)* kitakachokuwa kinapokea na kugawa fedha kwenye Bodi za Mazao mbalimbali ya uendelezaji wa mazao ya biashara ikiwemo Bodi ya Korosho. Hata hivyo, katika msimu wa mwaka wa 2016/2017 Bodi ya Korosho bado haijapokea kiasi cha shilingi bilioni 88.9 kama sheria inavyotaka kutoka katika makusanyo ya ushuru wa mauzo ya zao hilo nje.

Kwa Kuwa, Tanzania ina fursa katika sekta ya kilimo ambayo bado haijaweza kutumika vizuri kuongeza mauzo nje;

Na Kwa Kuwa, zao la korosho limekuwa ni la mfano mzuri katika kuongeza mauzo nje ya nchi;

Hivyo Basi, Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kuziwezesha Bodi za Mazao mbalimbali kama vile korosho, chai, pareto, pamba, ngozi na kahawa ili ziweze kuweka mazingira wezeshi katika uendelezaji wa mazao hayo. Mfano ujenzi wa maghala, ununuzi wa pembejeo na viuatilifu, utafiti, usambazaji wa miche bora, usimamizi wa masoko na utoaji wa elimu kwa wakulima, endapo Serikali itasaidia katika hili tunauhakika kabisa Sekta ya Kilimo itaongeza mchango wake katika Pato la Taifa na vinginevyo vilevile tusipofanya tutaangamiza mazao haya. *(Makofi)*

Kwa Kuwa, marekebisho ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 yaliyofanywa, yameitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai Mosi hadi Desemba 31 na mwelekeo hadi Juni. Lengo ilikuwa ni kuipa Serikali muda wa kutosha kuandaa taarifa hiyo kwa ufasaha na kwa kuzingatia ujumuishaji wa takwimu zote muhimu;

Na Kwa Kuwa, taarifa iliyowasilishwa na Serikali imetoa takwimu zinazotofautiana vipindi ambapo baadhi ni za mwezi Julai – Septemba na nyingine ni za Julai – Desemba;

Hivyo Basi, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa takwimu kwa kipindi kimoja cha nusu mwaka ili kuliwezesha Bunge kuishauri Serikali katika nyanja za ukusanyaji wa mapato, viashiria vya uchumi, mwenendo wa matumizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kukushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wenzako, kwa namna mnavyoliongoza Bunge hili kwa umahiri na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa kuchambua na kujibu hoja mbalimbali kwa Kamati.

Vilevile, nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi mbalimbali za fedha ambao wameshirikiana na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa uhai wa Kamati utaishia mara baada ya Mkutano huu wa Kumi kumalizika na kwa namna ya pekee kabisa napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wa wawaalikwa kwa ushirikiano walionipatia kipindi chote nilichohudumu kama Mwenyekiti wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umakini na umahiri wao ulikuwa na mchango mkubwa katika kuwezesha Kamati kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali ya kuwezesha na kuishauri Serikali kupitia taarifa ambazo Kamati ya Bajeti iliwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru sekretalieti ya kamati inayoongozwa na Ndugu Lina Kitosi na Makatibu Ndugu Michael Kadebe, Godfrey Godwin, Emmanuel Roby, Ndugu Lilian Masabala na Ndugu Maombi Kakozi kwa umahiri wao wa kuihudumia Kamati vema hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI MACHI, 2017 HADI JANUARI, 2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Bajeti, na kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu

za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati kuanzia mwezi Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya mwaka kuhusu masuala mbalimbali yaliyotekelezwa na Kamati katika kipindi husika. Aidha, kupitia Taarifa hii nitaeleza kuhusu uchambuzi wa Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Desemba, 2017 na mwelekeo hadi Juni 2018.

**Mheshimiwa Spika,** tangu kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na Bunge lako Tukufu, kwa mara ya kwanza Kamati ya Bajeti inawasilisha Taarifa ya mwaka ambayo pia imebeba maudhui ya uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa Bungeni jana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hatua hii ni utekelezaji wa matakwa ya Kifungu cha 56 cha Sheria ya Bajeti ambacho pamoja na kutoa fursa kwa Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha Taarifa husika *(compliance report)* kinaipa Bunge mamlaka ya kujadili Taarifa hiyo. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kujadili Taarifa hii pamoja na Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango iliyowasilishwa jana.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kutumia fursa hii pia kuwapongeza Wajumbe Watatu kutoka Kamati hii, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kushika wadhifa wa Naibu Waziri katika Wizara mbalimbali. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Mheshimiwa Japhet Ngalilonga Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa niaba ya Kamati napenda kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2017, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kama ilivyorejewa Mwaka 2017, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Sera za Kodi, Sheria za Fedha pamoja na Sheria nyingine, taratibu na miongozo mbalimbali iliyopo inayohusiana na masuala ya fedha, kodi na Bajeti katika kutekeleza shughuli hizo. Kamati ilikutana na Serikali, Taasisi, Mashirika, Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine ili kupokea Taarifa mbalimbali ambazo Kamati ilizitumia wakati wa kutekeleza majukumu yake na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, zifuatazo ni kazi zilizotekelezwa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2017:-

a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17;

b) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2016/17;

c) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Bunge;

d) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2017/18 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo visivyo vya kodi;

e) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/17; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/18;

f) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2017 (*The Finance Act, 2017*);

g) Kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao;

h) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19 na hatimaye kutoa maoni na ushauri wake;

i) Kufanya uchambuzi kuhusu Sera za kodi, Sera za kifedha na Sera za Kiuhasibu zinazopendekezwa na Serikali;

j) Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;

k) Kutoa ushauri wa jumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge;

l) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2016/17 kwa ajili ya kuishauri Serikali.

## 2.1 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17 NA MAPENDEKEZO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilichambua na kutathmini utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/18.

### i. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muhtasari utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2016/17 unaonesha kuwa Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 29,539.6.** kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 17,798.1** ni mapato ya ndani ambapo **Shilingi bilioni 15,105.1** yalikuwa mapato ya kodi

na **Shilingi bilioni 2,693.01** yalikuwa mapato yasiyo ya kodi. Aidha, Serikali ilipanga kukusanya **Shilingi bilioni 665.4** kutoka katika mapato ya Halmashauri.

Aidha, katika mwaka 2016/17 Wadau wa Maendeleo waliahidi kutoa misaada na mikopo yenye jumla ya **Shilingi bilioni 5,701.7,** kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3,600.8** ilikuwa ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti na **Shilingi bilioni 2,100.9** ilikuwa ni mikopo yenye masharti ya kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 Serikali ilikusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 20,710.5** sawa na **asilimia 70.1** ya lengo la mwaka la **Shilingi bilioni 29,539.6.** Kati ya fedha hizo mapato ya kodi yalikuwa ni **Shilingi bilioni 11,644.6** sawa na **asilimia 77.1** ya lengo. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia **Shilingi bilioni 1,611.0** sawa na **asilimia 59.8** ya lengo. Mapato ya Serikali za Mitaa yalikuwa **Shilingi bilioni 399.3** sawa na **asilimia 60** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Aprili, 2017 kiasi cha Shilingi **bilioni 2,340.1** kilikuwa kimepokelewa sawa na **asilimia 65** ya ahadi ambayo ni **Shilingi bilioni 3,600.8** za washirika wa maendeleo**.** Mwenendo wa utoaji fedha za washirika wa maendeleo unaonyesha ni pungufu kwa **asilimia 35** ya fedha yote iliyotarajiwa kutolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipanga kupata Mikopo kutoka katika vyanzo vya ndani kiasi cha Shilingi **bilioni 5,374.3.** Hadi kufikia mwezi Juni 2017, Serikali ilikuwa imekopa mikopo ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 4,715.6.** Hii ni sawa na **asilimia 87.7** ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa mwaka 2016/17. Kiasi hiki **kimepungua** kwa **asilimia 12.3** chini ya kile kilichotarajiwa kukopwa na Serikali kutoka kwenye vyanzo vya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mwenendo wa matumizi ya Serikali, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017, Serikali ilitoa mgao wa matumizi wenye thamani ya **Shilingi bilioni 20,036** sawa na asilimia 67.83 ya bajeti ya mwaka kwenda kwenye mafungu mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 4,555.5** kwa ajili ya miradi ya maendeleo (sawa na **asilimia 38.5** ya lengo la **Shilingi bilioni 11,820.5** zilizotengwa kwa ajili ya bajeti yote ya mwaka ya Maendeleo). Kamati ilibaini kuwa moja ya sababu ambazo zilisababisha Serikali kushindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo kwa kiwango kilichokusudiwa ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kutosha hasa kutoka kwa wahisani na wafadhili wa nje.

ii. **Mapitio ya Mwenendo wa ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2016/17**

**Mheshimiwa Spika**, uchumi umeendelea kuimarika ambapo Pato la Taifa lilifikia kiwango cha **asilimia 7.0** kwa mwaka 2016 kama ilivyokuwa mwaka 2015. Hata hivyo, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017 (Januari – Juni), Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 6.8** ikilinganishwa na asilimia 7.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za habari na mawasiliano **asilimia 13.0,** usafirishaji na uhifadhi wa mizigo **asilimia 11.8,** uchimbaji madini na mawe **asilimia 11.5** na uzalishaji viwandani **asilimia 7.8.** Aidha, Sekta ya Kilimo ambayo inaajiri zaidi ya **asilimia 70** ya Watanzania ukuaji wake umekuwa sio wa kuridhisha ambapo imekua kwa **asilimia 2.1** tu ikilinganishwa na maoteo ya **asilimia 2.9** kwa mwaka husika, ukuaji huu ni mdogo hivyo kuchangia kiasi kidogo katika pato la Taifa ukilinganisha na **asilimia 3.4** mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa mfumuko wa bei unaonyesha kwamba wastani wa mfumuko huo katika mwaka 2016 umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja. Wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2016 ulipungua hadi kufikia **asilimia 5.2** ikilinganishwa na **asilimia 5.6** mwaka 2015. Katika kipindi cha Januari hadi Aprili 2017, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa **asilimia 6.4** ikilinganishwa na **asilimia 5.6** katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Mwezi Julai hadi December 2017, mfumuko wa

bei ulikuwa asilimia kwa wastani wa **asilimia 4.8** kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

iii. **Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18.**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako Tukufu kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 liliidhinisha tozo, kodi na ada mbalimbali zenye lengo la kuongeza au kupunguza viwango vya kodi kwenye maeneo mbalimbali. Aidha, kupitia Sheria hiyo misamaha ya kodi ilipunguzwa, kuondolewa na kusamehe kwenye baadhi ya maeneo kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza ukusanyaji wa mapato. Hatua hizo zililenga kuongeza mapato kutoka **Shilingi bilioni 29,539.6** kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi Shilingi **bilioni 31,711.9** kwa mwaka wa fedha 2017/18 sawa na ongezeko la asilimia 7. Kati ya Shilingi bilioni 31,711.9 zilizotengwa katika Bajeti ya mwaka 2017/18, kiasi cha **Shilingi bilioni 19,712.3** sawa na **asilimia 62** ya Bajeti ni kwa ajili ya **Matumizi ya Kawaida** na **Shilingi bilioni 11,999.5** sawa na **asilimia 38** ya Bajeti yote ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

## 2.2 HOJA ZA KAMATI ZA BUNGE ZA KISEKTA ZENYE MASLAHI YA KITAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea hoja mbalimbali zenye maslahi ya kitaifa ambazo zilibainishwa na Kamati za Bunge za Kisekta zilipokuwa zikichambua na kupitia utekelezaji wa Bajeti za Wizara wanazosimamia kwa mwaka wa fedha 2016/17 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea jumla ya hoja arobaini na mbili (42) kutoka kwenye Kamati za Bunge za Kisekta. Kati ya hoja hizo, hoja shirini na moja (21) zilihusu maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17 na fedha za matumizi ya kawaida ambazo zilikuwa hazijatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja nyingine **21** zilihusu maombi ya nyongeza ya fedha kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka

wa fedha 2017/18 ambapo maombi yenye jumla ya kiasi cha **Shilingi bilioni 86.22** yaliwasilishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 46.64** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Shilingi bilioni 39.58** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Kamati ya Bajeti ilipokea **Hoja Tano (5)** zilizojitokeza Bungeni wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hoja hizo ni zifuatazo;

i. Kampuni ya Simu ya TTCL kuongezewa mtaji ili iweze kujiendesha kibiashara na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

ii. Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kujenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam-Tanga-Moshi-Arusha –Musoma.

iii. Kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira;

iv. Kufanya tathmini ya gharama za ujenzi wa vituo vya afya na zahanati nchi nzima ili ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya na zahanati ufanyike katika mwaka wa fedha 2017/18.

v. Kuongeza Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kuongeza tozo ya Shilingi 50/= kwa Lita 1 kwenye bei ya Mafuta (Petroli na Dizeli) kwa ajili ya kuboresha zaidi Mfuko wa Maji. Kiasi kitakachopatikana asilimia 70 ya mapato itumike kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 30 ya makusanyo yatumike kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji mjini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 105 (1) Kamati ya Bajeti ilifanya kikao cha pamoja na Kamati ya Uongozi na Serikali kwa lengo la kufanya mashauriano kuhusu hoja hizo. Katika kikao hicho, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilisha Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati.

## 2.3 MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 94 Bunge lilijadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2017/18 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Kamati ilipata fursa ya kufanya tathimini ya Utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17, kuchambua na baadaye kutoa maoni na mapendekezo kuhusu mpango wa 2017/18 kupitia Taarifa ya Kamati iliyowasiilishwa Bungeni. Hatimaye Bunge lilitoa maoni na mapendekezo na kuidhinisha mapendekezo ya Mpango huo.

## 2.4 MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2017 (THE FINANCE BILL 2017)

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2017 uliokuwa na lengo la kurekebisha kwa kuongeza, kuondoa ama kusamehe kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Kamati ilipitia na kujadili Muswada huo kwa kupokea maoni kutoka kwa wadau *(Public Hearing)* pamoja na kushauriana na Serikali. Kamati ilikamilisha jukumu hili kwa kuwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo yake kuhusu Muswada huo na hatimaye Bunge lako Tukufu liliidhinisha Muswada huo kuwa Sheria ambayo ilianza kutumika na Serikali tarehe 1 Julai, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muhtasari Sheria zifuatazo zilifanyiwa marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017;

i. **Sheria ya Benki Kuu, Sura 192**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilifanya marekebisho katika kifungu cha 32 ambacho kinaweka masharti kwa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma kufungua akaunti katika Benki Kuu ya Tanzania. Lengo la marekebisho haya lilikuwa ni kuongeza udhibiti wa matumizi ya Fedha za Umma.

ii. **Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki, Sura ya 306**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya EPOCA ilifanyiwa marekebisho katika kifungu cha 3 na 26 ili kuondoa sharti la kuuza hisa za makampuni ya mawasiliano kwa raia wa Tanzania pekee na kutoa fursa kwa hisa hizi ziuzwe pia kwa watanzania wanaoishi nje ya nchi, kampuni zinazomilikiwa kwa pamoja baina ya watanzania na raia wa nje, raia na kampuni au taasisi za nchi Wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki au raia na kampuni kutoka nchi nyingine yoyote.

iii. **Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147.**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilirekebisha viwango maalumu vya ushuru *(specific duty rates)* vinavyotozwa kwenye bidhaa zisizo za petrol kwa kiwango cha mfumuko wa bei cha asilimia 5 kupitia kifungu cha 124 (2) cha sheria hiyo.

iv. **Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilirekebishwa katika kifungu cha 31,31A na 32 ili Mamlaka ya Mapato Tanzania iweze kuanza kukusanya Kodi hiyo kwa niaba ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

v. **Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilifanya marekebisho katika sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kwa kurekebisha vifungu vya 3, 11, 14 na 19 kwa lengo la kufanya marekebisho mbalimbali ya kiuandishi ili kuwezesha utekelezaji wa pendekezo la kutoza Kodi ya zuio kwa wachimbaji wadogo wa madini pamoja na kuzuia ukwepaji wa kodi ya zuio itokanayo na mikataba ya utoaji wa huduma.

vi. **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho ya Sheria hii yalifanywa katika kifungu cha 31A ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa mabango nchi nzima.

vii. **Sheria ya Madini, Sura 123**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Madini ilifanyiwa marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 18, 19, 90A, 112 ili kuweka

viwango vya tozo pamoja na kuwezesha uandaaji wa kanuni na taratibu za ukaguzi wa madini kabla ya kusafirishwa.

viii. **Sheria ya Usalama Kazini, Sura 297**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilifanyiwa marekebisho katika kifungu cha 17 ili kuondoa sharti la kulipa ada ya usalama mahali pa kazi kwa wamiliki wa shule binafsi.

ix. **Sheria ya Bandari, Sura 166.**

**Mheshimiwa Spika, kifungu kipya kidogo cha 67 cha sheria ya Bandari kilifanyiwa** marekebisho ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa bandari *(wharfage)* na kuweka akaunti itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania.

x. **Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilifanyiwa marekebisho katika kifungu cha 6 cha Sheria ili kuweka mifumo wa kieletroniki (*Government e-payment Gateway Systerm*) wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara na Taasisi za Serikali.

xi. **Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ya kifungu cha 16 cha sheria hii ili kuwawezesha maafisa wa Mamlaka ya Mapato kuiwakilisha Mamlaka kwa niaba ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Lengo likiwa ni kupunguza mlolongo wa mashauri ya kimahakama yanayowasilishwa na wadau wa kodi kutoka sehemu mbalimbali.

xii. **Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438**

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu 8(1), 22A, 47(1), 52, 81(4) na 95 vilifanyiwa marekebisho ya kiuandishi ili kuleta maana iliyokusudiwa.

xiii. **Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289**

**Mheshimiwa spika,** Sheria hii ilifanyiwa marekebisho katika kifungu cha 6 ili kuanza kutoza Kodi ya Majengo kwa nyumba zote katika Majiji, Manispaa na Miji kwa viwango vitakavyopangwa na Waziri wa Fedha na Mipango.

xiv. **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilifanyiwa marekebisho kifungu cha 59 kwa kuongeza muda wa kuhifadhi bidhaa/mizigo kutoka nje inayosafirishwa kwenda nje kupitia bandari zilizopo (*ancillary transport services*) kutoka siku 7 hadi 30.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, marekebisho ya sehemu ya **Kwanza ya Jedwali** yalisamehe kodi inayotozwa kwenye vyakula vya mifugo na mayai pamoja mashine za kutotoresha vifaranga na marekebisho ya **Sehemu ya Pili ya Jedwali** yametoa fursa ya msamaha wa kodi kwenye bidhaa za mitaji hususani kwenye uingizaji wa mashine na mitambo ya uzalishaji wa mafuta ya kula yatokanayo na mimea, nguo, madawa, ngozi kwa lengo la kukuza viwanda na kuvutia uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha majadiliano na Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 kuna baadhi ya masuala Kamati iliafikiana na Serikali na mengine haikuafikiana. Masuala ambayo Kamati haikuafikiana na Serikali ni pamoja na pendekezo la kamati la kutoongeza bei ya vinywaji baridi kwa kiwango cha mfumuko wa bei na kuondoa ushuru wa asilimia 10 kwenye sukari ya viwandani. Serikali haikuafiki pendekezo hilo na matokeo yake ni kushuka kwa mapato yatokanayo na sekta husika, kupunguzwa kwa wafanyakazi na kuathiri biashara ndogo zinazotegemea makampuni hayo. Ifahamike kwamba mapendekezo ya kamati yanatokana na utafiti pamoja na uzoefu wa miaka iliyopita na wa nchi nyingine hasa za jirani.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ilivyo hivi sasa, baada ya Kamati kushauriana na Serikali imekubali kuachia shehena ya Sukari iliyokuwa imekwama bandarini kwa masharti ya kwamba ni lazima walipe gharama ya mizigo yao kutokana na kukaa bandarini kwa muda mrefu *(Demorage Charge).* Kamati inaona jambo hili si sawa kwa sababu kimsingi ucheleweshaji wa kuondoa shehena hiyo Bandarini unatokana na hatua ambazo Serikali ilikuwa ikichukua kuhakiki matumizi ya sukari hiyo kwa vibali vilivyokuwa vimetolewa awali. Ushauri wa

Kamati kwa Serikali ni kuondoa gharama hizo ili Sekta ya vinywaji baridi isiendelee kuathirika.

### 2.5 MAREKEBISHO YA SHERIA YA BAJETI YA MWAKA 2015 *(THE BUDGET ACT 2015)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inatambua marekebisho ya Sheria ya Bajeti yaliyofanywa na Bunge kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2016 *(Miscellenious Ammendments 2016).* Kamati kama mdau wa Sheria hiyo ilipata fursa ya kutoa maoni yake kuhusu marekebisho yaliyoletwa na Serikali. Mabadiliko yaliyofanywa kupitia Sheria hiyo yalihusu uwasilishwaji wa Taarifa za Serikali *(Compliance Reports)* Bungeni, ambapo sasa Taarifa hizo zitawasilishwa kila baada ya nusu mwaka badala kila robo mwaka ambapo utekelezaji wake umeanza mwaka huu. Aidha, pamoja na kuunga mkono mabadiliko haya, Kamati inaendelea kufanya tathmini ya utaratibu huu mpya.

### 2.6 HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2017/18 NA MWELEKEO HADI JUNI 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea, ilijadili na kutathmini Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2017/18 kwa kipindi cha Nusu Mwaka kuanzia mwezi Julai hadi Desemba, 2017 na mwelekeo wa hadi mwezi Juni, 2018 kaa ambavyo iliwasilishwa mezani jana na Waziri wa Fedha na Mipango.

#### 1.1.1. Hali ya Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2017, Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 6.8,** ukuaji huo ulichangiwa zaidi na sekta za uchimbaji madini, habari na mawasiliano, biashara, ujenzi na uzalishaji wa viwanda. Sekta ambazo hazikuwa na ukuaji wa kuridhisha ni huduma za fedha, kilimo, upangishaji wa majengo na utawala. Mfumuko wa bei katika kipindi cha nusu mwaka ulikuwa kwa wastani wa **asilimia 4.8** kama ilivyokuwa katika kipindi kama

hicho mwaka 2016 hivyo kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja. Aidha, thamani ya Shilingi iliendelea kuimarika dhidi ya dola ya marekani ambapo thamani yake ilishuka kwa asilimia 3 tofauti na asilimia 18.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16.

**Mheshimiwa Spika,** Kulingana na takwimu za Serikali Sekta ya Benki imeendelea kuimarika baada ya Benki Kuu ya Tanzania kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha Sekta hiyo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha amana ya Benki Kuu *(Statutory Minimum Reserve)* kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 8** mwezi Aprili, 2017 na kupunguza viwango vya riba ya kukopa Benki Kuu *(discount rate)* kutoka **asilimia 16** hadi **asilimia 12** mwezi Machi, 2017 na hatimaye **asilimia 9** mwezi Agosti, 2017. Hatua hizi kwa ujumla zilisaidia kuongeza ukwasi katika mabenki na hivyo kupelekea kupunguza viwango vya riba baina ya benki na benki. Hata hivyo, bado Sekta hii ina changamoto ya mikopo chechefu ambayo imefikia **asilimia 12.1.**


**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla Kamati imeona mwenendo wa ukuaji wa uchumi na inaendelea kuishauri Serikali kuongeza juhudi katika kusimamia na kutekeleza Sera za uchumi ipasavyo.

### 1.1.2. Makusanyo ya Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia **Shilingi trilioni 31.711**, kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalitarajiwa kuwa **Shilingi trilioni 28.68** na mapato ya nje **Shilingi trilioni 3.029.** Kwa upande wa matumizi, Serikali ilikusudia kutumia **Shilingi trilioni 31.711** ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 19.712** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi trilioni 11.999 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2017 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi trilioni 12.955**, kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalikuwa **Shilingi trilioni 11.926** na mapato ya nje **Shilingi trilioni 1.028**. Kwa upande wa matumizi, Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi trilioni 12.955**, ambapo matumizi ya kawaida

yalikuwa **Shilingi trilioni 9.815** na matumizi ya maendeleo yalikuwa **Shilingi trilioni 3.140**.

**Jedwali Na.1:Ulinganisho wa Makusanyo**




*Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango, 2018.*


**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na.1 hapo juu limeanisha ulinganisho wa makusanyo ya mapato ya kodi,mapato yasiyo ya kodi na mapato ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Bajeti iliyoidhinishwa, makadirio ya nusu mwaka, makusanyo halisi na ufanisi katika kipindi hicho. Katika kipindi cha nusu mwaka Serikali imefanikiwa kukusanya **asilimia 44.4** tu ya mapato yote yaliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka mzima. Aidha, Kamati imebaini kuwa mwenendo wa makusanyo hadi kufikia nusu mwaka Desemba, 2017 Serikali imeweza kukusanya mapato kwa **asilimia 82.8** ya malengo yaliyowekwa katika kipindi hicho. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali iongeze juhudi za makusanyo katika kipindi kilichobaki.

**Mheshimiwa Spika,** Mwezi Machi, 2017 Deni la Taifa lilikuwa dola za Marekani **billioni 17.93,** hadi kufikia mwezi Desemba, 2017 Deni hili lilikuwa dola za Marekani **bilioni 21.308** sawa na ongezeko la dola za marekani **bilioni 3.37**. Kulingana na tathmini ya uhimilivu wa Deni *(Debt Sustainability Analysis)* uliyofanyika, deni hilo bado ni himilivu. Hata hivyo, kwa kuwa

kiasi kikubwa kinachokopwa kinatumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali ni vyema mikopo hiyo ikaelekezwa kwenye sekta zitakazokuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa na si vinginevyo**.**

**Mheshiwa Spika,** Katika kipindi cha nusu mwaka (Julai-Desemba) Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi Trilioni 12.955** kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 9.8** zilikuwa za matumizi ya kawaidia na **Shilingi trilioni 3.14** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.** kwa upande wa utoaji wa fedha kwa matumizi mengineyo wa Wizara, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Sekretariet za Mikoa, Kamati imeona kuwa Serikali imepeleka fedha katika maeneo husika kwa zaidi ya **asilimia 90** ya fedha zilizokuwa zimepangwa kutolewa katika kipindi cha nusu mwaka.

**Jedwali Na.2:Ulinganisho wa Matumizi**




*Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango,2018*

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na. 2 hapo juu limeonesha ulinganisho wa matumizi na namna Serikali ilivyotoa fedha

za matumizi mengineyo kwenda kwenye Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa upande wa Wizara inaonesha kuwa wamepokea fedha kwa **asilimia 114** zaidi ya lengo la nusu mwaka, Sekretarieti za Mikoa wamepokea fedha kwa **asilimia 140** zaidi ya lengo la nusu mwaka na Mamlaka ya Serikali za Mitaa wamepokea fedha kwa **asilimia 90** ya lengo la Nusu mwaka. Kwa Mafungu ambayo yamepokea fedha zaidi ya lengo la nusu mwaka ni kutokana na fedha hizo kujumuisha madeni ya watumishi, wazabuni, watoa huduma pamoja na uhamisho wa viongozi. Kamati imeona hii ni hatua njema kwa kuwa inamesaidia kupunguza mlundikano wa madeni yasiyokuwa ya lazima hususan yale ya muda mrefu ambayo Kamati imekuwa ikishauri yalipwe kwa wakati bila kuathiri wahusika.

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa utoaji wa fedha za Maendeleo za ndani na nje kwa Sekretarieti za Mikoa kwa Nusu Mwaka wa 2017/2018.**





| | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | LENGO LA NUSU MWAKA | KIASI KILICHOTOLEWA | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 64,940,000,00 | 32,470,000,00 | 6,284,459,920 | 10% |
| FEDHA ZA NJE | 10,319,322,00 | 5,159,661,000 | 3,219,998,010 | 31% |

*Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, 2018.*

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na.3 hapo juu linaonesha kuwa mwenendo wa utoaji wa fedha za maendeleo kwenda

kwenye Sekretarieti za Mikoa kwa fedha za ndani na nje unaonesha kwamba fedha za nje zilizotolewa ni **asilimia 31** na fedha za ndani ni **asilimia 10**. Mwenendo huu ni kwa mujibu ya bajeti yote iliyoidhinishwa kwa mwaka wa 2017/ 2018. Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudi kwenye ukusanyaji wa fedha za ndani ili ziweze kupelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa utoaji wa fedha za Maendeleo za ndani na nje kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Nusu Mwaka wa 2017/2018.**




| | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | LENGO LA NUSU MWAKA | KIASI KILICHOTOLEWA | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 529,646,004,0 | 264,823,002,0 | 165,967,186,7 | 31% |
| FEDHA ZA NJE | 13,800,412,00 | 6,900,206,000 | 12,906,306,04 | 94% |

*Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, 2018.*

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na.4 hapo juu linaonesha kuwa mwenendo wa utoaji wa fedha za maendeleo kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa fedha za ndani na nje unaonesha kwamba fedha za nje zilizotolewa ni **asilimia**

**94** na fedha za ndani ni **asilimia 31**. Mwenendo huu ni kwa mujibu ya bajeti yote iliyoidhinishwa kwa mwaka wa 2017/ 2018. Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudi kwenye ukusanyaji wa fedha za ndani ili ziweze kupelekwa kwenye Serikali za Mitaa kwa sababu huduma za msingi kama vile upatikanaji wa huduma za afya na maji bado sio za kuridhisha ikilinganishwa na maeneo ya mijini.

## 2.7 CHANGAMOTO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla Serikali imeweza kutekeleza Bajeti yake katika kipindi cha nusu Mwaka kwa **asilimia 40.5** tu. Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:-

i. Sekta za Afya na Maji kupata mgao mdogo wa Fedha ukilinganisha na mahitaji halisi ya Sekta hizo ambazo zinagusa maisha ya Wananchi wengi. Sekta ya Afya ilipata mgao wa Shilingi bilioni 84 kati ya **Shilingi bilioni 168.2** zilizopangwa kwa nusu mwaka ambazo ni fedha za ndani. Maji mjini na vijiji ilipata mgao wa **Shilingi bilioni 103.5** kati ya **Shilingi bilioni 204.3** zilizopangwa kwa nusu mwaka ambazo ni fedha za ndani; kwa msingi huo Sekta ya Afya ilipokea **asilimia 25.20** ya bajeti yote ya maendeleo kwa wakati sekta ya Maji ilipokea **asilimia 25.32** ya bajeti yote;

ii. Sekta ya Kilimo ilipelekewa kiasi cha **Shilingi bilioni 11.3** kati ya **Shilingi bilioni 29.8** zilizopangwa kwa nusu mwaka ambazo ni fedha za ndani. Kiasi hicho kilichopokelewa ni sawa na asilimia 18.95 ya Bajeti yote ya maendeleo iliyopangwa kwa mwaka;

iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinahudumia wananchi wengi zimepokea kiasi cha **Shilingi bilioni 165.9** kati ya **Shilingi bilioni 264.8** zilipangwa kwa kipindi cha nusu sawa na **asilimia 31.36** tu ya fedha za ndani za maendeleo katika mwaka wa fedha 2017/18;

iv. Ucheleweshaji wa kutolewa fedha na Hazina pamoja na upatikanaji kidogo wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;

v. Washirika wa Maendeleo *(Development Partners)* kutokutoa kwa wakati au kutoa kwa kiwango pungufu cha fedha walizoahidi wakati wa maandalizi ya Bajeti na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

vi. Ukuaji wa kasi wa Deni la Taifa ambao unaweza kusababisha Serikali kushindwa kugharamia utekelezaji wa bajeti yake;

vii. Serikali kutokuwa na ubunifu katika kufanyia utafiti wa kupata vyanzo vipya vya mapato na pia kutochukua uamuzi wa haraka kutumia vyanzo vipya vya mapato vinavyopendekezwa na wadau wa masuala ya kodi;

viii. Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Serikali kwa baadhi ya Wizara, Taasisi za Serikali na Halmashauri;

ix. Kuwepo kwa mwitikio mdogo wa matumizi ya mashine za kielektroniki (EFDs) kwa baadhi ya wateja na walipakodi;

x. Wigo mdogo wa Kodi unaosababishwa na kutofanyika kwa maboresho ya mfumo wa kodi ili uwe rafiki zaidi kwa wafanyabiashara wadogo; kutorasimishwa kwa sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi hususan wafanyabiashara wadogo ambao hawajasajili biashara zao;

xi. Serikali bado haijaweza kukamilisha zoezi la kutathmini uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni *(Sovereign credit ratings)* ili Serikali iweze kukopa mikopo yenye masharti nafuu katika soko la kimataifa kwa ajili ya kugharamia nakisi ya Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, sekta za maji kilimo na afya ni mtambuka na zinagusa maisha ya Watanzania moja kwa moja, ni vema Serikali ikaongeza juhudi za kupeleka fedha kwenye sekta hizi.

## 2.8 MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA PAMOJA NA MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2018/19.
## 1.0

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kupitia na kujadili Taarifa ya Serikali kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/19. Kimsingi, Kamati iliridhika na maelekezo ya Serikali katika vyombo husika hasa kuhusu utaratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini za Mipango na Bajeti zao ili kuhakikisha matumizi ya Serikali yanazingatia thamani ya fedha *(value for money)* kama miongozo ya kisheria inavyoelekeza. Muongozo huo pia unaelekeza namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, mapendekezo ya mwongozo yalielekeza namna ya kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na wadau wengine kwa kuzingatia utekelezaji wa sera za fedha na kodi tukielekea mwaka wa fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mapitio hayo, Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala mengine mbalimbali yanayohusu Mpango huo kama ifuatavyo;

i. Kutoa ufumbuzi wa kutatua changamoto ya upatikanaji wa fedha kutoka kwa wafadhili ambazo kiasi kikubwa huelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

ii. Serikali kuweka mikakati thabiti na kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo ili kuwainua zaidi ya asilimia 70 ya wananchi waliojiajiri katika sekta hii;

iii. Serikali kuweka mikakati thabiti ya kupunguza gharama za kufanya biashara nchini *(Cost of Doing Bisiness)* ili kuvutia wawekezaji;

iv. Mwongozo ujikite katika kuondoa changamoto

zinazoikabili sekta ya fedha katika kutatua tatizo la uhaba mkubwa wa Mitaji unaohitajika kusaidia kukuza uchumi wa Tanzania;

v. Serikali ione umuhimu wa kushirikisha Sekta Binafsi ama kutekeleza miradi ya maendeleo yenye sura ya kibiashara yenyewe au kwa kutumia mfumo wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership);* Kamati inaamini moja ya jawabu la kupunguza ongezeko la Deni la Taifa ni kuanza kutekeleza miradi kwa njia ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Nchini kama Ethiopia, Ivory Coast na Afrika kusini ni mifano mizuri katika utekelezaji wa miradi kwa njia hii. Njia hii imeyasaidia sana mataifa hayo katika uendelezaji wa miradi ya miundombinu na maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje (Export Processing Zones).

vi. Serikali ione uwezekano wa kutekeleza kwa awamu miradi yake ili kuweza kuikamilisha haraka badala ya kubeba miradi mingi kwa wakati mmoja.

## 2.9 MAFUNZO NA SEMINA KWA KAMATI YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwezi Januari – Desemba 2017, Wajumbe wa Kamati walipata mafunzo ya ndani kuhusu usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Bajeti, Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na masuala mbalimbali ya kibajeti na kiuchumi yanayohusu sekta binafsi ambayo yalisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, baadhi ya Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kuhudhuria makongamano ya kimataifa nchini Marekani na Finland. Hata hivyo, Kamati inahitaji kupata mafunzo na uzoefu kutoka katika Mabunge mengine ambayo yana Kamati za Bajeti au Kamati zenye majukumu yanayofanana na Kamati hii, mathalani katika Mabunge ya nchi za Kenya, Uganda, Nigeria, Ghana au Australia ambayo yamepiga hatua kubwa katika usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti zao.

## 2.10 VIKAO VYA KAMATI NA WADAU MBALIMBALI WA MASUALA YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ingependa kuwatambua wadau wa masuala ya bajeti na uchumi ambao wameshirikiana na Kamati kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake kwenye kipindi husika: -

a) Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Ofisi ya Msajili wa Hazina (Treasury Register), Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana (CMSA);

b) Sekta Binafsi, chini ya umoja wao *(Tanzania Private sector Foundation)* ambao Kamati ilikutana nao mara kadhaa kupata maoni yao kuhusu hatua na utekelezaji wa kodi nchini;

c) Shirikisho la watoa Huduma za Utalii nchini *(Tourism Confederation of Tanzania)* ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta ya utalii;

d) Umoja wa watoa huduma za simu nchini *(Mobile Operators Association of Tanzania)* ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta ya mawasiliano;

e) Umoja wa wenye mabenki nchini *(Bankers Association of Tanzania)* ambao walijadiliana na Kamati masuala kadhaa ya kibenki na namna bora ya Serikali kupata mapato ya Serikali kupitia njia mbalimbali za kibenki;

f) Umoja wa watoa huduma za Bima nchini *(Tanzania Insurers Association)* ambao walishauriana na Kamati kuhusu uwezekano wa kupanua huduma za bima hususan katika shughuli za bima ya uchimbaji wa gesi na madini; na

g) Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kujadili Taarifa kuhusu masuala ya usimamizi na uwekezaji katika biashara na

masuala yanayohusu sera na sheria mbalimbali zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yao.

h) Asasi ya Kiraia *(Tanzania Coalition on Debt and Development - TCDD)* inayojihusisha na masuala ya Deni la Taifa na Maendeleo ambayo iliwaongezea

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawapongeza na kuwashukuru wadau na taasisi zote zilizoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake mbalimbali. Aidha, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake thabiti wa kufanya majadiliano ya mara kwa mara na Sekta Binafsi, yenye lengo la kuimarisha uhusiano na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara. Majadilaino hayo yatakuwa na tija endapo yatakuwa na matokeo chanya na yataimarisha Sekta Binafsi kama injini ya ukuaji wa uchumi na kuipatia Serikali mapato zaidi.

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi chote ambacho Kamati ilikutana na Serikali na hata katika Taarifa zake ambazo Kamati imeziwasilisha katika Bunge lako Tukufu iliendelea kuishauri na kutoa maoni mbalimbali yanayohusu Uchumi na Bajeti. Katika kipindi cha kuanzia Januari – Desemba 2017 Kamati ilitoa maoni na mapendekeo kususu masuala mengi, baadhi ya masuala hayo ni yafuatayo:-

### 3.1 Utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017;

**Mheshimiwa Spika,**
**KWA KUWA** Bunge limepewa mamlaka la kujadili na kupitisha utaratibu wa ukusanyaji mapato ya Serikali kupitia Sheria ya Fedha kila mwaka,

**NA KWA KUWA** katika mwaka wa fedha 2017/18 Sheria ya Fedha iliyotungwa iliruhusu Serikali kurekebisha viwango vya kodi kwa kuongeza, kuondoa ama kusamehe kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali na baadhi ya maeneo kwenye Sheria hiyo Kamati imeridhishwa na utekelezaji wake,

**HIVYO BASI,** Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha inatekeleza Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 kama ilivyopitishwa na Bunge hususan katika maeneo yafuatayo:-

i. Sheria ya Fedha za Umma Sura 348: Serikali ihakikishe mfumo ya kielektroniki (*Government e-payment gateway system)* wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara na Taasisi za Serikali unakamilishwa ili makusanyo yote ya Serikali yapitie katika mfumo huo kama Sheria inavyoelekeza;

ii. Sheria ya Kodi ya Majengo Sura 289: Serikali ihakikishe inakamilisha mfumo wa PTMS (*Property Tax Management System)* na kwa kuunganisha GIS *(Geographical Information System)*unaotumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika utambuzi wa majengo na mabango ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi hizo.

## 3.2 Usimamizi wa Deni la Taifa

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA** Deni la Taifa ni himilivu kwa mujibu wa maelezo ya Serikali na kwamba fedha nyingi zinazokopwa na Serikali ni kwa ajilii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

**NA KWA KUWA** Serikali haijakamilisha zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni (*Sovereign Credit Rating*) ili kuiongezea uwezo zaidi wa Serikali kukopa kutoka katika vyanzo afuu;

**HIVYO BASI,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha ukopaji na ulipaji wa Deni hilo hauathiri ugharamiaji wa bajeti ya Serikali kwa kila mwaka wa fedha. Pia ikamilishe zoezi la tathmini ya nchi kukopa na kulipa madeni (*Sovereign Credit Rating*). Aidha, iendelee kufanya majadiliano na Taasisi, nchi na Benki ya Dunia ambao wanaidai nchi kwa madhumuni ya kupata masharti nafuu katika ulipaji wa Deni la Taifa *(Debt Reprofiling)* kama walivyofanya wenzetu wa Kenya na Malawi.

## 3.3 Sekta ya Mabenki

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA,** hivi karibuni sekta ya Benki hasa Benki za Jamii *(Community Banks)* zimekumbwa na msuko suko hasa baada ya Benki 3 kuwekwa chini ya uangalizi na 5 kufungiwa kati ya Benki 12.

**NA KWA KUWA**, moja ya tatizo kubwa liliokumba Benki hizo ni usimamizi mbovu wa Bodi za Mabenki hayo;

**HIVYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kupitia Benki Kuu kuanzisha Kitengo Maalumu chini ya Idara ya Usimamizi wa Mabenki ili kitengo hicho kiwe na jukumu la kuhakikisha kwamba bodi za mabenki ya jamii zinaendeshwa kwa weledi na ufanisi na kuzisaidia kutoa ushauri wa kitaalamu.

## 3.4 Utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo kwa Mwaka 2017/18

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA,** Mpango wa maendeleo 2017/18 umeainisha viapumbele mbalimbali ambavyo Serikali imelenga kutekeleza katika kipindi hicho ambavyo ni kukuza uchumi wa viwanda, uendelezaji wa miundombinu, maji, elimu na afya;

**NA KWA KUWA,** utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mpango huo unahitaji ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye sura wa kibiashara;

**HIVYO BASI,** Kamati inaendelea kushauri Serikali kupeleka fedha kwa wakati kugharamia miradi hiyo na kushirikisha Sekta Binafsi katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ili Serikali ibaki na jukumu la kutekeleza miradi ya maendeleo yenye lengo ya kutoa huduma zaidi kama vile afya, usambazaji maji na utoaji wa elimu.

### 3.5 Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati (*Flagship Projects*)

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Nusu Mwaka haikuainisha utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Kimkakati;

**NA KWA KUWA**, Miradi hiyo ina manufaa makubwa kitaifa kama vile ujenzi wa Reli nzito kwa kiwango cha ratili 80 (*Standard Gauge Rail - SGR)*, Mradi wa Makaa ya Mawe ya Linganga na chuma cha Mchuchuma, ujenzi wa gati namba13 na 14 *(Berth 13&14)* pamoja na ujenzi wa maeneo maalumu ya mauzo ya nje *(Export Processsing Zone na Special Economic Zone)*;

**HIVYO BASI**, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kusimamia ipasavyo utekelezaji wa miradi hiyo muhimu pamoja na kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa Bunge na Wananchi kwa ujumla.

### 3.6 Urasimishaji wa Sekta isiyo rasmi

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA,** Serikali bado inahitaji kuongeza ukusanyaji wa mapato hasa ya ndani kuptia vyanzo mbalimbali;

**NA KWA KUWA,** Bunge kupitia Sheria ya Fedha 2017/18 ilifanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ilikutoa fursa kwa Serikali kuwatambua wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi *(broaden tax base)*kwa kuongeza watozwa kodi wapya;

**HIVYO BASI,** Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali kuhakikisha inaongeza kasi katika zoezi la urasimishaji wa biashara na shughuli ndogondogo za kiuchumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mapato na kudhibiti upotevu wa mapato.

### 3.7 Utatuzi wa Changamoto zinazo athiri mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini *(Doing Bussiness and Investment in Tanzania)*

**Mheshimiwa spika,**

**KWA KUWA,** Mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ni muhimu katika kuimarisha Sekta Binafsi ya ndani na kuvutia uwekezaji kutoka nje, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali;
**NA KWA KUWA**, Kamati imefurahishwa na muongozo uliotolewa na TAMISEMI kwa ajili ya kuboresha utoaji wa vibali vya ujenzi katika Halmashauri na Wizara ya Ardhi kwa kuanzisha mfumo wa kielectroniki wa utoaji wa hati;

**HIVYO BASI,** Kamati inazitaka Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuandaa mkakati madhubuti wa kutanzua vikwazo vinavyo athiri mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara. Mikakati hiyo izingatie fursa zilizopo mfano matumizi ya eneo la kijiografia na wingi wa rasilimali zilizopo. Hatua hii itasaidia kukuza uchumi haraka, kuongeza ajira, kupanua wigo wa mapato na kuondoa umaskini.

### 3.8 Ukusanyaji na Urejeshaji wa Kodi ya Majengo *(Property rate)*

**Mheshimiwa Spika,**
**KWA KUWA,** katika mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilihamisha ukusanyaji wa kodi ya majengo kutoka Serikali za Mitaa na kupeleka Serikali Kuu (TRA) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji;

**NA KWA KUWA**, Kamati ilikubaliana na pendekezo hili kwa makubaliano kwamba chanzo hiki cha mapato ni cha Serikali za Mitaa na fedha zitarejeshwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyopangwa. Hata hivyo, utaratibu ulivyo hivi sasa unazitaka Halmashauri kuwasilisha mahitaji yao Hazina ndipo warejeshewe fedha hizo kulingana na mahitaji.

**HIVYO BASI,** Kamati imeona kuwa utaratibu huu unaleta ugumu kwa Halmashauri kutofautisha fedha zinazotokana na kodi ya majengo na ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hivyo, Kamati inapendekeza Serikali itafute utaratibu rahisi wa kuzirejesha fedha hizo Halmashauri ili zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 3.9 Maombi ya Fedha Nje ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika,**
**KWA KUWA,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka, miongoni mwa mafungu yaliyo Fombewa fedha nje ya Bajeti ni Bodi ya Korosho kiasi cha **Shilingi bilioni 10;**

**NA KWA KUWA,** Kwa mujibu wa Sheria ya Korosho Na 203, (The Cashewnut Industry Act, (Cap.203)) Kifungu cha 17A (1) vipengele (a) na (b) vimeainisha kwamba asilimia 35 ya makusanyo ya ushuru wa masafirisho ya korosho ghafi nje ya nchi utapelekwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali na asilimia 65 itapelekwa Bodi ya Korosho kwa ajili ya kuendeleza tasnia hiyo;

**HIVYO BASI,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuweka kifungu *(sub-vote)* kitakachokuwa kinapokea na kugawa fedha kwenye Bodi za Mazao mbalimbali ya uendelezaji wa mazao ya biashara ikiwemo Bodi ya Korosho. Hata hivyo, katika msimu wa mwaka wa 2016/17 Bodi ya Korosho bado haijapokea kiasi cha Shilingi billioni 88.9 kama sheria inavyotaka kutoka katika makusanyo ya ushuru wa mauzo ya zao hilo nje.

### 3.10 Uendelezaji wa zao la Korosho na Mazao mengine ya Biashara

**Mheshimiwa Spika,**
**KWA KUWA,** Tanzania ina fursa katika sekta ya kilimo ambayo bado haijaweza kutumika vizuri kuongeza mauzo nje;

**NA KWA KUWA**, Zao la korosho limekuwa ni la mfano mzuri katika kuongeza mauzo nje ya nchi;

**HIVYO BASI**, Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kuziwezesha Bodi za Mazao mbalimbali kama vile korosho, chai, pareto, pamba, ngozi na kahawa ili ziweze kuweka mazingira wezeshi katika uendelezaji wa mazao hayo. Mfano ujenzi wa maghala, ununuzi wa pembejeo na viuatilifu, utafiti, usambazaji wa miche bora, usimamizi wa masoko na utoaji wa elimu kwa wakulima, endapo Serikali haitawezesha bodi hizi itaangamiza mazao hayo.

### 3.11 Utoaji wa Takwimu kwa Vipindi Husika;

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA,** marekebisho ya Sheria ya Bajeti ya 2015 yaliyofanywa yameitaka Serikali ya kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai 1 hadi Desemba 31na mwelekeo hadi Juni. Lengo ilikuwa ni kuipa Serikali muda wa kutosha kuandaa Taarifa hiyo kwa ufasaha na kwa kuzingatia ujumuishaji wa takwimu zote muhimu;

**NA KWAKUWA,** Taarifa iliyowasilishwa na Serikali imetoa takwimu zinazotofautiana vipindi ambapo baadhi ni za mwezi Julai - Septemba na nyingine ni za Julai- Desemba;

**HIVYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa takwimu kwa kipindi kimoja cha nusu mwaka ili kuliwezesha Bunge kuishauri Serikali katika nyanja za ukusanyaji wa mapato, viashiria vya uchumi, mwenendo wa matumizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyoo mnaliongoza Bunge hili kwa umahiri na umakini mkubwa. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isidori Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri

wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa kuchambua na kujibu hoja mbalimbali kwa Kamati. Vilevile, nawashukuru pia Wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi mbalimbali za Fedha ambao wamefanya kazi na Kamati hii katika kipindi hiki. Pia, napenda kuwashukuru wadau mbalimbali wa masuala ya biashara na kodi ambao wameshirikiana na Kamati hii katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua kuwa uhai wa Kamati utaisha mara baada ya Mkutano huu wa Kumi (10) kumalizika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Wajumbe Waalikwa kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote nilichohudumu kama Mwenyekiti wa Kamati. Umakini na umahiri wao ulikuwa na mchango mkubwa katika kuwezesha Kamati kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali kwa Serikali kupitia taarifa ambazo Kamati ya Bajeti iliwasilisha Bungeni. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - Aliyekuwa M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb -Mjumbe
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb -Mjumbe
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb -Mjumbe
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb - Aliyekuwa Mjumbe
17. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb - Mjumbe

18. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb - Mjumbe
20. Mhe. David Ernest Silinde, Mb -Mjumbe
21. Abdallah M. Bulembo, Mb -Mjumbe
22. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb -Mjumbe
23. Mhe. Andrew John Chenge, Mb -Mjumbe
24. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb Mjumbe
25. Mhe. Dalaly Peter Kafumu, Mb Mjumbe
26. Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb - Aliyekuwa Mjumbe
27. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb -Mjumbe
28. Mhe. Mussa A. Zungu, Mb -Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndg. Lina Kitosi na Makatibu Ndg. Michael Kadebe, Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Lilian Masabala na Ndg. Maombi Kakozi kwa umahiri wao na kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Hawa A. Ghasia, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
02 Februari, 2018

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Mwenyekiti tunakushukuru sana, tunaendelea na taarifa inayofuata ni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka, inawasilishwa na Mheshimiwa Obama, Mwenyekiti karibu. *(Makofi)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuwasilisha taarifa hii. Hii ni taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018. Kwa sababu ya muda naomba taarifa yote ingie katika kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) cha Kanuni za Kudumu ya Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa mwaka 2017 na kuliomba Bunge Tukufu kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji na utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ina majukumu yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma unaufanisi na kuwa umezingatia taratibu na sheria na miongozo mujarabu ya biashara.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchambua na kujadili taarifa ya mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari 2017 hadi Januari 2018, Kamati imetekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao kwa kujadili na kuchambua taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma

kuhusu uwekezaji na utendaji wa taasisi hizo. Aidha Kamati imefanya ziara katika baadhi ya taasisi za umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji uliofanywa na taasisi hizo una tija.

Vilevile Kamati ilipatiwa semina za mafunzo kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kutoka katika taasisi mbalimbali za umma kwa ajili ya kuongezewa uwezo wa utendaji wa kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma na matokeo yake; Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi lina dhima ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika maeneo mbalimbli ikiwemo uwekezaji wa mitaji ya umma. Ili kutekeleza hadhima hiyo jicho la Bunge katika uwekezaji ni Kamati ya Kadumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kamati ilichambua taarifa ya uwekezaji na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, Serikali ilifanya uwekezaji katika jumla ya taasisi 669 za ndani na taasisi 10 za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha uwekezaji wa umma katika taasisi hizo kinatofautiana, mchanganuo unaoonesha kuwa Serikali inamiliki kwa asilimia 100 taasisi 231 na asilimia pungufu ya 100 katika taasisi 38. Mchanganuo wa umiliki wa hisa inaonyesha katika jedwali Namba mbili la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kuwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilifanya uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma na makampuni ambayo hisa *domestic investment* kwa jumla ya shilingi trilioni 47.8, kati ya fedha hizo trilioni 46.9 ziliwekezwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma ndani ya nchi, ambapo shilingi bilioni 894 ziliwekezwa katika makampuni ambayo Serikali ina hisa ambayo ni asilimia 50 na pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa umeonesha kuwa katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 Serikali ilipata faida ya kukusanya mapato yasiyo ya kodi *(non tax revenue)* jumla ya shilingi bilioni 845

zilipatikana kutokana na uwekezaji uliofanywa katika taasisi na mashirika ya umma yaliyo ndani ya nchi. Aidha, kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 Serikali ilipata faida ya jumla ya shilingi bilioni 40 kutokana na uwekezaji uliofanywa katika makampuni ambayo Serikali ina hisa asilimia 50 na pungufu ya asilimia 50.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2017, Serikali imefanya uwekezaji wenye thamani ya shilingi bilioni 529 katika taasisi 10 zilizo nje ya nchi orodha ya taasisi hizo zipo katika kiambatanisho namba mbili.

Mheshmiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa mitaji ya umma yamebaini kuwa uwekezaji wa Serikali katika taasisi na mashirika ya umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa umeongezeka kwa asilimia ya 107, ambapo katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni Serikali iliwekeza jumla ya shilingi trilioni 23 ukilinganisha na kiasi cha trilioni 47.8 kilichowekezwa katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017.

Vilevile faida inayotokana na uwekezaji huu imeongezeka kwa asilimia 109 ambapo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 faida ya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa ilikuwa ni shilingi bilioni 422.9. Aidha, faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 ni shilingi bilioni 885.6.

Mheshmiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 ni asilimia 1.9 tu ya uwekezaji wote. Kiasi hicho ni kidogo sana ikilinganishwa na fedha nyingi zilizowekezwa katika taasisi na mashirika ya umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa uwekezaji, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na taarifa zimewasilishwa na taasisi na mashirika ya umma ili kubaini tija na uwekezaji uliofanywa na taasisi hizo, katika uchambuzi

wake Kamati ilitumia njia zilizooneshwa hapo namba moja hadi namba nne. Kwa kutumia njia hizo Kamati ilifuatilia uwekezaji huo wa mitaji ya umma kwa kufanya uchambuzi na kubaini mambo makuu yafuatayo:-

Mheshmiwa Mwenyekiti, upungufu wa mitaji, Kamati ilichambua taarifa za mashirika na kubaini kwamba kuna upungufu mkubwa wa mitaji unaosababisha taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na kutoleta tija inayotarajiwa. Mfano wa mashirika ambayo mitaji imekuwa kidogo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Shirika la Bima la Taifa, Kituo cha Zana za Kilimo Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)*, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa - Suma JKT na Bodi ya Utalii Tanzania. Kamati ilichambua taarifa za benki ya Maendeleo ya Kilimo na kubaini kwamba mtaji wake ni mdogo kama ilivyooneshwa hapo chini.

Mbili; kutokuwepo na uwiano mzuri wa mapato na matumizi. Katika kuchambua mizania ya mashirika mbalimbali ya umma ilibainika kuwa baadhi ya mashirika ya umma yana matatizo kwenye uwiano wa mapato na matumizi kwa kuwa yamekuwa yakitumia kiasi kikubwa ya mapato na au mapato yote yanayozalishwa na zaidi hali hiyo husababisha taasisi hizo za umma kutokuwa na ziada au kupata nakisi. Mfano wa taasisi hizo ni kama Wakala wa Uchimbaji wa Visima Mabwawa *(DDCA)* ambao taarifa inaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 uwiano wa mapato na matumizi ulikuwa 0.99 kwa moja tafsiri ni kuwa kila shilingi moja inayozalishwa na wakala senti 99 zinatumika kwa matumizi mbalimbali.

Tatu; Serikali kutolipa madeni yake kwa wakati. Suala lingine lililobainika ni baadhi ya mashirika kushindwa kujiendesha na kukamilisha miradi yake kwa ufanisi na kwa wakati hali imetokana na kuchelewa kulipwa madeni kutoka kwa wateja wake ikiwemo hasa Serikali Kuu, Halmashauri na Taasisi za Umma. Serikali imekuwa ikidaiwa mfano na Bodi ya Bohari ya Madawa *(MSD)* ambayo sasa deni lake limekuwa kubwa mpaka kufikia sasa bilioni 144.

Nne; changamoto ya kisheria manunuzi ya umma, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini upungufu katika Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kamati imepitia taarifa ya wakala wa uchimbaji visima na mabwawa *(DDCA)* na kubaini changamoto inayotokana na sheria ya manunuzi. Sheria ya Manunuzi ya Umma imeziangalia Taasisi za Umma za Serikali kama taasisi nunuzi yaani *procuring entity* na hazikuzingatia Taasisi za Serikali kama mkandarasi. Kutokana na hali hiyo wakala umekuwa ukikosa kazi kwa kuchelewa kwa michakato ya ununuzi hususani miradi ya uchimbaji ambayo utekelezaji wake ni wa muda mfupi.

Tano; utegemezi mkubwa wa ruzuku ya Serikali. Katika uchambuzi wa taarifa mbalimbali za Mashirika ya Umma Kamati imebaini kuwa baadhi ya mashirika na taasisi za umma zinategemea kwa kiasi kikubwa ruzuku ya Serikali katika kujiendesha na kutekeleza miradi yake. Hali hii imezifanya baadhi ya taasisi kutokuwa na juhudi ya kutafuta mitaji na hivyo kutegemea Serikali kupita kiasi. Baadhi ya taasisi hizo ambazo zimeshindwa kutekeleza majukumu yake pale inaposhindwa kuchangia au kucheleweshewa hela za ruzuku ni pamoja na Bodi ya Utalii, Shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Kampuni za Ndege *(ATCL)* na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo. *(SIDO)*

Sita; utendaji na uendeshaji usioridhisha wa Taasisi na Mashirika ya Umma. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika utendaji na uendeshaji wa taasisi za umma, katika eneo hili kamati ilifanya uchambuzi katika maeneo makuu matatu, viongozi wa taasisi kutopewa mikataba ya ufanisi *(performance base contract)*, mbili; taasisi kujiendesha kwa hasara na matumizi makubwa; tatu, taasisi kutokuwa na vipaumbele katika kutekeleza miradi na kufanya kazi zilizo nje ya jukumu la msingi. Maelezo yako pale chini na yapo kwenye ripoti yetu.

Saba; uwiano hasi wa mali kwa madeni. Uchambuzi mwingine wa Kamati ulilenga katika kuangalia uwiano wa ulipaji wa madeni kwa mali. Taarifa zilizochambuliwa na Kamati zinaonyesha mapungufu kwa baadhi ya taasisi za

umma ambapo zimeshindwa kulipa madeni yake kwa kutumia mali zake. Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Shirika la Elimu Kibaha  na kubaini hali mbaya ya ukwasi. Hali ya ukwasi ya shirika ni mbaya kwa kuwa mali za muda mfupi haziwezi kulipa madeni yake ya muda mfupi inapolazimika kufanya hivyo. Hali hii imeoneshwa na uwiano wa mali za muda mfupi kwa muda mfupi *current asset ratio* ambazo ni 0.36 kwa moja, badala ya uwiano wa 2:1. Shirika linatakiwa kuwa na mikakati ya kuongeza mapato ya taasisi.

Nane; uwiano hasi wa mapato na mali pale tumeelezea.

Tisa; changamoto za miundo ya Ttaasisi na mashirika ya umma, ufanisi wa utendaji wa taasisi na mashirika ya umma unapimwa kutokana na vigezo mbalimbali, moja ya vigezo hivyo ni muundo wa taasisi ambao unaiwezesha taasisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, miundo ya baadhi ya taasisi na mashirika ya umma hauendani na mazingira wala mwelekeo wa uwekezaji wenye tija hali inayosababisha taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundo ya taasisi za umma zilizo nyingi iliandaliwa wakati wa uanzishwaji wa taasisi hizo. Kutokana na mabadiliko ya muda na teknolojia miundo hiyo imekuwa haiendani na wakati sasa na kutokidhi mahitaji ya taasisi za umma. Baadhi ya taasisi zinahitaji kufaniwa marejeo katika miundo yake ni Benki Kuu ya Tanzania, Shirika la Elimu Kibaha, JKT, Zana za Kilimo na Mazao Mchanganyiko.

Mheshmiwa Mwenyekiti, uchambuzi ulifanywa na Kamati katika taarifa za Benki Kuu ya Tanzania ulibaini kuwa muundo wa Benki Kuu umempa mamlaka Gavana wa Benki kuwa ni Mwenyekiti wa Bodi na wakati huo huo ni Mtendaji Mkuu wa Benki. Muundo huu unakinzana na uendeshaji mzuri wa taasisi kwani Mwenyekiti wa Bodi atashindwa kuisimamia taasisi ipasavyo kwa kuwa yeye ndiyo mtendaji mkuu.

Mheshmiwa Mwenyekiti, changamoto za jumla,

Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika kipindi cha Januari, 2017, hadi Januari 2018 changamoto kadhaa zimejitokeza, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mchache wa kupitia taarifa za taasisi na mashirika ya umma. Aidha, katika mwaka 2016 Kamati iliweza kuchambua taarifa za taasisi na mashirika ya umma 41 kati ya 243 ambayo yamesalia. Pia katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za taasisi na mashirika ya umma 23 ambapo Kamati imepata nafasi ya kufanya ukaguzi wa miradi ya uwekezaji katika taasisi tatu tu. Kwa hiyo muda ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za kisheria; Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi 2018 Kamati ilikabiliwa na changamoto za kisheria kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Mwenyekiti, sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma hazimtambui Msajili wa Hazina kama Msimamizi wa Uwekezaji unaofanywa na Serikali, hivyo taasisi hizo zinajikuta zikifanya uwekezaji wa mitaji ya umma katika miradi mbalimbali bila kufuata miongozo ya uwekezaji inayotolewa na Msajili wa Hazina pamoja na sheria nyingine hapo tumeziorodhesha.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati. Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma iliwasilisha taarifa yake ya mwaka 2016 mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa hiyo ilijumuisha maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo Serikali ilitakiwa kuzifanyia kazi. Hata hivyo, baadhi ya mapendekezo yaliyotolea na Kamati hayajafanyiwa kazi.

Moja; Kamati ilipendekeza mamlaka zinazohusika kufanya uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi katika taasisi na mashirika yote ya umma ili taasisi hizo zipate usimamizi madhubuti na ziweze kufanya kazi kwa ufanisi kwa hali ya juu ili kuhakikisha kuwa malengo ya kuanzishwa kwa taasisi

na mashirika hayo yanafikiwa. Aidha, pamoja na mapendekezo hayo muhimu kwa Serikali bado kuna taasisi na mashirika mengi ya umma ambayo hayana Bodi za Wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo haijafanyiwa kazi kikamilifu ni upungufu wa mitaji na hii imejiorodhesha kwenye mitaji ya Benki ya Kilimo. Kulikuwa na hoja ya kutolipa madeni nayo imezungumzwa.

Hoja nyingine kutozingatia Sheria ya Msajili tuliizungumza, Serikali haijafanyia kazi kikamilifu mapendekezo ya Kamati kuhusu watendaji wenye sifa wanaokaimu kwa muda mrefu kuthibitishwa nalo ni jambo ambalo tulilisisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo; kutokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kuhusiana na uwekezaji wa mitaji ya umma Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Mwenyekiti, moja; upungufu wa mitaji. Kwa Kuwa, baadhi ya taasisi na mashirika ya umma ambayo Serikali imewekeza zimebainika kuwa na upungu wa mitaji;

Na Kwa Kuwa, upungufu huo umesababisha Taasisi na Mashirika hayo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na kutoleta tija inayotarajiwa;

Kwa Hiyo Basi, Bunge inashauri kuwa Serikali ipeleke mtaji kwa taasisi na mashirika ambayo ilihaidi kufanya hivyo wakati wa uwazishwaji wa taasisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija.

Mbili; kutokuwepo kwa uwiano mzuri wa mapato na matumizi. Kwa kuwa uwiano wa mapato na matumizi kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma umekuwa siyo wa kuridhisha kutokana na taasisi nyingi kuwa na kiasi kikubwa cha matumizi ikilinganishwa na mapato;

Na Kwa Kuwa, matumizi makubwa yamekuwa yakisababisha taasisi na mashirika ya umma kutokuwa na ziada na kupata hasara,

(i) Kwa Hiyo Basi, Bunge linashauri kuwa Serikali iziagize taasisi za umma ziweze kupunguza matumizi yayoendana na uwekezaji.

(ii) Iziagize taasisi na mashirika ya umma kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Serikali kutolipa madeni yake kwa wakati.

Kwa Kuwa, Serikali imekuwa na utamaduni wa kutolipa kwa taasisi na mashirika ya umma kwa wakati baada ya kupata huduma;

Na Kwa Kuwa, hali hiyo imesababisha taasisi na mashirika ya umma kushindwa kujiendesha na kusababisha kutokukamilisha miradi yake kwa ufanisi na kwa wakati;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linashauri kuwa Serikali ilipe madeni ambayo inadaiwa na taasisi na mashirika ya umma. Aidha, Serikali iendelee kulipia huduma inazozipata kwa wakati ili taasisi na mashirika ya umma yaweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; changamoto ya Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Kwa Kuwa, Sheria ya Manunuzi ya Umma imeziangalia Taasisi za Serikali kama taasisi zenye kufanya manunuzi na kutozingatia kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali ni wakandarasi;

Na Kwa Kuwa, upungufu huo wa Sheria ya Manunuzi ya Umma umezisababishia Taasisi za Umma ambazo ni Mkandarasi kukosa kazi kwa kuchelewa kwa mchakato wa manunuzi kutokana na miradi yake kuwa ni ya muda mfupi;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linashauri kuwa Serikali iondoe changamoto za kisheria ya manunuzi ya umma zinazosababisha utekelezaji wa miradi ya baadhi ya taasisi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano; utegemezi mkubwa wa ruzuku ya Serikali,

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita; tumeonesha pale ni utendaji na uendeshaji usioridhisha wa Taasisi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba; tumeonyesha uwiano hasi wa mali kwa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane; tumeonyesha uwiano hasi wa mapato kwa mali.

Kwa Kuwa, taasisi na mashirika ya umma yaliyo mengi yamekosa ubunifu wa kushindwa kutumia vema mali zake kwa ajili ya kuongeza mapato na kusababisha uwiano wa mapato kwa mali kutoridhisha;

Na Kwa Kuwa, kukosekana kwa uwiano mzuri wa mapato kwa mali kumesababisha mali za Taasisi na Mashirika ya Umma kutotumika kuongeza mapato hivyo kuzifanya Taasisi hizi kutumia mali zake chini ya kiwango na kukosa tija inayotarajiwa;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linashauri kuwa Serikali izielekeze taasisi na mashirika yake kuzitumia vizuri mali zake kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuleta tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za miundo ya taasisi na mashirika ya umma.

Kwa Kuwa, miundo ya baadhi ya taasisi na mashirika ya umma haiendani na mzingira wala mwenendo wa uwekezaji wenye tija kutokana na mabadiliko ya muda na teknolojia;

Na Kwa Kuwa, miundo hiyo kutokidhi mahitaji ya sasa ya taasisi na mashirika hayo, imekuwa kikwazo cha utendaji usioridhisha wa kutekeleza majukumu ya taasisi husika na kutofikia tija inayotarajiwa;

Kwa Hiyo Basi, Bunge inashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ifanye mapitio au marejeo ya miundo ya taasisi na mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni.

Pili, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe kwma walivyoorodheshwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati.

Shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati, Ndugu Amina Salum na Ndugu Elieka Saanya na msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde.

Pia nawashukuru watumishi katika Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphine Tamba, Ndugu Matamus Fungo na Ndugu Hawa Manzurya pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ni matokeo ya

uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni ya Kamati na Mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma, na kuijadili ikiwa na maoni na mapendekezo ili hatimae Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAELEZO YA JUMLA**

## 1.0 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa mwaka 2017 na kuliomba Bunge lako tukufu kuipokea na kuijadili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji na utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa.

## 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari,

2016, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ina majukumu yafuatayo:-

a) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

b) Kuchambua na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Kamati pia imefanya kazi zake kwa kuzingatia miongozo mingine kama ifuatavyo:-

i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011,

iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001,

iv) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370; na

v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992.

## 1.2 Shughuli zilizotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao kwa kujadili na kuchambua Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu Uwekezaji na Utendaji wa Taasisi hizo. Aidha, Kamati imefanya ziara katika baadhi ya Taasisi za Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo una tija. Vile vile, Kamati ilipatiwa Semina za mafunzo kuhusu uwekezaji wa Mitaji ya Umma kutoka katika Taasisi mbalimbali za Umma kwa ajili ya kuongezewa uwezo wa utendaji kazi wake. Ufafanuzi kuhusu shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

**a) Semina za Mafunzo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipatiwa Semina za mafunzo ikiwa ni njia mojawapo ya kuijengea uwezo, Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina ziliratibu mafunzo yaliyolenga kuwapa Wajumbe uelewa kuhusu mambo yafuatayo:-

i. Muundo wa Uwekezaji (Investment Structures & Models & Financing Structures–Including PPP),

ii. Utambuzi wa viashiria vya hatari vya miradi ya Uwekezaji (Risk analysis in project management)

iii. Uchambuzi wa Sera ya Uwekezaji (Investment policies),

iv. Uelewa kuhusu uchambuzi wa mradi iwapo malengo ya mradi yamefikiwa au la (Project monitoring and evaluation),

v. Kuwapa uelewa Wajumbe kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Taasisi mbalimbali za Umma

vi. kuwapa Wajumbe uelewa kuhusu Miradi ya Uwekezaji inayotekelezwa na Taasisi za Umma

**b) Kupokea, Kujadili na kuchambua Taarifa ya Msajili wa Hazina Kuhusu Uwekezaji na Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari 2018, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilipokea, ilijadili na kuchambua Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji na Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma yapatayo Ishirini na Tatu (23). Orodha ya Taasisi hizo ni kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii.

**c) Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Machi, 2017 Kamati ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji

inayotekelezwa na Mashirika ya Umma katika mkoa wa Arusha. Mantiki ya ukaguzi ni kuiwezesha Kamati kufanya tathmini ya ufanisi wa uwekezaji. Miradi iliyotembelewa na ufafanuzi wake inaonekana katika Jedwali Na 01.

**Jedwali Na. 1**

| NA | JINA LA TAASISI | JINA LA MRADI | THAMANI YA MRADI | MAONI YA KAMATI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) | a) Mradi wa Jengo la Maonesho (Exhibition Center)<br>b) Mradi wa Majengo ya Makazi yaliyopo Amani na River Road Arusha | Bilioni 4.88<br><br>Bilioni 5.7 | i) Kasi ya ujenzi iongezeke ili liweze kukamilika kwa haraka na kutoa huduma inayostahiki<br>ii) Marekebisho yafanyike katika miundo mbinu ya jengo ili liwe rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu.<br>iii) Taasisi ijikite zaidi kwenye uwekezaji wa utalii wa mikutano<br>iv) Taasisi iwe na Sera ya Uwekezaji (investment policy) ili kila mradi uweze kufuatiliwa kwa urahisi |
| 2. | Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) | Mradi wa Jengo la Jakaya Kikwete Ngorongoro Tower | Bilioni 45.3 | Taasisi izingatie ufanisi wa kiuchumi na kutafuta mapema wateja watakaopanga katika jengo hilo. |
| 3. | Hifadhi za Taifa (TANAPA) | a) Mradi wa kuweka mfumo wa Tehama kwenye uendeshaji wa Shughuli za Shirika<br>b) Mradi wa TANAPA phase II | Bilioni 12.5<br><br>Bilioni 2.5 | Changamoto ya mkataba kati ya Tanapa na wapangaji wake Wizara ya Mambo ya Nje katika ulipaji wa kodi ya pango umalizwe haraka. |

## 1.3 Muhtasari wa dosari zilizobainika katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kutoa maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma, naomba kulidokeza Bunge lako tukufu kwa muhtasari dosari kuu zilizobainika katika utaratibu wa uwekezaji wa mitaji ya umma. Dosari hizo ni:-

i. Kukosekana kwa usimamizi madhubuti ambapo baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yanafanya uwekezaji wa mitaji ya umma bila kuzingatia sheria, taratibu na miongozo mujarabu ya biashara kama Chuo Kikuu Mzumbe;
ii. Baadhi ya Taasisi na Mashirika yanayowekeza kwa kutumia mitaji ya umma, zimekosa mikakati ya kulipa madeni na kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kama:-

a) Shirika la Elimu Kibaha,
b) Bodi ya Utalii Tanzania

iii. Kuwepo kwa baadhi ya miradi ya uwekezaji isiyokuwa na tija na yenye ufanisi mdogo;
iv. Baadhi ya Taasisi na Mashirika yanayowekeza kuendelea kuwa na miundo isiyoendana na mazingira wala mwelekeo wa uwekezaji wenye tija Mfano Benki Kuu ya Tanzania (BOT);
v. Taasisi na Mashirika mengi yanayowekeza kwa kutegemea ruzuku ya Serikali kushindwa kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi na hivyo, kushindwa kujiendesha kibiashara kama :-

a) Bodi ya Utalii Tanzania,
b) Shirika la Elimu Kibaha,
c) Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko,
d) Kampuni ya Ndege ya Tanzania, na
e) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA NA MATOKEO YAKE

### 2.1 Maelezo ya jumla kuhusu uwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** Bunge ambalo ni chombo cha Uwakilishi wa wananchi lina dhima ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika maeneo mbalimbali ikiwemo Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Ili kutekeleza dhima hiyo, jicho la Bunge katika Uwekezaji ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge imeainisha jukumu la msingi la Kamati hii ambalo kwa ujumla ni kufuatilia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma hufanyika kwa njia mbalimbali zikiwemo uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji na ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji. Katika Kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018, Kamati ilichambua Taarifa za Uwekezaji na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017, Serikali ilifanya Uwekezaji katika jumla ya Taasisi Mia Mbili Sitini na Tisa (269) za ndani ya nchi na Taasisi Kumi (10) za nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi umeonesha kuwa, kati ya Taasisi hizo za ndani, Taasisi Mia Moja Sabini na Tano (175) hazichangii katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kuwa zipo katika utaratibu wa utoaji wa huduma kama vile, Elimu, Afya, Kilimo, Mifugo, Utafiti na Hifadhi ya Jamii. Aidha, Taasisi nyingine kumi ni Mamlaka za Udhibiti na huchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kutoa asilimia 15 ya Mapato Ghafi (*Gross Revenue*) kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwango cha Uwekezaji wa Umma katika Taasisi hizo kinatofautiana. Mchanganuo unaonesha kuwa Serikali inamiliki kwa 100% katika Taasisi 231 (Mia mbili thelathini na Moja) na asilimia pungufu ya 100 katika Taasisi 38 (thelathini na Nane). Mchanganuo wa Umiliki wa Hisa unaoneshwa katika Jedwali Na. 2.


**Jedwali Na. 2**

| NA. | KIASI CHA UMILIKI KATIKA ASILIMIA (%) | IDADI YA TAASISI |
|---|---|---|
| 1. | 100 | 231 |
| 2. | 50+ | 2 |
| 3. | 50 | 4 |
| 4. | Pungufu ya 50 | 32 |
| 5. | Jumla | 269 |

Chanzo: Taarifa ya TR 2016/2017

Picha halisi ya mchanganuo uliopo kwenye Jedwali Na. 01 inaonekana katika kupitia Chati Duara Na. 01 ya Taarifa hii.

**Chati Na. 01: Picha halisi ya Mchanganuo wa umiliki wa Hisa za Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni.**




**Mheshimiwa Spika,** Taarifa zinaonesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, Serikali ilifanya Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa (domestic Investment) kwa jumla ya **shilingi 47,780,068,565,041.50.**

Kati ya Fedha hizo **Shilingi 46,885,087,652,684.60** ziliwekezwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma ndani ya nchi ambapo Serikali ina hisa kuanzia asilimia 51 mpaka 100. **Shilingi 894,980,912,356.88** ziliwekezwa katika Makampuni ambayo Serikali ina hisa asilimia 50 na pungufu.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa umeonesha kuwa katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2017, Serikali ilipata faida kwa njia ya kukusanya mapato yasiyo ya kodi (non-tax

revenue). Jumla ya kiasi cha **Shilingi 845,280,649,095.93** zilipatikana kutokana na Uwekezaji uliofanywa katika Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo ndani ya nchi. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

- Gawio (Dividends) – Shilingi 348,695,839,200.00;

- Mchango wa asilimia 15 ya Mapato Ghafi Shilingi 288,663,694,156.09;

- Mapato kutoka kwenye Mfumo wa Kusimamia na Kuratibu Mawasiliano ya Simu Nchini (TCRA-TTMS) Shilingi 10,655,403,748.10;

- Urudishaji wa Mikopo na Riba – Shilingi 2,040,000,000; na

- Michango Mingineyo – Shilingi 2,472,546,789.90.

- Mtaji uliozidi (redemption of excess capital) – Shilingi 192,753,165,201.84;

Aidha, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2017 Serikali ilipata faida ya Jumla ya **Shilingi 40,355,186,930.39** kutokana na uwekezaji uliofanywa katika Makampuni ambayo Serikali ina hisa asilimia 50 na pungufu ya asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017, Serikali imefanya uwekezaji wenye thamani ya **Shilingi 529,847,591,370.02** katika Taasisi Kumi (10) zilizo nje ya Nchi. Orodha ya Taasisi hizo ni Kiambatisho Na. 2.

Aidha, Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi za nje haujalenga moja kwa moja katika rudisho la faida kifedha (financial return). Uwekezaji katika mashirika haya ni kutokana na mikataba ya ushirikiano wa nchi kikanda na kimataifa. Kutokana na uwekezaji huu, nchi imekuwa ikipata misaada ya kifedha na mikopo ya riba nafuu ambayo imesaidia katika utekelezaji wa miradi yake mbalimbali ya maendeleo. Mara chache sana nchi imekuwa ikipata gawio kutokana na

ufanisi wa uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika haya ya nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa Mitaji ya Umma yamebaini kuwa, Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa umeongezeka kwa **asilimia 107** ambapo, katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2016, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 23,062,742,976,499** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 47,780,068,565,041.50** kilichowekezwa katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2017.


Aidha, ongezeko hili kubwa limetokana na utaratibu wa Uandaaji wa Taarifa ya uwekezaji kufanyika kwa kutumia hesabu za kuishia tarehe 30 Juni, 2017 tofauti na awali ambapo taarifa ya uwekezaji ilikuwa inatumia hesabu za mwaka mmoja nyuma, Kuongezeka kwa thamani kutokana na uthamini wa Barabara chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ambapo, thamani ya uwekezaji wa TANROADS unachukua **asilimia 39.4** ya uwekezaji wote wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma na ongezeko la Idadi ya Mashirika yanayowasilisha hesabu kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina kutoka Taasisi 243 Mwaka 2015/16 hadi Taasisi 255 Mwaka 2016/17. Aidha, kuna Taasisi 14 ambazo hazijaanza kuandaa hesabu zake za kujitegemea

Vile vile, faida inayotokana na uwekezaji huo imeongezeka kwa **asilimia 109** ambapo, kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2016 faida ya uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa ilikuwa ni **Shilingi 422,968,027,083.68**. Aidha, faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2017 ni **Shilingi 885,635,836,026.32**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji uliofanywa na Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2017 ni **asilimia 1.9** tu ya uwekezaji wote. Kiasi hicho ni kidogo sana ikilinganishwa na fedha nyingi zilizowekezwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha mwenendo wa ukuaji

wa uwekezaji wa mitaji na faida umeoneshwa katika Graph Namba 1

**Mchoro(Graph) Na 01: Sura ya ongezeko la thamani ya uwekezaji na faida kwa mwaka 2015/16 na 2016/17**




## 2.2 Uchambuzi wa Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa zilizowasilishwa za Taasisi na Mashirika ya umma ili kubaini tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

i) Kupitia Taarifa za Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika na Taasisi za umma zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya umma.

ii) Kupitia sheria zilizoanzisha Mashirika na Taasisi za Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji umezingatia taratibu, sheria na miongozo mujarabu ya biashara;

iii) Kupokea na kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu Uchambuzi wa Utendaji na Uwekezaji wa Mashirika na Taasisi za Umma. Lengo ni kupokea maoni ya Msimamizi wa Mashirika na Taasisi zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya umma;

iv) Kufanya mahojiano na Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutumia njia hizo, Kamati ilifuatilia uwekezaji huo wa Mitaji ya Umma, kwa kufanya uchambuzi na kubaini mambo makuu yafuatayo:-

i) Upungufu wa mitaji,

ii) Kutokuwepo kwa uwiano mzuri wa mapato na matumizi,

iii) Serikali kuchelewa kulipa Madeni kwa Taasisi zake,

iv) Changamoto ya Sheria ya Manunuzi ya umma,

v) Utegemezi Mkubwa wa Ruzuku ya Serikali,

vi) Uendeshaji na Utendaji usioridhisha wa Taasisi za Umma,

vii) Uwiano Hasi wa Mali kwa madeni,

viii) Uwiano Hasi wa mapato kwa mali, na

ix) Changamoto za Miundo ya Taasisi na Mashirika ya Umma.

### 2.2.1 Upungufu wa Mitaji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua Taarifa za Mashirika na Taasisi za umma na kubaini uwepo wa upungufu wa Mitaji kwa baadhi ya Taasisi za umma ambazo Serikali imewekeza. Upungufu huo umesababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na kutoleta tija inayotarajiwa. Mfano wa Taasisi zilizo na upungu wa Mitaji ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Shirika la Bima la

Taifa (NIC), Kituo cha zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Shirika la Uzalishaji mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua Taarifa ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na kubaini kuwa, Benki inashindwa kutimiza malengo yake ya kimkakati (Strategic Plan) kutokana na upungufu wa mtaji walionao. Benki ilianza na Mtaji wa **Shilingi Bilioni 60** ingawa Mtaji ulioidhinishwa (Authorised Capital) ni **Shilingi Bilioni 800**. Kiasi hicho ni pungufu kwa **asilimia 92.5.** Ili kufikia lengo la mtaji ulioidhinishwa, Serikali iliahidi kutenga katika Bajeti yake ya kila Mwaka kiasi cha **Shilingi Bilioni 100** kwa muda wa miaka nane. Kwa msingi huo, hadi kufikia Mwaka 2016 Benki ilipaswa kuwa na mtaji wa **Shilingi Bilioni 300**. Hata hivyo hadi Benki inawasilisha Taarifa yake mbele ya Kamati Benki hiyo haikupata mtaji ulioahidiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** upungufu wa mtaji pia unalikumba Shirika la Bima la Taifa (NIC) ambapo shirika lilitakiwa kuwa na mtaji wa **shilingi Bilioni 5.12** lakini hadi kufikia Juni, 2017 shirika lilikuwa na mtaji wa **shilingi bilioni 2.95** pekee ikiwa ni **asilimia 57.5** ya mtaji wote unaohitajika**.**

### 2.2.2 Kutokuwepo kwa Uwiano Mzuri wa Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchambua mizania ya Mashirika mbalimbali ya umma ilibainika kuwa, baadhi ya Mashirika ya Umma yana matatizo kwenye uwiano wa mapato na matumizi kwa kuwa yamekuwa yakitumia kiasi kikubwa cha mapato au mapato yote yanayozalishwa na zaidi hali inayosababisha Taasisi hizo za Umma kutokuwa na ziada au kupata nakisi. Mfano wa Taasisi hizo ni Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa (DDCA) ambapo taarifa inaonesha kuwa, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2016 uwiano wa mapato na matumizi ulikuwa **0.99:1** tafsiri ni kuwa kwa kila **shilingi 1** iliyozalishwa na wakala, **senti 99** ilitumika kwa matumizi mbalimbali. Vile vile, Taarifa ya Shirika la uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa ( SUMA JKT) inaonesha kuwa, uwiano

wa mapato na matumizi ulikuwa unatofautiana mwaka hadi mwaka ambapo katika mwaka 2014/15 uwiano ulikuwa **0.86:1** ukimaanisha kuwa kwa mapato ya **shilingi 1000** yaliyokuwa yakipatikana kulikuwa na matumizi ya shilingi 860. Mwaka 2015/16 uwiano ulikuwa **0.87** na mwaka 2016/17 uwiano ulikuwa **0.91**.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganifu unaonesha kuwa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) imekuwa na uwiano unaobadilika kwa kuwa matumizi yaliongezeka na kupita kikomo na baadae yakapungua. Katika mwaka 2014/15, uwiano ulikuwa **152.2:1** ikimaanisha kuwa, kwa kila **shilingi 100** iliyopatikana kulikuwa na matumizi ya **shilingi 152.2**. Aidha, mwaka 2015/16 uwiano huo ulipungua na kufikia **92.7:1** ikimaanisha kuwa, kwa kila shilingi 100 kulikuwa na matumizi ya **shilingi 92.7.**

Kamati imechambua Taarifa ya Chuo Kikuu Mzumbe na kubaini uwiano usioridhisha. Uchambuzi unaonesha kuwa mwaka 2013/14 uwiano wa mapato na matumizi ulikuwa **0.97:1** ikimaanisha kuwa, kwa kila mapato ya **shilingi 1000** yaliyopatikana kulikuwa na matumizi ya **shilingi 970**. Katika mwaka 2014/15 uwiano ulikuwa **0.99:1** ambapo matumizi yaliongezeka. Mwaka 2015/16 uwiano uliongezeka zaidi hadi **1.05:1** ukimaanisha kuwa, kwa kila mapato ya **shilingi 1000** kulikuwa na matumizi ya **shilingi 1,105**.
Tatizo la uwiano wa mapato na matumizi pia limebainika katika Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

### 2.2.3 Serikali Kutolipa Kulipa Madeni Yake kwa Wakati

**Mheshimiwa Spika**, Suala lingine lililobainika ni baadhi ya mashirika kushindwa kujiendesha na kukamilisha miradi yake kwa ufanisi na kwa wakati. Hali hii inatokana na kuchelewa kulipwa madeni kutoka kwa wateja wao ikiwemo hasa Serikali kuu, Halmashauri na Taasisi za Umma.

Mfano wa mashirika ambayo yanaidai serikali madeni makubwa na ya muda mrefu ni Mamlaka ya Uchimbaji wa Visima na Mabwawa inayodai jumla ya **shilingi bilioni 2.7** na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma (DUWASA)

inayodai jumla ya **shilingi bilioni 2** ikijumuisha na Ankara ya mwezi Januari, 2017. Vile vile Shirika la Uzalishaji mali la Jeshi la kujenga Taifa (SUMA JKT) kupitia Kampuni yake ya ulinzi inadai Taasisi za Serikali na Mashirika ya umma jumla ya **Shilingi Bilioni 5.8.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikidaiwa na Bohari ya Madawa (MSD) ambapo, deni hilo limekuwa likiongezeka kwa asilimia 0.4 kutoka Shilingi **Bilioni 143.8** kwa mwaka 2016 hadi kufikia Shilingi **Bilioni 144.39** kwa mwaka 2016/17. Aidha, kiasi kilicholipwa na Serikali kwa mwaka 2016/17 ni Shilingi **Bilioni 11.2** ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi **Bilioni 70** kilichotengwa kulipwa kwa mwaka 2017/18 ambacho hakijalipwa hadi sasa.

Hali hii imesababisha mashirika hayo kudaiwa na wazabuni na kushindwa kuwalipa kwa wakati na hata kushindwa kukuza mitaji yake. Hata hivyo, Taasisi nyingi za Umma zimekuwa na uwezo mdogo wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa wao kwa kukosa mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni.

### 2.2.4 Changamoto ya Sheria ya Manunuzi ya Umma

**Mheshimwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini upungufu katika Sheria ya manunuzi ya Umma. Kamati imepitia taarifa ya Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa (DDCA) na kubaini changamoto inayotokana na Sheria ya Manunuzi. Sheria ya manunuzi ya Umma imeangalia Taasisi za Serikali kama Taasisi nunuzi (*Procuring Entity*) na haikuzingatia Taasisi za Serikali kama Mkandarasi. Kutokana na hali hiyo, Wakala umekuwa ukikosa kazi kwa kuchelewa kwa michakato ya ununuzi hususan miradi ya uchimbaji ambayo utekelezaji wake ni wa muda mfupi. Aidha Taasisi imekuwa ikinunua vifaa kwa bei kubwa. Pamoja na changamoto hiyo, Wakala inaelekezwa kuzingatia Sheria na taratibu za ununuzi.

Aidha, Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi (VETA) imekabiliwa na changamoto hiyo kwa kuwa utekelezaji wa miradi

unahusisha kutumia taratibu za Benki ya AFDB na PPRA kwa pamoja hatua inayochangia ucheleweshaji katika kutekeleza miradi kwa wakati.

Vilevile, Bohari ya Madawa (MSD) inakabiliwa na changamoto ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ambapo, kutokana na muda mrefu unaotumika katika kukamilisha mchakato wa manunuzi ya madawa nje ya nchi, MSD imekuwa ikitumia gharama kubwa ya kutunza dawa kwa muda mrefu kwakuwa mchakato wa kupatikana kwa dawa zilizoagizwa nje ya nchi unachukua takriban miezi tisa pamoja na kupunguza ufanisi wa dawa.

### 2.2.5 Utegemezi Mkubwa wa Ruzuku ya Serikali

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa taarifa mbalimbali za Mashirika ya umma, Kamati imebaini kuwa baadhi ya mashirika na taasisi za umma zinategemea kwa kiasi kikubwa ruzuku ya serikali katika kujiendesha na kutekeleza miradi yake. Hali hii imezifanya baadhi ya taasisi kutokuwa na juhudi ya kutafuta mtaji na kutegemea Serikali kupita kiasi. Baadhi ya taasisi ambazo zimeshindwa kutekeleza majukumu yake pale Serikali iliposhindwa kuchangia au kuchelewesha hela za ruzuku ni pamoja na Bodi ya Utalii, Shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Aidha, kumekuwa na uwiano usio mzuri katika Taasisi za Umma zinazofanya uwekezaji kwani Taasisi nyingi zimekuwa zikitegemea kuwezeshwa na Serikali kwa kiasi kikubwa (ruzuku) pasipo kutegemea mikopo kutoka taasisi za fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Taasisi na kurejesha mikopo hiyo. Hali hii imefanya Mashirika ya Umma kushindwa kuwajibika ipasavyo (accountability).

Uchambuzi uliofanywa na Kamati katika taarifa ya Shirika la Elimu Kibaha umebaini kuwa, uwiano wa Ruzuku ya Serikali kwa mapato ya jumla ya Shirika unaonesha kuwa, Ruzuku ya Serikali ni sawa na wastani wa **asilimia 73** ya mapato

yote kwa kila mwaka. Hivyo mapato ya ndani ya Shirika yanachangia wastani wa **asilimia 27** tu ya mapato yote. Hali hii inatokana na Shirika kushindwa kutumia vizuri vyanzo vya ndani kwa ajili ya kujipatia mapato.

### 2.2.6 Utendaji na uendeshaji usioridhisha wa Taasisi na Mashirika ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulijikita katika utendaji na uendeshaji wa Taasisi za Umma. Katika eneo hili, Kamati ilifanya uchambuzi katika maeneo makuu matatu ambayo ni; Viongozi wa Taasisi kutopewa Mikataba ya ufanyaji kazi (Peformance Base Contract), Taasisi kujiendesha kwa hasara na matumizi makubwa, Taasisi kutokuwa na vipaumbele katika kutekeleza miradi na kufanya kazi zilizo nje ya jukumu la msingi

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo la utendaji na uendeshaji wa taasisi za umma, kamati ilibaini kuwa Taasisi nyingi zimeshindwa kufikia malengo yake kwa kiwango kilichotarajiwa kwa kuwa katika Mikataba ya utendaji kazi ya viongozi wa Mashirika, hapakuainishwa kipimo cha utendaji kazi na muda wa utekelezaji wa miradi (Performance Based Contract). Hali hii inasababisha miradi ya Taasisi hizo kutokamilika kwa wakati na kutoleta tija iliyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwa taasisi nyingi zimekuwa zikijiendesha kwa hasara kwa sababu mbalimbali ambazo ni matumizi makubwa kuliko mapato, Mfano matumizi ya Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) yamekuwa yakiongezeka kwa kiasi kikubwa na hivyo kuifanya Kampuni kujiendesha kwa hasara. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2016/17 matumizi yaliongezeka kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa na kupelekea Kampuni kupata hasara kwa miaka yote mitatu kama ifuatavyo; mwaka 2014/15 **Shilingi 94,355,952,000.00,** mwaka 2015/16 **shilingi 109,271,250,000.00** na mwaka 2016/17 **shilingi 113,770,184,000.00.** Hali hii hairidhishi na kama itaendelea itafanya uhai wa Kampuni kuwa mashakani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini uwepo wa matumizi makubwa katika Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TAN TRADE) ambapo, Mamlaka imekuwa na matumizi makubwa kuliko mapato hali iliyosababisha kuwepo kwa **nakisi** ya kiasi cha **shilingi Milioni 397.9** mwaka 2013/14, **shilingi milioni 614.6** mwaka 2014/15 na **shilingi milioni 838.2** mwaka 2015/16.

Uchambuzi umebaini kuwa, ongezeko hili kubwa la matumizi limechangiwa na ongezeko la matumizi mengineyo, mishahara na gharama za utawala wakati gharama za uwekezaji (gharama za maonesho na kutangaza bidhaa na gharama za utafiti) zimepungua kutoka **asilimia 32.5** mwaka 2011/12 hadi **asilimia 16.8** mwaka 2015/16 ambazo kimsingi zilipaswa kupanda kwa lengo la kukuza kipato cha taasisi hii.

Kupungua kwa uwekezaji kumeathiri mapato yatokanayo na upangishaji kipindi kisicho cha maonesho, maonesho ya viwanda, elimu na Uhuru ambapo mapato yalipungua kutoka **asilimia 22.3** ya mapato yote mwaka 2011/12 hadi **asilimia 8.5** ya mapato yote mwaka 2015/16. Hali hii imechangia kushuka kwa mapato mengineyo kutoka **shilingi bilioni 1,117.2** mwaka 2011/12 hadi **shilingi bilioni 546.9** mwaka 2015/16.

Vile vile, Kamati imebaini kuwa, Shirika la Elimu Kibaha limekuwa likipata **nakisi** (Deficit) kwa miaka mitano mfululizo ya wastani wa **Shilingi Bilioni 1.2** kwa mwaka. Katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo, nakisi imeongezeka kutoka **Shilingi Milioni 482** Mwaka 2012/13 hadi **Shilingi Bilioni 3.2** Mwaka 2014/15. Aidha, katika miaka miwili ya mwisho, nakisi imekuwa ikipungua hadi kufikia **Shilingi Milioni 955** Mwaka 2016/17.

**Mheshimwa Spika**, Katika upande wa vipaumbele, Kamati imebaini kuwa baadhi ya taasisi zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya umma hazina vipaumbele katika kuwekeza mitaji yake kwenye miradi ya maendeleo. Taasisi zimekuwa zikitawanya mtaji mdogo walionao kwa kuwekeza kwenye

miradi mingi kwa wakati mmoja, hali inayosababisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati na kutoleta matokeo yaliyotarajiwa. Mfano Shirika la uzalishaji Mali SUMA JKT pia limejikuta likishindwa kukamilisha miradi yake kwa kuwa haikuweka vipaumbele katika miradi yake na kuamua kuanzisha miradi mingi kwa wakati mmoja wakati mtaji wake hauwezi kuikamilisha yote kwa pamoja.

Vile vile, Taasisi zimekuwa zikifanya uwekezaji mkubwa kwenye miradi ambayo haiendani na jukumu la msingi la kuazishwa kwa taasisi husika. Mfano, Chuo kikuu cha Mzumbe kwa kiasi kikubwa kimeacha jukumu lake la msingi la kuwekeza kwenye taaluma (kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri elekezi) ambapo majukumu hayo ni vyanzo vya mapato na badala yake wamejikita kwenye miradi ya majengo na ardhi ambapo mtaji umetawanywa kiasi cha kugeuka mzigo mkubwa wa kulipa kodi ya ardhi na majengo ambayo bado hayajaanza kuzalisha.

### 2.2.7 Uwiano Hasi wa Mali kwa Madeni

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi mwingine wa Kamati ulilenga katika kuangalia uwiano wa ulipaji wa madeni kwa mali. Taarifa zilizochambuliwa na Kamati zimeonesha mapungufu kwa baadhi ya Taasisi za Umma ambapo zimeshindwa kulipa madeni yake kwa kutumia mali zake.

Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Shirika la Elimu Kibaha (KEC) na kubaini hali mbaya ya **ukwasi**. Hali ya ukwasi ya Shirika ni mbaya kwa kuwa mali za muda mfupi haziwezi kulipa madeni yake ya muda mfupi inapolazimika kufanya hivyo. Hali hii inaoneshwa na uwiano wa mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi (current Asset Ratio) ambao ni 0.36:1 badala ya uwiano wa 2:1. Shirika linatakiwa kuwa na mkakati wa kuongeza mapato ya Taasisi.

Aidha, uwiano wa mali kwa madeni wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) hauridhishi kwani sehemu kubwa ya mali zake zimelipwa kwa madeni na kiasi kidogo tu cha mali kimelipwa kwa mtaji. Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 uwiano wa mali

kwa madeni ulikuwa asilimia 77.6 ambao ni mkubwa, hali hii kama itaendelea inaweza kusababisha Bodi kufilisiwa ili kulipa madeni husika.

#### 2.2.8 Uwiano Hasi wa Mapato kwa Mali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imechambua pia uwiano wa mapato kwa mali wa Taasisi za Umma na kubaini changamoto za kiutendaji katika upande wa mapato yatokanayo na mali. Changamoto hiyo ilionekana kwenye Shirika la Elimu Kibaha ambapo, uwiano wa mapato kwa mali (Revenue to Asset) ambao ni asilimia 11 unaashiria kuwa, Shirika limeshindwa kutumia vyema mali zake kwa ajili ya kuzalisha mapato. Uwiano huu umejumuisha mapato yanayotokana na ruzuku. Aidha, iwapo mapato ya ndani pekee yatahusishwa, uwiano utakuwa ni asilimia 3. Hali hiyo imesababishwa na kuwepo majengo mengi ya shule na vyuo ambavyo havizalishi mapato ya kutosha. Vile vile, Shirika limekuwa na viwanja vingi ambavyo havitumiwi na vingine vimekodishwa kwa mikataba ambayo haileti mapato ya kutosha.

#### 2.2.9 Changamoto za Miundo ya Taasisi na Mashirika ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Ufanisi wa utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma unapimwa kutokana na vigezo mbalimbali. Moja ya vigezo hivyo ni Muundo wa Taasisi ambao unaiwezesha Taasisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Miundo ya baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma haiendani na mazingira wala mwelekeo wa kufanya uwekezaji wenye tija na kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Miundo ya Taasisi za Umma zilizo nyingi iliandaliwa wakati wa uanzishwaji wa Taasisi hizo. Kutokana na mabadiliko ya muda na teknolojia, miundo hiyo imekuwa haiendani na wakati wa sasa na kutokidhi mahitaji ya Taasisi za Umma. Baadhi ya taasisi ambazo zinahitaji kufanyiwa marejeo katika miundo yake ni Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Shirika la Uzalishaji mali JKT (SUMA JKT), Kituo

cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB)

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Taarifa za Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ulibaini kuwa, Muundo wa Benki umempa mamlaka Gavana wa Benki kuwa Mwenyekiti wa Bodi na wakati huo huo ni Mtendaji Mkuu wa Benki. Muundo huu unakinzana na uendeshaji mzuri wa Taasisi kwani Mwenyekiti wa Bodi atashindwa kuisimamia Taasisi ipasavyo kwa kuwa ndiye Mtendaji Mkuu.

## 2.3 Changamoto za Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 changamoto kadhaa zilijitokeza, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

### i) Muda mchache wa kupitia Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inaipa Kamati mamlaka ya kuchambua Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa. Jumla ya Taasisi hizo ambazo zipo chini ya Msajili wa Hazina ni 269. Aidha, kutokana na muda ambao umekuwa ukitengwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za Kamati, imekuwa ni shida kwa Kamati kuweza kupitia idadi kubwa ya Taasisi na Mashirika ya Umma ili kubaini iwapo uwekezaji wa Taasisi hizo una tija kwa Taifa.

Aidha, Kwa mwaka 2016, Kamati iliweza kuchambua Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma Arobaini na Moja (41) kati ya Mia Mbili Arobaini na Tatu (243). Idadi hiyo imepungua ambapo, kwa mwaka 2017 Kamati imechambua Taarifa za jumla ya Taasisi na Mashirika ya Umma yapatayo Ishirini na Tatu (23) kati ya Taasisi Mia Mbili Sitini na tisa (269) zilizo chini ya Msajili wa Hazina.

### ii) Ziara za Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati imepokea na kuchambua Taarifa ya Taasisi na Mashirika ya Umma Ishirini na Tatu (23) ambapo kamati imepata nafasi ya kufanya ukaguzi wa miradi ya uwekezaji katika Taasisi Tatu pekee. Kamati imeshindwa kufanya ukaguzi katika Taasisi ambazo zimewasilisha taarifa zake mbele ya Kamati kutokana na ufinyu wa muda uliopangwa kwa Kamati kufanya ziara. Hali hii imesababisha Kamati kushindwa kuona uhalisia wa miradi inayosimamiwa na Taasisi za Umma na kutoa ushauri stahiki.

### iii) Changamoto za Kisheria

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ilikabiliwa na changamoto za kisheria kama ifuatavyo:-

a) Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma hazimtambui Msajili wa Hazina kama Msimamizi wa uwekezaji unaofanywa na Serikali hivyo Taasisi hizo zimejikuta zikifanya uwekezaji wa mitaji ya Umma katika miradi mbalimbali bila kufuata miongozo ya uwekezaji inayotolewa na Msajili wa Hazina. Hali hii inatokana na Kutokuwepo kwa sheria moja mahsusi inayoainisha majukumu ya Msajili wa Hazina ya kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma;

b) Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 umekuwa na changamoto kwa kuwa mchakato wa manunuzi ambao umewekwa na masharti ya Sheria hii umekuwa ukichelesha utekelezaji wa miradi hali inayosababisha gharama za mradi kuongezeka pamoja na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji wa mradi. Baadhi ya masharti ya Sheria ya Manunuzi yaliyoainishwa ni:-

i) Utaratibu wa mchakato wa Manunuzi kuanzia siku za kutangaza zabuni( local 21days/ 30 days international) hadi mchakato wake ukamilike;

ii) Utaratibu wa kumchukua mzabuni mwenye bei ya chini (Lowest bidder);

iii) Utaratibu wa rufani kwa mzabuni ambaye hajaridhishwa na mchakato wa kumpata mzabuni; na

iv) Masharti yanayokataza uzabuni usifanywe moja kwa moja kati ya taasisi ya manunuzi na mzabuni.

c) Sheria za baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kuweka masharti magumu ya vyanzo vya fedha ikiwepo masharti ya ukopaji wa mitaji kutoka Taasisi za fedha Mfano SUMA JKT na Taasisi zingine ambazo zinaanzishwa chini ya Sheria *The Corporation Sole (Esterblishment) Act* Kifungu cha 5 (2) imeweka masharti kuwa Taasisi za Fedha ambazo wanazoruhusiwa kukopa ni TIB, NBC na CRDB suala la hili limekuwa kikwazo kwa Taasisi hizo kukopa mitaji.

**2.4 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliwasilisha Taarifa yake ya Mwaka 2016 mbele ya Bunge lako Tukufu. Taarifa hiyo ilijumuisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambayo Serikali ilitakiwa kuyafanyia kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake kupitia kwa Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamaizi mkuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali.

Hata hivyo, baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hayajafanyiwa kazi kikamilifu na Serikali hali inayosababisha Utendaji na Uwekezaji wa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutoleta tija kwa Taifa. Hoja ambazo utekelezaji wake haujakamilika kikamilifu ni kama ifuatavyo:-

i) Kamati ilipendekeza Mamlaka zinazohusika kufanya uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi katika Taasisi na Mashirika yote ya Umma ili Taasisi hizo zipate usimamizi madhubuti na ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa malengo ya

kuanzishwa kwa Taasisi na Mashirika hayo yanafikiwa. Aidha, pamoja na mapendekezo haya muhimu kwa Serikali, bado kuna Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo hayana Bodi za Wakurugenzi. Mfano Bodi ya Wakurugenzi ya Bohari ya Dawa (MSD) imemaliza muda wake mwaka mmoja sasa na uteuzi wa bodi mpya haujafanyika. Mfano mwingine wa Taasisi ambayo haina bodi ya wakurugenzi ni Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO)

ii) Hoja nyingine ambayo haijafanyiwa kazi kikamilifu ni upungufu wa mitaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Kamati ilipendekeza Serikali ipeleke mitaji ya kutosha kama ilivyoahidi kufanya wakati wa uanzishwaji wa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma. Hata hivyo, bado kuna Taasisi ambazo hazijapelekewa mitaji hali inayosababisha taasisi hizo kushindwa kujiendesha kwa ufanisi. Mfano wa Taasisi hizo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ambapo mtaji uliopo sasa ni **asilimia 7.5** tu ya mtaji wote unaotakiwa.

iii) Hoja ya Serikali kutolipa madeni yake kwa wakati bado haijafanyiwa kazi na Serikali kwa kuwa Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo mengi ambayo yanatoa huduma kwa Serikali yanashindwa kujiendesha na kutekeleza miradi yake kutokana na fedha nyingi wanazodai kuwa mikononi mwa Serikali.

iv) Hoja nyingine ni Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina ya Taasisi kutofanya matumizi yanayozidi asilimia 60 ya mapato ghafi. Serikali imeshindwa kuziwajibisha Taasisi na Mashirika yanafanya matumizi makubwa zaidi ya mapato hali inayopelekea Taasisi kupata nakisi.

v) Serikali haijafanyia kazi kikamilifu mapendekezo ya Kamati kuhusu Watendaji wenye sifa wanaokaimu kwa muda mrefu kuthibitishwa katika nafasi zao. Aidha, bado kuna Watendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ambao hawajathibitishwa na wamezitumikia nafasi hizo kwa muda mrefu hali inayowafanya wakose mamlaka kamili katika utendaji kazi na hivyo kupunguza ufanisi.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

**3.1 Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kuhusiana na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-
Taasisi na Mashirika ya Umma yameendelea kukosa ufanisi na tija kutokana na kutozingatia miongozo mbalimbali ya kibiashara. Taasisi na Mashirika ya Umma yanayotegemea ruzuku ya Serikali bado hayajaweza kuwa na mikakati madhubuti ya kujiondoa kwenye utegemezi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa Serikali iliyaanzisha Mashirikia hayo ili kutoa huduma bora kwa jamii. Hata hivyo, miundo isiyoendana na mazingira wala mwelekeo wa uwekezaji wenye tija imesababisha mashirika hayo kukosa ufanisi na tija.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida inayotokana na uwekezaji wa mitaji ya umma kuongezeka kutoka **shilingi billion 422** kwa mwaka 2016 hadi **Shilingi bilioni 885** kwa mwaka 2017, bado faida hiyo ni kidogo ikilinganishwa na uwekezaji ambao serikali imeufanya kwenye mashirika hayo.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya sababu zilizopelekea ongezeko la faida hiyo ni maoni na mapendekezo ambayo Kamati hii iliyatoa kwenye taarifa yake ya mwaka 2016/17.

### 3.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maoni ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa mitaji ya umma, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

#### 3.2.1 Upungufu wa Mitaji

**Kwa kuwa,** baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo Serikali imewekeza zimebainika kuwa na upungufu wa mitaji,

**Na kwa kuwa,** upungufu huo umesababisha Taasisi na Mashirika hayo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na kutoleta tija inayotarajiwa,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali ipeleke mitaji kwa Taasisi na Mashirika ambayo iliahidi kufanya hivyo wakati wa uanzishwaji wa Taasisi hizo ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija.

### 3.2.2 Kutokuwepo kwa Uwiano Mzuri wa Mapato na Matumizi

**Kwa kuwa**, uwiano wa mapato na matumizi kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma umekuwa si wa kuridhisha kutokana na Taasisi nyingi kuwa na kiasi kikubwa cha matumizi ikilinganishwa na mapato,

**Na kwa kuwa,** matumizi makubwa yamekuwa yakisababisha Taasisi na Mashirika ya umma kutokuwa na ziada na kupata nakisi,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali:-

a) Iziagize Taasisi za umma ziweze kupunguza matumizi yasiyoendana na uwekezaji ili Taasisi hizo zijielekeze zaidi katika kufanya uwekezaji wenye tija, na

b) Iziagize Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 na kuziwajibisha endapo zitavuka kiwango cha matumizi cha asilimia 60 ya mapato ghafi.

### 3.2.3 Serikali Kutolipa Madeni Yake Kwa Wakati

**Kwa kuwa,** Serikali imekuwa na utamaduni wa kutolipa madeni yake kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa wakati baada ya kupata huduma,

**Na kwa kuwa,** hali hiyo imesababisha Taasisi na Mashirika ya Umma kushindwa kujiendesha na kukamilisha miradi yake kwa ufanisi na kwa wakati,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali ilipe madeni ambayo inadaiwa na Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha, Serikali iendelee kulipia huduma inazozipata kwa wakati ili Taasisi na Mashirika ya Umma yaweze kujiendesha.

### 3.2.4 Changamoto ya Sheria ya Manunuzi ya Umma

**Kwa kuwa,** Sheria ya manunuzi ya umma imeangalia Taasisi za Serikali kama Taasisi zenye kufanya manunuzi na kutozingatia kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali ni mkandarasi,

**Na kwa kuwa,** upungufu huo wa Sheria ya manunuzi ya umma umesababisha Taasisi za umma ambazo ni Mkandarasi kukosa kazi kwa kuchelewa kwa michakato ya ununuzi kutokana na miradi yake kuwa ni ya muda mfupi,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali iondoe changamoto za Sheria ya manunuzi ya umma zinazokwamisha utekelezaji wa miradi kwa baadhi ya taasisi za umma.

### 3.2.5 Utegemezi Mkubwa wa Ruzuku ya Serikali

**Kwa kuwa,** taarifa mbalimbali za Taasisi na Mashirika ya umma zimebainisha kuwepo kwa utegemezi mkubwa wa ruzuku ya Serikali katika kujiendesha na kutekeleza miradi yake,

**Na kwa kuwa,** Hali hii imezifanya Taasisi hizo kutokuwa na ufanisi na kushindwa kutekeleza majukumu yake pale Serikali iliposhindwa kuchangia au kuchelewesha hela za ruzuku,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali izisimamie vizuri taasisi zake ili ziweze kuwa wabunifu na kutumia rasilimali walizonazo kwa ufanisi ili ziweze kujiendesha kibiashara, kuzalisha mapato, kupunguza na hata kuachana na utegemezi wa Serikali.

### 3.2.6 Utendaji na Uendeshaji usioridhisha wa Taasisi na Mashirika ya Umma

**Kwa kuwa,** Uendeshaji na Utendaji wa Taasisi za Umma umekuwa na changamoto ya Viongozi na watendaji wa taasisi kutopewa mikataba ya ufanyaji kazi *(Performance based Contract),*

**Na kwa kuwa,** ukosefu wa mikataba hiyo husababisha kukosekana kwa kipimo stahiki cha utendaji wa kazi na muda wa utekelezaji wa majukumu yao na hivyo kuyafanya mashirika yaendeshwe kwa hasara,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina, iweke utaratibu madhubuti utakaowalazimu Viongozi na Watendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma kufanya kazi zao kulingana na vipimo vilivyowekwa (Performance Based Contract) ili kuyafanya mashirika yaendeshwe kwa ufanisi na tija

### 3.2.7 Uwiano Hasi wa Mali kwa Madeni

**Kwa kuwa,** Taarifa zilizochambuliwa na Kamati zimeonesha mapungufu kwa baadhi ya Taasisi za Umma ambazo zimeshindwa kulipa madeni yake kwa kutumia Ukwasi,

**Na kwa kuwa,** hali hii kama itaendelea inaweza kusababisha Taasisi na Mashirika ya Umma yenye tatizo la uwiano usioridhisha kufilisiwa ili kulipa madeni wanayodaiwa,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali iboreshe usimamizi wa Taasisi na Mashirika yake ili kuongeza tija pamoja na kulipa madeni ya muda mfupi na muda mrefu.

### 3.2.8 Uwiano Hasi wa Mapato kwa Mali (*Revenue to Asset*)

**Kwa kuwa,** Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo mengi yamekosa ubunifu na kushindwa kutumia vyema mali zake kwa ajili ya kuongeza mapato na kusababisha uwiano wa mapato kwa mali kutoridhisha,

**Na kwa kuwa,** kukosekana kwa uwiano mzuri wa mapato kwa mali kumesababishwa na mali za Taasisi na Mashirika ya umma kutotumika kuongeza mapato hivyo kuzifanya Taasisi kutumia mali zake chini ya kiwango na kukosa tija inayotarajiwa,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali izitake Taasisi na Mashirika yake kuzitumia vizuri mali zake kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuleta tija inayokusudiwa.

### 3.2.9 Changamoto za Miundo ya Taasisi na Mashirika ya Umma

**Kwa kuwa,** Miundo ya baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma haiendani na mazingira wala mwelekeo wa uwekezaji wenye tija kutokana na mabadiliko ya muda na teknolojia,

**Na kwa kuwa**, miundo hiyo kutokidhi mahitaji ya sasa ya Taasisi na Mashirika hayo imekuwa kikwazo cha utendaji na utekelezaji mzuri wa majukumu ya Taasisi husika na kutofikia tija iliyotarajiwa,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ifanye mapitio/marejeo ya miundo ya Taasisi na Mashirika ambayo imeonekana kutokidhi mahitaji ya sasa ili kupata miundo inayokidhi mahitaji ya sasa ya mashirika na kuleta ufanisi.

### 3.2.10 Changamoto za Kisheria

**Kwa kuwa**, Uchambuzi wa Kamati katika eneo la Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma umebainisha changamoto mbalimbali zinazokwamisha Utendaji wenye ufanisi ikiwa ni pamoja na Kukosekana kwa Sheria moja inayoelezea majukumu ya Msajili wa Hazina,

**Na Kwa kuwa,** Changamoto hizo zimesababisha Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma kutoleta tija kutokana na kukosekana kwa usimamizi madhubuti,

**Kwa hiyo basi,** Bunge linashauri kuwa Serikali iwasilishe Bungeni muswada wa sheria unaoainisha kwa ufasa na kubainisha majukumu yote ya Msajili wa Hazina ili kuimarisha usimamiaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, Kamati imeweza kutekeleza majukumu yake kutokana na maelekezo ya kiti chako. Vile vile, Kiti chako kimeweza kutoa ushauri na msaada kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Prof. Osward Mashindano Msajili wa Hazina kwa ushirikiano wake alioutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika ya Umma ziwe na ufanisi katika utendaji na uwekezaji na kuleta tija kwa Taifa. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-
1. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba, Mb – M/Mwenyekiti

3. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb _ Mjumbe
4. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb _ Mjumbe
5. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Fatuma Hassan Toufiq, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Juma Othman Hija, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Maftah Abdallah Nachuma, Mb -Mjumbe
13. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb Mjumbe
14. Mhe. Muhammed Amour Muhammed, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Othman Omar Haji, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Riziki Saidi Lulida, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb- Mjumbe
19. Mhe. Sannda Edwin Mgante, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Stephen Hilary Ngonyani, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Zainab Athuman Katimba, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Zaynab Matitu Vulu, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati, Ndugu Amina Salumu na Ndugu Elieka Saanya na msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde. Pia tunawashukuru Watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphine Tamba, Ndugu Matamus Fungo na Ndugu Hawa Manzurya pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

## 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na

Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni ya Kamati na Mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, na kuijadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili hatimaye Serikali iyafanyie kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa Hoja.

……………………………….
Mhe. Albert O. Ntabaliba, Mb
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.**

02 Februari, 2018

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti kwa wasilisho lako, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Tunaendelea na taarifa inayofuata inawasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Murad Saddiq, Mbunge wa Mvomero. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi mchana wa leo na mimi niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kusimama katika eneo hili siku ya leo. Sambamba na hilo, naomba niwashukuru wananchi wangu wa Mvomero kwa

kuniamini, naomba waendelee kuniamini, nitaendelea kuwatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa namna ya kipekee wamenipa ushirikiano wa kutosha, tumefanyakazi pamoja na hatimae leo nipo hapa kwa niaba yao ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu nawasilisha taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imezifanya katika kipindi cha kuanzia Machi, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayowasilisha mezani mapema leo asubuhi ina sehemu kuu nne zinazoelezea maelezo ya ujumla, uchambuzi, matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati, inabainisha maoni, ushauri, mapendekezo na hitimisho la taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati yameelezwa katika fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu hayo yamerejewa katika taarifa ya Kamati. Naomba taarifa hii iingizwe yote kwenye *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 imeruhusu Kamati kupendekeza kupewa majukumu ya nyongeza au Spika kuipatia Kamati majukumu ya nyongeza. Naomba kuliarifu Bunge hili kuwa Mheshimiwa Spika, hakutupa majukumu ya nyongeza hivyo Kamati imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kupokea na kujadili taarifa ya Kamati;

(ii) Utekelezaji kutoka kwenye Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira; na

(iii) Kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi wa maendeleo, Kamati ilipata pia fursa ya kutembelea viwanda binafsi ambavyo vinachakata malighafi zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilikutana na wadau mbalimbali katika sekta za viwanda, biashara, uwekezaji na mazingira. Kamati ilifanikiwa kuhudhuria semina mbalimbali kwa lengo la kujijengea uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu shughuli zilizofanywa na Kamati. Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati pia ilipokea na kuchambua Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ya Wizara, Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali. Aidha, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara inayosimamia pamoja na baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kwa kipindi cha nusu mwaka 2017/2018 kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi ambazo zilikutana na Kamati katika kipindi hiki ni pamoja na Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE),* Wakala wa Usajili wa Leseni *(BRELA),* Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC),* Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* Wakala wa Vipimo *(WMA),* Mamlaka ya *EPZ* na Shirikisho la Viwanda Vidogo *(SIDO).* Aidha, Kamati ilikutana na Baraza la Uhifadhi wa Mazingira *(NEMC)* iliyopo Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo illiyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ili kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo, Kamati pia ilitembelea miradi

isiyotengewa fedha vikiwemo viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa lengo la kujifunza shughuli zao, mafanikio na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira kwa ajili ya kusikiliza maoni yao. Wadau mbalimbali walifika mbele ya Kamati kutoa maoni na ushauri na kueleza changamoto zao katika namna ya kuboresha sekta ya Viwanda Biashara, Uwekezaji na Mazingira. Wadau waliofika mbele ya Kamati ni pamoja na *CTI* na viwanda vingi vilivyoko chini ya *CTI* ambao ni wanachama wake wakiwemo *SAYONA, CocaCola, Ivory, Five Star, Anjari,* Viwanda vya Maziwa, *Serengeti Breweries* na *Coca Cola Kwanza.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilihudhuria mafunzo, semina na kukutana wadau mbalimbali. Mafunzo yalihusu sekta zilizo chini ya Wizara inazosimamia na yalilenga kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata mafunzo yaliyosimamiwa na Mradi wa *Legislative Support Program* ulio chini ya Ofisi ya Bunge na Shirika la Mazingira la *Heifer International.* Aidha, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria kikao cha majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kuhusu namna ya kuhamasisha na kukuza sekta za Viwanda, Biashara na uwekezaji. Kamati inaipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuandaa mikutano ya namna hii ambayo inasaidia kukuza uchumi na kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya pili ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Kamati ilitekeleza majukumu yake katika kipindi cha Machi, 2017 hadi Januari, 2018 kwa kuwa taarifa yetu ya mwisho tuliitoa hadi Machi, 2017. Katika kipindi cha kuanzia Machi, 2017 hadi Januari, Wajumbe walipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu za Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo. Kutokana na changamoto ya muda nitawasilisha taarifa chache lakini nitaomba taarifa nyingine ziingie kwenye *Hansard* kama zilivyo kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokea taarifa ya kujadili viwanda, biashara kupitia *CTI.* Kamati ilipata fursa ya kukutana na Shirikisho la wenye Viwanda Nchini *(CTI)* na baadhi ya wamiliki kwa lengo la kufahamu majukumu ya shirikisho, changamoto za wadau, mafanikio yao pamoja na maoni ya juu ya namna ya kuboresha sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirikisho hili linatekeleza majukumu mbalimbali, kuiwakilisha, kuisemea Serikalini jumuiya katika kuwakilisha mambo ambayo yanaleta changamoto katika kufanya biashara. *CTI* pia hufanya tafiti na kushauri kwa mambo yanayotatiza jumuiya, kuviwakilisha viwanda katika majadiliano katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, *EAC* na *SADC,* kutoa taarifa za biashara, wawekezaji, wazalishaji na washirika wao, kusuluhisha migogoro kati ya Serikali na wanachama inapotokea na kuiwakilisha jumuiya katika kuandaa viwango vya kodi wakati wa kuandaa bajeti

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza changamoto zifuatazo kutoka *CTI:-*

(i) Mabadiliko ya mara kwa mara ya kodi; Serikali katika mwaka wa fedha imekuwa ikifanya mabadiliko ya mfumo wa kodi ambao hupelekea mabadiliko ya vivutio mbalimbali vya uwekezaji. Wawekezaji wengi huvutiwa kuwekeza mahali palipo na mfumo wa kodi unaotabirika na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Mabadiliko ya mara kwa mara yanapunguza sifa ya kuwa na mazingira mazuri ya biashara na hivyo kuwafukuza wawekezaji.

(ii) Marejesho ya kodi ya thamani *(VAT Refund)*. Wazalishaji wengi waliofika kwenye Kamati walikuwa wanalalamika kuhusu changamoto ya upungufu wa mitaji waliyonayo ambayo inatokana na wao kutorudishiwa *refund* katika *VAT,* hili ni suala nyeti ambalo limechukua fedha nyingi na naomba nitaje tu mfano wa viwanda viwili lakini bado kuna viwanda vingi vinadai fedha hizi. Kiwanda cha *CocaCola refund* yake ni *4.5 billions,* kiwanda cha *A2Z*

wanadai *9.6 billions* na viwanda vingine kama Kioo na wengine wanadai kama *1.9 billions,* lakini kuna orodha ndefu ya wale wanaodai *refund* ya *VAT.* Hili ni suala ambalo tutahitaji Serikali ikae na wadau waone namna ya kuhakiki hizi *refund* ili waweze kurudishiwa waendelee na mitaji yao ya kuungana na Serikali katika azma ya Tanzania ya viwanda

(iii) Uingizaji wa bidhaa zisizokidhi viwango na *fake* kwa njia za panya. Uingizaji wa bidhaa kwa njia za panya hivyo kukwepa kodi na kupelekea bidhaa hizo kuuzwa kwa bei rahisi na kusababisha viwanda vya ndani ambavyo ninalipa kodi kushindwa kushindana na bidhaa hizo katika soko. Hili tumelizungumza na tumetoa ushauri kwa wadau ambao walikuja mbele ya Kamati.

(iv) Uwepo wa mamlaka nyingi za udhibiti katika ushirikiano hafifu baina yake na uwepo wa mamlaka nyingi za udhibiti ambazo zinafanyakazi zinazofanana. Mfano, *TBS, TFDA,* Mkemia Mkuu, *OSHA, NEMC, Fire* wakati mwingine Manispaa, hawa wote wanafanyakazi zinazofanana na kila kukicha wanakwenda kwenye viwanda na kuleta usumbufu ambao unapunguza uzalishaji na gharama zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yaliyozungumzwa na wadau kwa upande huo lakini suala lingine lililozungumzwa ni kukosekana kwa nishati ya umeme wa uhakika. Wadau waliofika mbele ya Kamati mmoja alionesha barua kutoka Tanga - *TANESCO* ikisema kwamba anatakiwa kuzalisha kuanzia saa mbili usiku mpaka saa mbili asubuhi, mchana haruhusiwi kuzalisha, *TANESCO* imempa barua hiyo afanye uzalishaji kwa muda wa miezi mitatu. Kwa hali kama hiyo viwanda vingi vitaendelea kuzalisha kwa kiwango cha chini, tunaiomba Serikali ilisimamie hili suala la nishati ya umeme kwa uhai wa viwanda vyetu. Pamoja na juhudi nyingi zlizopo lakini tunaomba Serikali ilisimamie tuhakikishe viwanda vinaendelea kufanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la kuanzishwa kwa utaratibu mpya wa ulipaji kodi wa *electronic tax stamp*; viwanda vya pombe, sigara, soda, maji wamepewa taarifa

na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kuwa mamlaka hiyo inatarajia kuleta utaratibu wa *electronic* wa kukusanya kodi ambazo watatumia Taasisi ya Kiswiss ambao watafunga mtambo katika mifumo ya uzalishaji kwa ajili ya kupima uzalishaji na kiwanda kitalipa kodi ya dola za Marekani 10 kwa *unit* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mfumo huu kama utaingizwa utaongeza gharama kwa viwanda kwa asilimia 50 ya kodi inayokusanywa na hatimaye viwanda vitaongeza bei ya bidhaa na kumuumiza mlaji. Pia inaweza kupunguza soko la bidhaa na gharama za kukusanya kodi hii itakuwa kubwa kuliko mapato ya Serikali. Kamati inaomba suala hili Serikali ilifanyie kazi kwa kina ili likija likifanyika lilete tija kwa Taifa lisije likaleta upungufu wa kodi.

Mheshimiwa mwenyekiti, upatikanaji wa vibali vya sukari viwandani na nyongeza ya asilimia 15 ya kodi kuingiza sukari ya viwandani. Kuna usumbufu usio wa lazima katika kuagiza na kutoa sukari ya viwandani kutoka Bandarini, hili linasababisha baadhi ya viwanda kupunguza uzalishaji na vingine kufungwa kabisa. Aidha, wawekezaji walilalamika mbele ya Kamati kuhusu nyongeza ya asilimia 15 ya kodi kuingiza sukari ya viwandani ambayo ilikuwa irudishwe baada ya kuingiza mzigo na kufanyiwa uhakiki. Fedha hii hairudishwi kwa wakati jambo linalopelekea kupungua kwa mitaji yao. Mfano; viwanda vinavyodai nyongeza ya asilimia 15 kwa kuingiza sukari ya viwandani ni pamoja na *CocaCola* wanadai bilioni 5.5, Kiwanda cha *Pepsi* wanadai bilioni 8.4 na kiwanda cha *Bakhresa Group Company* wanadai bilioni tisa na viwanda vingine vingi taarifa yake ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muingiliano wa mamlaka za Serikali yaani Ardhi, Uchukuzi na Viwanda kushindwa kufanya kazi pamoja. Taasisi za Serikali hazina uelewa mmoja katika kuhamasisha wawekezaji, wafanyabiashara na wenye viwanda na inasababaisha usumbufu mkubwa kiasi cha kuamua kufunga baadhi ya viwanda. Hili tunaomba Serikali ilifanyie kazi na waliokuja kwenye Kamati walikuja na ushaihidi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa malighafi ya kutengeneza karatasi *(unbleache paper).* Tanzania ina kiwanda kimoja tu ambacho kinazalisha malighafi ya kutengeneza karatasi ambazo hutumika kutengeneza maboksi, kiwanda hicho ni *Mufindi Paper Mill na* kwa kuwa kinatumia malighafi za ndani kimewekewa kinga kwa kutoza ushuru wa asilimia 25 ya aina za bidhaa wanazozalisha wao zinazotoka nje ya nchi, suala hili ni zuri kwani Serikali imelinda kiwanda chake cha ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha Mufindi kinazalisha malighafi hiyo na kiasi kikubwa sana inazipeleka katika viwanda vyake vilivyopo nchini Kenya na baadae kuzalisha maboksi na kuyaingiza kama *packing material* katika soko la Tanzania. Viwanda vya ndani vinakosa malighafi hiyo na kuamua kuingiza kutoka nje ya nchi na kutozwa kodi ya asilimia 25 na hivyo kuvifanya viwanda hivyo kuwa na gharama kubwa zaidi ya bidhaa zake kuliko bidhaa za nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina viwanda 17 vya bidhaa ya karatasi na uzalishaji wa malighafi hiyo kutoka katika kiwanda cha Mufindi haukidhi mahitaji ya ndani. Kamati inashauri iangalie upya kodi za malighafi kutoka nje ili kuleta ushindani sawia na viwanda vya nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya kodi 10% katika mafuta ghafi ya mchikichi. Serikali iliongeza kodi asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya michikichi yanayoagizwa kutoka nje kwa lengo la kulinda viwanda vinavyozalisha mafuta kutokana na mbegu, nchi za Afrika Mashariki zilikubaliana kuingiza mafuta bila kodi *zero rate.* Hatua hii inavipunguzia ushindani wa ndani viwanda vinavyoagiza malighafi ya michikichi *crued palm oil,* Kamati ina maoni kwamba mafuta ya michikichi siyo mbadala wa mafuta ya alizeti.

Kamati inashauri Serikali kuondoa kodi hiyo ili kuwapa uwezo viwanda vya ndani kukabiliana na ushindani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwapa unafuu walaji wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huu Serikali ifanye utafiti wa kina katika eneo hili tusije tukaua viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi ya ndani hasa malighafi inayotakana na wakulima wetu wa alizeti na mazao mengine. Kamati inashauri Serikali iwe makini katika eneo hili ili tusije tukaleta matatizo mengine badala ya kuondoa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT)* kwenye bidhaa ya maziwa, viwanda vya bidhaa ya maziwa Tanzania vinakabiliwa na changamoto ya ushindani wa soko la bidhaa katika nchi za Afrika Mashariki kutokana na kutozwa Kodi ya Thamani ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* hatua hii inafanya maziwa yanayozalishwa nchini kuuzwa bei ya juu ikilinganishwa na maziwa yanayotoka nchi za nje, maziwa yanayoingia kutoka nchi ya jirani hayatozwi kodi ya *VAT* katika nchi zao, hivyo basi kuleta ushindani mkubwa kwa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iangalie eneo hili kwa sababu wakulima na wafugaji wamehamasika katika eneo hili na sasa hivi maziwa mengi ya wafugaji yana soko la uhakika. Ni vema basi Serikali ikalifanyia kazi suala hili kwasababu viwanda vingi sasa hivi vinajengwa katika eneo hili la viwanda vya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokea na kujadili taarifa ya ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhusu hali ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Mazingira.

Kwa miaka kadhaa sasa tumeshuhudia ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutengewa bajeti ndogo sana kulingana na umuhimu wa majukumu inayotekeleza. Aidha, bajeti hii imeendelea kushuka mwaka hadi mwaka ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira katika kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa bajeti iliona umuhimu ya kuanzisha Mfuko wa Mazingira ambao ulianzishwa kwa lengo la kuiwezesha kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya kushughulikia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira bila ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mazingira ulioanzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kifungu cha 213, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kupitia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ilitenga shilingi bilioni mbili kama kianzio *(seed money)* kwa ajili ya kugharamia shughuli za mfuko, lakini hadi kufikia Septemba, 2017 ni kiasi cha shilingi milioni 34 tu kilikuwa kimepokelewa kwa ajili ya mfuko jambo ambalo linapeleka kukwamisha utekelezaji wa mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisistiza na inaomba fedha hizi bilioni mbili zitolewe mara moja ili mfuko uweze kufanyakazi yake na kuleta tija. Pamoja na uhaba wa fedha katika mfuko, bado umefanikiwa kutekeleza baadhi ya kazi na mpaka kufikia Juni, 2017 kazi zilizokuwa zimetekelezwa na mfuko ni pamoja na kuandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Mfuko wa Mazingira, kuandaa rasimu ya kanuni ya uendeshaji wa mfuko, kuandaa rasimu ya mwongozo na utoaji wa fedha kwa ajili ya miradi inayofadhiliwa na mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mazingira unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ufinyu wa bajeti, ukosefu wa watumishi na wahudumu wa mfuko, Sekretarieti ya Mfuko ni watumishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais ambao wana majukumu mengine ukiacha haya ya mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais kufanya tathmini na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kutoka katika shughuli zinazohusu mazingira na kuwasilisha mapendekezo hayo, Wizara ya Fedha tangu mwaka 2016 bado kibali cha kuwapatia mapato hayo hakijatoka, changamoto hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa kazi zilizopangwa kutekelezwa na mfuko kutofanyika. Kamati inaomba Serikali itoe kibali mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa kuruhusu tozo za mazingira angalau

kwa asilimia chache kuingia kwenye Mfuko wa Mazingira ili kuwezesha mfuko kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia Desemba 2017 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni nane tu sawa na asilimia 9.98 iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mafungu yote mawili (Fungu 44 na Fungu 60).

Kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira hadi kufikia Desemba, 2017 fedha zilizokuwa zimepokelewa na ofisi hii ni kwa upande wa miradi ya maendeleo ni shilingi 1,061,779,000, fedha kutoka nje kiasi hiki ni sawa na asilimia 15.63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha wa miradi sio wa kuridhisha jambo linalopelekea kutokukamilika kwa miradi hiyo kwa wakati na kupelekea Serikali kuwa na matumizi makubwa yasiyoakisi thamani ya kazi zinazofanyika. Kamati inaendelea kusisitiza fedha za miradi za maendeleo vitolewe kama zilivyokuwa zimeidhinishwa na Bunge tena zitolewe kwa wakati.

Aidha, Serikali haijalipa kipaumbele suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira na hili linajidhihirisha katika bajeti ya Wizara hii ambapo miradi ya maendeleo hutengwa kiasi kidogo sana na bado kiasi hicho hakipelekwi kwa wakati hivyo kukwamisha shughuli za utekelezaji wake. Kamati inashauri Serikali kuwa pamoja na nia yake nzuri ya kusimamia uhifadhi wa mazingira iangalie namna ya kuongeza bajeti ya mazingira jambo hili litawezesha kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa wajasiliamali *NEDF- SIDO,* Serikali hadi leo haijaleta fedha shilingi 7,146,800,000 hadi fedha hizi hazijatolewa, mfuko huu ulianzishwa na Serikali mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge, Kamati inashauri Serikali kuharakisha utoaji wa fedha hizi za mfuko katika kipindi hiki muafaka cha Tanzania ya viwanda. Iwapo fedha hizi zitatolewa zitasaidia kuamsha ari ya

Watanzania wenye kipato cha kati kuweza kuingia katika biashara mbalimbali za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kukosa mapato, Serikali inapoteza mapato mengi kutokana na kitengo cha *TRA - Long Room* kinachotoa *assessment* imekuwa na urasimu *assessment* hazitoki kwa wakati, malalamiko ya wadau ni mengi wafanyabiashara wanalalamika wanaingia katika gharama kubwa na ziko *assessment* ambazo tokea Desemba hadi leo hazijatoka, suala hili linaonekana bado linaendelea kulelewa na watu wa *TRA* upande wa *Long Room.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri wa Fedha yupo hapa leo nimwombe hapa Serikali inakosa mapato, Wawekezaji wanaingia hasara, Serikali itoe Azimio leo au itoe tamko rasmi kuhusu urasimu *assessment* ambazo hazitoki pale *Long Room*.

Maoni, ushauri na mapendekezo ni kwa muda mrefu sana Kamati tangu ilipoundwa mwaka 2015 imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali na pia kukutana na wadau wa sekta binafsi ili kujadili na kushauriana namna ya kukuza sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji nchini.

Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kulifanyia kazi jambo hili na kuanza utaratibu wa kukutana na wadau mbalimbali mara nne kwa mwaka na kusikiliza changamoto zao. Suala hili tunaipongeza Serikali na huu ni utaratibu mzuri na tunaomba waendelee nao tunampongeza Mheshimiwa Waziri Charles Mwijage na timu yake yote pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu waendelee kuwashirikisha wadau lakini wasisite kuishirikisha Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaendelea kuipongeza Serikali kwa kukubali kuondoa kodi ya *VAT* kwenye huduma za mizigo iliyopita Bandari ya Dar es Salaam hiyo imeongeza sana ufanisi na utoaji wa mizigo bandarini na imeongeza sehemu ya shehena ya mizigo inayopita katika Bandari ya Dar es Salam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira katika kusimamia sheria za utunzaji wa mazingira na ni vema Wizara ihakikishe kwamba inaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika kulinda migodi pamoja na viwanda, kinga ni bora kuliko tiba.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo Kamati inaendelea kushauri maeneo mbalimbali, Kamati inaomba kushauri katika eneo hili nyeti kusimamia na kufufua viwanda vilivyobinafsishwa. Ni jukumu la Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kufuatilia kuhakikisha viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanyakazi na kuleta ajira, mapato na huduma za bidhaa katika hatua ambayo mpaka sasa hivi haijaonyesha matunda.

Kamati inashauri Serikali iweke mkakati maalum kuhakikisha viwanda hivi vinazalisha, pia Serikali kuhakikisha wahusika wanatekeleza mikataba ya ununuzi na Serikali kuchukua hatua kwa watakaobainika wamekiuka mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wa mamlaka ya udhibiti, tunaomba Serikali iangalie sana kuna mamlaka nyingi ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja katika suala la upungufu ya nishati ya umeme. Naomba Serikali iendelee na mikakati yake ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata umeme wa kutosha ili tuweze kwenda sambamba na Tanzania ya viwanda. Miradi mikubwa kama *Stiegler's Gorge* na miradi mingine ya gesi Kamati inabariki ifanyike mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Uwekezaji *(TIB)*, Benki ya Uwekezaji Tanzania *TIB* ndiyo benki muhimu inayotegemewa katika sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji katika kutoa mikopo kwa kuwa benki hii ni muhimu na mustakabali wa Tanzania ya viwanda, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kupitia *TIB* fedha za mitaji ya kutosha ili

Watanzania wafaidike na azma ya Tanzania ya viwanda kwa kuwapatia mitaji ambayo itawasaidia kuanzisha, kukuza biashara zao na hatimae kuongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niende moja kwa moja kwenye utekelezaji wa mradi wa kufufua kiwanda cha matairi cha *General Tyre*. Serikali bado haina mpango madhubuti wa kutekeleza mradi wa kufufua kiwanda cha *General Tyre* ambacho kingeweza kutoa ajira, kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika katika kuagiza matairi ya magari, hivyo basi Kamati inaendelea kusisitiza Serikali iweke mazingira rafiki ili wawekezaji waje kushirikiana na Serikali kufufua kiwanda hicho. Mahitaji ya matairi katika nchi yetu ni makubwa, kukosekana kwa kiwanda hiki Serikali inapoteza mapato mengi na kuagiza matairi kutoka nje ya nchi.

Kwa Kuwa wawekezaji wengi hawazingatii Sheria ya Mazingira na hivyo basi kuwa hatarishi kwa mazingira na binadamu;

Na Kwa Kuwa, wanaofanya hivyo wanatumia vibaya dhana ya Tanzania ya viwanda;

Hivyo Basi, Kamati inaishauri Serikali kusimamia sheria zilizopo katika kudhibiti uharibifu wa mazingira unaofanywa na wenye viwanda nchini kwani suala la uhifadhiwa mazingira halina mbadala. Aidha, Kamati inawashauri wenye viwanda na migodi kufuata na kutii sheria za mazingira ambazo zikizingatiwa kutatunza mazingira na kulinda afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba nimalizie kwa kusema Kamati inampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika azma yake ya Tanzania ya viwanda ambayo inatekelezwa na Serikali yake kwa vitendo. Kamati inampongeza yeye na Serikali yake na Kamati inaunga mkono juhudi zake na itaendelea kutoa ushirikiano ili azma hiyo itimie. Aidha,

Kamati inawashauri Watendaji wengine wa Serikali kuendana na kasi ya Rais, kasi ya Rais imekuwa kubwa lakini bado Watendaji hawaendani na kasi ya Rais hatutafikia ile azma ya Tanzania ya viwanda kwa wakati muafaka.

Kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru Wajumbe wangu wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwangu mimi na kwa Taifa hili na kwa Wabunge naomba *Hansard* iwatambue Wajumbe wangu wote 28.

Pia naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote wa Wizara zote zilizoko chini ya Wizara chini ya Kamati yetu pamoja na Makatibu Wakuu, watendaji wao, taasisi zilizoko chini zao kwa ajili ya ushirikiano mkubwa walionesha katika kipindi cha mwaka mmoja kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote walipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ulioutoa kwa Kamati na kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Wilfred Magova na Bi. Zainabu Mkamba pamoja na wasaidizi wa Kamati Ndugu Paulina Mavunde na Ndugu Mwimbe John kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatima ye ikubali maoni, ushauri, mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA MACHI, 2017 HADI JANUARI, 2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2016, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli ambazo Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imezifanya katika kipindi cha kuanzia Machi, 2017 hadi Januari, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4). Sehemu ya kwanza ni maelezo ya jumla, sehemu ya pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati, sehemu ya tatu inabainisha maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne ni Hitimisho la taarifa.

### 1.2 MUUNDO NA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imepewa majukumu yafuatayo:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya msingi ya Kamati kama yalivyo ainishwa hapo juu Kamati yoyote inaweza kupendekeza kwa Spika kupewa majukumu ya nyongeza, pia Mheshimiwa Spika, anaweza kukabidhi jambo lolote jingine kwa Kamati yoyote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

i) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji na utendaji kutoka kwenye Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira;

ii) Kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Katika ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kamati ilipata pia fursa ya kutembelea Viwanda binafsi ambavyo vinachakata malighafi zinazozalishwa hapa nchini.

iii) Kukutana na kujadiliana na wadau mbalimbali wa Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira; na

iv) Kuhudhuria Semina mbalimbali kwa lengo la kuijengea Kamati uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

## 1.3 SHUGHULI ZILIZOFANYIKA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kipindi cha Machi, 2017 hadi Januari 2018 ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

### 1.3.1 Kupokea Taarifa za Utekelezaji na utendaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi inazozisimamia

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018, na kutoa mapendekezo kwenye maeneo mbalimbali. Aidha, Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ya Wizara Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo na kutoa ushauri na Mapendekezo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, ilipokea na kuchambua taarifa za Taasisi ambazo zinatekeleza majukumu yake chini ya Usimamizi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Katika kipindi hicho Kamati ilikutana na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji zikiwemo; Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Vipimo (WMA), Mamlaka ya EPZ na Shirikisho la Viwanda Vidogovidogo (SIDO). Aidha, Kamati ilikutana na Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lililopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira.

### 1.3.2 Kufanya Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya Miradi ya Maendeleo illiyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati pia ilitembelea miradi isiyotengewa fedha vikiwemo viwanda vya kuzalisha bidhaa kwa lengo la kujifunza shughuli zao, mafanikio na changamoto.

### 1.3.3 Kukutana na kujadiliana na wadau wa Sekta ya Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingiza

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira kwa

ajili ya kusikiliza maoni yao. Wadau mbalimbali walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni na ushauri wao kuhusu namna ya kuboresha sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira. Wadau waliofika mbele ya Kamati ni pamoja na Shirikisho la wenye viwanda Tanzania *Confederation of Tanzania Industries* (CTI), kiwanda cha *SAYONA*, kiwanda cha *Cocacola*, kiwanda cha Ivori LTD, kiwanda cha *Fivestar Printing*, kiwanda cha *Anjari Soda*, na kiwanda cha bia cha *Serengeti Breweries*

### 1.3.4 **Kuhudhuria Semina na Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihudhuria Mafunzo, Semina na kukutana Wadau mbalimbali, katika Mafunzo yalihusu Sekta zilizo chini ya Wizara inazozisimamia na yalilenga kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata mafunzo yaliyosimamiwa na Mradi wa ***Legislative Support Program*** uliyo chini ya Ofisi ya Bunge, na Shirika la Mazingira la ***Heifer International***. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria Kikao cha Majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kuhusu namna ya kuhamasisha na kukuza Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ilitekeleza majukumu yake katika kipindi cha Machi, 2017 hadi Januari, 2018, kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kama ilivyoelezwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu hayo ni pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji na utendaji wa majukumu ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati na taasisi zilizo chini yake, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, kukutana na Wadau kwa ajili ya kusikiliza maoni yao na kuhudhuria Semina na Mafunzo. Katika

utekelezaji huu Kamati ilikutana na Wizara mbili (2) inazozisimamia, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira.

## 2.1 KUPOKEA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA TAASISI INAZOZISIMAMIA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza majukumu mbalimbali kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2017 na Januari, 2018 katika kuendelea kusimamia Wizara zake mbili pamoja na Taasisi zilizoko chini yake. Majukumu hayo ni haya yafuatayo:-

### 4.3 2.1.1 Taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo Serikali haikuyatekeleza ipasavyo Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza ushauri huo.

### 2.1.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2016, Kamati ilichambua utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazozisimamia kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama inavyoelezewa hapa chini.

### a) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kupokea, kujadili

na kuchambua taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa Bajeti, makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**i) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipanga kukusanya shilingi bilioni **20** kutokana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni.

**Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha **2017/2018** ni sawa na makadirio ya mwaka wa fedha unaoishia wa **2016/2017** ambayo hayakufikiwa. Kamati inashauri kuwa, ili kufikia makadirio yanayopangwa Serikali lazima kuangalia upya changamoto zilizopelekea kutofikia malengo hayo na ifanye jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ili kuhakikisha wanafikia malengo wanayojiwekea hususani katika kipengele cha uuzaji wa nyaraka za zabuni.

**ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi **122,215,109,201** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa mafungu **44** na **60.** Kati ya fedha hizo Shilingi **80,190,377,451** sawa na asilimia **65.6** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi **42,024,731,750** sawa na asilimia **34.4** ya fedha zote zinazoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo huu ni kwa mafungu yote mawili (2) Fungu **44-**Viwanda na Fungu **60-**Biashara na Uwekezaji. Bajeti iliyopitishwa ya Shilingi **122,215,109,201** ni zaidi kwa asilimia **49.2** ikilinganishwa na Shilingi **81,871,992,000** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha **2016/2017**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara hususani kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, jambo hili linatarajiwa kufanikisha utekelezaji wa

Miradi mingi ya Maendeleo na kama ongezeko hili liende sambamba na utoaji wa fedha zilizotengwa tena kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ongezeko hilo la asilimia 49.2, Kamati bado inaona kutokana na majukumu na azma ya Serikali kwenda kwenye uchumi wa Viwanda Bajeti hii bado ni ndogo. Kamati inashuri Serikali kutenga fedha za kutosha kukabili masuala yote ambayo ni ya msingi kutofanyika kwake yanasababisha gharama za ziada kwa Serikali.

**iii) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

- **Makusanyo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa hadi kufikia Disemba, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi **8,598,083,500.07** sawa na asilimia **42.99** ya makusanyo yaliyokuwa yamekadiriwa kukusanywa. Makusanyo haya ni karibia ya nusu ya lengo, Kamati inashuri Wizara kuongeza jitihada ili kuhakikisha wanafikia lengo ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

- **Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia disemba, 2017 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **29,687,552,982** sawa na asilimiwa **24.3** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwenye mafungo yote mawili (Fungu **44**&**60**) ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Kati ya kiasi kilichotolewa ni Shilingi **8,000,000,000** tu sawa na asilimia **9.98** ilitolewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo si wakuridhisha jambo linalopelekea kutokamilika Miradi hiyo kwa wakati na kupelekea Serikali kuwa na matumizi makubwa yasiyo akisi thamani ya kazi inayofanya (Value for Money). Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha za miradi ya maendeleo zitolewe kama zinavyokuwa zimeidhinishwa na Bunge tena kwa wakati.

**b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018**

**i) Makusanyo ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais haifanyi makusanyo ya Maduhuli hivyo basi hakuna makusanyo ya maduhuli kutoka Ofisi hii.

**ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliidhinishiwa Shilingi **15,002,988,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha zilizoidhinishwa Shilingi **10,634,020,440.00** ni kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira, ambapo Shilingi **6,788,452,437.00** ni kwa ajili ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi **3,845,568,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida Shilingi **2,215,044.000.00** ni ruzuku kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kiasi kinachosalia Shilingi **1,630,524,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zilizoombwa kwa ajili yakutekeleza Miradi ya Maendekeo katika Mwaka wa Fedha **2017/2018** ni Shilingi **6,788,452,437.00** ambapo Shilingi **3,000,000,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **3,788,452,437.00** ni fedha za nje. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **38** ikilinganishwa na Shilingi **10,973,083,448.00** zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zinaonyesha dhahiri jinsi bajeti ya Ofisi hii muhimu imeendelea kushuka mwaka hadi mwaka jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake.

**iii) Utekelezajiwa wa Bajeti ya Ofsi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

- **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha **2016/2017** Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **14,817,377,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi **8,028,925,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **6,788,452,437.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Disemba, 2018 fedha zilizokuwa zimepokelewa na Ofisi hii ni kwa upande wa Miradi ya Maendeleo ni shilingi **1,061,079,990** fedha kutoka nje. Kiasi hiki nia sawa na asilimia **15.63**. Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida upo vizuri kwakuwa fedha hizo zinachangiwa na mishahara.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali haijalipa kipaumbele suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira na hii inajidhihirisha katika Bajeti ya wizara hii ambapo Miradi ya Maendeleo hutengewa kiasi kidogo sana na bado kiasi hicho hakipelekwi kwa wakati hivyo kukwamisha utekelezaji wake. Miradi ya maendeleo ya mazingira inatekelezwa kwa kutegemea fedha za wafadhili. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha taratibu ya kutoa vibali ili kodi zote zitokanazo na shughuli za Mazingira zianze kupelekwa katika Mfuko wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mazingira ukiwezeshwa kujikusanyia mapato yake utakuwa na fedha za kutosha kushughulikia masuala ya mazingira bila kutegemea msaada kutoka kwa wafadhili.

**4.4 2.1.3 Taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Taasisi zilizo chini yake**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Machi 2017

hadi Januari, 2018, Wajumbe walipokea Taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kama ifuatavyo:

**a) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi ya TRADEMARK East Afrika.**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilipokea na kujadili Taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za Taasisi ya TRADEMARK East Afrika (TMEA). TRADEMARK-East Africa ni Taasisi inayofadhiliwa na wafadhili mbalimbali kwa lengo la kukuza biashara na masoko kwa nchi za Afrika Mashariki kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Mfadhili mkubwa wa TMEA ni Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (*Department for International Development-DFID*). TMEA-Tanzania inafanya kazi chini ya uratibu wa Wizara ya Afrika Mashariki, kupitia kamati ya uratibu ambayo ipo chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji TMEA imefadhili Mradi wa Uboreshaji na Kuongeza Ufanisi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kuandaa na kutekeleza Viwango Nchini. Lengo la Mradi huu ni kuliwezesha Shirika katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuboresha uwezo wake katika kutoa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, TMEA imefadhili Mradi wa Upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na ujenzi wa Vituo vya Mipakani, kwa kuwa miradi hii ilitarajiwa kutachochea ukuaji wa biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Uboredhaji na Kuongeza Ufanisi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kuandaa na kutekeleza Viwango Nchini, kuwa utekelezaji wake unaendelea, awamu ya kwanza imekamilika vizuri na awamu ya pili inatarajia kuanza tarehe 1 Septemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa awamu ya pili utahusika na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA ya Shirika, ambapo itaboresha mifumo ya mawasiliano, mifumo ya kuhifadhi kumbukumbu za Uandaaji Viwango, uhakiki wa ubora, ugenzi na upimaji; ili kuboresha utoaji huduma kwa wateja kwa kuongeza ufanisi na kupunguza gharama zisizo za lazima.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu umekuja wakati muafaka ambapo Serikali inasisitiza kuimarisha ujenzi wa Viwanda hivyo kuongeza upatikanaji wa bidhaa zitakazohakikiwa ubora wake katika mfumo unaotambulika kikanda na kimataifa utasaidia kujipatia soko la ndani na nje ya nchi. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuandika andiko zuri ambalo limewezesha kupata mradi huu muhimu.

**Mhesimiwa Spika,** kwa kuwa Trademark East Afrika ipo kwa ajili ya kuihudumia Afrika Mashariki kwa Ujumla wake, Kamati inashauri Serikali kuwandaa na kupeleka maandiko mengi iwezekanavyo ya ufadhili ili nchi iweze kunufaika na miradi hii ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Makao Makuu ya TRADEMARK East Africa yapo nchini Kenya, na kwa kuwa Taasisi hii ina wafanyakazi 100 lakini kati ya hao watanzania ni watatu(3) tu, uwakilishi huu mdogo sana, Kamati inashauri Serikali kujitahidi sana kushauriana na washiriki ili kuongeza ajira kwa watanzania kwenye taasisi hii.

**b) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mkakati/Mpango wa Serikali katika kutekeleza Mradi wa Kituo cha Biashara cha Kurasini.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kituo cha Biashara cha kurasini (Kurasini logistic Center) ni miongini mwa miradi ya kielelezo ya taifa (*National Flagship Project*) kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) ambao ni Mradi wa Ujenzi wa Kituo kikubwa cha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unatarajia kutekelezwa kwa kutumia utaratibu wa Ubia (*Joint Venture*), mchango wa

Serikali katika ubia huo utakuwa ni Ardhi ya eneo la Mradi na hisa za Serikali hazitapungua 25 na kwa namna yoyote hazitapungua katika kipindi chote cha Ubia. Utekelezaji wa Mradi ulitegemewa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 kwa kuanzisha Viwanda visivyopungua ishirini 20 hadi kufikia 2020.

**Mheshimiwa Spika,** mradi umakabiliwa na changamoto nyingi ikiwani pamoja na kushindwa kufidia na kubomoa nyumba tatu. Kwa sasa nyumba zimefanyiwa uthamini lakini fedha kwa ajili ya kulipa fidia hazijatolewa. Changamoto nyingine ni upatikanaji wa hati miliki ya eneo la mradi kwa jina la Mamlaka ya EPZ; na gharama kubwa ya malipo ya *Premium* na kodi ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu umechelewa sana kutekeelzwa na umedumu kwa miaka saba sasa na kusababisha kupanda kwa gharama za utekelezaji wake. Mradi ulipoanza kutekelezwa mwaka 2010 ulihitajika kulipa fidia ya Shilingi **bilioni 60** na malipo yalipaswa kufanyika kwa awamu nne lakini kwa ajili ya kuchelewa gharama ilipanda na kufikia Shilingi **bilioni 191** kutokana na riba.

**Mheshimiwa Spika, pamoja na** mradi huu kudumu kwa miaka saba (7) sasa bado Serikali haifahamu namna bora ya kutekeleza mradi huu kwa maana haijaamua kama utatekelezwa kwa *Joint Venture* mara *Design Build and Transfer*, kamati haioni jitihada za dhati katika kutekeleza mradi huu kwani mkanganyiko uliopo hauhamasishi wawekezaji kuja kuwekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mradi huu huwa ni moja ya miradi ya kielelezo na inayotarajiwa kuchochea ukuaji wa Viwanda, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuutekeleza mradi huu.

**c) Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa Mradi wa NEDF.**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa kuwaendeleza wajasiriamali

Nchini (NEDF) ulianzishwa mwaka 1994 kwa azimio la Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu unalenga kuondoa umasikini kwa kuwasaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza miradi katika sekta ya uzalishaji inayohusika na viwanda vidogo, kilimo na biashara na sekta nyingine kama vile afya, ujenzi, utalii na uchukuzi. Mfuko unaendeshwa na Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) chini ya usiamamizi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu ulianza na mtaji wa shilingi **500,000,000** na sasa umefanikiwa kufikia shilingi **7,413,283,433**. Tangu mfuko kuanzishwa umetoa mikopo wenye thamani ya shilingi **62,812,532,000** kwa wajasiriamali.

**Mheshimiwa Spika,** mikopo hiyo ilitolewa kwa maombi **85982** ambayo ni asilimia **40.13** ya maombi yote. Kwa sasa Serikali kupitia taasisi yake ya imepanga pia kuanzisha Mfuko wa dhamana kwa kushirikiana na CRDB ambao utasaidia Wajasiriamali wadogo kuweza kukopa kiasi kikubwa cha fedha hivyo kuimarisha shughuli zao za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko unakabiliana na changamoto ya ufinyu wa fedha, kwa miaka mitatu mfululizo sasa Mfuko haujapata fedha yoyote kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** chanzo kikubwa cha fedha za Mfuko ni ruzuku kutoka Serikalini, Kamati inaishauri Serikali kupeleka fedha za kutosha kwenye Mfuko ili kuweza kuongeza idadi ya wanufaika.

**d) Kupokea Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya KAIZEN, SMES, ASDP, SIDO, Implementation of BEST Programme na Strenthening TWLB Capacity.**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na

Uwekezaji katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilitenga shilingi 40,000,000,000 sawa na asilimia 49 ya bajeti yake kwa mwaka huo kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kamati ilipata fursa ya kupatiwa taarifa ya utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara hii. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**i) KAIZEN**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusisha mafunzo na kubadilishana ujuzi baina ya nchi kwa lengo la kuongeza tija katika maeneo ya uzalishaji na ujasiriamali; mbinu za uendeshaji biashara; na utumiaji na uhifadhi wa mahesabu na gharama zake. Mradi ulitegemewa kuendelea kufanya mabadiliko kwa kuongeza tija na ubora kwa kutumia rasilimali zillizopo kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika**, mradi ulitengewa shilingi 100,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali katika kutekeleza mradi huu. Mradi unakabiliwa na changamoto ya fedha, kwani mpaka kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulikuwa haujapokea fedha yoyote hivyo mradi ulikwama.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaishauri Serikali kutekeleza utoaji wa fedha kwenye miradi iliyopangiwa fedha ili kufanikisha azma ya kujenga Uchumi wa Viwanda.

**ii) Mradi wa Smes Industrial Infrastructure Expansion and Capacity Building**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu mkakati wa Wilaya moja bidhaa moja (one District one Product ODOP) ambao Shirika la Viwanda vidogo SIDO kwa kushirikiana na Wilaya husika huibua na kuendeeza bidhaa moja kwa awamu katika wilaya kwa kuzingatia rasilimalli zillizopo katika wilaya husika.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Mkakati huu ni kuchochea maendeleo ya Viwanda vidogo ili kuongeza kipato na ajira ya wananchi wa vijijini. Kutekelezwa kwa mradi huu kutasaidia kutumia rasilimali zilizopo katika wilaya jambo

litakalochochea ukuaji wa uchumi vijijini kupitia viwanda hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, faida nyingine za kutekeleza mradi huu ni kuupunguza wimbi la vijana wanaohamia mjini kutafuta ajira kwani katika wilaya zinazotekeleza mradi huu kutakuwepo na ajira kwa vijana wetu kuanzia katika kilimo mpaka viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zinaonyesha kwa mradi umefanikiwa kugusa maeneo ya uzalishaji wa chumvi, ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo, usindikaji wa vyakula, uhunzi, useremala, ukamuaji wa mafuta ya kula, uzalishaji wa asali, usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa sabuni na mishumaa.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unakabiliwa na changamoto ya fedha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 ulitengewa kiasi cha Shilingi 2,400,000,000 kwa ajili ya kutunisha mfuko wa NEDF ambazo ndio zingetumika kuwakuzia mtaji wenyeviwanda vidogo na kuweza kuendeleza viwanda hivyo lakini fedha hizo hazikutolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuwa inapotenga fedha kwenye Bajeti ni vema kuzitoa ili zitekeleze miradi iliyopangwa.

**iii) Mradi wa SIDO Institutional Support**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu kuliwezesha shirika la SIDO kujenga uwezo na kuendelea kutekeleza majukumu iiliyopangiwa. Kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017 SIDO ilitengewa shilingi 6,050,000,000 kama "*institution support*" kwa ajili ya uendelezaji wa Maeneo ya viwanda katika mikoa mitano, ya Dar es Salaam (Vingunguti Industrial Estate), Mbeya (kitalu U), Mwanza (Nyakato Industrial Estate), Morogoro (Kihondo) na Arusha. Fedha zilizotengwa hazikutolewa na hivyo haukutekelezwa. Kamati inashuari Serikali kupeleka fedha katika mradi huu kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

### iv) Mradi wa TIRDO Institutional Support

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya TIRDO ilitengewa Shilingi 500,000,000 ili kuwezeshwa kutekeleza majukumu yake iliyopangiwa. Fedha hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya; kufanya tafiti mbalimbali na kutoa mafunzo ya kukabiliana na utunzaji wa siri (Cyber Security) katika taasisi na Wakala za Serikali; kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi ili kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kurejelesha ngozi; kuendelea kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya Mazingira; na kuendelea kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa mazao kwa kutumia tecknohama.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2016/2017 taasisi ya TIRDO ilikuwa na jukumu kubwa la kutekeleza Mradi wa kuongeza Thamani katika Taka Ngumu na ngozi kwa kusimika mashine ya kuongeza thamani kwenye taka ngumu zitokanazo na uzalishaji katika viwanda vya ngozi. Mradi ulitengewa kiasi cha shilingi **53,050,000** katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 na kiasi kilichopokelewa ni shilingi **41,500,000** ambazo zilitumika kununua vipuri na kusimika mashine.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa majukumu ya taasisi hii bado inakabiliana na changamoto ufinyu wa Bajeti katika kutekeleza majukumu. Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Taasisi ni ndogo haitoshi, Mradi bado unahitaji kiasi cha shilingi 67,000,000 kwa ajili ya kuhaulisha teknolojia hii kwa wajasiriamali.

### v) Mradi wa Best Programme Implementation

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unajihusisha na uboreshaji wa mazingira ya kufanyia biashara nchini kwa lengo la kurahisisha taratibu za kuanzisha biashara, uwekezaji na kuendesha biashara na hivyo kuvutia wawekezaji na wafanyabishara nchini. Mradi unajukumu la kuboresha sheria ya leseni ya mwaka 1972 ili iwezeshe kutoa leseni kwa njia ya mtandao, pia unajukumu la kuandaa kanuni za sheria zitakazorekebishwa, kukamilisha na kuzindua *Tanzania*

*Business Portal* kwa ajili ya kuharakisha upatikanaji wa taarifa muhimu za biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto ya mradi huu ni kuwa mradi huu bado hajapatiwa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

**vi) Mradi wa Strenghering TWLB Capacity**

**Mheshimiwa Spika**, Huu ni mradi wa kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unaotekelezwa kwa ufadhili wa *Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA)* Mapinduzi ya Kijani na Serikali ya Tanzania. Mradi ulianzishwa kufuatia changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala chini ya Sheria Namba 10 ya 2005. Mradi ulianza kutekelezwa Januari, 2013 na ulitekelezwa kwa miaka miwili tu ambapo mwaka 2015/2016 mfadhilli alisitisha kutoa hela kwa madai kuwa anataka mabadiliko ya sera ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya mfadhili kujitoa katika mradi huu tulibaki na ruzuku kutoka Serikalini ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 ulitengewa shilingi 200,000,000 kwa ajili ya kutekeza majukumu yake lakini hadi kufikia Disemba 2016 Fedha zilikuwa hajiapelekwa hivyo kukwamisha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, miradi yote hii inakabiliana na changamoto ya upatikanaji wa fedha, Wizara ilijipangia kutekeleza Miradi hii kwa kuzingatia umuhimu wake jambo la kushangaza ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wake hazipelekwi na kusababisha kuchelewesha utekelezaji wake. Ni ushauri wa kamati kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo zipelekwe kwenye miradi kwa wakati ili kukamilisha utekelezaji wake na ili tuweze kunufaika na miradi hiyo.

**e) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Kongano la Sekta ya Ngozi na bidhaa za Ngozi (Dodoma Leather Cluster) katika eneo la Zuzu Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya ngozi ni moja ya ya sekta za kipaumbele katika mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sekta hii ina mnyororo mrefu wa thamani hivyo inauwezo mkubwa wa kutoa ajira kwa wingi. Aidha, Tanzania ni nchi ya pili Barani Afrika kwa wingi wa mifugo hivyo kufanya upatikanaji wa malighafi hii kuwa rahisi. Changamoto inakuja katika uwezo wa usindikaji ngozi nchini ambao si wakuridhisha na hii ni kutokana na changamoto ya ukosefu wa ubora wa ngozi.

**Mheshimiwa Spika,** zaidi ya asilimia 50 ya ngozi inayovunwa ni daraja la tatu, zinazobaki kwa asilimia 25 ni za daraja la pili na kwanza. Hili linatokana na mifungo kutokutunzwa vizuri; kuweka mifugo alama; kuchapa mifugo; kuchuna bila kutumia vifaa sahihi; na kutokuwa na uwezo wa kuongeza ngozi thamani hadi hatua ya mwisho.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania inasindika futi za mraba milioni 25.9 ambayo ni sawa na asilimia 30 ya uwezo wake uliosimikwa, usindikaji huo huwa hadi hatua ya awali tu (*wet blue/white/brown*). Ngozi zilizosindikwa mpaka hatua ya awali (*wet blue/white/brown*) huuzwa nje ya nchi ambako huongezwa thamani hadi hatua ya mwisho.

**Mheshimiwa Spika,** Mahitaji ya ngozi ni makubwa ukilinganisha uwezo wa Nchi kusindika ngozi hadi hatua ya mwisho, kwa sasa tuna Viwanda tisa (9) vinavyosindika ngozi, kati ya viwanda hivyo ni vitatu (3) tu ndio vina uwezo wa kuongeza thamani hadi hatua ya mwisho tena kwa kiwango kidogo tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na umuhimu wa kuongeza kiasi cha ngozi zinazosindikwa hadi hatua ya mwisho pamoja na kuzalisha kwa wingi bidhaa za ngozi, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kutafuta eneo la Zuzu

Mkoani Dodoma lenye ukubwa wa Ekari 107 ambapo inategemewa kuanzisha na kuendeleza vijiji vya Viwanda (*Industrial Villages*) vya ngozi kwa lengo la kuchochea na kuvutia wawekezaji katika viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, faida zitakazopatikana kutokana na kuanzishwa kwa kongano la ngozi la zuzu ni; kuongeza uwezo wa matumizi ya malighafi (ngozi na kemikali kama vile chumvi na chokaa); kuimarika kwa mnyororo wa uongezaji wa thamani ngozi kukokana ngozi bora; kuongezeka kwa uwekezaji katika mnyororo wa uongezaji wa thamani ya ngozi; kuongezeka wa ajira kutoka katika mnyororo wa uongezaji wa thamani; na nyingine nyingi.

**Mhesimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na wazo la uanzishwaji wa kongano hili ila inaishauri Serikali kuwa katika utekelezaji wa suala hili ni lazima kuwa na Mkakati mzuri wa utekelezaji wa mradi huu maana uzalishaji wa ngozi utakuwa na manufaa makubwa sana kwenye uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa mradi wa Zuzu wakulima na wafugaji wengi wapatiwe elimu juu ya ufugaji bora na wenye viwanda wapewe elimu ya kutosha juu ya usindikaji ngozi.
**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufufua viwanda vya ngozi vilivyokufa kwa kuangalia namna ya kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji hao waweze kufufua viwanda hivyo, ili ngozi itakayozalishwa kwa wingi na wakulima wetu iwe na soko la uhakika.

**f) Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Kufufua Kiwanda cha General Tyre**

**Mheshimiwa Spika,** kamati haioni jitihada za dhati za Serikali katika kutekeleza Mradi wa Ufufuaji kiwanda cha Matairi cha General Tyre kwani mara kwa mara imekuwa ikiomba taarifa ya Utekelezaji wa Mradi huu na imekuwa ikipata taarifa zisizoridhisha**.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwisho wa mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali ilikuwa haijatekeleza jambo lolote la kufufua kiwanda cha matairi cha General Tyre, Arusha bali iliamua tena kuunda Kamati ya wataalamu kwa ajili kufanya tena Upembuzi Yakinifu ambao ungeshirikisha wadau mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** kazi hiyo ilitarajiwa kukamilika katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/2017 lakini hadi leo hakuna taarifa yoyote ya kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Oktoba, 2017 iliomba tena taarifa ya hatua iliyofikia katika kutekeleza Mradi, kwa masikitiko naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Taarifa iliyoletwa na Serikali haikuwa ya kuridhisha. Hata katika mwaka wa Fedha 2017/2018 hakuna hatua yoyote ya utekelezaji wa Mradi huu uliofikiwa pamoja na kuwa Mradi huu umetajwa kwenye Mpango wa Miaka mitano. Tangu utekelezaji wa Mradi huu umeanza yamekuwa ni majadiliano na Upembuzi Yakinifu tu ndio vinaendelea takribani miaka kumi (10) sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali mambo yafuatayo;

- Serikali kufanya maamuzi stahiki ambalo mradi huu uweze kutekelezwa na Wawekezaji Binafsi jambo hili litaipunguzia majukumu.

- Kama Serikali inashindwa kuutekeleza mradi ni vema kubadilisha matumizi ya ardhi ya mradi na fedha zinazotengwa kwa ajili ya mradi zipelekwe katika Miradi mingine inayotekelezeka na kuacha kupoteza muda na fedha katika Mradi ambao wameshindwa kuutekeleza.

**g) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu hatua iliyofikiwa Mamlaka ya EPZ katika kutenga na kuhamasisha kuendeleza maeneo maalumu ya Uwekezaji.**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ kwa

kushirikiana na Mamlaka za Mikoa na Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini imetenga maeneo yenye ukubwa tofautitofauti kwa ajili uzalishaji wa Kanda Maaluum za Kiuchumi (*SEZ na -EPZ*). Kutengwa kwa maeneo haya kutasaidia kuandaa meneo tayari kwa ajili ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya EPZ inajukumu la kuainisha, kuendeleza na kusimamia kanda maalumu za kiuchumi. Maeneo haya baada ya kainisha huendelezwa kwa njia tatu ambayo moja ni EPZA kuyaendeleza kwa niaba ya Serikali (mfano *Benjamini William Mkapa Special Economic Zone),* pili ni EPZA kuyahawilisha na kuyakodisha kwa kutoa hatimiliki kwa wawekeaji wayaendeleze (mfano Mtwara *SEZ na* Bagamoyo *SEZ)*, na tatu ni EPZA kushirikiana na Sekta binafsi kuendeleza maeneo hayo (mfano eneo la Star City SEZ mkoani Morogoro). Katika kutenga maeneo hayo vinazingatiwa baadhi ya vigezo ambavyo ni maeneo ya Mipakani mwa nchi, maeneo ya karibu na bahari na kuzingatia malighafi inayopatikana katika eneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu haya EPZA inakabiliana na changamoto kadhaa ambazo ni; uhaba wa rasilimali fedha ukilinganisha na mahitaji ya EPZA kwa ajili ya kulipa fidia na gharama nyingine za awali za uendeshaji wa maeneo yaliyobainiwa kabla ya kuishirikisha Sekta binafsi; Gharama kubwa za malipo ya mbele (*Premium*) na kodi ya ardhi kwa ajili ya umilikishwaji wa ardhi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli chini ya EPZA;

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ni Ushirikiano mdogo kati ya EPZA na Taasisi au Idara nyingine za Serikali, katika huduma kwenye maeneo haya. Kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa kwa baadhi ya Taasisi katika kutoa huduma zingine, kukinzana hivyo kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya EPZA.

**Mheshimiwa Spika**, EPZA inamiliki ardhi kwa niaba ya Serikali hivyo basi kuitoza EPZA kodi ya Premium na kodi ya ardhi ni sawa na kuomba hela Hazina na kuzirudisha katika Hazina jambo hili ni usumbufu na gharama zisizo za lazima. Kamati

inashauri kuwa katika maeneo yanayotambuliwa na kumilikiwa na EPZA kodi zote za ardhi kwa maeneo hayo zifutwe ili kuipunguzia EPZA mzigo wa uendeshaji.

**Mhesimiwa Spika,** baadhi ya maeneo yalikwisha bainishwa na taratibu za awali za kuyaendeleza zilikwishakamilika lakini utekelezaji wa taratibu nyingine umekuwa ukienda kwa taratibu sana jambo linalopelekea wananchi kushindwa kufanya shughuli zao za maendeleo na uzoefu huu umesababisha wananchi kuwa wazito wanapotakiwa kutoa maeneo yao kwa ajili ya miradi ya EPZA.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mzuri wa ucheleweshaji ni eneo la EPZA-Kurasini ambapo mradi huu umeanza kutekelezwa tangu mwaka 2011 takribani miaka 7 sasa hakuna jambo ambalo EPZA inaweza kujivunia kuwa limefanikiwa. Kamati inashauri kuwa, ni vema Serikali inapofikia uamuzi wa kutwaa maeneo na kuwahamisha wananchi iwe tayari na mpango wa kuyaendeleza ili kuepusha dhana ya kuwa wanafukuzwa katika maeneo halafu hayafanyiwi kazi yoyote.

**h) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Chuo cha Biashara (CBE)**

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Elimu ya Biashara (*College of Businaess Education CBE*) kilianzisha mwaka 1965 chini ya Sheria ya Bunge Namba 31 kwa lengo la kuanzisha taasisi ya Mafunzo ya Biashara nchini ili kuziba pengo lililokuwepo la wataalamu wa biashara na kuwa na kituo chenye ubora wa kimataifa katika utoaji wa stadi za mafunzo, tafiti na ushauri wa kitaalamu katika nyanja za biashara na taaluma zinazohusiana na biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Elimu ya Biashara kinatoa mafunzo kuhusiana na mbinu na taratibu za biashara katika maeneo ya uendeshaji wa biashara, usimamizi wa manunuzi na ugavi, usimamizi wa biashara, uhasibu, usimamizi wa masoko, mizani na vipimo, tecknolojia ya Habari na Mawasiliano (TECNOHAMA)

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza majukumu yake Chuo cha elimu ya Biashara kinakabiliana na changamoto zifuatazo; kukosekana fedha kutoka Serikalini kwa shughuli za Maendeleo; upungufu wa maktaba za kutosha na za kisasa, Maktaba iliyopo Dar es Salaam kwa sasa inauwezo wa kuchukua wanafunzi 130 tu wakati uhitaji wa wastani kwa wakati mmoja ni wanafunzi 7000 waliopo. Aidha, Chuo kina uhaba mkubwa wa madarasa; kushuka kwa idadi ya wanafunzi, idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa imeshuka kwa mwaka 2016/2017 ukilinganisha na miaka iliyopita.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa madarasa chuo kimetafuta maeneo kwa ajili ya kujenga majengo yake. Changamoto inayokumbana nayo ni fedha kwa ajili ya ujenzi huo, Chuo hakina uwezo wa kupata fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Kamati inaishauri Serikali ishirikiane na chuo kutafuta wawekezaji watakaowekeza katika majengo marefu ambayo yatatumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na hosteli kama ulivyo mpango wa chuo.

**Mheshimiwa Spika,** ni wazi kuwa wajasiriamali wetu wengi wamekuwa wakifika mahali wanakwama na hii ni sababu ya kukosa elimu ya biashara, ni ushauri wa Kamati kuwa CBE kama chuo mahsusi kwa kutoa elimu ya biashara kingeanzisha kozi fupi ambazo zitatolewa kwa wajasiriamali ili kuwapatia uelewa mpana kuhusu biashara kuanzia uzalishaji, ufungashaji, upangaji bei na upatikanaji wa mikopo na masoko. Jambo hii litawasidia wajasiriamali wetu kuendelea tena wakiwa wanajiamini.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati inaishauri Serikali kupitia CBE kuanzisha program maalumu ya elimu ya Viwanda ili kuwezesha kupata wataalamu wazawa ambao watashiriki katika mambo ya viwanda na kuacha kutegemea wataalamu kutoka nje tu.

**i) Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo (WMA) ilianzishwa ikiwa ni utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma (PSRP I) kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma kupitia matumizi ya Vipimo sahihi. Wakala wa Vipimo anatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura Na. 340.

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo ina majukumu yafuatayo; kudhibiti na kuhakiki vipimo vyote vinavyotumika kwenye Sekta za bishara, mazingira, afya na usalama na hii inahusisha kuhakiki vipimo vipya vilivyoingizwa toka nje na vile vinavyoundwa hapa nchini; kusimamia matumizi sahihi ya vipimo kwa njia ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kukagua na kuhakiki bidhaa zilizofungashwa toka nje ya nchi na zile zizalishwazo nchini; kutoa vibali/leseni kwa watu wanaojihusisha na uundaji pamoja na utengenezaji wa vipimo mbalimbali; na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na vipimo kwa Serikali, mashirika, taasisi na wadau wengine;

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake Wakala wa Vipimo inakabiliana na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na; uhaba wa fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakala wa vipimo (Capacity Building) ili iweze kutekeleza majukumu yao na kukabiliana na mabadiliko ya tecknolojia; uhaba wa watumishi hasa maafisa vipimo ambapo inakwamisha Wakala kufika maeneo mengi; na uwepo wa matumizi ya Vipimo batili hususani mizani ambayo inachangiwa na uingizaji wa mizani zisizokidhi viwango kutoka nje ya nchi kwa njia za panya.

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo inajukumu kubwa sana la kusimamia vipimo kuhakikisha kuwa wanamlinda mlaji ipasavyo, katika kutekeleza jukumu hili inailazimu wakala kuzunguka nchi nzima ila changamoto ya watumishi/maafisa Vipimo wachache hukwamisha

utekelezaji wa majukumu hili kiufanisi. Kamati inashauri Serikali kuwa Taasisi hii muhimu katika kulinda usalama wa mlaji ni vema iwezeshwe kwa kupatiwa fedha na watumishi inayostahili ili iweze kutekeleza majukumu yake kiukamilifu.

**j) Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Shirikisho la wenye Viwanda Nchini (*Confederation of Tanzania Industries - CTI*) na maoni yao kuhusu namna ya kukuza sekta za: Viwanda, Biashara na Uwekezaji.**

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilipata fursa ya kukutana na Shirikisho la wenye viwanda Nchini (CTI) na baadhi ya wamiliki wa viwanda nchini kwa lengo la kufahamu majukumu ya Shirikisho, changamoto na mafanikio yao pamoja na maoni ya juu ya namna ya kuboresha Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** shirikisho linatekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo; kuiwakilisha/kuisemea Serikalini Jumuiya katika kuwasilisha mambo ambayo yanaleta changamoto katika kufanya biashara. CTI pia hufanya tafiti na kushauri kwa mambo yanatatiza Jumuiya; kuviwakilisha viwanda katika majadiliano katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa (EAC na SADC) kutoa taarifa za kibishara kwa wawekezaji kwa wazalishaji na washirika wao; kusuluhisha mgogoro kati ya Serikali na mwanachama inapotokea; na kuiwakilisha Jumuiya katika kuandaa viwango vya kodi wakati wa kuandaa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilipata fursa ya kusikiliza changamoto ambazo zinazoikabili CTI ambazo ni;-

**i) Mabadiliko ya mara kwa mara ya kodi**

Serikali katika kila mwaka wa fedha imekuwa ikifanya mabadiliko ya mfumo wa kodi, ambapo hupelekea mabadiliko ya vivutio mbalimbali vya uwekezaji. Wawekezaji wengi huvutiwa kuwekeza mahali palipo na mfumo wa kodi unaotabirika na kuleta mazingira mazuri ya uwekezaji.

Mabadiliko ya mara kwa mara yanapunguza sifa ya kuwa na mazingira mazuri ya biashara na hivyo kuwafukuza wawekezaji.

**ii) Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT refunds)**

Wazalishaji wengi wanakumbana na changamoto ya upungufu wa mitaji kutokana na malimbikizo makubwa ya madai ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) refund na nyongeza ya asilimia 15 ya kodi ya kuingiza Sukari ya Viwandani yaliyopo katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mfano Viwanda viwavyodai VAT refund ni kiwanda cha Tanga Phatmacetical and Plastic LTD wanadai shilingi **bilioni 9.6**, kiwanda cha A to Z Textile Mills LTD wanadai Shilingi **bilioni 16** na kiwanda cha Kioo LTD wanadai shilingi **bilioni 1.9** na vingine vingi**.**

**iii) Uingizwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango na feki kwa njia za panya**

Uingizaji bidhaa kwa njia za panya hivyo kukwepa kodi na kupelekea bidhaa hizo kuuzwa kwa bei rahisi na kusababishia bidhaa za viwanda vya ndani ambavyo vinalipa kodi kushindwa kushindana na bidhaa hizo katika soko.

**iv) Uwepo wa Mamlaka nyingi za udhibiti na ushirikiano hafifu baina yake.**

Uwepo wa mamlaka nyingi za udhibiti ambazo zinafanya kazi zinazofanana, mfano ukiwa ni TBS, TFDA, Mkemia Mkuu, OSHA, FIRE, NEMC n.k mamalaka hizi zinafanya kazi inayofanana na kila mmoja anatembelea kiwanda kwa wakati wake na tozo zake jambo ambalo huleta usumbufu na gharama kubwa kwa wawekezaji/wenye viwanda.

**v) Kukosekana kwa Nishati ya Umeme ya uhakika**

Kukosekana kwa nishati ya umeme ya uhakika ambapo umeme viwandani hautoshi na unakatika mara kwa mara na kusababishia hasara kwa mitambo kuungua na viwanda vyetu kutofikia malengo ya uzalishaji.

**vi) Kuanzishwa kwa utaratibu mpya wa ulipaji kodi wa *electronic tax stamp***

Viwanda vya pombe, sigara, soda na maji wamepewa taarifa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwa Mamlaka hiyo inatarajia kuleta utaratibu wa kielektronic wa kukusanya kodi ambapo watatumia taasisi ya Kiswis ambao watafunga mtambo katika mifumo ya uzalishaji kwa ajili ya kupima uzalishaji na Kiwanda kitalipa kodi ya dola za Kimarekani 10.1 kwa uniti 1000

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya mfumo huu utaongeza gharama kwa Viwanda kwa asilimia 50 ya kodi inayokusanywa, na hatimaye Viwanda vitaongeza bei ya bidhaa na kumuumiza mlaji, pia inaweza kupunguza soko la bidhaa na gharama za kukusanya kodi hii itakuwa kubwa kuliko mapato ya kodi kwa Serikali.

**vii) Upatikanaji wa Vibali vya kutoa Sukari ya Viwandani Bandarini na nyongeza ya asilimia 15 ya kodi ya kuingiza Sukari ya Viwandani**

Kuna usumbufu usio wa lazima katika kuagiza na kutoa sukari ya Viwandani kutoka Bandarini hilo linasababisha baadhi ya Viwanda kupunguza uzalishaji na vingine kufungwa kabisa. Aidha, wawekezaji wanalalamikia nyongeza ya asilimia 15 ya kodi ya kuingiza Sukari ya Viwandani ambayo ilikuwa irudishwa baada ya kuingiza mzigo na kuuvanyiwa uhakiki. Fedha hii hairudishwi kwa wakati jambo linalopelekea kuwapunguzia mitaji. Mfano wa Viwanda vinavyodai nyongeza ya asilimia 15 ya kodi ya kuingiza Sukari ya Viwandani ni kiwanda cha Coca cola wanadai shilingi **bilioni 5.5** Kiwanda cha Pepsi (SBC) wanadai shilingi **bilioni 8.4** kiwanda cha Bakharessa group of Companies wanadai shilingi **bilioni 9** na vingine vingi.

**viii) Muingiliano wa Mamlaka za Serikali yaani ardhi, uchukuzi na Viwanda na kushindwa kufanya kazi pamoja**

Taasisi za Serikali hazina uelewa mmoja katika kuhamasisha

wawekezaji, wafanyabiashara na wenye viwanda na zinasababisha usumbufu mkubwa kiasi cha kuamua kufunga viwanda na biashara.

**ix) Upatikanaji wa malighafi ya kutengenezea karatasi (*unbleach paper*)**

Tanzania inakiwanda kimoja tu ambacho kinazalisha malighafi ya kutengenezea karatasi (*unbleach paper*) ambazo hutumika kutengeneza mabox kiwanda hicho ni Mufindi Paper Mill na kwa kuwa kinatumia malighafi za ndani kimewekewa kinga kwa kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 aina hiyo ya malighafi kutoka nje. Suala hili ni zuri kwani Serikali imelinda kuwanda chake cha ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Mufindi kinazalisha malighafi hiyo na kwa kiasi kikubwa sana inazipeleka katika viwanda vyake vilivyopo nchini Kenya na baadae kuzalisha maboksi na kuyaingiza katika soko la Tanzania. Viwanda vya ndani vinakosa malighafi hiyo na kuamua kuingiza kotoka nje ya nchi na kutozwa kodi hiyo kubwa ya asilimia 25 hivyo kuzifanya bidhaa zao kuuzwa kwa gharama kubwa kuliko zile zinazoingia kutoka nje. Tanzania ina viwanda kumi na saba (17) vya bidhaa za karatasi na uzalishaji wa malighafi hiyo kutoka katika Kiwanda cha Mufindi haukidhi mahitaji ya viwanda vya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Serikali iangalie upya kodi za malighafi kutoka nje ili kuleta ushindani sawia na Viwanda vya nchi jirani.

**x) Nyongeza ya Kodi ya asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya michikichi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliongeza kodi ya asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya michikichi yanayoingizwa kutoka nje kwa lengo la kuvilinda viwanda vianavyozalisha mafuta kutokana na mbegu. Nchi za Afrika ya Mashariki zilikubaliana kuingiza mafuta bila kodi (Zero rated), hatua hii inavipunguza ushindani kwa viwanda vya ndani vinavyoagiza malighafi

ya mafuta ya mchikichi (Crude Palm Oil). Kamati ina maoni kwamba mafuta ya mchikichi siyo mbadala wa mafuta ya alizeti. Kamati inaishauri Serikali kuondoa kodi hiyo ili kuwapa uwezo viwanda vya ndani kukabiliana na ushindani wa Jumuiya ya afrika Mashariki na kuwapa unafuu walaji wa mafuta hayo.

**xi) Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye bidhaa ya Maziwa**

Viwanda vya bidhaa ya Maziwa Tanzania vinakabiliana na changamoto ya ushindani wa soko la bidhaa hiyo katika nchi za Afrika Mashariki kutokana na kutozwa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hatua hii inafanya maziwa yanayozalishwa ncihni kuuzwa bei ya juu ikilinganishwa na yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Maziwa yanayoingia kutoka nchi jirani hayatozwi kodi ya VAT katika nchi zao hivyo kuyafanya kuleta ushindani mkubwa na maziwa ya Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kuondoa kodi hiyo ili kuongeza ushindani na kuwa na tija kwa wafugaji ambao soko lao la maziwa hivi sasa ni la uhakika viwanda vingi vinatumia maziwa hayo.

**k) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa nusu ya kwanza (Mid year) ya mwaka wa fedha 2017/2018.**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **122,215,109,750** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake fedha hizo ni kwa ajili ya mafungu yote mawili (Fungu 44 na 60). Pia ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ha Shilingi 20,000,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa hadi kufikia Disemba, 2017 wizara ilikuwa imekusanya shilingi **8,598,083,500.07** sawa na asilimia 42.99 ya makusanyo yaliyokuwa yamekadiriwa kukusanywa. Makusanyo haya ni karibia ya nusu ya lengo, Kamati inashuri Wizara kuongeza

jitihada ili kuhakikisha wanafikia lengo ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia disemba, 2017 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **29,687,552,982** sawa na asilimiwa **24.3** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwenye mafungo yote mawili (Fungu 44&60) ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Katika kiasi kilichotolewa ni Shilingi **8,000,000,000** tu sawa na asilimia **9.98** ilitolewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo si wakuridhisha ni nusu ya Mwaka wa Fedha sasa lakini fedha zilizopokelewa ni asilimia 9.98 tu ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya mipango ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni kufuatiliana kuhimiza Viwanda vilivyobinafsishwa kufanya kazi, katika kufuatilia zoezi hilo Kamati ilipewa taarifa kuwa idadi ya viwanda vilivyokuwa vimebinafsishwa vilikuwa 156 kati ya hivyo viwanda 62 vinafanya kazi vizuri, 28 vinasuasua, vilivyofungwa kabisa ni 56 na 10 viliuzwa kwa mali moja moja. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinatekeleza makubaliano walioingia wakati ubinafsishaji na kama kuna ukiukwaji wa makubaliano hatua stahiki za kisheria zichukuliwe.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha Tanzania ya Viwanda ni lazima Serikali iweke mazingira ya kusaidia wawekezaji wadogo wa ndani, Kamati inaona kuwa hili linawezekana kwa kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wajasiriamali NEDF. Mfuko huu umekuwa ukitengewa fedha katika Bajeti za Wizara za kila mwaka lakini fedha hizo hazipelekwi. Kamati inashuri Serikali kuuendeleza mfuko huu kwa kuupatia fedha zinazopitishwa na Bunge ili uendelee kuwasaidia na kuwanufaisha watanzania wengi.

**l) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission FCC*).**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ushindani ilianzishwa na Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003 kwa madhumuni ya Kusimamia na Kuendeleza ushindani katika Soko la Tanzania ili kuongeza ufanisi, uzalishaji, usambazaji wa huduma na bidhaa na kumlinda mlaji. Tume ya Ushindani inatekeleza majukumu mbalimbali ikiwepo; kusimamia ushindani katika soko nchini; kuhamasisha wananchi kuhusu wajibu na haki za mlaji; kusimamia mambo yote yanayofanana na ushindani na masuala ya maji;

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Ushindania imefanikiwa katika mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na; kupamba na kudhibiti bidhaa bandia kwa kufanya ukaguzi Bandarini na Bandari Kavu, kufanya ukaguzi wa kushitukiza kwenye maduka na maghala, kushiriki kuteketeza bidhaa bandia na kuendelea kushiriki operesheni za pamoja na taasisi nyingine za uthibiti; kufanya utafiti na kusimamia muungano wa Makampuni na utetezi wa ushindani; kudhibiti muungano wa makampuni na mikataba inayofifisha ushindani; kufanya ushawishi na Uhamasishaji wa Ushindani kwa kutoa elimu ya ushindai kwa Umma na kufanya mapitio ya Sera na Sheria zenye kudhohofisha ushindani katika uchumi na kuishauri Serikali ipasavyo; kufanya uchunguzi na kusikiliza mashauri ya ushindani na kutatua matumizi mabaya ya nguvu ya soko na miunganiko ya Makampuni iliyofanywa bila kuarifu Tume.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu yote na mafanikio ya Tume ya ushindani bado inakabiliana na changamoto za kimuundo na kifedha inayoathiri utekelezaji wa kazi za Tume, Bajeti ya Tume inachangiwa na mamlaka za udhibiti kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za uchangiaji wa fedha kwa shughuli za tume lakini wadau hawa wamekuwa hawapeleki mgao huo kama inavyotakiwa na hivyo kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Tume. Sheria ya Ushindani na Sheria ya Alama za Biahsara ni za miaka mingi sana na yamebainika mapungufu katika utekelezaji wake, sharia hizi zinahitaji marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ushindani ni taasisi muhimu sana katika kulinda ushindani katika masoko yetu na kumlinda mlaji. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea rasilimali ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**m) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya kituo cha Uwekezaji (TIC);**

**Mheshimiwa Spika,** kituo cha Uwekezaji Tanzania ni taasisi iliyoundwa kwa lengo la kuhamasisha na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ili kukuza sekta ya binafsi na hatimaye kuinua uchumi wa nchi. Kituo kinatekeleza majukumu mbali mbali ikiwemo; kuwasaidia wawekezaji kupata vibali na hati mbalimbali za kisheria ili waweze kuwekeza nchini; na kuandaa na kusambaza taarifa sahihi kwa wawekezaji kuhusu fursa za uwekezaji zipatikanazo nchini;

**Mheshimiwa Spika,** majukumu mengine ya TIC ni kuwasaidia wafanyabishara wadogo na wakati kuibua fursa za uwekezaji kwa lengo la kukuza biashara zao na kipato chao kwa ujumla; kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta zitakazo kuza uchumi kwa haraka; na kufanya tafiti za uwekezaji ili kuwezesha kushauri maboresho ya mazingira ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** taasisi ya TIC kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2017 imefanikiwa katika mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na; kusajilli Miradi 144 ya Uwekezaji ambayo inatarajiwa kuwekeza mitaji ya kiasi cha dola za Kimarekeani milioni 4,141.38 na kuajiri wafanyakazi 17,077; kuanzishwa kwa Kamati ya Kiataifa ya kusaidia uwekezaji, ambapo kamati hii inaundwa na wakuu wa Taasisi zinazohusika katika kufanikisha uwekezaji na hukutana mara moja kwa mwezi kwa ajili ya kujadiliana namna ambayo zinaweza kuondoa changamoto kwa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine ni kuwaunganisha wawekezaji wadogo na wakubwa (Business Linkage

Programe) ambapo inawaunganisha kwa lengo wawekezaji wadogo wa ndani waweze kuwasambazia bidhaa wawekezaji wakubwa kulingana na ubora na mahitaji ya wawekezaji wakubwa;

**Mheshimiwa Spika,** taasisi pia imeanzisha kitengo cha Uperembaji wa miradi ambapo wanafanya ukaguzi wa miradi ya uwekezaji ambayo imesajiliwa na kupewa cheti cha Uwekezaji cha TIC kama ilifanikiwa na kujua namna ilivyonufaika na misamaha ya kodi na kujua mchango wa miradi hiyo kwa Serikali kwa kodi na ajira.

**Mheshimiwa Spika,** kituo kinajitegemea katika kuendesha mifumo mbalimbali ya mawasiliano inayotumika katika kuendesha kazi za Taasisi za kilasiku, Mifumo ya uandikishaji miradi (IBM lotus Platform), tovuti mpya taasisi ambayo imewekwa taarifa zote za taasisi kuanzia gharama, taarifa za mikoa yote na vivutio vyake vya uwekezaji vilivyopo kwa lengo la kuwawezesha wawekezaji kuja nchini wakiwa na taarifa kamili na mawazo ya wapi wanataka kwenda kuwekeza.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu na mafanikio yote ya taasisi bado inakabiliana na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na; mazingira ya uwekezaji yasiyotabirika, kumekuwepo na mabadiliko ya mara kwa mara ya vivutio vya uwekezaji jambo linalowakwamisha wawekezaji kupanga mipango ya utekelezaji kwa muda mrefu; na mlolongo mrefu wa uhaulishaji ardhi, uhaulishaji wa ardhi kutoka ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya jumla baada ya kukidhi vigezo villivyo ainishwa kisheria mchakato huchukua muda mrefu sana kati ya miaka miwili hadi mitatu jambo ambalo wawekezaji wengi hushindwa kuvumilia na kuamua kuahirisha.

**Mheshimiwa Spika,** ukosefu wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji, tatizo la upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali kama vile miradi ya kilimo, utalii, viwanda, majengo makubwa ya biashara na hii inatokana na kukosekana kwa maeneo maalumu

yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji; na uandaaji wa hati ndogo (*Subtitle*) kutoka hati isiyo halisi (*Derivative Rights*).

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya sasa ya haitoi fursa kuandaa hati ndogo kutoka kwenye hati isiyohalisi ambayo hutolewa na kituo cha Uwekezaji kwa wawekezaji wa kigeni wanaowekeza katika majengo ya nyumba za kuuza hivyo kukwamisha aina hii ya uwekezaji;

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya Sheria ya Uwekezaii ya 1997 na Sera ya Uwekezaji ya 1996, hayaendani na hali ya sasa ya dunia ya uwekezaji kwani sera na Sheria hizi zimepitwa na wakati na hivyo hazikidhi matakwa ya kuwavutia na kuwahudumia wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni kuwa; urasimu katika baadhi ya taasisi za Serikali katika kuwahudumia wawekezaji ili kutoa huduma kwa haraka; kutokuwepo kwa maafisa wenye mamlaka ya kutoa vibali na leseni kwa wawekezaji katika *One Stop Facilitation Centre,* ambapo kuna taasisi nyingi lakini ni Idara ya Uhamiaji na Wizara ya kazi tu ndio wenye mamlaka ya kutoa Vibali tu; uhaba wa miundombinu muhimu kwa ajilli ya Uwekezaji kwenye maeneo mengi hasa maeneo ya mikoani hivyo kupelekea wawekezaji na miradi mingi kurundikana katika maeneo ya mikoa yenye miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali haijaipangia fedha za Ruzuku toka 2016/2017 hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Taasisi. Aidha, Taasisi inakabiliwa na upungufu wa rasilimali watu; ufinyu wa ofisi, Jengo la ofisi ni dogo hivyo kusababisha msongamano wa watumishi na wageni, pia jengo limechakaa sana hivyo kuleta sura mbaya kwa wawekezaji ikizingatiwa kuwa TIC ndio kioo cha nchi katika masuala ya Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za makusudi kukabiliana na changamoto tajwa za TIC ili kuiongezea ufanisi na kukuza uwekezaji nchini.

**n) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji majukumu ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).**

**Mheshimiwa Spika,** wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni ni Mamlaka iliyoanzishwa na Serikali kwa lengo la ufanisi na ubora na kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali kuu huduma hizo ni pamoja na kusimamia Sheria za usajili wa Makampuni; kusajili Majina ya Biashara; kusajili Alama za Biashara na Huduma; kutoa hataza za uvumbuzi; kusajili na kutoa Leseni za Biashara na Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake BRELA imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wake wa Mwaka 2016/17 hadi Disemba, 2017 ambapo; kutengeneza na kuboresha mifumo ya usajili kwa njia ya Mtandao, kukamilisha mfumo mpana wa kusajili kwa njia ya mtandao unaounganisha mifumo ya taasisi nyingine za Serikali; kuboresha mazingira ya utoaji huduma na kupeleka huduma karibu na wananchi na hii imetekelezwa kwa kufungua ofisi za Kanda na kuanzisha kituo cha kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao; na kutoa elimu na uhamasishaji wa usajii na urasimishaji wa Biashara mikoani kwa njia ya Semina mbalimbali, kushiriki katika maonyesho ya Sabasaba na Nanenane na wiki ya Viwanda, kushiriki katika makongamano mbalimbali mikoani na kufanya vipindi vya TV na Radio.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake BRELA inakabiliana na changamoto za Uelewa mdogo wa wadau hususani wilayani na vijijini juu ya matumizi ya TEHAMA katika kupata huduma; uelewa mdogo wa wadau juu ya sheria za usajili na umuhimu wa kusajili makampuni, majina ya biashara, alama za biashara, huduma na hataza za uvumbuzi. Katika kukabiliana na hilo wakala inaendelea kuelimisha wadau wake kwa kutumia semina, warsha, vipeperushi, radio, TV, magazeti pamoja na kuanzisha vituo vya kutoa elimu katika ofisi za maafisa biashara nchini.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Agizo la Serikali la

kupupeleka makusanyo ya Taasisi zake katika Mfuko wa Mkuu wa Serikali halafu kurudi kuomba kwa matumizi ya Serikali inakwamisha tu utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizokuwa zinauwezo wa Kukusanya fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kamati inashauri kuwa ni vema fedha hizo Taasisi zingebaki nazo na kuendelea kutekeleza majukumu yake na mwisho wa siku zikawa zinafanyiwa ukaguzi kama zimetumia pesa hizo inavyostahili.

**4.5 2.1.4 Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Taasisi zilizo chini yake**

**a) Kupokea na Kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Hali ya Uhifadhi wa Mazinira katika maeneo ya Madampo.**

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya Mazingira katika Madampo nchini sio ya kuridhisha. Kumekuwa na changamoto katika usimamizi wa taka ngumu nchini hasa katika maeneo ya miji mikubwa. Madampo mengi hayajajengwa katika viwango vinavyotakiwa hali hii inasababisha uchafuzi na kuhatarisha mazingira na afya za wakazi wa maeneo husika. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na tatizo hili Ofisi ya Makamu wa Rasi-Mazingira chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 vifungu vya 114-119 inaipa wajibu Mamlaka ya Serikali za Mitaa kusimamia masuala ya ukusanyaji utupaji na uhifadhi wa taka ngumu kutoka kwenye maeneo ya masoko, maeneo ya biashara, viwandani n ahata makazi.

**Mheshimiwa Spika,** ukusanyaji wa taka ngumu uhifadhi na utupaji kutoka kwenye maeneo ya miji na vijijini linahitaji kutenga vituo vya taka vya muda; na kubaini hatua bora za kuzingatia kwenye utupaji wa taka hizo. Sheria hii inaipa Serikali za Mitaa mamlaka ya kuhakikisha kuwa kunakuwa na mazingira yanayoridhisha na kuwawajibisha wale wanaochafua mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** hali mbaya ya madampo inachangiwa sana na mambo yafuatayo; ukuaji wa miji, ujenzi wa

miundombinu ya kushughulikia taka ngumu zinazozalishwa. Uwezo wa kuzoa taka ngumu upo chini ya asilimia hamsini. Kuna upungufu wa vitendea kazi kama malori, skip containers, compactor truck, tipper truck; na ufinyu wa bajeti kwa ajili ya usimamizi wa taka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazo taarifa kuwa, baadhi ya maeneo hayana madampo yanayokidhi viwango; baadhi ya miji haina wataalamu wa mambo ya mazingira; mifumo isiyo sahihi ya majitaka; na ukosefu wa maeneo maalumu ya kukusanyia taka hivyo kusababisha wananchi kujikusanyia taka mahali popote pale.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Sheria ya Mazingira kuzipa Mamlaka za Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia taka ngumu, Serikali za Mitaa nyingi zimeshindwa kumudu na halijapewa uzito. Kamati inashauri Serikali izipunguzie Serikali za Mitaa jukumu hili na iunde mamlaka yenye nguvu chini ya Wizara inayosimamia Mazingira, mamlaka itakayosimamia suala la taka ngumu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, katika kukabiliana na changamoto ya kuzagaa kwa taka katika maeneo ya madampo, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za kujenga madampo ya kisasa katika kila mkoa.

**b) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Hali utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Mazingira.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka kadhaa sasa tumeshushuhudia Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutengewa bajeti ndogo sana kulingana umuhimu wake na majukumu inayoyatekeleza. Aidha, bajeti hii imeendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira katika kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa Bajeti iliona umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Mazingira ambao ulianzishwa kwa lengo la kuiwezesha kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya kushughulikia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mazingira ulianzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kifungu 213. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali kupitia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ilitenga shilingi **bilioni 2** kama kianziao (*Seed money*) kwa ajili ya kugharamia shughuli za mfuko. Lakini hadi kufikia Septemba, 2017 ni kiasi cha shilingi Milioni 34 tu ndio kilikuwa kimepokelewa kwa ajili ya Mfuko jambo linalopelekea kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Mfuko.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uhaba wa fedha katika Mfuko bado umefanikiwa kutekeleza baadhi ya kazi na, mpaka kufikia Juni, 2017 kazi zilizokuwa zimetekelezwa na Mfuko ni pamoja na kuandaa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Mfukio wa Mazingira; kuanda Rasimu ya Kanuni za Uendeshaji wa Mfuko; kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Utoaji wa Fedha kwa ajili ya miradi inayofadhiliwa na Mfuko.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mazingira unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwepo za Ufinyu wa Bajeti; Ukosefu wa Watumishi wa kudumu wa Mfuko; Sekretarieti ya Mfuko ni watumishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais ambao wana majukumu mengine ukiacha hayo ya Mfuko.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kufanya tathimini na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kutoka katika shughuli zinazohusu Mazingira na kuwasilisha mapendekezo hayo Wizara ya Fedha tangia mwaka 2016 bado kibali cha kupatiwa mapato hayo hakijatoka. Changamoto hizi zinachangia kiasi kikubwa kazi zilizopangwa kutekelezwa na Mfuko kutofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa kuruhusu tozo za Mazingira angalau kwa asilimia chache kuingia kwenye Mfuko wa Mazingira ili kuuwezesha Mfuko kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

**c) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Hali ya Mazingira katika Mifumo ikolojia ya Milima.**

**Mheshimiwa Spika**, Mifumo ikolojia ya milima ni chanzo kikuu cha mito mikubwa duniani, asilimia 50 ya binadamu duniani wamekuwa wakitegemea maji kutoka milimani. Aidha, milima imekuwa muhimu sana katika maendeleo ya jamii kiuchumi, milima ni hifadhi kubwa ya bioanuai (mimea na wanyama), hali nzuri ya hewa, ardhi yenye rutuba, vyakula vya binadamu na asili ya dawa na sehemu za utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya mazingira katika Mifumo Ikolojia ya milima ni mbaya na iko hatarini kupoteza bioanuai yake kutokana na ukuaji mkubwa wa mahitaji na matumizi ya rasilimali zake. Kwa mfano, milima Mkoani Iringa ilikuwa imefunikwa na misitu mizito ya miyombo lakini kwa sasa imepungua sana kutokana na shughuli za kibinadamu.

**Mheshimiwa Spika**, utunzaji wa Mifumo ikolojia ya milima una faida kubwa ukizingatia kuwa takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 50 ya binadamu wanaishi katika maeneo ya milima na kufanya shughuli zao za kimaendeleo katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuongeza jitihada katika kisimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ili kutunza maeneo ya Mifumo Ikolojia ya Milima na kuhakikisha kuwa shughuli za binadamu zinanzofanyika katika maeneo hayo ni endelevu. Aidha, utekelezaji wa Sheria hii uende sambamba na Elimu ya uhifadhi wa Mazingira, hivyo basi Ofisi iwezeshwe kifedha ili iweze kutekeleza zoezi la kutoa elimu ya Mazingira.

**d) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Binadamu na Hifadhi Hai (Man and Biosphere Reserve).**

**Mheshimiwa Spika**, Binadamu na Hifadhi Hai (*Man and Biosphere Reserve*) ni program ya kimataifa ambayo ipo chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni

UNESCO iliyoanzishwa miaka ya 1970 kufuatia kongamano lililoandaliwa na UNESCO -1968 kujadili hali halisi na changamoto za maeneo lindwa. Hifadhi hai ni njia ya hali ya juu ya uhifadhi wa maeneo ambayo yanatambulika kimataifa katika program hii, maeneo hayo yanaweza kuwa baharini au nchi kavu. Dunia nzima kuna hifadhi hai 651 katika nchi 120 ikiwemo Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, katika ngazi ya kitaifa Program ya Binadamu na Hifadhi Hai inasimamiwa na Baraza la Taifa la usimamizia wa Mazingira NEMC kwa kushirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Binadamu na Hifadhi Hai. Zoezi la kuainisha maeneo ya hifadhi hai hapa nchini lilianza mwaka 2008 ambapo yaliainishwa maeneo mbalimbali na zoezi hili lilifanywa na Kamati ya Kimataifa ya Hifadhi Hai.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa nchi ya Tanzania maeneo ya Hifadhi Hai ni Ngezi- Vumawimbi Nature Forest Resot iliyopo Pemba na hifadhi ya Taifa ya Ras ya Jozani-Chwaka iliyopo Unguja; Saadani National Park (SANAPA); Mnanzi Bay Ruvuma Estuary; Mlima Kilimanjaro - Amboseli (Tanzania na Kenya); Kimisi/ Burigi- Akagera (Tanzania na Rwanda); Mifumo ikolojia ya Malagarasi ecosystem (Tanzania na Burundi); na Selous – Niasa (Tanzania na Mozambique).

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na zoezi hilo la uteuzi wa maeneo ya hifadhi hai kuanza mwaka 2008 lakini mpaka sasa ni maeneo mawili tu ndio yameweza kukidhi vigezo vya kimataifa na kufanikiwa kuingia katika Hifadhi hai za kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, Hifadhi Hai zikiwa kama moja ya rasilimali za nchi ina faida zake ambazo ni; uhifadhi maeneo hayo na kuyapatia ulinzi kunahamasisha uhifadhi wa bioanuai zetu ambazo hutumika Kusaidia na kuhamasisha shughuli za kitafiti, mafunzo, ufuatiliaji na kubadilishana taarifa; Kuchoche maeneo ya binadamu kijamii na uchumi ambayo ni endelevu kiikolojia; hutumika kama mpango wa matumizi bora ya ardhi; Hifadhi hai zinaiwezesha nchi kufahamika na kujitangaza kimataifa; na Kushiriki katika mtandao wa dunia

wa binadamu na Hifadhi hai katika kubadilishana taarifa, uzoefu na ujuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni mshiriki wa Mtandao wa Afrika wa kuhifadhi bioanuai (Network of African Biosphere Reserve) na inapaswa kulipa gharama za ushiriki na kuchangia mfuko wa AfriBio Fund lakini haijaweza kulipa ada hiyo. Jambo hili linaonyesha kuwa Serikali ya Tanzania haijalitilia maana ni suala la uhifadhi wa bioanuai na hivyo kuikosesha nchi fursa ya kupata fedha kutoka katika Mfuko huu kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa ili kuhakikisha wakazi wa maeneo yanayozunguka Hifadhi Hai zetu wanashiriki katika kulinda hifadhi zetu, Serikali inatakiwa kuanzisha program mbalimbali za kuishirikisha jamii katika zoezi hili, na pia watoe huduma ambazo zinatokana na uhifadhi huo kwa jamii inayozunguka hifadhi jambo ambalo litawapelekea kuona faida ya kuyahifadhi maeneo hayo na kuwafanya waendelee kuyahifadhi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi iliyobarikiwa sana katika suala la rasillimali, tuna hifadhi lindwa nyingi sana lakini mpaka sasa ni hifadhi nne (4) tu ndo zimefanikiwa kuingia katiaka Hifadhi Hai. Kamati inaishauri Serikali iongeze jitihada na kuhakikisha maeneo mengi ya hifadhi lindwa yanaingia katika utaratibu wa Hifadhi Hai ili tuweze kunufaika na utaratibu huo.

**e) Kupokea na Kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu maendeleo ya Bonde la Kihansi na Matarajio ya Taifa katika Mradi huu.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata maelezo juu ya Bonde la Kihansi na Mradi wa uhifadhi wa Bonde la Kihansi. Kamati pia ilipata fursa ya Kutembelea Bonde la Kihansi na kujionea Utekelezaji wa Mradi wa kuhifadhi Bonde la Kihansi- *Kihansi catchment Convention Management Project* (KCCMP).

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu usimamizi wa

rasilimali maji katika dakio na ushirikishwaji wa jamii katika kutunza mazingira. Mradi huu unahusu unasimamia rasilimali maji katika bonde la Kihansi, utunzaji wa bioanuai, shughuli mbalimbai za maendeleo za kijamii na mafunzo kwa jamii, zinazopatikana katika Bonde la Kihansi na ufuatiliaji na usimamizi wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, bonde hili ni chanzo kikubwa cha maji kwa uzalishaji wa umeme, pia ni muhimu kiikoloji maana rasilimali za misitu/upumuaji wa hewa ukaa na shughuli za kilimo na mifugo zianafanyika katika eneo hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza mradi huu NEMC na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira hufanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira wakiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, Taasisi ya Utafiti na Wanyamapori (TAWIRI), Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Ofisi ya Bonde la Rufiji, Wizara ya Kilimo na Uvuvi, TANESCO, Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu Tanzania na Toledo and Brox Zoological Society, chuo kikuu cha Dar es Salaam na Sokoine.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepata ufadhili wa dola za kimarekeani 5.98M ili kutekeleza mradi wa kuhifadhi mazingira ya bonde la Kihansi na mradi huu utatekelezwa kwa miaka mitano toka 2013 hadi 2017. Mradi unasimamia shughuli zote zinazohusu utunzaji wa wa vyanzo na rasilimali maji kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa maji kwa matumizi mbalimbali ambapo bonde la Kihansi lina vyanzo vya maji 901 toka katika wilaya ya Mufindi, Kilolo na Kilombero na kati ya vyanzo hivyo ni asilimia 27 tu ndo imefanikiwa kuhifadhiwa na vilivyobaki havijahifadhiwa.

**Mheshimiwa Spika,** mradi unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na; uwelewa mdogo wa wananchi kuhusu uhifadhi wa mazingira na vimbe wengine ambapo wananchi wanaamini kuwa Serikali inapoteza fedha kwa kutunza na kuhifadhi bioanuai (mfano chura wa Kihansi); ongezeko la idadi wa wayu na shughuli za uchepushaji maji katika vyanzo vya maji ya binde la Kihasi;

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni pamoja na ukosefu wa mpango mkakati mzuri ambao utaruhusu shughuli zote zifanyikazo katika Bonde la Kihansi kuendelea na shughuli zake na kutunza mazingira hayo (kilimo-upande wa juu wa mto na uzalishaji umeme- upande wa chini wa bonde); matumizi makubwa ya kemikali kwenye kilimo ambazo huathiri ubora wa maji na maisha ya baadhi ya viumbe hai hasa chura wa Kihansi;

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni kukosekana kwa mpango/mkakati endelevu baada ya ufadhili wa sasa wa wadau wa mazingira kutoka nje kumaliza mkataba wao. Kamati inashuri Serikali itenge fedha kwa ajili ya mradi huu na wanufaika kama TANESCO watoe tozo kiasi kwa ajili ya uhifadhi wa bonde la Kihansi.

**f) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Usimamizi wa Mazingira katika Ukanda wa Pwani.**

**Mheshimiwa Spika,** athari za mabadiliko ya tabianchi zinazidi kujidhihirisha katika maeneo mengi ya Dunia na hapa nchini pia. Maeneo ya Pwani ya Jiji la Dar es salaam ni miongoni mwa maeneo ambayo athari za mabadiliko ya Tabianchi zinazidi kuongezeka na zinadhihirika, athari hizi ni kama mafuriko, kumomonyoka kwa udongo kutokana na kuongezeka kwa maji ya bahari na kuongezeka kwa magonjwa ya kuambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuliona hili Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilifanya jitihada za kuanzisha Mradi wa Kujenga Uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi. Utekelezaji wa Mradi ulianza Novemba, 2012 na ulitarajiwa kuisha Oktoba, 2017. Mradi unatekelezwa kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), maeno ya Mradi ni Obama/Ocean Road, Kigamboni, Bungoni, kata ya Buguruni, Mibulani-Mtoni, Salenda bridge, Kunduchi, Mbweni na Ununio.

**Mheshimiwa Spika**, shuguli zianazotekelezwa katika Mradi huu ni ujenzi wa ukuta wa Ocean road na Kigamboni; ujenzi

wa mitaro ya Buguruni, Ilala, Mtoni na Temeke; kurudisha matumbawe katika eneo la Bahari ya Hindi (Eneo la Sinda); kutoa mafunzo kuhusu Nishati safi; na kurudisha mikoko ya mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Bajeti ya kutekeleza mradi ni Dola za Kimarekani 3,489,482. Utekelezaji wa shughuli hizi unaendelea.

**Maheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mradi huu Ofisi inakabiliana na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na utupaji wa taka ngumu na utiririshaji wa maji machafu kwenye mitaro; nyumba za makazi kujengwa karibu sana na mitaro hivyo kuwafanya watupe uchafu na kuziba mitaro; utofauti wa mwinuko katika makutano ya barabara inayosababisha maji kutuama (Mfano makutano ya Barabara ya Temeke-Mbagala na Kilwa); ukataji haramu wa Mikoko katika maeneo mengi pamoja na uvuvi haramu; na ung'oaji wa mikoko inayopandwa kabla haijakuwa kwa lengo la kuhujumu zoezi.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya mabadiliko ya tabianchi sio jambo la kutania ni kweli Mradi huu unatakiwa kutekelezwa kwa Jitihada sana. Lakini Serikali haijaonyesha kulitilia mkazo sana na badala yake kuacha Mradi huu muhimu kutekelezwe kwa Ufadhili kwani katika maenoa ambayo wamepanga kutekeleza Serikali hawapeleki fedha kwa wakati jambo linalipelekea kuchelewa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Ni Imani ya Kamati kuwa kuanzishwa Mfuko wa Mazingira na kuupa ruhusa ya kukusanya mapato kwa asilimia ndogo kutoka katika shughuli zote zinazohusu Mazingira kutaipunguzia Serikali majukumu mengi yahusuyo utunzaji wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ikamilishe zoezi la kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira kwa kuipatia ile *Seed Money* na kutoa kibali kwa kodi zitokanazo na Shughuli za mazingira kuingia katika Mfuko huu.

**g) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu hatma ya Viwanda vya mifuko ya Plastiki nchini kutokana na utekelezaji wa agizo la kutotumia mifuko ya plastiki.**

**Mheshimiwa Spika,** mifuko ya plastiki imekuwa maarufu sana kutokana na kuwa imara, kuuzwa kwa bei nafuu na kupatikana kiurahisi jambo linayoipelekea kuwa chaguo la wengi. Kutokana na sifa hizo imepelekea kuwa na ongezeko la uzalishaji na matumizi yake. Usimamizi wa taka za mifuko ya plastic hasa katika maeneo ya mijini ni changamoto hasa kutokana na utupaji hovyo wa taka hizo. Bado hatujapata mpango madhubuti wa kuzirejelesha taka hizi hata viwanda vinavyozalisha bidhaa hizi bado hazijafanikiwa katika zoezi hilo na kati ya Viwanda 46 ni viwanda kumi (10) tu ndio vinamifumo ya kurejesha taka hivyo badala yake zinatupwa na kuzagaa hovyo mitaani.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto ya kudhibiti uchafuzi na athari za kimazingira zinazotokana na mifuko ya plastiki nchi nyingi ziliamua kudhibiti/kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, mpango wa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ulianza kutekelezwa mwanzoni mwa miaka ya 2000. Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki mnamo mwezi Julai, 2017 lilipokea na kupitisha muswada wa Sheria ya kupiga marufuku Matumizi, Uzalishaji, Uingizaji na Uuzaji wa mifuko ya plastiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2011. Tanzania imeunga mkono mswada huu na utaanza kufanya kazi baada ya kutiwa saini na wakuu wa nchi za Jumuiya hii.

**Mheshimiwa Spika,** athari za kimazingira zitokanazo na taka za mifuko ya plastiki ni kuwa; asilimia kumi (10) tu ya mifuko inayozalishwa ndiyo inachakatwa iliyobaki huishia kuzagaa katika mazingira; huelea kwenye maji na hewa na kusafiri umbali mrefu ambapo katika kuzagaa huko huishia kuliwa na wanyama na ndege; huharibu mandhari ya miji; huathiri uwezo wa kuozesha na uchakataji wa taka; na huziba mifumo ya majisafi na majitaka.

**Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mifuko ya plastiki hapa nchini ni mdogo sana mfano kwa mwaka 2016 takwimu zinaonyesha kuwa tulizalisha tani 73.6 wakati takwimu za TRA zinaonyesha kwa mwaka 2016 ziliingizwa tani 1354.38 za mifuko ya plastiki. Hivyo basi kuruhusu matumizi ya mifuko ya pastiki ni kuruhusu nchi yetu kuwa soko la bidhaa hiyo. Nchi nyingi zimekwishapiga marufuku matumizi ila uzalishaji unaendelea kwa ajili ya kuuza nje ya nchi zao. Mfano Kenya wamepiga marufuku matumizi ya bidhaa hii lakini uzalishaji bado unaendelea kwa ajili ya masoko ya nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** udhibiti wa taka za plastiki imekuwa changamoto sana, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali ihamasishe wawekezaji kuwekeza katika Viwanda vya kurejelesha taka za plastiki. Aidha, katika kupiga marufuku uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki, viwanda vinavyozalisha bidhaa hii vipewe muda wakubadili teknolojia na kuzalisha bidhaa mbadala ya hii. Mfano mifuko ya nguo na karatasi au mifuko itakayo oza baada ya muda mfupi.

**Mheshimiwa Spika,** kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ni fursa kwa taasisi ya SIDO na TIRDO kushirikiana na wajasiriamali kubuni bidhaa mbadala ya mifuko ya plastiki.

**h) Kupokea na Kujadili Taarifa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Utekelezaji wa majukumu Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa nusu ya kwanza (Mid year) ya mwaka wa fedha 2017/2018;**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha **2016/2017** Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **14,817,377,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi **8,028,925,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **6,788,452,437.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** upatiakanaji wa fedha za Ofisi ya Makamu wa Rais –Mazingira, kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha Mfano kati ya Shilingi **6,788,452,437.00** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya

Maendeleo ni Shilingi **1,061,079,990.00** tu ndizo zilizopokelewa ambapo ni sawa na asilimia **15.63** jambo hili hupelekea kukwamisha utekelezaji wa mipango ya Wizara kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukosefu wa fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wameendelea kutekeleza masuala mbalimbali katika kuhakikisha wanaendelea kusimamia Hifadhi ya Mazingira, mambo yaliyotekelezwa ni pamoja na; kusimamia uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mazingira kuhusu miongozo katika kufanya kaguzi za kimazingira; kuendelea kutoa elimu ya mazingira kwa kuendesha vipindi mbalimbali vya redio, TV, na warsha mbalimbai; kuendelea kutekeleza Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Dar es Salaam, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ufadhili; na kuandaa miradi mipya inayohusu Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira linakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama kubwa wa TAM zinazotozwa na baraza na kulalamikiwa na wadau, Baraza limewasilisha mapendelezo ya namna ya kuzipunguza gharama hizo; na ujenzi wa majengo na uendeshaji wa shughuli mbalimbali ndani ya mita 60 kinyume na Sheria; na Uhaba wa wafanakazi, vitendea kazi na Ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira wameendelea kutekeleza majukumu yake kwenye mazingira magumu ya kibajeti. Tumeshuhudia Bajeti ya Ofisi hii muhimu ikiwa ndogo sana na bado haipelekwi kwa wakati jambo linalopelekea kukwama kwa miradi mingi ya Mazingira. Kwa kuzingatia umuhimu wa kutunza mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuitenga Bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**i) Kupokea na Kujadili Taarifa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Hali ya Mazingira katika maeneo ya viwanda na Migodi pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kudhibiti mazingira ya maeneo hayo.**

**Mheshimiwa Spika,** hali ya mazingira katika maeneo ya Viwanda na Migodi si ya kuridhisha na hii ni kutokana na kiwango kidogo cha uzingatiaji wa Sheria na kanuni za Mazingira. Kwa mujibu wa ukaguzi uliofanya kuanzia mwaka 2015 hadi 2017 ni asilima 30 ya viwanda na asilimia 4 tu ya migodi ndio vinazingatia sharia na maelekezo ya kuimarisha hali ya usafi na uhifadhi wa mazingira. na hii ni kutokana na kutokuwa na vifaa vya kuhifadhi taka na mfumo usioridhisha wa uondoshaji wa taka ngumu zinazozalishwa katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto za kimazingira zilizojitokeaza katika maeno ya Viwanda na Migodi ni;- ukiukwaji wa mashariti yaliyoainishwa kwenye vyeti vyeti vya mazingira; baadhi ya Viwanda na migodi kuanzishwa karibu na maeneo ya migodi kuanzishwa karibu na maeneo ya makazi ya watu; uhifadhi duni wa taka hatarishi; utoaji wa hewa yenye vumbi kinyume na kanuni za mazingira; utupaji holela wa taka ngumu kwenye mazingira; utoaji wa kelele na mitetemo Zaidi ya viwango vilivyobainishwa kwenye kanuni za mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** utiririshaji wa majitaka katika maeneo ya viwanda na migodi ni changamoto nyingine, baadhi ya viwanda na migodi havina mitambo ya kutibu majitaka aidha imeharibika au hawaitumii makusudi na hivyo kutiririsha maji yenye kemikali kwenye mazingira kinyume na sheria. Changamoto nyingine ni mitetemo inayotoka katika shughuli za viwandani na uchimbaji wa madini, hali hii inachangiwa Zaidi na ukaribu wa makazi ya watu na shughuli hizi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hizo Ofisi inachukuka hatua mbalimbali zikiwemo;- kutoa amri za mazingira kwa mujibu wa Sheria, hapa hutoa amri kwa wamiliki wa kiwanda kutekeleza masharti ya mazingira, amri

ya urejeleshaji wa mazingira na amri ya kusitisha shughuli zenye madhara makubwa kwa mazingira; kupeleka mahakamani viwanda na migodi iliyokiuka sharia na kukaidi amri za mazingira; kutoza faini viwanda na migodi inayokiuka sharia na kanuni za mazingira; kuendelea kutoa elimu kwa wenye viwanda na migodi kuhusu uzuiaji na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, wajibu wao katika kuhifadhi mazingira namatakwa ya sharia ya Usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake; na kusitisha shughuli za uzalishaji kwa viwanda na migodi hadi wanapofanya marekebishi stahiki kama inavyoamrishwa kwenye amri zao.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya mazingira katika maeneo ya viwanda na mazingira si yakuridhisha kabisa, jitihada za dhati zinatakiwa katika kusimamia maeneo hayo. Ofisi ya Makamu wa Rais ina wajibu wa kusimamia maeneo haya lakini hayajawezeshwa vya kutosha.

**j) Kupokea na Kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Fukwe na Maziwa.**

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imebarikiwa rasilimali kubwa ya maji inayokadiriwa kufikia kilometa za mraba 62,000 sawa na asilimia 6.5 ya eneo lote la nchi, ukubwa huu unajumuisha bahari, mito mikubwa na midogo na mabwawa. Maeneo haya yanakabiliwa na changamoto ya uharibufu wa mazingira kutokana na shughuli za kibinadamu na mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ya ukanda wa pwani, Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa yana umuhimu mkubwa kiuchumi na kijamii. bahari na ukanda wa pwani ni muhimu kwa shughuli za utalii, usafirishaji, utengenezaji wa chumvi na kilimo cha mwani; Shughuli hizi hutoa ajira kwa wakazi wa pwani na kuwaingizia kipato; maeneo ya pwani ni muhimu kiikolojia kwa viumbe waishio baharini; Bahari zetu zina rasillimali kubwa sana ya samaki ambao pia hutoa ajira kupitia uvuvi; mito na maziwa ni chanzo kikubwa cha maji kwa matumizi ya manyumbani na viwandani, katika shughuli za umwagiliaji, usafirishaji na uzalishaji umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Sababu zinazopelekea mazingira na rasilimali ya fukwe za bahari, maziwa, mito na mabwawa kuharibika ni pamoja na;- utekelezaji wa sheria hasa tafsiri ya mita 60 na tika chanzo cha maji; rasilimali zipatikanazo katika bahari, maziwa, mito na mabwawa kuwa chanzo kikubwa cha kujipatia kipato kwa wananchi wa maeneo ya pwani; usimamizi hafifu wa utekelezaji na uzingatiaji hafifu wa sheria zinazohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira; kamati za mazingira kwenye maeneo ya vijijini kuwa na uelewa mdogo wa masuala ya mazingira; ukosefu wa program ya pamoja za kusimamia rasilimali za maji zinazovuka mipaka (mfano hifadhi ya maziwa kama ziwa Jipe); na kuendelea kutumia rasilimali ya majikwa upande wa nchi ya Kenya kwa kujenga mabwawa manne bila kuzingatia mahitaji ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kuwa katika usimamizi wa maeneo ya Bahari, maziwa, Mito na Mabwawa ni utekelezaji wa Sheria za usimamizi wa maeneo hayo hususani Sheria ya Mita 60, tafsiri ya mita 60 haijaeleweka kwa watu walio wengi jambo linaloleta changamoto katika utekelezaji wake. Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kutoa elimu na tafsiri sahihi ya sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Sheria ya Mita 60 umekuwa ukisimamiwa kwa baadhi ya shughuli na watu tu kwani tumeendelea kushuhudia makazi na shughuli mbalimbali zikikiuka sheria hii kwa kuendelea kufanyika katika maeneo hayo bila kuchukuliwa hatua yoyote. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa utekelezaji wa Sheria hii usibague watu au shughuli Fulani tu.

## 2.2 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2016, inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha na inatekelezwa na Wizara inazozisimamia.

### 2.2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha Kwa Mwaka Wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa lengo la kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake ambapo kamati ilitembelea Mradi namba **6260** unaojulikana kama *NDC-Industrial Park (TAMCO-Kibaha),* na Mradi Mradi namba **5301** wa *Climate Change Adaptation Programme* ambao ni mradi wa Ujenzi wa ukuta katika Ukanda wa Pwani na Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

#### a) Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu **44** iliidhinishiwa shilingi **9,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi namba **6260** unaojulikana kama *NDC-Industrial Park (TAMCO-Kibaha)* .Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Jukumu la Shirika la Maendeleo la Taifa katika kuanzisha miradi ya aina hii ni kutafuta ardhi ya Mradi, kujenga miundombinu inayohitajika na kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kujenga Viwanda katika maeneo hayo. Lengo la Shirika ni kuendeleza eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya tisa (9)

Mpango wa matumuzi ya ardhi katika eneo la TAMCO lenye ukubwa wa ekari **230** ni kutumia hekari 95 kwa ajili ya Viwanda vya nguo na Mavazi ekari 64 Viwanda vya Kuungankisha magari na mitambo mbalimbali, ekari 43 Viwanda vya Kibaiolojia na Vifaa tiba, ekari 5 kwa ajili ya mabwawa ya kutibu maji taka, ekari 5 kwa huduma mbalimbali za uzalishaji na ekari 18 kwa ajili ya Barabara na maegesho ya magari.

**Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni kukamilika kwa mpango wa matumizi ya ardhi (*Land*

*Use Plan*) na upimaji wa viwanja kulingana na Mpango ulioidhinishwa na Mamlaka husika (*Cadastral Survey*). Pia usanifu (*Engineering design*) wa matangi ya maji safi, mabwawa ya maji taka na mfumo (*Network*) wa kusambaza maji safi na kukusanya taka umekamilika. Kwa upande wa barabara, usanifu umefanyika kwa kipande cha urefu wa Km 1 ambapo sehemu yanye urefu wa meta 400 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami mpaka kilipo kiwanda cha Viuadudu (*Biolarvicides*).

**Mheshimiwa Spika**, Mradi unahitaji kiasi cha Shilingi **Bilioni 16.4** kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya barabara, kituo cha kupozea umeme, mtandao wa nyaya za kusambaza umeme, matanki ya kuhifadhi maji safi, mabwawa ya kutibu maji yaliyotumika na mitandao ya mabomba kwa ajili ya kusambaza maji safi na kukusanya maji taka.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mradi huu ni kivutio kikubwa kwa ajili ya uwekezaji kwani eneo hili la Viwanda lipo katika barabara kuu ya Dar es salaam Morogoro hivyo ni rahisi kusafirisha malighafi kwenda katika eneo hili na kusafirisha bidhaa kuelekea sokoni.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto za utekelezaji wa mradi huu ni ukosefu wa fedha jambo linalokwamisha utekelezaji wake. Kamati inaishauri Serikali kupeleka fedha zilizosalia kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

### b) Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi wa Mradi namba **5301** wa *Climate Change Adaptation Programme* ambao ni mradi wa Ujenzi wa ukuta katika Ukanda wa Pwani na Zanzibar kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la usawa wa bahari linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Katika Mradi huu Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo la Pangani-Tanga na Oceanroad-Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu kwa upande wa mto Pangani unajumuisha urefu wa meta **950** kwa upande wa Kaskazini yaani Pangani Mjini na meta **660** upande wa Bweni. Ujenzi wa ukuta huu ulianza rasmi tangu tarehe 01 Machi, 2017, Mkandarasi aliyepewa kazi hii ni DEZO Civil Contractors. Mradi huu unakisiwa kugharimu kiasi cha Shilingi **2.4** bilioni mpaka kukamilika kwakwe, ulianza rasmi tarehe 01 Machi, 2017, chini ya Mkandarasi DEZO Civil Contractors.

**Mheshimiwa Spika**, Asilimia **90** ya fedha za Mradi ni fedha za wafadhili na Asilimia 10 ni fedha za ndani, fedha za wafadhili zimekwishatolewa ambazo ni kiasi cha Shilingi **2.4** bilioni ambazo zimeanza kutekeleza mradi kwa upande wa Pangani Mashariki, asilimia **10** ya fedha za ndani ambazo zinatekeleza mradi kwa upande Pangani Magharibi bado hazijatolewa. Mradi huu ulikuwa unakadiriwa kukamilika Novemba, 2017 iwapo mipango yote ingekwenda kama ilivyokuwa imepangwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokamilika kwa ukuta wa mto wa Pangani kumecheleweshа juhudi za kuanza mchakato wa kuanza Upembuzi Yakinifu kwa upande wa PANGA DECO ambapo hali yake ni mbaya na eneo hili la ufukweni mwa mji wa Pangani ni hatarishi kwa maisha ya wanadamu kwahiyo zinahitajika juhudi mahususi ili kukabiliana na athari hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi huu kwa upande wa Pangani Magharibi unategemea fedha za ndani ambazo bado hazijapelekwa hivyo kuchelewesha utekelezaji wake. Kamati inashauri Serikali ipeleke fedha za bajeti ya ndani asilimia **10** ya fedha zote za mradi ili utekelezaji usikwame kwani kutokamilika kwa mradi huo kuendelea kuhatarisha maisha ya wakazi wa eneo hilo kwani makazi ya watu yapo karibu sana na ufukwe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata fursa ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa eneo la *Ocean Road.* Hali ya utekelezaji wa Mradi inaendelea vizuri Mkandarasi amekwisha anza kazi baada ya kupata fedha

za wafadhili kutoka *Adaptation Fund*. Kamati inapongeza hatua ya Wizara ya kuamua kutafuta wafadhiri na kuutekeleza mradi huu kwa haraka. Kwani utekelezaji wa mradi huu utasaidia kukabiliana na kupungua athari za mabadiliko ya tabia ya nchi yanayosababisha ongezeko la kina cha Bahari yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilishauri kuwa Serikali itoe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya uhifadhi wa Mazingira kwa kutenga fedha za kutosha lakini pia fedha hizo zitolewe kwa wakati. Kwa Mfano Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2017 ilikuwa haijapokea kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo jambo linalokwamisha utekelezaji wa Miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa pamoja na nia yake nzuri ya kusimamia uhifadhi wa Mazingra nchini, iangalie namna ya kuongeza bajeti ya Mazingira. Jambo hili litawezesha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa wakati kwani **usipoziba ufa utajenga ukuta**.

### 2.2.2 Kutembelea shughuli za Viwanda (kiwanda cha Saruji cha Tanga)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea shughuli za Viwanda kwa lengo la kujionea mafanikio na changamoto yao katika uendeshaji wa Sekta ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea katika kiwanda cha Saruji Tanga (Tanga Cement PLC) na kuelezwa baadhi ya changamoto zinazowakabili na hizi ni changamoto kubwa kwa Tanga Cement na Viwanda Vingine vya Cement:-

- **Kutokuwepo kwa nishati ya Umeme ya uhakika na yakutosha.**

**Meshimiwa Spika,** kukatika mara kwa mara kwa nishati hii muhimu kunawapunguzia uwezo wa kuzalisha lakini pia kunasababisha uharibifu wa malighafi na mitambo. Aidha,

aaeneo mengine umeme hauna nguvu ya kutosha *(low voltage)* hivyo kusababisha kusuasua kwa shughuli za Viwanda.

- **Kuzuia uingizaji wa Makaa ya Mawe kutoka nje ya nchi**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imezuia kuagiza makaa ya mawe kutoka nje ya nchi wakati yaliyopo hayatoshelezi mahitaji. Hatua hii imeongeza bei ya Makaa ya mawe ya yanayozalishwa hapa nchini. Kutokana na gharama ya upatikanaji wa makaa ya mawe ya ndani ya nchi imepelekea makaa ya mawe kuchangia asilimia **70** ya gharama zote za kuzalishaji wa Saruji hivyo kuongeza sana gharama za uzalishaji. Aidha, miundombinu ya kusafirisha malighafi hiyo ni duni sana na inasababisha gharama kubwa.

## 2.3 SEMINA NA MAFUNZO KWA WAJUMBE WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wa Kamati walihudhuria Semina kwa lengo la kuwajengea uwezo. Semina hizo ni pamoja na:-

### 2.3.1 Semina ya Uchambuzi wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Semina hii iliendeshwa na Mradi wa ***Legislative Support Program*** uliopo chini ya Ofisi ya Bunge. Katika Semina hizo Wajumbe walijifunza namna ya kuchambuzi Bajeri za Wizara, pia walipewa muongozo wa Uchambuzi wa Miswada na muongozo wa Ushirikishwaji wa Wadau katika kazi za Kamati.
**4.6**

### 2.3.2 Semina kuhusu utunzaji wa Mazingira

Semina hii iliendeshea na Shirika la ***Heifer International*** ambapo wajumbe walipata fursa ya kuufahamu mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi unaotekelezwa na shirika hili. Mradi huu ni Mradi shirikishi unaolenga kuboresha hali ya maisha ya wananchi vijijini kwa kupitia mikakati endelevu ya kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unaitwa Igunza Eco Village na unatekelezwa katika kata tatu za wilaya ya Igunga-Mkoani Tabora. Katika Mradi huu kuna miradi midogo mbalimbali inayotekelezwa ili kuifanya jamii iache kufanya shughuli zinazochochea uharibifu wa mazingira. Miradi hiyo ni kama utengenezaji wa majiko bunifu ambayo yanatumia kuni kidogo hivyo kupunguza ukataji miti kwa ajili ya kuni, miradi ya ufugaji wa kuku ba ng'ombe wa maziwa, ujenzi wa miundombinu ya Biogas, mradi wa upandaji miti na ufugaji samaki. Miradi hii licha tu ya kuongeza kipato kwa wananchi pia inatunza mazingira.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa muda mrefu sana Kamati tangu ilipoundwa mwaka 2015 imekuwa ikiishauri Serikali kukutana na wadau wa Sekta Binafsi ili kujadiliana na kushauriana namna ya kukuza Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kulifanyiakazi jambo hili na kuanza utaratibu wa kukutana na wadau mara nne kwa mwaka na kusikiliza changamoto zao, kuzifanyia kazi na baadae kuleta mrejesho kwa wadau kwa zilezilizofanyiawa kazi. Hii ni jambo nzuri hongera kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaendelea kuipongeza Serikali kwa kukubali kuondoa Kodi ya VAT kwenye huduma ya mizigo inayopitia Bandari ya Dar es Salaam. Hii imeongeza sana ufanisi wa utoaji mizigo Bandarini na imeongeza shehena ya mizigo inayopita Bandari ya Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira katika kusimamia Sheria za utunzaji wa Mazingira ya Viwandani na Migodini. Aidha, Kamati inashuri Baraza la Taifa na Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kulinda na kuhifadhi Mazingira. KINGA NI BORA KULIKO TIBA.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizi kamati inaendelea kuishauri Serikali kuyashughulikia ipasavyo masuala yafuatayo:-

**i) Kusimamia na Kufufua Viwanda vilivyobinafsishwa**

**KWAKUWA,** ni jukumu Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kufutilia na kuhakikisha Viwanda vilivyobinafishwa vinafanya kazi na kuleta ajira na mapato na huduma za bidhaa na kuchukua hatua kwa vile ambavyo bado havizalishi na vingine vimebadili matumizi.

**HIVYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wahusika wanatekeleza Mikataba ya ununuzi na Serikali kuchukua hatua kwa watakaobainika kukiuuka.

**ii) Wingi wa mamlaka za Udhibiti**

**KWAKUWA,** Mamlaka za udhibiti ni muhimu katika kuhakikisha bidhaa inayoingia sokoni inakidhi viwango stahiki,

**NA KWAKUWA** zipo Mamlaka nyingi za udhibiti ambazo ushirikiano wake ni hafifu,

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuendeleza kasi katika kutekeleza mpango wa kuziunganisha mamlaka zinazofanya kazi zinazoingiliana. Mfano TBS, TFDA, FCC, FIRE, OSHA, TRA na nyingine nyingi.

**iii) Malimbikizo ya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT refund)**

**KWA KUWA**, wawekezaji walio wengi wanalalamikia ucheleweshaji wa TRA katika kurejesha kodi ya Ongezeko la Thamani (*VATrefund)*

**NA KWA KUWA**, kutorejeshwa kwa kodi VAT mapema kunawapunguzia Mitaji na uwezo wa kujiendesha,

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kufanya marejesho ya kodi hiyo kwa wakati.

**iv) Upungufu wa Bajeti katika Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira**

**KWA KUWA** bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira haitoshelezi katika kapambana na kasi ya uharibifu wa Mazingira nchini,

**NA KWA KUWA** Mfuko wa Mazingira ndiyo kimbilio katika kutekeleza jukumu hilo lakini unakabiliwa nachangamoto ya ufinyu wa bajeti,

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuwa tozo mbalimbali zinazohusu Mazingira ziingizwe kwenye Mfuko wa Mazingira angalau kwa asilimlia chache ili kuuwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**v) Agizo la Serikali kupiga marufuku matumizi ya Mifuko ya Plastiki**

**KWA KUWA** mifuko ya plastiki ina mchango mkubwa kwenye suala la uharibifu wa mazingira nchini,

**NA KWA KUWA**, Kamati iliagiza Serikali kuchukua hatua za makusudi ili kufikia muafaka wa jambo hili na wamiliki wa viwanda vya plastiki,

**HIVYO BASI**, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali itekeleze agizo la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastic kutoka nje ya nchi na baadae viwanda vya ndani ili kuondoa kabisa matumizi ya mifuko ya plastic (TOTAL BAN). Kamati inashauri Serikali kulifanyia kazi suala la upatikanaji wa viwanda vya mifuko mbadala kwa haraka.

**vi) Upungufu wa Nishati ya Umeme**

**KWA KUWA** Nishati ya umeme ni muhumu katika ujenzi wa Uchumi wa Viwanda,

**NA KWA KUWA** Tanzania bado ina upungufu wa Nishati hii muhumu kwa ajili ya maendeleo,

**HIVYO BASI**, kamati ianpongeza mipango na juhudi mbalimbali inayoendelea hivi sasa sambamba na hilo

inaisisitiza Serikali kuharakisha utekelezaji wa mipango hiyo ya kuongeza Niashati ya umeme nchini ukiwemo mradi mkubwa wa Stiegler's Gorge na miradi mingine ya gesi.

**vii) Serikali kutokuwa na Mipango Madhubuti ya kuendeleza Miradi ya Mazingira inayotekelezwa na Wafadhili**

**KWA KUWA,** Miradi mingi ya maendeleo hususani ya mazingira kwa sehemu kubwa inatekelezwa na Wafadhili,

**NA KWA KUWA**, Serikali haina mipango madhubuti ya kuiendeleza mara baada ya muda wa utekelezaji wa miradi hiyo unapomalizika.

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kabla ya miradi hii kuisha imejenga uwezo wa ndani wa kuiendeleza.

**viii) Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB)**

**KWA KUWA** Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ndio benki muhimu inayotegemewa na sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika kutoa mikopo,

**NA KWA KUWA** benki hii ni muhimu kwa mustakabali wa Tanzania ya Viwanda,

**HIVYO BASI** Kamati inaishauri Serikali kuipatia TIB fedha ya mitaji ya kutosha ili watanzania wafaidike na azma ya Tanzania ya Viwanda kwa kuwapatia mitaji ambayo itawasidia kuanzisha na kukuza biashara zao na kujenga viwanda na kuongeza thamani ya mazao.

**ix) Kuanzishwa kwa utaratibu mpya wa ulipaji kodi wa electronic tax stamp**

**KWA KUWA,** TRA inakusudia kuanzisha utaratibu mpya ulipaji kodi wa *electronic tax stamp* kwa ajili ya kukusanya kodi viwandani vya vinywaji ambao Kamati inaona utaratibu huo unaweza kuwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wake.

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali iangalie upya mfumo huu kabla ya kuanza utekelekelezaji.

**x) Upatikanaji wa Vibali vya kutoa Sukari ya Viwandani Bandarini na nyongeza ya kodi ya asilimia 15**

**KWA KUWA**, wawekezaji wanalalamikia upatikanaji wa Vibali vya kutoa Sukari ya Viwandani Bandarini na urejeshwaji wa nyongeza ya kodi ya asilimia 15 kwa Sukari hiyo.

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali iandae utaratibu rafiki wa uingizaji na utoaji wa Sukari ya Viwandani Bandarini na kurejesha kwa wakati asilimia 15 ya kodi ya kuingiza Sukari ya viwandani. Aidha, kamati inawashauri wafanya biashara wawe waaminifu kwa Serikali katika kutoa taarifa za uzalishaji na kodi. Taarifa ambazo zitasaidia katika kufanya uhakiki na kupata vibali vya Sukari ya Viwandani kwa wakati.

**xi) Utekelezaji wa Mradi wa Kurasini Logistic Centre**

**KWA KUWA,** Mradi wa Kurasini Logistic Centre ni moja ya miradi ya kielelezo na unatarajiwa kuchochea ukuwaji wa Viwanda,

**NA KWA KUWA,** utekelezaji wa mradi huu umechukua muda mrefu sana takribani miaka saba (7),

**HIVYO BASI** Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kuutekeleza mradi huu ambao utaleta tija kwa watanzania ikiwemo kuwapatia ajira, unafuu wa bidhaa na Serikali kupata kodi mbalimbali.

**xii) Utekelezaji wa Mradi wa kufufua kiwanda cha matairi cha General Tyre**

**KWA KUWA,** Serikali bado haina mpango madhubuti wa kutekeleza Mradi wa kufufua kiwanda cha General Tyre ambacho kingeweza kutoa ajira na kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumia katika kuagiza matairi ya magari.

**HIVYO BASI,** Kamati inaendelea kusisitiza Serikali iweke mazingira rafiki ili wawekezaji waje kushirikiana na Serikali kufufua kiwanda hicho. Mahitaji ya matairi katika nchi yetu ni makubwa sana hivo kukosekana kwa kiwanda hiki Serikali inapoteza mapato mengi kwa kuagiza matairi yote kutoka nje ya nchi.

**xiii) Usimamizi wa Sheria ya Mazingira**
**KWA KUWA,** wawekezaji wengi hawazingatii sheria ya mazingira na hivyo kuwa hatarishi kwa Mazingira na binadamu,

**NA KWA KUWA** wanaofanya hivyo wanatumia vibaya dhana ya Tanzania ya Viwanda.

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu sheria zilizopo katika kudhibiti uharibifu wa Mazingira unaofanywa na wenye viwanda nchini, kwani suala la uhifadhi wa Mazingira halina mjadala. Aidha, kamati inawashauri wenye viwanda na migodi kufuata na kutii Sheria za Mazingira ambazo zikizingatiwa tutatunza mazingira na kulinda afya za Watanzania.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa **Mheshimiwa John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza azma ya Tanzania ya Viwanda. Kamati inaunga mkono juhudi zake na itaendelea kutoa ushirikiano ili azma hiyo itimie. Aidha, Kamati inawashauri watendaji wengine wa Serikali kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais katika kutekeleza azma ya Tanzania ya Viwanda na kuondoa urasimu usio wa lazima katika taasisi mbalimbali zinazosimamia Viwanda, Biashara na Uuwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na

kuwapongeza kwa ushirikiano walioutoa katika kuandaa Taarifa hii mpaka kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| i. | Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb | **Mwenyekiti** |
| ii. | Mhe. Vicky P. Kamata, Mb | Mjumbe |
| iii. | Mhe. Salim H. Turky, Mb | Mjumbe |
| iv. | Mhe. Kalanga J. Laizer, Mb | Mjumbe |
| v. | Mhe. Dkt Dalaly P. Kafumu, Mb | Mjumbe |
| vi. | Mhe. Khatib S. Ally, Mb | Mjumbe |
| vii. | Mhe. Tauhida C. Gallos, Mb | Mjumbe |
| viii. | Mhe. Munira M. Khatibu, Mb | Mjumbe |
| ix. | Mhe. Anthony C. Komu, Mb | Mjumbe |
| x. | Mhe. Godbless J. Lema, Mb | Mjumbe |
| xi. | Mhe. Lameck O. Airo, Mb | Mjumbe |
| xii. | Mhe. Hawa S. Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| xiii. | Mhe. Balozi Dkt Diodorus B. Kamala, Mb | Mjumbe |
| xiv. | Mhe. Jesca D. Kishoa, Mb | Mjumbe |
| xv. | Mhe. Mbarouk S. Ali, Mb | Mjumbe |
| xvi. | Mhe. Mussa R. Sima, Mb | Mjumbe |
| xvii. | Mhe. Anatropia L. Theonest, Mb | Mjumbe |
| xviii. | Mhe. Faida M. Bakar, Mb | Mjumbe |
| xix. | Mhe Ibrahim H. Raza, Mb | Mjumbe |
| xx. | Mhe. Abdulaziz M. Abood, Mb | Mjumbe |
| xxi. | Mhe. Raphael M. Chegeni, Mb | Mjumbe |
| xxii. | Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb | Mjumbe |
| xxiii. | Mhe. Gimbi D. Massaba, Mb | Mjumbe |
| xxiv. | Mhe. Martha M. Mlata, Mb | Mjumbe |
| xxv. | Mhe. Joyce J. Mukya, Mb | Mjumbe |
| xxvi. | Mhe. Eng. Ramo Makani, Mb | Mjumbe |
| xxvii. | Mhe. Getrude Rwakatare, Mb | Mjumbe |
| xxviii. | Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote wa Wizara zilizochini ya usimamizi wa Kamati, pamoja na Makatibu Wakuu, Watendaji wote wa Wizara na Taasisi chini ya Wizara husika kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote walipohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano akitoa kwa Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kiukamilifu. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba pamoja na wasaidizi wa Kamati Ndg. Pauline Mavunde na Ndg. Mwimbe John, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Kutoa Hoja kwamba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA**

2 Februari, 2018

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mchana huu tufikie tamati ya shughuli zetu. Nilisahau kumtangaza mgeni wa Naibu Waziri Mheshimiwa Ikupa Alex ambaye ni mdogo wake kutoka Pangani, lazima atakuwa ametoka lakini ni afadhali nitamke kwamba alikuwepo hapa anaitwa Neema Alex karibu sana, umeona Dada yako akifanya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sote ni wasimamizi wa kanuni hizi tukienda kwa dakika 15 kuchangia watapata nafasi watu sita tu, tumeongeza na muda na hii ni kwa sababu kwenye maswali ya nyongeza tumechukua muda, niliruhusu yale ya pamba, korosho kwa sababu ndiyo yanayogusa wananchi wetu, ndiyo siasa.

Ombi langu kwenu ni kwamba ili tupate wachangiaji zaidi ya hao Sita tufanye kama tulivyokuwa tunafanya huko nyuma niwahoji mkubali, badala ya dakika 15 kila mmoja apewe dakika saba, tukienda hivyo na ukatumia muda wako vizuri ninyi ni watu mmesoma vizuri tu, ukijielekeza kwenye hoja utafika na utaeleweka sana.

Kwa hiyo, dakika saba hizo zitatupatia Wabunge 13, 10 ni *less than that*, mmetuletea hapa majina ya kutoka kwenye kambi zenu tumefanya mahesabu hapa nisingelisimama kusema mimi na *manage* muda hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nawahoji kuhusu kutumia dakika saba badala ya 15 kuchangia.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, ili tujiandae vizuri watakaoanza mchana watakuwa ni Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala ajiandae, tutaanza na hao wawili halafu sasa tutashuka vizuri tu. Niwashukuru sana kwa kazi mliyofanya, ninawashukuru Wenyeviti kwa taarifa zenu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Tunaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Kamala.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati. Nakushukuru kwa kunichagua na mimi kuwa mmoja wapo wa kuchangia siku ya leo. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na nitoe pole za dhati kwa Watanzania wenzangu na wananchi wa Mkoa wa Lindi hasa katika Wilaya ya Kilwa kwa kifo cha Mzee wetu Kingunge Ngombale Mwiru, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niangalie Tanzania kwa ubora wake na jinsi Mwenyezi Mungu alivyoipendelea. Ameipendelea Tanzania kwa kuturuzuku vitu mbalimbali ikiwemo mito mikubwa unaikuta Tanzania. Tanzania ni nchi ya kumi na moja kuwa na vyanzo vikubwa vya maji ikiwemo Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, mito mikubwa tumeipata Tanzania lakini Mwenyezi Mungu akatujaalia tukapata bahari Tanzania, hivyo hata tukisema mizigo inateremshwa Tanzania, nchi za wenzetu wanashindwa kupata vitu kama rasilimali ambazo tumepata Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumeruzukiwa mbuga kubwa za wanyamapori na urithi wa dunia tumeupata Tanzania ikiwemo Kilimanjaro, Serengeti, Selous *Game Reserves* na nyinginezo. Mwenyezi Mungu bado akaendelea kutusaidia sisi kutupa madini ya kutosha. Sasa hivi Tanzania nzima kila mkoa unaokwenda kuna madini. Kuna madini ambayo hata nchi zingine hawana kama *Tanzanite,* lakini tunajiuliza bado Tanzania wananchi ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajiuliza tumekwama wapi mpaka Watanzania tumekuwa maskini namna hii?

Suala hili tujiulize Watanzania wote kwa uchungu wa nchi yetu kujiuliza kwa pamoja sio kumwacha mtu mmoja anakimbia peke yake, huku nyuma watu wamemwachia anachokifanya peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuziona *resources* kama hizo ambazo Tanzania zinachezewa chezewa nataka niongee katika zao ambalo liko katika Mkoa wangu wa Mtwara na Lindi. Hili ni zao la korosho. Zao la korosho sasa hivi limezagaa Tanzania nzima, lakini cha kushangaza baadhi ya wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na baadhi ya mikoa wanayolima korosho kufaidika katika kipindi cha miaka miwili na nusu kutoka korosho Sh.600 mpaka kufikia Sh.4,000. Kinachoshangaza sasa hivi kumetokea *sabotage* kubwa sana katika hili zao za korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuachia nyani shamba utavuna mabua na usipoziba ufa, utajenga ukuta. Tunajua kabisa haya ni mambo yanafanyika na Serikali inasema ina mkono mpana, huu mkono mpana uko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho kama korosho Tanzania haionekani pamoja na kwamba sisi ndio tunaolima korosho. Inaonekana ya kwanza Vietnam; ya pili, India; ya tatu Nigeria; Ghana, Brazil, lakini Tanzania hatupo. Wafanyabiashara wakubwa wa korosho wanakuja kununua korosho Tanzania. Ametokea Vietnam kuja kununua korosho Tanzania amekutana na mazingira magumu sana ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza wali-*hold* makontena yote akajikuta ana korosho imekaa katika *warehouses* hawezi kuziondoa, hivyo anaanza kufanya biashara yake kwa hasara, mpo Watanzania? Sasa hivi tumeyaona, mimi nilirusha *clip* kwa Wabunge kuwaonesha jinsi korosho za Lindi zimetiwa mawe, kokoto, mchanga zimezunguka tayari ziko Vietnam korosho zetu ambazo zimewekwa mchanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema mna mkono mpana, mkono mpana uko wapi hapo? Kama ni hivyo, hata mimi nina mkono mpana, kama kwa mkono wenyewe namna hii kujikuta mazao yetu yanapelekwa India, yanapelekwa Vietnam yakiwa na kokoto ni aibu kwa Taifa na uchumi huu utadorora kwa vile kuna kundi la watu hawataki kuona Watanzania wanafanikiwa, hawataki waone katika Tanzania hii wananchi wa Tandahimba, Naliendele, Mchinga ambao sasa hivi walikuwa wanaweza kupata milioni 50, hawataki, wanataka kuturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu isilitazame suala hili kwa kawaida, ilitazame suala hili kwa mapana yake. Wewe ni shahidi, tupo humu ndani kwa muda mrefu, tulikuwa na viwanda vya korosho, viko wapi? Humu ndani tunasikia maneno, tutafufua, tutafufua! Viko wapi? Bado wamevishika, wamevifunga, hawajavifufua, viwanda hivyo wananchi hawana ajira na wao wanafanya kazi zao kwa sababu hawaoni thamani na viwanda vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda 13 viko wapi? Masasi kulikuwa na viwanda, Newala kulikuwa na viwanda, Lindi kulikuwa na viwanda, Dar es Salaam kulikuwa na viwanda mpaka leo havijafufuliwa, viko wapi viwanda? Halafu mnasema mtakuja mtuletee viwanda tena, vile mlivifanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wanatafuta ajira, kwa vile korosho mnapeleka India, ajira inakwenda India! Sisi hatuonekani kama *producer* wa korosho, Watanzania tuko katika aibu kubwa. Kahawa ya Tanzania inauzwa Uganda, sisi wenyewe tuko wapi? Mazao ya Tanzania yanauzwa Kenya, ina maana Kenya *they are strong enough* kusimamia mazao yao na maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *natural resources* tulizokuwa nazo Tanzania tumepitwa na nchi zote tunazoziona, Kenya, Uganda, mpaka Rwanda imetupita,

Tanzania ya mwisho. Tujiulize tumerogwa na nani? Mtanijibu mtasema tena wewe, basi tumejiroga sisi wenyewe kwa kuwakumbatia watu ambao wana-*sabotage* uchumi wetu lakini tunawaangalia kwa sababu ya maslahi binafsi na *corruption. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PIC. MSD* wamekuja katika meza yetu na baadhi ya Taasisi nyingine, *MSD* wamebuni tenda ya ku-*supply* dawa nchi 15, sheria zilizokuwa mbovu za Tanzania, *feasibility study* tu inatakiwa ifanyike kwa muda wa mwaka mmoja, *strategic plan one year, action plan one year... (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ahsante kwa maoni yako. Mheshimiwa Balozi Kamala.

**MHE. BALOZI DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuchangia mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukiri kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Pamoja na kuwa Mjumbe wa Kamati, hainiondolei haki ya kutoa maoni yangu pale ambapo kuna jambo naliamini, nalielewa vizuri na kuna jambo ambalo nilishawahi kulisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba asilimia 10 kwenye mafuta ya michikichi, ile ambayo wanaita *crude palm oil* kutoka nje iondolewe. Kama unavyokumbuka jambo hili tulishalifanyia kazi kwa muda mrefu, tunalielewa, kwamba ukitaka kuendeleza viwanda vidogo vidogo vinavyosindika mafuta, kwa mfano vya alizeti na vinginevyo lazima udhibiti haya mafuta yanayotoka nje yanayoitwa *crude* wakati si *crude.* Nisingependa kuingia kwenye mjadala huo, Wizara ya fedha wanaelewa na walishafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa maoni yangu nafikiri asilimia 10 iendelee kuwepo ili kuweza kusaidia viwanda vidogo vidogo vinavyosindika alizeti na vinginevyo. Nilisimamia hili nikiwa Naibu wako, unakumbuka, jambo hili nililisimamia nikiwa Waziri, nilisimamia pia nikiwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki na naendelea kuamini hivyo nikiwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa vyovyote vile sitakuwa sehemu ya maoni tofauti na hayo ingawa huwezi ukazuia watu wengine kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme suala la kongano la ngozi kule Zuzu...

*(Hapa kulitokea hitilafu ya umeme)*

**MWENYEKITI:** Hebu subiri kidogo Mheshimiwa Balozi. Jamani kuna shoti huko juu. Wataalam! Imeungua pale juu. Imeungua tu, hakuna kitu cha kuhatarisha hapo. Tuendelee.

**MHE. BALOZI. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye hilo. Kama nilivyosema, nadhani licha ya hiyo changamoto, hoja yangu ibaki pale pale na *Hansard* wachukue kama nilivyosema kwa sababu siku zijazo watu watasoma hiyo *Hansard* na naomba msimamo wangu ubaki vile vile kwa sababu ndivyo ninavyoamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ukienda mbele ya Kamati ukaeleza changamoto zako tutazipokea changamoto hizo, lakini kupokea changamoto zako si kwamba tumepokea ziwe zetu, changamoto zako zitaendelea kuwa changamoto zako hadi pale tutakapoona uamuzi wa maana unaotakiwa kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Zuzu, kongano la ngozi la Zuzu ni jambo jema, limeelezwa vizuri na Wizara inafanya kazi nzuri, Wizara yetu ya Biashara na Viwanda na kwenye taarifa yetu tumeshauri ni jambo jema. Hata hivyo

napenda nishauri, kama wenzetu wa Ethiopia walivyofanya; Ethiopia walivyofanya ili kusaidia Sekta ya Ngozi, wao walitoa *temporary Government guarantee,* ni *temporary.* Maana changamoto kubwa hata pale Zuzu tukiwatengea eneo tukasema sasa wanaotaka kuwekeza kwenye ngozi waje wawekeze hatimaye hawa wawekezaji wadogo wadogo tatizo kubwa ni mtaji. Mtaji wa kununua mitambo na mashine na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Ethiopia walivyofanya wao wana ngozi kama tulivyo na ngozi sisi huku, wanatoa *temporary guarantee;* kwa maana ya kwamba kama wewe ni mfanyabiashara wa ngozi unataka kuwekeza kwenye viwanda vidogo vinavyozalisha bidhaa za ngozi basi Serikali inaku-*guarantee* unapata hizo mashine, unajenga jengo zuri, unaweka mitambo yako, ukimaliza kuweka hivyo basi ile *guarantee* ya Serikali inaondolewa kwa sababu unakuwa sasa unaweza kusimama kwa miguu yako sasa Seriakli inasema tembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia wamefanya hivyo na sisi kuna sababu ya kujifunza kutoka Ethiopia, tukifanya hivyo, nina uhakika hii Zuzu, tunasema kongano la ngozi la Zuzu litakuwa la manufaa lakini tusipofanya hivyo tutakuwa na kongano la ngozi la Zuzu na litaendelea kuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kidogo kwenye Wizara ya Mazingira. Tulienda kule Kihansi, kule kuna Maprofesa wazuri kutoka *SUA.* Walitufundisha mambo mengi, wanafanya kazi nzuri kuhusu masuala ya mazingira, ni wataalam wa kuhakikisha vyura wa Kihansi wanaendelea kuwepo. Hata hivyo mtaalam kutoka Wizara ya Mazingira moja alilotuambia kwamba wale vyura wa Kihansi wanapoendelea kuwepo; hoja sio vyura kuwepo, hoja ni kwamba wanapokuwepo wanasema mazingira mnayatunza vizuri. Wakipotea maana yake wanakwambia sasa mmeanza kuharibu mazingira. Kwa hiyo tusije tukaangalia

vyura wa Kihansi kama vyura bali tuangalie wale vyura kama kielelezo kinachotueleza tunafanya kazi gani kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Profesa mmoja pale alituambia akisema ukiwa msafi sana unaishia kuugua sana. Sasa sitaki kuingia huko lakini na hilo somo tumejifunza pia kwamba ukiwa msafi sana basi wewe unaugua sana kuliko wasiokuwa wasafi. Kwa hiyo alitoa *theory* yake pale, wale maprofesa ni wazuri kwa *theory* lakini alituzindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa tuliyoiona pale wale watalam Maprofesa kutoka *SUA* wanatumia fedha za wafadhili na fedha za wafadhili zinafikia mwisho wakati wowote. Sasa inabidi tuangalie tunasaidiaje tafiti kama hizo ziweze kuendelea. Kama fedha ya wafadhili zikimalizika na zile tafiti zikafungwa basi tutakuwa hatuyatendei haki mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Mazingira inabidi tuiangalie katika siku zijazo kuhakikisha tunaitengea fedha za kutosha kwa sababu mazingira yanapoleta changamoto kila mtu analalamika. Sasa tusiwe wazuri wa kulalamika tu bila kuchukua hatua; na hatua ya kwanza ni kuhakikisha tunatenga fedha za kutosha ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hii dhana ya Tanzania ya viwanda. Nimesoma na sote tumesoma hapa, ule mpango wa miaka mitano na zile taarifa mbalimbali kutoka Wizara ya Biashara na Viwanda. Tunaposema Tanzania ya Viwanda hatumaanishi na sidhani kama kuna mtu alishafikiria kumaanisha hivyo; hatumaanishi kwamba sasa Serikali itaanza kujenga viwanda, hapana! Tunaposema Tanzania ya viwanda ni kwamba tungependa kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji katika viwanda, watu waje wawekeze katika viwanda, Watanzania wawekeze katika viwanda, hatumaanishi sasa kwamba Serikali itaanza kujenga viwanda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Balozi kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Gibson na Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati ya Bajeti, *PIC* pamoja na Kamati ya Viwanda na Biashara kwa jinsi ambavyo wameweza kutoa hoja zao lakini pia wameweza kulishauri Bunge na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya *PIC* ambayo inazungumzia masuala ya uwekezaji wa mitaji ya umma. Katika Taifa la Tanzania ni kwamba Serikali iliweza kuanzisha mashirika zaidi ya 269 kwa lengo kubwa kwamba mashirika haya yaweze kufanya kazi zake vizuri na hatimaye yaweze kuweka mchango mkubwa kwa ajili ya pato la Taifa katika Taifa hili la Tanzania. Hata hivyo kwa uhalisia, baada ya kuwa tumepitia mashirika haya tumeona changamoto zipo; na ndiyo maana mashirika mengi na taasisi za umma zimeshindwa kufikia yale malengo ambayo yamekusudiwa wakati yalipoundwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati ya *PIC* ambayo imezungumzia kwamba Taasisi nyingi zimeshindwa kujiendesha kutokana na kuwepo na madeni makubwa ambapo Serikali inapata huduma kutoka katika Taasisi hizi, lakini Serikali inachelewa kulipa madeni hayo na hatimaye taasisi inashindwa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika suala hilo tulivyokuwa tukichambua tuliona kabisa kwamba kuna baadhi ya mashirika mengi tu ikiwemo taasisi ya *MSD* ambayo inafanya shughuli kwa ajili ya kupeleka dawa sehemu mbalimbali katika nchi ya Tanzania. *MSD* inaidai Serikali zaidi ya bilioni mia moja kumi na nne; kwa hiyo kutokana na deni

hilo kubwa taasisi hii inashindwa kujiendesha kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo naishauri Serikali sasa iweke mkakati madhubuti, iangalie taasisi zote ambazo inadaiwa ihakikishe kwamba inalipa madeni yote ambayo inadaiwa na taasisi hizi muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika madeni haya tumeona kwamba si taasisi tu ambazo zinadaiwa, tumeona pia hata halmashauri nyingi kuna wakandarasi ambao wametoa huduma mbalimbali na hatimaye Serikali imeshindwa kuwalipa kwa wakati, matokeo yake taasisi nyingi au mashirika mbalimbali yameshindwa kufanya shughuli zao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo sasa naendelea tu kuiomba Serikali, kama ambavyo Mheshimiwa Rais anasisitiza kwamba unapopata huduma ni vizuri ukalipia kwa wakati. Kwa mfano katika suala la umeme yeye mwenyewe amesema kama mtu umetumia umeme ukishindwa kulipa basi watu wa *TANESCO* wakate umeme. Kwa hiyo, nasisitiza sasa kwamba Serikali iangalie uwezekano mzuri wa kuangalia madeni yote na kuweka mkakati maalum wa kuweza kuyalipa madeni hayo ili taasisi hizi ziweze kuendelea vizuri kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika sheria za manunuzi tuliona pia kuna changamoto kubwa kwamba taasisi nyingi zinashindwa kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi kutokana na kwamba Sheria ya Manunuzi inakwamisha baadhi ya juhudi na shughuli mbalimbali katika kujiendeleza na kuweza kufikia ufanisi ambao taasisi inakuwa imekusudiwa. Kwa hiyo niombe Serikali sasa iangalie sheria hizi, hasa hii Sheria ya Manunuzi katika vipengele ambavyo vinakwamisha ifanye marekebisho ili taasisi hizi ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo katika taasisi nyingi tuliona kwamba hazimtambui Msajili wa Hazina,

wakati Msajili wa Hazina ndiye ambaye anasimamia taasisi hizi. Kwa hiyo tuombe Serikali iboreshe zaidi ili taasisi hizi ziweze kumtambua Msajili wa Hazina, kwa sababu ndiye anayesimamia uwekezaji wa kila siku katika taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Msajili wa Hazina aimarishwe zaidi kama alivyo *CAG,* tunaona *CAG* anafanya kazi kubwa kwa sababu ana wafanyakazi wengi na ana bajeti kubwa. Kwa hiyo niombe Serikali ili tuweze kuona mashirika haya zaidi ya 269 yanafanya kazi kwa ufanisi, ni vizuri Serikali ikaangalia uwezekano wa kumwezesha sasa hivi Msajili wa Hazina ili aweze kufanya kazi zake vizuri kwa kuzisimamia taasisi vizuri na hatimaye ziwe na mchango mkubwa kwenye pato la Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika masuala mazima ya uwekezaji. Tumeona pia kwamba Serikali inapeleka mtaji kidogo sana kwa baadhi ya taasisi ambazo ni muhimu kama benki. Kwa mfano kuna Benki ya *TIB*; ambapo benki hii ni muhimu sana kwa ajili ya kuwezesha masuala ya kilimo; na tunakoelekea kwenye suala la viwanda hatuwezi kufikia kama benki hii haitawezwa inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali iangalie namna ya kuwezesha taasisi hii, hasa Benki ya *TIB* kwa kuwa ni benki ambayo inashughulika na kutoa mikopo pia kwa ajili ya wakulima; na tunajua zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo na hasa waishio vijijini. Serikali ikitoa mtaji huu itaiwezesha *TIB* kuweza kujitanua zaidi hata kwenye mikoa kwa sababu sasa hivi ilivyo iko kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwa mfano kanda yetu ya ziwa Benki hii ya *TIB* iko Mwanza Mjini. Sasa mkulima atoke Geita huko vijijini aende asafiri mpaka Mwanza mjini kwenda kutafuta huduma za fedha ili kujiimarisha naona kama ni changamoto kubwa. Kwa sababu hiyo sasa, ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mzuri taasisi hii *TIB,* tunaomba kwa kweli Serikali ingalie uwezekano

mzuri wa kuweza kuiwezesha zaidi ili iweze kufanya kazi zake vizuri kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya uwekezaji wa mitaji ya umma tumegundua kwamba taasisi nyingi za Serikali zinafanya kazi lakini zinafanya kazi vizuri hatimaye yale mapato ambayo inapata yanatumika yote au unakuta kwamba zaidi ya asilimia iliyowekwa kwamba kila taasisi inatakiwa itumie isizidi asilimia 60 lakini unakuta mashirika mengi yanatumia zaidi ya asilimia 60 mengine hata mpaka 90. Kwa hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nami nichukue fursa hii kuchangia katika Kamati hizi tatu muhimu sana. Moja naomba wakati ujao ikiwezekana kwa baadhi ya hizi Kamati zingepewa umuhimu siku zingeongezwa ili watu wengi zaidi waweze kuchangia. Ni muhimu kwa kuleta tija ili Serikali iweze kupata mafanikio makubwa sana na wapate mawazo ya Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja naomba niishauri Serikali; tumeanza vizuri sana, ndoto ya kuwa na nchi ya viwanda na inawezekana, lakini naomba kabisa Serikali itathmini upya, tuangalie mahali ambapo gharama za uzalishaji. Tusipoweza kuangalia gharama za uzalishaji kwa ajili ya tozo, kodi na ushuru mbalimbali ambao unatozwa na taasisi za udhibiti na taasisi mbalimbali ili mtu aweze

kuzalisha hatutaweza kufikia hayo malengo; kwa sababu hatimaye mfanyabiashara anachohitaji ni faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bidhaa nyingi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na hasa kwa mfano kwenye Afrika Mashariki au *SADC* ambazo zinaingia bila kodi, halafu huku ndani ya nchi unakuwa na utitiri wa kodi na tozo mbalimbali, ndoto hiyo hatutaifikia. Tuna hizi taasisi za udhibiti ziko nyingi sana lakini pia ushuru na kodi mbalimbali ambayo inafanya bidhaa zetu za Tanzania zisiweze kushindana kutokana na gharama kubwa ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mmoja tu *net* ambazo zinazalishwa hapa ni kiwanda kikubwa kuliko chochote cha Afrika *A to Z*. Pia mbolea tunayoizalisha ndani ya nchi unakuta kodi mbalimbali ambayo ile *import tax* wanatozwa hawaruhusiwi ku-*claim back* lakini neti ikitoka nje ya nchi au mbolea ikitoka nje ya nchi haina kodi. Sasa viwanda vyetu tunavilinda au ndio tunavimaliza? *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba Serikali iangalie suala hili kwa mapana zaidi na tuwe na *one stop center.* Kwamba mtu akija akitaka kukata leseni ya biashara yoyote akishakata hapo basi gharama na tozo zote kila kitu viwe hapo hapo ili baadaye pasiwe na kurudi nyuma, kwamba tunadaiwa, leo umekata leseni umeanza biashara, baada ya miaka mitatu anakuja mtu wa *OSHA,* anakuja *NEMC,* hizo zote zinakuwa ni kero. Natakiwa nikishalipia hapa; si kila mtu anajua sheria zote na kwenye sheria wansema kutokujua sheria sio kinga, lakini sio wananchi wote watajua hizo sheria, ni vizuri tuwe na *one stop center* kama *TIC* iwe ngazi ya mkoa, ngazi ya wilaya mtu akishalipa wagawane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la muhimu ni Serikali kuwa na e-*government* na malipo yote yaendelee kufanyika kwa kupitia hiyo hiyo *TRA* lakini wabadilishe mfumo. Kwa mfano kodi hii ambayo tumekubaliana ya majengo na kodi ya mabango hayo yote mtu akishalipia pale basi risiti ikitoka na halmashauri yangu iwe inajua kwamba mtu fulani amelipa kiasi fulani na mgao wa Serikali kuu ni kiasi fulani,

mgao wa halmashauri yangu ni kiasi fulani na mgao ambao unatakiwa kwenda mpaka ngazi ya chini ni kiasi gani. Kila mmoja akijua hiyo tutawezakufanikiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine kubwa ni kuwekeza kwenye utafiti. Sisi tunaimba tu pesa zote za utafiti asilimia kubwa zaidi ya asilimia 99.8 zinatoka nje ya nchi, za kwetu za ndani hakuna. Ilikuwa tumekubaliana 1% ya *total budget* imeshindikana, tumekuja thirty billion imeshindikana. Bila utafiti hatutaweza kusonga mbele, hivyo ni vizuri tuwekeze kwenye utafiti hasa kwenye sekta ya kilimo, madini kote huko hata kwenye biashara inataka tuwe na fedha za kutosha za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Tume ya Ushindani *(FCC)* pia iweze kufanya kazi yake vizuri iangalie mambo haya yote lakini mbali na hilo iharakishe lile suala la *CETAWICO* ambayo inazalisha mvinyo hapa Dodoma iweze kuchukuliwa na *breweries* ili wakulima wa zabibu hapa Dodoma waweze kunufaika na Watanzania tunywe mvinyo ambao unatoka Tanzania, si huu wa sasa hivi ambao asilimia kubwa unatoka South Africa na sawa na *juices* nyingi ambazo tunanunua *concentrates* kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie kwamba bidhaa zote ambazo tunaweza kuzalisha ndani ya nchi tuwe na muda maalum; kwamba ndani ya miaka miwili au mitatu tutakuwa tunazalisha hapa nchini ikiwa ni pamoja na hizo juice *concentrates,* mafuta ya kupikia, kwa sababu baada ya bili kubwa ya mafuta ya magari au mafuta ya dizeli ya pili inayofuata kwa gharama kubwa tunayoagiza ni mafuta ya kula ambayo ni *vegetable oil* tunayoagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sukari; na haya mambo yote tunaweza kuzalisha hapa nchini kwa gharama nzuri, wakulima wetu wakanufaika na pesa zote hizo zikabaki ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie suala la *budget cycle.* Ni muhimu sana sisi tuangalie kubalisha *budget*

*cycle* kama Bunge kwa sababu kipindi tunakaa Kamati ya Bajeti na Kamati zingine zote kupitia hizi bajeti hakuna mabadiliko tunayoweza kuleta zaidi ya asilimia moja au mbili. Tungekaa sisi kuanzia Agosti, Oktoba ili kama kuna *inputs* zote, mawazo yote yaingizwe ili halmashauri zetu na taasisi zote zinapokwenda kupanga bajeti zao basi wajue hii itapanda, itashuka au haitakuwepo; hiyo itatusaidia sisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba tuangalie kwenye sekta ambayo ni rasmi na ambayo isiyo rasmi *(formal and informal sector).* Hii *informal sector* yaani sekta isiyo rasmi inazidi kukua kutokana na haya masuala ya kodi, tozo na usumbufu mbalimbali. Ingekuwa tumeweka viwango maalum na mtu anajua akishakuja kulipa sehemu moja hatasumbuliwa tena kila mtu atapenda kuwa *formal.* Pia kila mtu atapenda kwamba mambo yake yaendelee vizuri, lakini yule ambaye hatakiwi kuwa na rekodi yeyote unakuta ana unafuu sana kuliko yule ambaye anaweka *record* ndiye anayekamuliwa mpaka dakika ya mwisho. Kwa hiyo naomba na hilo pia lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye masuala ya madini kuna mengi ambayo tumezungumza kwenye Kamati kama tulivyokuwa tunasema kwamba, ni vizuri kodi nyingi ambazo ziko ni vizuri tupate muda wa kutosha ili tuweze kutoa mawazo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine muhimu ni suala la kulinda ardhi yetu. Nina uhakika kwa kazi nzuri sana ambayo anafanya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ambaye ameondoa kero nyingi pia atatusaidia kuhakikisha ardhi za kilimo zinalindwa. Tukiwa hapa Makao Makuu yetu ya Dodoma, nina uhakika atalinda mashamba yote ya zabibu yasibadilishwe kuwa makazi na utakuwa mfano kama nchi zingine unakuwa na mashamba ndani ya mji, inakuwa ni *green belt.* Mheshimiwa Waziri najua hicho kitu anakiweza na nina uhakika kwamba hiyo kazi tutafanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kupanua wigo wa kodi, tusipopanua wigo wetu wa kodi hatuta...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni kwa mchango wako tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi ya Maftaha.

**MWENYEKITI:** Unasemaje?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi ya Maftah.

**MWENYEKITI:** Umetokea wapi?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayupo.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya Maftaha nami niweze kuchangia. Naomba nianze mchango wangu kwanza kwa kuzishukuru Kamati zote tatu kwa michango yao mikubwa na kuona haya waliyotuletea sisi yanatufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe angalizo letu moja tu kwamba sisi kama Watanzania ni watu wazuri sana wa kupanga mipango; na mimi ningependekeza tuunde taasisi ya kupanga mipango pengine tukiuza mipango yetu nchi za nje tukapata pesa za kigeni. Kwa sababu tumekuwa wapangaji wazuri sana lakini kwenye utekelezaji tuko *zero*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya tuliyaongelea wakati tunapanga bajeti hapa, kwamba hizi bajeti hazitoshi

kwa maana kwamba hazitakwenda kukidhi matakwa ya kile tunachokitarajia; na hiki ndicho ambacho Wenyeviti wa Kamati wametuletea. Kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati amesema kwamba *CAG* hana *resources* za kutosha, kwa maana kwamba hana pesa za kutosha kuyaendea majukumu yake na haya tuliyaongea tangu mwanzo kwamba hizi pesa ambazo *CAG* tunamtengea hawezi kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hata kwenye Kamati zetu za Bunge nazo tumeshindwa kuyaendea majukumu yetu, kukagua miradi iliyopelekewa pesa na Serikali kwa sababu ya tatizo la pesa. Ukienda kwenye halmashauri zetu nako huko watu wenyewe wanakaimu. Sasa ukiangalia bajeti ya Serikali asilimia 70 zinakwenda kwenye halmashauri. Hivi, Waheshimiwa Wabunge kama hawawezi kwenda kukagua miradi, *CAG* kama hawezi kwenda kukagua hesabu za Serikali, hivi tunatarajia weledi gani tulionao wa matumzi bora, matumizi sahihi ya hizi pesa tunazozipeleka kwenye halmashauri zetu.  Hili ni jambo linaloshangaza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie wenzetu mliopata uteuzi au madaraka ya kuisimamia nchi mtuone sisi nasi ni wazalendo. Hayo tunayoyasema tunasema kwa uzalendo kama ambavyo ninyi mnajiona; kwamba ninyi ni wazalendo zaidi kuliko sisi na ndiyo maana hata tunaposhauri mnatuona kwamba tunashauri kama vile tunawapuuza, lakini tunawashauri tukiwa na nia ile ile kwamba na sisi ni wazalendo na tunashauri kwa uzalendo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye viwanda. Hapa tunapigiwa kelele tu kila siku kwamba viwanda vinafufuliwa, lakini sisi watu wa kusini tunalalamika kwamba kulikuwa na viwanda vya korosho kila wilaya, lakini hakuna kinachofufuliwa hata kimoja na vyote leo hii tunaambiwa vilivyo vingi viko kwenye kesi, kwa hiyo haviwezi kufufuliwa viko kwenye kesi tunabaki kuwa maskini. Kama mama yangu alivyokuwa anasema, kwamba sisi tumebaki kama nchi kama vile haina mwenyewe, hili jambo hata sisi linatuumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye uwekezaji sekta ambayo kama kweli Serikali ya Awamu ya Tano kama imeamua kuwekeza kwa ajili ya kumkomboa Mtanzania basi sekta mojawapo ambayo ilikuwa ni muhimu ni sekta ya kilimo; lakini sekta ya kilimo imebaki kwenye makaratasi. Mheshimiwa Waziri wa kwanza wa Wizara hii alisema awamu ya tano tunaweka jembe la mkono litakuwa makumbusho, lakini mpaka leo hii tunafika huko katikati jembe la mkulima bado halijaenda makumbusho na sidhani kama litakwenda makumbusho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado hata wale wachache wanaojitokeza kuwekeza kwenye kilimo bado hatuwatendei haki. Mimi hainiingii akilini mtu umewekeza, umelima, umevuna mahindi, inatoka Serikali inasema hayo mahindi usiuze halafu *NFRA* hawanunui, huyu mkulima amewekeza, kwamba amechukua mikopo benki, anailipaje? Yaani tunategemea mkulima yeye ndiye awe *food security unit* ya Taifa, hii haingii akilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kama tulivyosema, kwa mfano kama sasa hivi korosho ndizo zinazofanya vizuri kwenye soko la kimataifa; lakini hizi korosho ni Mwenyezi Mungu tu katupendelea, Serikali haijawekeza mkakati wowote wa kuendeleza zao hili zaidi ya kwenda tu kutafutia soko hapa Vietnam basi, lakini, hakuna mkakati wowote ule ambao umesimamiwa kwamba Serikali imefanya mkakati huu, zao hili la korosho limefika hapa lilipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna matamko ya viongozi. Naomba hayo matamko ya viongozi lazima yaendane na uhalisia. Tulipokuja kwenye zao la korosho katikati ya msimu tumekuja kuambiwa *sulfur* itatolewa bure, magunia yatatolewa bure, lakini ukienda kwenye Bodi ya Korosho wanakwambia wao bajeti yao ilikuwa wamesha-*order* tayari *sulfur* ya tani elfu tisa, lakini mahitaji halisi ni tani elfu kumi na nane. Sasa tani hizo zingine elfu tisa zinapatikana wapi? Ndiyo maaana sasa hivi kwenye msimu tukahangaika mpaka sulfur ya 35, 000 tumenunua 75,000 lakini lile tamko lilikuja katikati ya mradi. Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hapa Mwenyekiti amesema Kodi ya Korosho mpaka leo hii ile asilimia 65 hawajapata lakini leo hii hawa hawa Bodi ya Korosho sasa hivi wanatakiwa waagize *sulfur*. Itakapofika mwezi wa Nne mwaka huu *sulfur* inatakiwa imfikie mkulima lakini mpaka leo Bodi hawajapata hela. Ndiyo maana nikasema hili zao la korosho nalo Mwenyezi Mungu tu kataka ndiyo hapo lilipofikia lakini mkakati wa Serikali sijauona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo, kama ambavyo waliotangulia kuchangia walivyosema mimi mwenyewe na-*declare interest* kwamba na mimi nina kiwanda kidogo cha usindikaji wa nafaka. Mkitaka kujua shida ya nchi hii wewe anzisha kiwanda chako. Atakuja *TFDA,* atakuja *OSHA,* atakuja *TBS,* atakuja bibi afya wa kata, atakuja *NEMC,* atakuja sijui wa mazingira gani hawa wote wanakuja wanakutafuna, wanakumaliza moja kwa moja, unatamani kwa nini nimeanzisha hiki kiwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi hizi taasisi zote basi ziingie kwenye mfumo mmoja, kwamba mtu unakwenda mahali pamoja unalipia hizo taasisi zote, lakini uzunguke leo niende *TFDA,* kesho niende *TBS,* kesho kutwa nakwenda *OSHA* yaani ni vurugu. Kwa kweli...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi. Tunaendelea na Mheshimiwa Frank Mwakajoka atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia taarifa za kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Msajili wa Hazina

aliyetumbuliwa Ndugu Lawrence Mafuru kwa kazi kubwa aliyokuwa akitushauri mpaka sasa hivi tumeona kuna mabadiliko makubwa sana. Toka kupata faida ya shilingi milioni 443 mpaka tulipata milioni 885.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi pia kupuuza mchango wa mzee wetu ambaye ni msajili wa sasa hivi, tunamshukuru pia. Nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana Wanasheria wetu wanafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba wanatushauri na tunafanya vizuri kuishauri taasisi pamoja na taasisi zinazokuja kwenye vikao vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze na madeni ya Serikali. Ukijaribu kuangalia kwenye taasisi mbalimbali ambazo tumeweza kuziita na kuzikagua tumekuta Serikali inadaiwa fedha nyingi sana. Baadhi ya mashirika mbalimbali yameweza kutoa huduma, lakini Serikali imeshindwa kulipa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiyataja mashirika mbalimbali ambayo yanaidai Serikali ukianza na Mamlaka ya Kuchimba Visima inaidai Serikali karibu bilioni 2.7; ukija Mamlaka ya Maji *DUWASA* Dodoma hapa inadai Serikali bilioni mbili; ukija SUMA JKT wanaidai Serikali bilioni 5.8; ukija *MSD* wanaidai Serikali bilioni 144.9; Haya yote ni madeni ambayo Serikali inadaiwa, lakini wananchi wa kawaida wanapokuwa wanadaiwa hata Sh.10,000 wanapigwa *penalty* na wanakatiwa huduma katika maeneo yao, lakini Serikali imekuwa ikidaiwa na haijali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni madeni ya muda mrefu, si madeni ya siku moja wala ya mwaka mmoja. Haya ni madeni ambayo mengine yana miaka mitano, mengine miaka mitatu, Serikali haitaki kabisa kuhakikisha kwamba, inalipa haya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni la kuanzisha mashirika haya tulitaka yatoe tija kwenye nchi hii, lakini pia, yaajiri watu wengi, lakini mashirika mbalimbali sasahivi yako katika hali mbaya na yanataka kufa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu na Shirika la Ndege *(ATCL).* Shirika hili la Ndege *ATCL* ndani ya miaka mitatu limeendeshwa kwa hasara kubwa kabisa. Shirika hili mwaka 2014/2015, liliendeshwa kwa hasara, lakini matumizi yake kila mwaka yanazidi kuongezeka. Mwaka 2014/2015, walitumia karibu 94,359,000,000/=; lakini mwaka 2015/2016, walitumia bilioni 109.2; na mwaka 2016/2017 wakatumia bilioni 13.7. Fedha hizi ambazo zinatumika tofauti na mapato ambayo yanapatikana ni hatari kabisa kwa mashirika mbalimbali na shirika hili linataka kufa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata maswali mengi sana kwamba, sasa hivi tunaona Serikali inajumua ndege nyingine, maana si kununua ni kujumua; inajumua ndege nyingine kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shirika hili linakuwa na ndege nyingi. Sasa nafikiria wamefanya utafiti gani wakati shirika linaendeshwa kwa hasara, halafu Serikali inakwenda kuwekeza fedha nyingi za Watanzania kwenda kununua ndege. Ni namna gani wamefanya utafiti ili shirika hili liweze kuleta tija kwenye nchi hii. Kwa hiyo, hali si nzuri. Shirika linaendeshwa kwa hasara na linaendelea kutumia fedha nyingi kupita kiasi ambacho kinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna shirika lingine, kuna *TANTRADE,* shirika hili pia limeendeshwa kwa hasara miaka mitatu mfululizo. Shirika hili mwaka 2013/2014, lilitumia fedha milioni 397. 9; lakini mwaka 2014/2015, lilitumia milioni 614.6; na mwaka 2015/2016, likatumia milioni 838.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi haya ambayo yanatofautiana na mapato linayopata shirika hili yamesababisha hasara kubwa kwenye shirika na mtaji wa uwekezaji kwenye shirika hili umeshuka kwa asilimia toka 32.7 hadi 16.5, ni hatari sana. Ni kwamba, mpaka sasa hivi usimamizi wa mashirika haya umeonekana kwamba Wakurugenzi pamoja na bodi ambazo zinachaguliwa zimeshindwa kusimamia mashirika haya na Serikali isipochukua hatua mashirika haya yanakwenda kufa na kupotea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo lingine, nataka kuzungumzia pia, kuhusiana na sheria mbalimbali ambazo zinaendesha mashirika yetu. Kwa mfano, Sheria ya Manunuzi; ukiangalia *MSD* sasa hivi Sheria ya Manunuzi inaathiri sana shirika hili. Sheria ya Manunuzi inafika mahali *MSD* ili waweze kupata dawa wanatumia miezi mitatu kutangaza zabuni, lakini pia inasababisha dawa zichelewe kufika nchini, zaidi ya miezi tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo la kuangalia sana kwamba. Hivyo, ni muhimu Serikali ikajaribu kuangalia Sheria hizi za Manunuzi zimekuwa ni tatizo katika mashirika haya na yanashindwa kuendelea na kufanya vizuri kwa sababu ya sheria kandamizi ambazo zipo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu shughuli mbalimbali ambazo zinafanyika kwenye mashirika haya. Ukijaribu kuangalia mashirika mbalimbali katika nchi hii hayana bodi. Ukiangalia Shirika la *MSD* Bodi yake sasa hivi imekwisha muda wake karibu mwaka mzima umepita, lakini mpaka sasa hivi hakuna jambo lolote ambalo linaendelea kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, bodi hizi zinateuliwa upya na kuhakikisha kwamba, zinafanya kazi kwa kusaidia mashirika haya ili yaweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwakajoka. Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Mbene.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kujadili hizi *report* zetu zote tatu, lakini zaidi nitajikita kwenye masuala ya uchumi, hususan kwenye Kamati yetu ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *report* kuandikwa na kuelezwa ndani ya Bunge; pamoja na majibu ya Serikali kwa kipindi cha huu mwaka uliopita 2017, kwamba

hali ya uchumi ni nzuri, lakini ukipitia kwenye *records* na taarifa mbalimbali ambazo zimekuwa zikitoka; kwa mfano, kwenye Taarifa ya *Easy of Doing Business* kwa maana ya wepesi wa kufanya biashara, kwenye viashiria 11 ambavyo vimetoka nchi yetu imeporomoka kwa viashiria saba, yaani kwamba, kila mwaka tumekuwa tukiporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye kiashiria kimoja tu, upitishaji shehena bandarini na usafirishaji wa bidhaa. Sasa hivi tuko nchi ya 182 kati ya nchi 190 na bandari ndiyo sehemu pekee katika nchi hii ambayo inatuongezea mapato mengi. Asilimia 40 ya mapato ya nchi hii yanapatikana bandarini, lakini hali ilivyo mpaka sasa hivi hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukienda pale bandarini makontena mengi yamezuiwa pale kwa sababu ya *contradictions* ambazo ziko pale. Watu wa *TBS* wanasema hawawezi kutoa vibali vya kuruhusu makontena yatoke mpaka wapate *certification* kutoka *TRA.* Watu wa *TRA* hawawezi kuwaruhusu watu kutoa makontena mpaka wapate *certification* kutoka *TBS,* unashindwa kujua *contradictions* za kimamlaka ya watu wawili wanaofanya kazi kwenye Serikali moja zinavyosababisha wananchi waweze kuumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mnajikuta kuna masuala ya *storage* mle ndani, ambayo ni *non statutory fee* ambayo mtu yeyote angeweza kuachiwa akafanya biashara, lakini leo imekuwa Serikali kama kuwakwamisha wafanyabiashara, ili walipe *storage fee,* ili kuongeza mapato ambayo yamekuwa yakiendelea. Kwa hiyo ni vizuri Serikali ikaja ikatueleza mikakati na namna ambavyo inaweza kukabiliana na hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, kutokana na muda najitahidi kukimbia kimbia. Jambo la pili, ukipitia Taarifa ya *IMF* na *World Bank* ambayo wameitoa mwisho wa mwaka, taarifa inatueleza kabisa kwamba, ukipitia Sera yetu ya Kifedha kwa maana ya *Monetary Policy* pamoja na *Fiscal*

*Policy,* hizi sera moja inamtafuna mwingine. Kwamba, benki unajikuta kama sasa hivi Benki Kuu inajitahidi kushusha riba, ili mabenki yapate fedha yaweze kukopesha wananchi, lakini ukweli wananchi wanashindwa kukopa pamoja na Benki Kuu kupunguza riba kule ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini; kwa sababu, ukija kwenye *Fiscal Policy* ndio Sera ambayo inakula. Yaani kodi ni nyingi kwa maana mtu anashindwa kukopa kwa sababu, anajua nikikopa nitashindwa kulipa, kwa hiyo, inabidi kuangalia hapa je, tunatengeneza uchumi wa namna gani katika hili Taifa na ukiangalia kama sasa hivi tangu Taarifa ya Benki ya Dunia imetolewa, sisi kama Taifa tumeshindwa kutoa maelezo ya kutosha ambayo yanaweza kulisaidia Taifa namna gani ambavyo tunaweza kukabiliana na hii hali ya ukwasi kupungua zaidi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuonesha uchumi kwamba umeendelea kuyumba; ukiangalia sasa hivi Serikali imefunga mabenki, inajitetea yale mabenki wigo wake ni mdogo, lakini ukweli ni kwamba, ukiangalia zile *community bank* 12, benki karibu nane zinatakiwa zifungwe kwa sababu na zenyewe bado zina-*run under profit,* kila mwaka zinapata *negative* ukiangalia kwenye *report* ambazo wao wenyewe wamezitoa. Kwa hiyo, napenda na jambo hilo vile vile Serikali iweze kukaa na kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukwasi kupungua; sasa hivi mzunguko wa fedha nchini umepungua kwa zaidi ya asilimia 45. Watu hawawezi kuagiza nje ya nchi na sisi wenyewe tumekuwa tukiiona hiyo hali, lakini bado Serikali imekuwa ikijinasibu kabisa kwamba, fedha zipo zinatosha, lakini hali ya uchumi wa nchi yetu bado umeendelea kuyumba kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zimeendelea kuonesha kwamba, ili sera na uchumi uwepo bado ufisadi ndani ya nchi yetu umeendelea kuwepo. Jana Mheshimiwa Heche alijaribu kuzungumzia kidogo tu kuhusu Mradi wa *Passport* Nchini. Mradi ule umekuwa *inflated* kwa *40 million*

*US Dollar.* Nina taarifa ambazo tumezipata, ni kwamba ule mradi thamani yake halisi ulikuwa ni dola milioni 16, sawasawa na paundi milioni 11, lakini umekuwa *inflated to dollar* karibu milioni 58, *forty million plus.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna taarifa hizi, kuna kampuni ambayo ilishakuwa imepewa *Memorandum of Understanding* ambayo walipewa vile vile mkataba ambao haukusainiwa mpaka dakika ya mwisho, lakini mwisho wa siku waliingia kampuni mpya ambayo inaitwa ya *HID.* Hii Kampuni ya *HID* ambayo ndiyo imefanya hii kazi haijawahi kufanya mradi wa *Passport* duniani mahali popote. Ni kampuni ambayo kazi yake ni moja tu, inatengeneza hizi *security doors,* yaani zile kazi ambazo za ku-*swap.* Sasa ndio kampuni ambayo imeingilia hiyo kazi na ndio imefanya. Imeingia ubia na watu ambao walikuwa *NIDA* katika kile kipindi ambacho kimepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ufisadi bado upo na uchumi umeendelea kuyumba, lakini watu wamekuwa wakifichaficha tu kwa namna fulani. Tuna *documents* zote kama ambavyo watu wakihitaji sisi tutazikabidhi. Kwa hiyo, tungependa vilevile tunapojadili Sera ya Uchumi na haya mambo lazima vilevile yaweze kujadiliwa, kama tunapinga ufisadi lazima hatua ichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naamini kabisa sisi humu ni Wanasiasa na tunaweza hata tukawa ni Mawaziri, tunaweza tukawa hatulijui hili, lakini taarifa za ndani tulizonazo ni juu ya hili jambo kuna ufisadi wa kutisha kwenye mradi wa *passport* za hapa nchini. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linahitaji lipatiwe ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni kuhusiana na *transfer pricing.* Nchi yetu pamoja na kwamba, tumekuwa tukipambana kuwakamata wananchi wa kawaida walipe kodi, lakini ukweli ni kwamba, makampuni makubwa yamekuwa yakikwepa kodi katika namna ambayo Serikali haiwezi kupambana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami hili nataka Wizara ya Fedha ijaribu kwenda kuangalia zile *regulations* (kanuni) zao kuhusiana na haya makampuni makubwa kwenye *issue* nzima ya *transfer of pricing.* Nilitoa mfano mmoja, wakati tunapitia kwenye moja ya Kamati, kwa mfano, kampuni ya *Petra Diamond,* ambayo inafanya kazi ya uchimbaji wa almasi, yenyewe…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Janeth Mbene. Atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. JANETH Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia. Naomba kwanza kuwapongeza sana Wenyeviti waliowasilisha ripoti za Kamati zao. Kwa kweli, nasikitika kuwa, muda hautatosha sana kwa sisi kuchangia kikamilifu, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja zinazotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kuwa nchi yetu ina rasilimali nyingi sana, lakini bado tuko maskini, kwamba mazao yetu yanauzwa nchi za jirani. Labda kwa ufupi tu niseme kuwa na rasilimali za kutosha peke yake si sababu ya kuwa tajiri, ila tunachotakiwa kufanya ni jinsi gani tunakuwa na taasisi zitakazoweza kugeuza kwa tija rasilimali hizi na kuzifanya kuwa mali, mapato na bidhaa zitakazoendesha uchumi wa nchi, lakini suala la mazao yetu kuuzwa Kenya, Rwanda, Burundi au Uganda vile vile sio tatizo; sisi *issue* kwetu ni kuwa tunapata mapato kutokana na biashara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa vyovyote vile itafika siku ambayo mazao, watu, bidhaa vitakuwa vinapita kama vile vinatoka hapa kwenda Morogoro. Kwa hiyo hilo lisiwe ni jambo la kuchukua muda mwingi kulizungumza,

tunachotaka kuona hapa ni kuwa mazao yetu au bidhaa zinazokwenda nchi nyingine yanasimamiwa vizuri, kwa maana ya bei nzuri na mapato yanayoingia katika Taifa letu, lakini vile vile na nchi yetu pia inaruhusiwa kuingiza mazao kutoka nchi nyingine za jirani kupitia kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala la magogo yanayotoka Congo na Zambia. Hakuna ubaya wowote magogo yale yakapitishwa Tanzania na sisi tukaya-*export* kama vile na sisi mali zetu zinavyokuwa *exported* na nchi jirani kwa sababu, mwisho wa yote ni biashara ya kimataifa. Kwa hiyo, nataka kuihamasisha Serikali, kama vile ambavyo sisi mazao yetu yanaenda kuuzwa nchi nyingine, basi na ya nchi nyingine yapitie kwetu, ili na sisi tuweze kuoata mapato yanayotokana na usafirishaji wa mazao hayo *and afterall* sisi ni *hub* kutokana na *location* yetu ya kijiografia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile kuzungumzia kwa kifupi sana suala la mashirika ya umma. Kwa kweli, mimi bado nina imani kubwa kuwa mashirika ya umma mengi ni mzigo kwa Taifa letu, kwa sababu, ni muda mrefu sana yanaendeshwa kwa hasara. Ingekuwa ni kampuni binafsi miaka mitatu, minne, mitano, inatosha kuonesha kuwa hili shirika halifai. Kwa hiyo, ninachotaka kusema aidha, tuweke menejimenti ambayo itayageuza haya mashirika yakaendeshwa kibiashara na kiushindani au tuyafunge kwa sababu, yanaendelea kutunyonya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuhakikihe kuwa watu tunaowaweka pale, wanawekwa pale kwa ushindani wa uwezo wao na sio wa kuteuliwa. Hili, jambo nafikiri limeshazungumzwa sana humu ndani; ukimweka mtu kwa kumteuwa inakuwa vigumu hata kumdhibiti, lakini ukimwajiri mtu kwa vigezo unampima kwa vigezo vyake vya *delivery,* akishindwa ku-*deliver* unamwondoa. Kwa hiyo, kwa kweli, nafikiri kwenye masuala ya Mashirika ya Umma hata tungelipa hayo madeni sidhani kama tutakuwa tumetatua tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la msingi ambalo nataka kulichangia leo, ni kuhusiana na kilimo. Bado kilimo ni fursa kubwa sana kwa Watanzania kujiondoa katika umaskini. Ningependa sana kuona Serikali sasa inakuja na mkakati badala ya kila siku kutuambia changamoto, tunazifahamu changamoto zote zilizoko kwenye sekta ya kilimo. Tunaomba sasa tupate mkakati wa Serikali, kwamba je, mnapanga kufanya nini, ili kilimo kiinuke? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuwa tayari kuna mikakati kwenye mazao. Mazao muhimu ya kibiashara au ambayo tunapeleka nje yana bodi zake na vilevile Serikali imejitahidi sana kuondoa tozo zile ambazo zilikuwa sumbufu. Hata hivyo bado tunataka kuona jinsi gani sasa bodi hizi zinafanya kazi ya kuhakikisha kuwa, wakulima wanawezeshwa kulima kwa tija na wanapata mapato stahili na mwisho wa yote uchumi unakuwa na asilimia kubwa zaidi ya pato letu la Taifa linachangiwa na kilimo ambacho kina watu zaidi ya asilimia 70 ambao wanakitumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tamko lake la hivi juzi, kuwa sasa hivi wakulima waweze kuuza mazao yao wao wenyewe bila kupitia madalali. Hata hivyo, hata kwa hivyo vyama vya ushirika vya mikoa au vya wilaya lazima watendaji wawe wenye weledi, wenye kujua kuendesha shughuli hizo kibiashara na wawe wazalendo. Kwa hiyo turudi kule kule, tuajiri watu ambao wana uwezo wa kuendesha vyama hivi vya ushirika la sivyo tutarudi, tutakuwa tuna-*recycle* watu tunaita majina haya tunarudi huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka kutoa pongezi sana kwa Mfuko wa Kahawa kwa jinsi ambavyo wamejitahidi kupunguza gharama za tozo. Hata hivyo bado tuna shida kubwa sana ya tozo nyingine ambazo zinatakiwa kuondolewa, ili ziwaguse wakulima moja kwa moja. Tozo nyingi zilizoondolewa kwa mtazamo wangu zinaenda kuwasaidia zaidi wasindikaji, lakini je, wasindikaji wa mazao mengine ni akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasindikaji kwenye mazao mengine ni haohao wakulima, kwa hiyo unakuwa hujamsaidia sana, lakini kuna tozo ambazo zinaenda kugusa uzalishaji moja kwa moja. Ningependa Serikali iziangalie na hizo iziondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukimbia haraka haraka kwa sababu ya muda. Kuna suala la korosho, zao la korosho limeonesha kabisa kuwa ni zao ambalo sasa hivi linafanya vizuri sana. Linafanya vizuri sana kwa sababu limewekewa mkazo na Serikali yenyewe, lakini vile vile na bodi yake. Nashangaa kusikia mtu hapa anasema eti zao la korosho halijasaidiwa chochote na Serikali, sijui huyu mwenzetu yeye yuko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho limewekewa mikakati mizuri, linasimamiwa vizuri na sasa hivi linaenda vizuri. Pamoja na hayo kuna suala la kuhakikisha kuwa wazalishaji wapya wa korosho wanawezeshwa, wazalishaji wapya wa korosho wanapewa pembejeo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbene kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Hussein Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa. Kwanza nitume nafasi hii kuwapa pole familia ya Mzee Kingunge na watu wote ambao kwa njia moja au nyingine wameguswa na msiba huu na nikipe pole Chama cha Mapinduzi na niwape pole kwa dhati kabisa Watanzania ambao wanaufahamu mchango wa mzee huyu katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema jambo moja, umefika wakati kama nchi hasa Wizara yetu ya Fedha kukubali kubadili Sera zake za Kibajeti. Kwa nini nasema

hivyo? Nitatoa takwimu chache ambazo ukitazama takwimu hizi zinaonekana katika taarifa za *BOT* za kuanzia mwaka 2011 mpaka 2017, Desemba. Hata hivyo, taarifa hizi zina *complement* taarifa iliyotolewa na *IMF* Januari, taarifa hizi sina *complement* taarifa iliyotolewa na *Economic Intelligence Unit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *real GDP growth* yetu mwaka 2011 ilikuwa 7.9 sasa hivi tuna- *project* itakuwa *6.8.* Hata hivyo, mzunguko wa fedha umeshuka kutoka asilimia 22 ya mwaka 2011 mpaka asilimia 1.8 ya sasa hivi. Ukiangalia *Export* ya hasa mazao ya kilimo ambayo ndiyo yameajiri asilimia 70 ya Watanzania, ukichukua zao la kahawa lilikuwa mwaka 2011, *growth rate* yake ilikuwa ni asilimia 55 sasa hivi asilimia *negative* 5.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukichukua *cotton* mwaka 2012 ilikuwa kwa asilimia 26, kwa sasa hivi imekuwa kwa asilimia hasi 3.8; ukichukua *Sisal* ndiyo imekuwa na ongezeko la asilimia 2.9 ya mwaka 2011, sasa hivi linakuwa kwa wastani wa asilimia 4.0; ukichukua zao la tumbaku ambalo mwaka 2011 lilikuwa kwa asilimia 56, sasa hivi mwaka 2017 kwa taarifa za *BOT* limekuwa kwa *negative* 62.7; na zao la korosho ambalo limekuwa kwa asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niangalie *manufacturing, export* ya *manufacturing* na hii ni *business export* naiongelea. *Manufacturing* ukichukua mwaka 2011 *ili-grow kwa* asilimia *96 growth rate.* Sasa hivi *ime-growth kwa negative* asilimia 244. Tuangalie *credits* kwenye *major economic activities; Trade, ilikuwa mwaka 2011* kwa asilimia *34* sasa hivi imekuwa kwa asilimia *16. Agro* mwaka *2011* ilikuwa *51.7* sasa hivi imekuwa kwa *negative 0.3. Transport* ilikuwa imeshuka mpaka asilimia *22.1. Building* yenyewe mwaka 2011 ilikuwa kwa asilimia 44 sasa hivi inakuwa kwa asilimia kwa wastani wa asilimia 5.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imports* za *Capital Goods* zimeshuka kwa asilimia 15. Tafsiri yake ni ndogo tu. *Our fiscal policies* hazichochei ukuaji wa biashara na uchumi katika

nchi. Nataka niwapeni mfano, takwimu zinaonesha Watanzania tunakuwa kwa wastani inasemekana asilimia mbili *point something* lakini ukuaji wetu wa kilimo ni 0.4 *growth,* hakuna *matching*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni jambo ambalo hata inawezekana tukasema humu ndani ya Bunge lisifurahishe upande wa Serikali kauli zetu, lakini *we have a duty to tell the truth*. Pia ni muhimu kabisa Wizara ya Fedha ikakubali kwamba Sera za Kibajeti za Wizara ya Fedha si rafiki katika ku-*accelerate* uchumi wetu kukuwa katika nchi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *non-performing loans*, sasa hivi zimefikia asilimia 12 na hii ni taarifa ya *BOT,* lakini taarifa ya *BOT* iliyoletwa na *Treasurer Registry* kwenye Kamati ya *PIC* inaonesha kwamba mapato ya *BOT* yanayotokana na *Trading* yameshuka kwa asilimia 63. *It is not a rocket science,* narudia, *this is just a fundamental principal* kwamba *our* Sera za kibajeti haziwezi ku-*accelerate* uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ushauri wangu, jambo la kwanza ambalo namshauri Waziri wa Fedha anapoleta Mpango wake wa mwaka 2018/2019 aje na *chapter* inayozungumzia *Tax Reforms* ili tukubaliane humu ndani *what is our direction*. *Number two,* ni lazima ije *chapter* inayoelezea ni namna gani *Agro Sector* tunawekeza iweze ku-*link* na *industrialization.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia na tunapiga makofi jitihada zilizofanywa Serikali kwenye zao la korosho. Leo Mkoa wa Dodoma ni *potential* kwa ajili ya korosho. Leo Mkoa wa Tabora ni *potential* kwa ajili ya korosho. Swali la kujiuliza, nini mpango wa Serikali kwa ajili ya *value addition* kwenye mazao ya korosho. Tutajikuta tumezalisha korosho nchi mzima halafu tunategemea soko la nje la kwenda kuuza *raw* korosho. Tujiulize, Mwijage atengeneze *clear structure* ya kuonesha namna gani tunatoa *incentive packages* kwa viwanda vinavyobangua korosho nje vije ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ardhi, tuna *raw material* na naamini tuna *cheap labour, what is our problem? It's our physical measures this is our biggest problem*. Nataka nijiulize swali kwa nini tuna-*charge* 30 *percent corporate tax* kwa mtu atakayewekeza kiwanda cha mazao ya kilimo? *Why?* Kwa nini tunaitaka *thirty percent?* Kwa nini tusimwambie *corporate tax zero?* Kwa sababu utapata *in Direct Tax* kutoka kwenye *Pay as You Earn, VAT* na *Excise Duty* ambazo watu wata-*spend. Why we don't see this. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha alituambia kwenye Kamati ya Bajeti na wewe ulikuwepo, alisema hivi wakati anamsindikiza Mtendaji Mkuu nadhani wa *World Bank or IMF*. Alimwambia nchi yenu ina bahati kubwa mbili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MJUMBE FULANI:** Mwongezee,

**MWENYEKITI:** Malizia

**MHE. HUSSEIN M.BASHE:** Moja ya bahati tuliyo nayo ni rasilimali za kutosha tulizo nazo katika nchi. Hizi rasilimali tusiposi -*turn* fursa hazina maana yoyote. Kwa hiyo ushauri wangu ni lazima *mentality* ya Serikalini iondoke kuwaza kodi, ianze kuwaza uzalishaji. Tusipofanya... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Livingistone Lusinde ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimefurahi sana nilipoona Wabunge wa CCM wakilia kwamba halmashauri zao hazina fedha. Nimesema hivyo kwa sababu, miezi sita iliyopita wakati tunapitisha bajeti ni Wabunge hao hao ambao walikuwa wanasema bajeti hii ya 2017/2018 ni bajeti ambayo haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani tulisema wazi kabisa kwamba kwa kitendo cha Serikali kupitia Wizara ya Fedha kunyang'anya vyanzo vya mapato vya halmashauri zetu, vikusanywe na *TRA* kutoka kwenye halmashauri zetu ni mwanzo wa kuvunja miguu halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana mmetoa muda mchache; kwa sababu ukiangalia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati anaonesha kama vile fedha za kawaida zilizopelekwa kwenye halmashauri zina-*range* kwenye asilimia 90; lakini ukipitia hili kabarasha ukiangalia fedha za kawaida, *including* mishahara yake. Fedha za kawaida ambazo...

**MWENYEKITI**: Fedha za kawaida ni nini?

**MHE. HALIMA J. MDEE ...** OC, haya matumizi ya Kawaida.

**MWENYEKITI:** Matumizi ya Kawaida.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Yes* sawa sawa hivyo hivyo tu Matumizi ya kawaida kwenye fedha ambazo zinaonekana ama zimezidi asilimia 100, ama zimezidi asilimia 150, utakuta ni kwenda kulipa madeni ya wazabuni ya watumishi, ukiwaambia tenganisheni zijulikane za utendaji wa kawaida wa halmashauri na madeni ni zipi, hawasemi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hiki kitabu, bajeti ya kilimo tunatakiwa tupelekwe bilioni 150 lakini zimepelekwa bilioni 11 nusu ya mwaka. Viwanda tunatakiwa tupeleke bilioni 74 zimepelekwa bilioni saba asilimia tisa. Ndiyo maana mnatupatia dakika saba, tutazungumza nini.(*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya majengo ni mbaya sana pale ambapo Mheshimiwa Waziri unavunja sheria ya bajeti kwa makusudi na nimeleta mabadiliko. Kwa nini nasema hivi; kwanza ufanisi mmeshindwa kukusanya kodi mnatudanganya kwamba mmefanikiwa. Nitakupa mfano

wa halmashauri yetu; 2016/2017, Kinondoni tulikusanya bilioni 10 tukiwa na Ubungo. Bilioni 10 *a hundred Percent* tulikuwa tunapanga kuongeza, mkapata tamaa mkachukua. Mwaka 2016/2017, mmechukua mmeleta bilioni hii, moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunaweza kukusanya 10 asilimia 100 mnaleta bilioni moja, hivi huo ni ufanisi? Mwaka 2017/2018, tulikuwa baada ya halmashauri kugawanywa Ubungo ikaenda 2.5, Kinondoni 7.5, tulikuwa tunauwezo wa kukusanya asilimia 100. Wamechukua; sasa hivi miezi sita imepita hata shilingi haijaja. Ninyi mnajua hivi ndivyo vyanzo vyetu vya mapato kisheria, tuliwapa nyie mtukusanyie siyo mchukue mwondoke nazo.

Mheshimiwa nyie mnajua, wamechukua kodi ya mabango. Tulikuwa tuna uwezo wa kukusanya 4.5, a *hundred percent billion* kwa mwaka uliopita tulikusanya bilioni 3.5 tukaweza kukusanya kwa asilimia 100. Tukasema mwaka huu makadirio yetu tukiongeza tutakuwa na uwezo wa kukusanya mmechukua hamrudishi. Kwa manispaa yangu ninavyozungunza Kinondoni, Iringa, Arusha, Morogoro, hiyo ndiyo mifano. Halafu mnakuja hapa mnasema ufanisi Kinondoni tunashindwa kufanya chochote. Tuna *deficit of twelve billion. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Bajeti iko hapa, tulifanya mabadiliko kifungu cha 65 kazi kununua Madiwani tu. Kifungu cha 65 kinasema hivi tulifanya marekebisho mwaka 2016/2017, tukasema, Waziri wa Fedha atashirikiana na Waziri wa TAMISEMI ili wagawane. Wizara inakusanya vipi kupitia *TRA* halmashauri inakusanya vyanzo vipi vya *Property*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 mkabadilisha mkamtoa Waziri wetu wa TAMISEMI mkajiweka wenyewe mkasema 65(2) kwamba hizi *Property Tax* zitakazokuwa *collected* zitakuwa *deposited* kwenye *Consolidated Fund.* Pili *65(2)(a)* inasema mgawanyo na msambazo wa zitakazokunywa zinatakiwa zipelekwe halmashauri kutokana na bajeti, ndiyo sheria inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajua hawa. Mchakato wa Bajeti huwa unaanzia ngazi ya halmashauri inapitishwa Hazina, inakuja Bungeni. Hizi bajeti za halmashauri tulishazipitisha tokea mwaka jana, inakuwaje leo Mpango eti watatoa kutokana na sisi tutakavyowaambia mahitaji yetu ni nini. Huo siyo utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili tutamtaka Mpango. Tunaomba na Bunge lako Tukufu tuweze kuungana pamoja kwenye azimio ambalo litasema mmeomba mtukusanyie kwa niaba kwa sababu ya ufanisi japokuwa ufanisi hakuna tumekubali; na kwa kuwa tukiwaambia mturudishie tunajua kwa wingi wenu mtakataa lakini tunasema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kidogo nimalizie kidogo

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MWENYEKITI:** Kile ambacho kimekusanywa na nyie Bunge hili lielekeze mrudishe kwa sababu mchakato wa bajeti ulishamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. SIXTUS R.MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi ili nichangie jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niseme kwa masikitiko makubwa kwamba natoa pole kwa familia ya Mzee wetu Kingunge Ngombale Mwiru, ambaye ndiye

alikuwa Mwalimu wetu sisi vijana wa siasa na amewahi kuwa Katibu Mkuu wa *TANU Youth League* na mwasisi wa Umoja wa Vijana wa CCM; kwa namna ya pekee sana natoa pole zangu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya hizi pole naomba nijielekeze sasa kwenye kuchangia kwenye hotuba zilizowasilishwa leo hapa Bungeni. Umuhimu wa mashirika na taasisi za umma kwa nchi yetu ni mkubwa sana. Mashirika mengi yalianzishwa kwa lengo moja, kwa kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la pili ni kutoa gawio kwa Serikalil; huo ndiyo ulikuwa moyo wa *sprit behind* ya kuanzisha haya mashirika. Kwa bahati mbaya ufanisi wa mashirika hayo yote hauwezi ukapimika kwa faida wanazotoa au hauwezi ukapimika vizuri na ukaonekana kwa aina ya huduma wanazozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hoja hiyo niiombe Serikali iyatazame haya mashirika na kuyasaidia kulingana na aina ya huduma au matokeo ambayo Serikali inatarajia. Huwezi ukalipima shirika linalotoa huduma kwa jamii kwa vigezo vya faida lakini huwezi ukalipima shirika ambalo unatarajia linaendeshwa kibiashara *one hundred percent* kwa vigezo vya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujumla wake *performance indicators* ni kipimo muhimu kwa kupima ufanisi wake. Nimelitizama kwa kina sana shirika la *ATCL* niombe Serikali iitizame *ATCL* katika jicho la tatu. Ukilitizama kwa kiasi gani linaleta faida na kiasi gani liko *efficient* unaweza usipate jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali sasa ingalie na kuisaidia *ATCL* kwenye kipimo kingine ambacho kinaitwa *spillover effects indicator* au *positive externalities indicator* au *a third party effect indicator.* Hiyo ikoje; unaweza ukawa na shirika kwa *nature* yake jinsi ilivyo mpaka Yesu anarudi ukipiga

pale ulichokiweka naulichokipata ndani ya lile lile shirika moja kwa moja usione faida, lakini likawa na faida nyingi sana zisizoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *ATCL* serikali msitegemee faida mtapata mwaka huu, mwakani au mwaka wa kesho kutwa, linaweza likanyumba katika nchi zozote itakazoelezeka lakini *ATCL* ina faida kubwa sana, kwanza ndiyo *brand* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *ATCL* inasaidia sekta nyingine zikimbie, zikue na zilete faida kwa Taifa. Wanakwambia *principal* ya faida ya duniani kote inatokana na *speed* ya mtu anavyo-*move* kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara yeyote duniani asingependa kukaa masaa mengi barabarani, kwa jinsi anavyofika kwenye huduma kwa urahisi ndivyo faida inavyopatikana kwa hiyo niiombe Serikali iitizame *ATCL* na wala isiache kununua ndege kwa sababu tulishaona kwenye mashirika mengine kama *Ethiopian Airline* wamenyumba hawakupata faida, lakini hawakuacha kununua ndege na wamenunua ndege. Emirates hawajawahi kupata faida hawajaacha kununua ndege na wameongeza ndege nyingine kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Air* Rwanda wameongeza Mabombadia *(Bombadier)* na mamboing *(Boeing)* haya yote wanayofanya KQ mwaka jana waliyumba kiasi kwamba watu wakafikiri shirika litafungwa hawajaacha kununua ndege na wameongeza kununua ndege; kwa nini hawa wanafanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya hivyo kwa sababu wanajua faida inayotokana na shirika hili siyo ya moja kwa moja ni ya huduma kwa upande mmoja, watu wata-*move* lakini kwa upande mwingine itasababisha sekta nyingine zikue hiyo ndicho wanachosema *a third part effect indicator* tunapaswa tuitazame katika lengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Serikali imewekeza jumla ya shilingi trilioni 47.7 kwenye mashirika yote mpaka ilipofika Juni, 2017 lakini faida iliyopatikana kwenye *investment* ya shilingi bilioni 47.7 ilikuwa ni shilingi bilioni 8.2 tu ambayo ni sawasawa na asilimia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haya mashirika yangewekezwa vizuri na yakatengenezewa mazingira angalau yalete asilimia kumi tu ya *investment* ambayo tuliiweka, maana yake tungepata shilingi trilioni 4.7 kwa mwaka jana, sawasawa na asilimia kumi ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini haya yanatokea hivyo? Haya ni masuala ambayo Serikali/Wizara ya Fedha lazima myafikirie kwa kina. Vilevile Msajili wa Hazina aangalie kuna mashirika ya hovyo, ni mzigo kwa Serikali, hata ukiyapima kwa huduma, huduma yake haitapimika na hata ukiya-*grade* ukayalea kama unavyoilea *ATCL* yatatutia hasara mpaka Yesu anarudi na faida inayotokana kwa *third party* hutaweza kuipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina, ndani ya Kamati tumetoa mapendekezo kwenye mashirika ya hovyo, ambayo yana mikataba ya hovyo, ambayo yana watendaji ambao hawana weledi, unakuwa na *CEO*, Wenyeviti wa Bodi na *Board of Directors* hawana *idea* hata moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kupata nafasi hii ya kuchangia hoja za Wenyeviti wa Kamati walizoziwasilisha mbele yetu. Nami nitoe pole kwa familia ya Ndugu Kingunge Ngombale-Mwiru, Mwanasiasa Mkongwe wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati mwingine Bunge zinapokuja hoja za msingi kama hizi tatu kwa pamoja zinaletwa na Kamati halafu sisi wenyewe Wabunge tunajinyima tena nafasi ya kuzichangia, kidogo hapo Bunge tunakuwa ni kama vile hatujitendei haki. Ukiangalia hoja hizi ni za Kamati zetu na wachangiaji ni sisi Wabunge, kuna sababu gani ya kujipa dakika saba wakati uamuzi ni wa Bunge lenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, nataka kwa haraka haraka nichambue baadhi ya mambo machache, nikijikita zaidi kwenye hoja ya Kamati ya Viwanda na Biashara. Kuna tofauti kubwa kati ya kujenga uchumi wa viwanda na kujenga viwanda vyenyewe. Unapotaka kujenga uchumi wa viwanda hasa kwa sisi Wabunge wa Vijijini ni vyema viwanda hivyo vikawa na *chain*. Kama vinahusu kilimo vikajipanga katika mpango ambao utawafanya wakulima wanufaike moja kwa moja na uwepo wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unapokuwa na viwanda vya mazao ya mifugo, halafu kukawa na viwanda vya mbolea ambavyo vinagusa moja kwa moja wakulima, kutaifanya nchi yetu ipate kodi ya kutosha kwa wakulima na wakulima wenyewe wakajiletea maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana la mwingiliano wa Taasisi za Serikali. Kwa mfano, ukiangalia kazi zinazofanywa na *TFDA* na *TBS* unaona ni kazi ileile moja, mfanyabiashara anaweza kupata *certificate ya TFDA* lakini *TBS* wakamkatalia. Kwa hiyo, unaweza kuona jinsi vyombo Serikali vinavyokuwa kikwazo cha kuhakikisha wanapata kodi ya kutosha na kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Kamati ya Viwanda na Biashara iliwahi kutembelewa na watu wa konyagi, wakaleta aina 32 za viroba na zikaonekana ni hatari Serikali ikazipiga marufuku, lakini leo viroba vinarudi tena kwa mlango wa uani, watu wanavipaki kwenye chupa, havina

stika za ubora za *TBS,* hazina stika za *TRA* wanakwepa kodi lakini vinauzwa. Wale wafanyabiashara ambao wanafuata utaratibu wanatozwa kodi kubwa wanajikuta wenzao wanauza kwa bei ya chini wao wanauza kwa bei ya juu, hawapati wateja, matokeo yake Serikali inashindwa kukusanya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtu anayeuza kinywaji kikali kwenye chupa ya plastiki, haina nembo zozote za Serikali, nani atajua ubora wa kinywaji hicho? Matokeo yake bado tunaendelea kuwaangamiza vijana wetu kutokana na uwepo wa viroba kwa njia ya uani. Tunaomba leo Mheshimiwa Mwenyekiti utakapokuwa ukipitia tupate majibu ya kutosha kwenye jambo hili.

Mheshimiwa mwenyekiti, unajua Mungu akikupa kilema anakupa na mwendo wa kukitembelea, hawezi akakupa kilema akakunyima mwendo. Nataka niweke usahihi kidogo tu, ukitazama makusanyo ya kodi, walipokuwa wakikusanya Halmashauri, 2014/2015 walikusanya shilingi bilioni 18.9. Baada ya Serikali Kuu kuchukua na kuanza kukusanya wenyewe kupitia *TRA* kwa mara ya kwanza mwaka 2015/2016 walikusanya shilingi bilioni 28.2. Mwaka uliofuata, 2016/2017, Serikali walikusanya shilingi bilioni 34.9 maana yake kuna ongezeko hapo. Mwaka wa 2017/2018, kwa robo mwaka wamekusanya shilingi bilioni 16.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu mimi siyo kukusanya ila ni namna gani zinarudi kwenye Halmashauri ili ziweze kujitegemea. Ni kweli mmekusanya sana kuliko walipokuwa wanakusanya Halmashauri wenyewe lakini ni namna gani zinarudi ili ziweze kuleta maendeleo kwenye Halmashauri zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine kubwa linaloleta mgongano kati ya Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha. Kwenye Halmashauri kunakuwa na bajeti ndogo za Halmashauri, wanapitisha vyanzo vyao vya ndani, wanapitisha namna ya kukusanya, inapokuja kwenye bajeti

kuu, vile vyanzo vinafutwa halafu hakuna namna ya kuvifidia. Kwa hiyo, tunajikuta tunakuwa na bajeti za Halmashauri ambazo zimefelishwa na kutokuwepo na vikao vya mwanzoni kati ya Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha. Mkiweza kukutana mapema mkaondoa mkanganyiko huu, maana yake Halmashauri haziwezi kupanga bajeti ambazo huko mbele ya safari zitakuja kukataliwa na Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwe kuna vikao vya kutazama bajeti vya mapema, tunashindwa nini? Kwa sababu leo hata zile tozo za kero ambazo tulizifuta, bado hazirudishwi kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, Halmashauri zinashindwa kujiendesha, zinakosa mapato ya kutosha kuweza kuwaletea maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwaomba sana, Wizara ya Viwanda na Biashara hebu tuleteeni orodha kati ya vile viwanda 130 na kitu vilivyobinafsishwa vingapi vinafanya kazi na vinafanya kazi kwa ufanisi gani? Leteni hapa orodha ili Waheshimiwa Wabunge tujue kumbe tangu tumeanza kuongelea viwanda kuna viwanda kadhaa vimeanza kufanya kazi na viwanda kadhaa bado vipo kwenye maandalizi ya kuhakikisha vinaendelea kufanya kazi. Vinginevyo tutakuwa tunapiga kelele hapa ya viwanda, viwanda kumbe hakuna kiwanda hata kimoja ambacho kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya namna gani tunaweza kuzisaidia Halmashauri zetu. Halmashauri zinaweza kujiendesha zenyewe lakini pale ambapo vyanzo vyake vya makusanyo ya ndani vinaheshimiwa na Serikali Kuu. Tusiwe tunakuja tunafuta halafu baadaye tunazitaka zijiendeshe, hawataweza! Waheshimiwa Madiwani wamepitisha vizuri makusanyo yao ya ndani, wameyatungia sheria ndogo tunapokuja sisi kukataza huku juu maana yake tunawaweka katika mazingira magumu sana ya kuhakikisha wanapata mapato ya kuendelea kujiendesha wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, niombe sana Serikali na Wenyeviti wa Kamati watakapokuwa wanayapitia haya wayatilie maanani sana ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika taarifa ya mwaka ya Kamati hii. Pia napenda kuwapongeza wanakamati wote wa Kamati hii kwa kuandika na kuiwasilisha kwa ufasaha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia taarifa hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo: Kwanza, Kamati kupewa semina za mafunzo. Kama inavyofahamika kuwa Kamati hii ni mpya hivyo ni vema semina za mafunzo kwa wanakamati zikapewa kipaumbele. Nashauri Serikali ni vizuri Wajumbe wakawa wanapewa semina ya taasisi fulani ambayo wanataka kuichunguza kabla ya kuichunguza ili kupata weledi wa kinachofanyika katika taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; utendaji usioridhisha. Kwenye ripoti ya Kamati hii imeonesha kwa kiasi fulani utendaji usioridhisha kwa baadhi ya taasisi hii. Hii imesababishwa na mambo mengi ikiwemo dhamana/majukumu ya Serikali katika kuchangia taasisi hizi. Hivyo naomba Serikali ikaiangalie taarifa kwa makini na kujirekebisha ili mashirika hayo yaweze kujiendesha shughuli zake kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutolipa madeni kwa wakati katika Mashirika ya

Umma. Ukipitia Taarifa ya *CAG* kwa ujumla katika maeneo mengi *CAG* ameshindwa kutembelea baadhi ya maeneo kwa sababu ya ukosefu wa pesa katika Ofisi yake. Ninaomba Serikali ilipe madeni ili tupate taarifa za kimahesabu kutoka katika Ofisi ya Ukaguzi na Serikali ijikite kulipa madeni ili tuendeshe kazi za wananchi waliowalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipe madeni ya *DAWASCO,* Jeshi, *TANESCO* na maeneo mengine ambayo Serikali hii imeshindwa kuyalipa kwa wakati na kusababisha taasisi za Serikali kushindwa kujiendesha zenyewe na matokeo yake taasisi hizi zimekuwa zikijiendesha kwa hasara na mikopo pia. Ni kwa nini Serikali inashindwa kulipa madeni hayo kwa wakati na huku mwananchi wa kawaida, mfano anadaiwa na Idara ya Maji 5,000/= tu anakatiwa maji. Je, hamuoni kwamba, Serikali inashinwa kujisimamia yenyewe kupitia taasisi zake? Ni lini sasa Serikali itaanza kulipa madeni haya makubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya Sheria ya Manunuzi ya Umma. Katika mfumo wa manunuzi nimeangalia mambo makuu mawili ambayo kwa upana wake Serikali iangalie namna ya kuboresha au kurekebisha sheria. Sheria hizi za manunuzi zinasababisha mchakato wa manunuzi kununua mali za Serikali kuchukua muda mrefu, mchakato wa kutangaza tenda unakuwa mrefu sana, lengo ni kupata *(Supplier)* mwenye vigezo, lakini Serikali ione namna ya kuziangalia sheria hizi kimfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya muda; Miradi kusimama kwa sababu tu vifaa vimechelewa kutokana na manunuzi kuchukua muda mrefu. Changamoto ya gharama, masuala ya manunuzi yanasababisha pia, Serikali kununua bidhaa kwa gharama kubwa na kwa baadhi ya watumishi wasio waaminifu wamekuwa wakipata 10 *percent* na huku wakiibia Serikali kupitia mfumo huu wa manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara za Ukaguzi wa *CAG* na Bunge. Kwa ujumla malalamiko yaliyopo ni *CAG*

kushindwa kufanya ukaguzi katika baadhi ya maeneo nchini na Bunge kupitia Kamati zake pia, zimeshindwa kukagua miradi. Dhamira ya uwazi wa pesa ya umma iko wapi? Au Serikali inafanya maksudi kunyima ofisi ya *CAG* pesa?

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii ya uwekezaji wa mitaji ya umma *(PIC)* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa mitaji; Mashirika mengi na Taasisi za Umma hazina mitaji ya kutosha. Mfano Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB).* Benki hii ingekuwa na mtaji wa kutosha ingepelekwa katika Mikoa yote ya Tanzania na ingeweza kuwainua Watanzania walio wengi, maana wakulima wengine kuliko wafanyakazi na wafanyabiashara, lakini Serikali haijachukua jitihada ya kutosha kuisaidia benki hiyo kwa kuipa mtaji wa kuweza kuendesha benki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki ilianza na mtaji wa shilingi bilioni 60 ingawa mtaji ulioidhinishwa ni shilingi bilioni 800. Kiasi hicho ni pungufu kwa asilimia 92.5. Serikali inaishia kuahidi lakini haitekelezi. Naiomba Serikali kutimiza ahadi yake ya kupeleka pesa yote ambayo iliidhinishwa kwa ajili ya uendeshaji wa Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kutolipa madeni yake kwa wakati; Mashirika mengi yanashindwa kujiendesha na kukamilisha miradi yake kwa ufanisi kutokana na Serikali kukopa lakini inachelewa kulipa madeni hayo. Naishauri Serikali kulipa madeni yake kila inapokopa. Hii inasikitisha kuona Serikali ndiyo inayodidimiza uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikikopa fedha zake kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Matokeo yake imedhoofisha mifuko hiyo, mfano *PSPF.* Naiomba Serikali ijirekebishe namna nyingine Serikali itadidimiza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kupongeza Kamati ya Uwekezaji Mitaji kwa taarifa ambayo inaeleza hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia juu ya Shirika la Elimu Kibaha *(KEC)* ambalo lilianzishwa kwa ajili ya shamba darasa kwa ajili ya wananchi kujifunza maendeleo mahali pale. Ningependa kusema kuwa tunapoangalia Shirika la Elimu Kibaha tulishuhudia uendelezaji wa shirika hilo huko nyuma miaka ya themanini lilikuwa na viwanda vya kutotolesha vifaranga na ufugaji wa ng'ombe ambao sasa hivi haliko hivyo na limekufa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuangalia taasisi hii ambayo ilikuwa na shule, Chuo cha Maendeleo kilichokuwa kinafanya shamba darasa na kutoa vijana kwenda kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri Serikali kuharakisha uundaji wa Bodi ya Wakurugenzi wa *RAHCO,* kampuni hodhi ya rasiliamli za reli. Nimeona niseme hivi kwani ni wakati ambao sasa tunatengeneza Reli ya *Standard Gauge* na kampuni hii haina bodi ya rasilimali hiyo itakuwa shida. Niishauri Serikali iharakishe uundaji wa bodi hii ili iweze kusimamia rasilimali za reli kuweza kuleta ufanisi wa uendelezaji wa reli nchini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji upande wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, dakika mbili tu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa ufupi sana nataka nizungumzie juu ya korosho zetu, hakika ni zao bora mojawapo la kimkakati, ambalo Serikali imewekeza na linafanya vizuri sana katika kumkomboa mkulima pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi karibuni kulikuwa na *allegations* za mawe kuwepo katika magunia ya korosho kule Vietnam. Sisi kama Serikali hatujakaa kimya tumejipanga

na kama Serikali pia tumeunda timu na tumewapa wiki mbili na tutapata majibu na wote watakaobainika tutawachukulia hatua kali na za kisheria na tuweze kujua adui yetu ni wa ndani ama ni wa nje. Kwa sababu hili ni suala la uhujumu uchumi, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba kama Serikali tunahakikisha kabisa kwamba zao la korosho ambalo ni zao mojawapo bora tunafika kiwango cha juu na tutakuwa katika ramani ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo. Naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba tunaandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo *(ASDP II)* na Waheshimiwa wote tutawaalika kwenye uzinduzi wa Mpango Mkakati huo wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, dakika saba.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hoja ambazo zimewekwa mezani. Kwanza kabisa nami nianze kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mzee wetu, Mzee Kingunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe hongera sana kwa Wenyeviti wote watatu kwa kuwasilisha vizuri kabisa hoja za Kamati zao mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika suala hili na moja kubwa ambalo nataka kuanza nalo ni hiki ambacho kinaelezwa kama mkanganyiko wakati hakuna mkanganyiko wowote ambacho ni kuhusu Kodi ya Majengo. Naomba niiseme vizuri na ikiwezekana nitumie dakika zangu zote saba na Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize kwa umakini na kwa pamoja tunapofanya maamuzi tufanye

maamuzi tukiwa tunaelewa nini tunafanya ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa vizuri mwaka 2016/2017, Serikali ilikuja hapa Bungeni na Sheria ya Fedha ya mwaka huo na tukaleta ndani ya sheria kodi hii ikusanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania lengo likiwa ni ufanisi. Tulipoleta tulifungua na akaunti maalum kwa ajili ya kuweka pesa hizi za Kodi ya Majengo katika Benki Kuu ya Tanzania. Tulifungua akaunti hiyo tukiwa na dhamira ya dhati ya kukusanya na kuzirejesha kule zilivyo na ndicho tulichokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na historia ambayo sio njema, imesemwa hata jana wakati Kamati ya *LAAC* na *PAC* walipowasilisha taarifa zao humu ndani kuhusu matumizi yasiyo mazuri kwenye Halmashauri zetu. Pesa za miradi zinazopelekwa hutumika ndivyo sivyo. Kama Serikali na Wizara ambayo tumepewa mamlaka ya kusimamia mambo ya fedha hatuwezi kuacha haya yanaendelea kutendeka ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kKwa umakini mkubwa wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anayechukia ufisadi, anayechukia ubadhirifu wa fedha za umma, ikaja ndani ya Bunge lako Tukufu na tukaleta hoja kwamba pesa hizi zikusanywe na Mamlaka ya Mapato na zitarejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niisome sheria tuliyoipitisha, baada ya kukusanywa kwa ufanisi tukasema, *the apportionment and disbursement of the proceeds collected under this section shall be made to a Local Government Authority based on its budget.* Nini tunabishana ndani ya Bunge lako Tukufu, sheria iko wazi na ndicho tunachokifanya kama Wizara, ndicho tunachokifanya kama Serikali. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Naomba mtulie mlipoongea tulitulia tukawasikiliza, sikilizeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili, kwanza naomba nitoe *caution* kwa Bunge lako Tukufu, tumwogope kama ukoma mtu anayetaka kuligawa Taifa hili vipande vipande. Tumekusanya tumeonesha ufanisi, matumizi sio mazuri na nini tumefanya baada ya kukusanya, tunazirejesha kulingana na sheria ilivyotuelekeza, *according to the budget of the Local Government Authority,* ndicho sheria inavyosema. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie tu watulie, tuwafundishe ili waweze kufahamu, hiki haiwezekani. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa leo tukisema kule Geita wakusanye kodi kutoka kwenye madini ibaki Geita na kule Manyara Mererani wakusanye kodi inayotokana na *Tanzanite* ibaki Mererani hatutokuwa na Taifa na Dar es Salaam wachukue kodi yote inayotoka bandarini wapi Taifa hili linakwenda? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja ambao umesemwa hapa bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni shilingi bilioni 14.2, nini Serikali tumefanya kwa pesa za ndani kwa Mkoa wa Dar es Salaam? Tumepeleka shilingi bilioni 11 ambayo ni asilimia 79, tunapeleka kwa Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeleka shilingi bilioni 11, nini tumekusanya kwenye Kodi ya Majengo Mkoa wa Dar es Salaam. Kwenye

Kodi ya Majengo Mkoa wa Dar es Salaam tumekusanya shilingi bilioni 10 na sisi tushapeleka shilingi bilioni 11, hii ndiyo Kodi ya Majengo tunayoulizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapi tunataka kuelekea? Jambo la msingi kabisa tunalotaka kulielewa hapa, tuwaulize hao wa Kinondoni wanaosema wao wakikusanya ni mradi upi Halmashauri ya Kinondoni iliwahi kutelekeza kupitia Kodi ya Majengo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watutajie tu mradi mmoja na kwenye bajeti ya mwaka huu, ndiyo maana nasema watulie, watueleze bajeti *item* iliyosema tutakusanya Kodi ya Majengo kiasi hiki na itakwenda kujenga kitu fulani twende kwenye bajeti ya Halmashauri ya Kinondoni. Kwa hiyo, tusiwadanganye Watanzania, tukalikatakata Taifa letu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mwingine mdogo kwenye kodi hii ili Waheshimiwa Wabunge tuelewane na tufanye maamuzi sahihi. Nini kimekusanywa Halmashauri ya Kinondoni kwa mwaka elfu mbili, Mheshimiwa Halima analidanganya Bunge lako, Halmashauri ya Kinondoni mwaka 2014/2015 ilikusanya shilingi bilioni tano.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukapeleka kwenye maendeleo zaidi ya shilingi bilioni tisa, Kinondoni peke yake. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongo, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Wabunge wanaopenda haki, wanaotaka Taifa letu liendelee kuwa Taifa moja ...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Kama tulivyoapa, tushikamane kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee tulia, tulia, wewe si una hoja ya *amendment* yako, unaweza ukalifanunua, haya tunaendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Tujifunze ule utulivu wa Kibunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa January Makamba, una dakika saba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kiti chako kiruhusu nichangie.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya mambo ya kujibishana *across* si kibunge. Mwenzako amejenga hoja na wewe ulipokuwa unajenga hoja alikusikiliza, sasa usijisikie vibaya. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Sasa mnajibishana na mimi tena.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitawataja *please*.

Mheshimiwa January Makamba, tuendelee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipatia ya kuchangia hoja zilizowasilishwa leo. Nianze kwa kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwanza kwa taarifa yao nzuri kwenye eneo letu lakini pia kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya katika kipindi chote ambapo tumekuwa tunafanya nao kazi. Tunawapongeza na kuwashukuru sana wametupa ushauri, miongozo na tumeelekezana na tumefanya kazi nzuri. Kwa hiyo, Mwenyekiti aliyetangulia na Mheshimiwa Murad sasa na Wajumbe wote hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mambo mengi kwenye taarifa lakini nitazungumza mawili tu

kutokana na uchache wa muda. Kwanza, ni suala zima la uwezo wa kifedha na fedha zinazotolewa kwa ajili ya usimamizi wa mazingira nchini. Nadhani wote tunakubali kwamba jambo hili tumelizungumza katika vikao mara nyingi kuhusu umuhimu wa hifadhi wa mazingira lakini uwezo mdogo wa rasilimali wa kufanya zile kazi zinazotakiwa kufanywa na Kamati ya Bunge imelieleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ambacho naweza kuliambia Bunge lako Tukufu ni kwamba tunaendelea kuzungumza ndani ya Serikali kati yetu sisi, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Fedha kuhusu namna ya kudumu ya kuweza kupata fedha za hifadhi ya mazingira kwa vyanzo mahsusi. Tulianza mwaka juzi kwa kupendekeza maeneo kadhaa ya mapato ambapo kufanyika kwa hizo shughuli moja kwa moja kunaathiri mazingira. Kwa mfano, mapato yanayotokana na magogo, mkaa na uingizaji wa bidhaa ambazo zinachafua mazingira, basi asilimia kadhaa ya mapato hayo iende kwenye Mfuko wa Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yamewasilishwa kwenye Kamati ya *Think Tank* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yametafakariwa na baadhi yametafakariwa na Kamati ya Bajeti ya Bunge katika Bunge lililopita. Imani yetu ni kwamba ndani ya Serikali tutamaliza mazungumzo ili mwaka ujao wa fedha sasa pale tutakapokuwa tumeelewana basi tutakuja na mapendekezo ya vyanzo vya kudumu na vya uhakika kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira ili tuweze kuwa uwezo na nguvu kubwa ya kusimamia Sheria ya Mazingira lakini kurekebisha pale maeneo ambapo mazingira yatakuwa yameharibika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi dhamira yetu ni pale Wabunge katika Majimbo yao watakapokuwa wanaona changamoto ya mazingira, basi iwe rahisi kwao wanapotuambia sisi, sisi tuweze kujibu kwa uharaka tukiwa na uwezo wa fedha wa kusaidia kurekebisha mazingira yanayoharibika. Kwa hiyo, hii ni kazi yetu sote sisi ndani ya Serikali lakini pia Wabunge kama watu wenye sauti na wenye uwezo wa kupanga fedha tushirikiane ili tuweze kuhakikisha

kwamba Mfuko huu unajaa fedha ili tuweze kufanya mambo ambayo Wabunge wanataka tuyafanye na mambo mengine ambayo tunaendelea kuyafanya ikiwemo kutafuta fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali huko duniani na kwa washirika wetu wa maendeleo wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la mifuko ya plastiki, limezungumzwa hapa na limezunguzwa kitambo humu Bungeni na Kamati yetu ya Bunge imelitafakari na tumetafakari kwa pamoja sisi pamoja na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Nataka kusema kwamba katika taarifa ya Kamati ya Bunge mtaona imeeleza kwamba nchi yetu viwanda vyote vilivyopo nchini mwaka jana 2016 vilizalisha tani 73.6 za mifuko ya plastiki lakini pia taarifa hiyo hiyo inasema mifuko ya plastiki iliyoingizwa kutoka nje ni tani 1,354. Kwa hiyo, utaona kwamba asilimia zaidi ya 90 ya mifuko ya plastiki inatumika nchini ni ile iliyotoka nje ya nchi siyo inayozalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna utata wa takwimu kuhusu idadi ya watu ambao wameajiriwa katika viwanda hivi kwa sababu kama viwanda viko 46 vinazalisha tani 73 kwa mwaka maana yake kila kiwanda kinazalisha chini ya tani moja na nusu kwa mwaka jambo ambalo kidogo ni gumu kulitafakari. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutaendelea kulishughulikia jambo hili na Kamati ya Bunge imeelekeza kwamba tupige marufuku uingizaji wa mifuko kutoka nje ya nchi ili hatimaye tuelekee katika kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba jambo hili lina *implications* kikodi, kiajira na kadhalika lakini sisi kama Serikali au sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tumeona kwamba madhara ya matumizi ya mifuko ya plastiki ni makubwa katika mazingira na afya ya watu wetu. Kwa hivyo basi, tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, bahati nzuri Sheria ya Mazingira, kifungu cha 80 kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya mazingira kwa kushirikiana na kushauriana na Waziri mwenye mamlaka ya

fedha kutengeneza nyenzo za kiuchumi zitakazoweza kushamirisha mbadala wa bidhaa zinazoharibu mazingira. Kwa hiyo, nitazungumza na mwenzangu wa Wizara ya Fedha tuone nyenzo zipi za kiuchumi zitakazotusaidia ili tutakapopiga marufuku mifuko ya plastiki basi kuwe na uchumi mpya wa mifuko mbadala na huko ndiko tunakoelekea na ndiko huko tunakotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu jirani zetu karibu wote wamepiga marufuku mifuko ya plastiki lakini hawajapiga marufuku uzalishaji wa mifuko ya plastiki. Kwa hiyo, mifuko ya plastiki kwa mfano kwenye nchi moja ya jirani hawaitumii pale lakini wanaizalisha na hawajafunga viwanda kwa sababu sisi tunaruhusu. Kwa hiyo, sisi tumekuwa ni dampo la mifuko ya plastiki. Tunaamini kwamba tutakapozuia na sisi matumizi ya mifuko ya plastiki basi hata mianya inayotumika kuingiza mifuko hii nchini mwetu na yenyewe itazibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uamuzi mkubwa ambao utaathiri maisha ya watu na namna wanavyoishi lakini naomba tu niseme kwamba tukubali na tuwe tayari kuupokea uamuzi huu wakati wowote. Wale wenzetu wenye viwanda tulishatoa tahadhari tangu mwezi Mei mwaka jana kwamba uamuzi huu unakaribia na tutakapofika tu kwamba kufanya uamuzi huu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nimalizie.

Wenzetu wanaozalisha na kuingiza mifuko ya plastiki itakapofika wakati Serikali itakapofanya uamuzi wa kupiga marufuku isije ikasemekana kwamba hatukuwa na taarifa ya kutosha. Hapa Bungeni katika Kiti hiki hiki mwezi Mei mwaka juzi 2016, tulitoa taarifa kuhusu dhamira hii ya Serikali. Kwa hiyo, tunaomba tu wajiandae kwamba tutafikia huko

lakini kama nilivyosema Serikali yetu kwa kujua kwamba lazima kupatikane mbadala basi itatengeneza mazingira ya kushamirisha uzalishaji wa mifuko mbadala ili watu wetu wasipate shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwijage, dakika saba.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Awali ya yote niwashukuru Wajumbe wa Kamati zote tatu wakiongozwa na Wenyeviti wao kwa taarifa zao nzuri hasa kwa maelekezo na ushauri tutauzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali nirekebishe kidogo tafsiri ambayo siyo. Mheshimiwa Mbunge nadhani alikuwa anasherehesha, aliyesema Serikali haijafanya lolote kwenye zao la korosho lakini mwisho akakiri kwamba labda kutafuta bei. Katika biashara ya uchumi kinacho-*drive* kila kitu ni bei. Panga bei nzuri watu watahangaika wenyewe. Kwa hiyo, nadhani alikuwa anasherehesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijibu kidogo hoja zilizozungumzwa lakini nimjibu na mchangiaji mmoja Mheshimiwa Mbunge aliyetafsiri taarifa za wepesi wa kufanya shughuli. Zile takwimu alizoziangalia aende akaangalie na *distance to frontier. Distance to frontier* inakueleza unapokuwa umepata maksi mbaya ujiangalie wewe ni wa ngapi katika yule aliyekutangulia. Ukiona upo *above 50%* hupaswi kulala bila usingizi, nakubali hatufanyi vizuri na pale ambapo hatufanyi vizuri tumejitathmini na tumeandika andiko '*The Blue Print*' maeneo yote yenye matatizo tutayakosoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye anaweza kukaribisha wageni halafu wageni hao unashindwa kuwawekea kiti au namna ya kuwakirimu. Namna ya kuwakirimu wawekezaji ni kuwatengenezea mazingira mazuri ya kufanya biashara. Mimi binafsi nakiri kwamba ninapopataka siyo hapa, nitaendelea kuhimiza kwa kushirikiana na wenzangu tuweze kwenda kwenye nafasi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la viwanda vilivyobinafsishwa. Siyo mapenzi ya Waziri mwenye dhamana wala mtu yeyote ni Ilani ya Chama inasema viwanda vilivyopo sasa vifanye mpaka ukomo (m*aximum capacity),* viwanda vilivyobinafsishwa vyote vifanye kazi na tuhamasishe viwanda vingine vije. Kwa hiyo, orodha ya viwanda vilivyobinafsishwa kama alivyozungumza *Comrade* Lusinde nitaileta hapa Bungeni mje muione, kazi inafanyika lakini ngoja niwaambie, viwanda vile lazima vifanye kazi, kama huwezi kufanya kazi mpe mwenzako na tutakapofika wakati wa *factoring* unaweza kushtakiwa kwa uhujumu uchumi na dhamana yake mnaifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa viwanda. Tunalo jukumu la kulinda viwanda na viwanda tunavilinda kwa ngeli mbili, moja ni kuangalia mpangilio wa kodi katika maeneo ya kikanda tulipo. Bado hilo zoezi linaendelea hatujafanya vizuri na Kenya wanajua kututegea kwenye suala hilo na tunalijadili Serikalini tutahakikisha kwamba hatupangi bei ambazo majirani zetu wana-*take advantage,* hilo tutalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo tunakiri upungufu katika shughuli hiyo ni tatizo la *under valuation* na *under declaration* na *smuggled items*. Tunalijua na tutalishughulikia na tutalifanya kazi. Kama alivyosema *Comrade* Lusinde watu wanaouza hivi vinywaji katika chupa za plastiki kumbe tatizo siyo chupa za plastiki, tatizo ni kuuza katika chupa za plastiki chini ya ujazo uliokubalika. Tatizo la pili ni kuuza bila kuweka ile stampu ya *TRA.* Kwa hiyo, wale ni

majambazi kama majambazi wengine, naomba mkiwaona mniambia mimi au mwende Polisi mtafute *RB*. Ulinzi wa viwanda ni jukumu la sisi wote sio jukumu la Serikali peke yake au Waziri mwenye dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo mkakati wa kuendeleza viwanda. Mkakati wa kuendeleza viwanda upo ni *Integrated Industrial Development Strategy* lakini tumezungumza ni viwanda gani tunavitaka, tunataka viwanda vile ambavyo vinaajiri watu wengi, tunataka viwanda vile ambavyo vinachakata malighafi za wananchi, tunataka viwanda vile ambavyo bidhaa zake zinatumika kwa wingi na imekuja kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais tutengeneze viwanda vitakavyochakata mali za asili ambazo tulipewa kipekee na Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana ukuta unajengwa pale kuzunguka *Tanzanite*. Hivyo ndivyo viwanda tunavyoshughulikia, tumefanya vizuri katika hilo. Jukumu la Serikali ukisoma Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ni kuhamasisha sekta binafsi iweze kuwekeza, tunajitahidi, tunafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtu asije akadhani kwamba sisi hatujafanya kazi na mambo yote haya yanajulikana tatizo ni mapenzi ya kufika *finally* wakati ndiyo mchezo unaanza. Tunajenga viwanda na tunategemea *come* 2025 itakuwa nchi ya uchumi wa kati tukiwa na viwanda, leo ndiyo mwaka wa pili na niliambie Bunge lako kwamba kwa kipindi cha miaka miwili viwanda 3,306 vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna *installed capacity* ya saruji *10.9 millions tans* wakati matumizi yetu ni *4.8 millions tans*. Tanzania tunazalisha vigae Kiwanda cha Mkuranga *square* 80,000, Kiwanda cha Chalinze kinazalisha 50,000, ukienda Rwanda ukipeleka kigae cha China hawanunui wanataka vya Tanzania. Kwa hiyo, msidhani kwamba tuna hali mbaya, tunataka kuwa mbele lakini hapa tulipo hatupaswi kujinyonga kwa sababu hatufanyi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kasi ya utendaji wa miradi ya Serikali. Imetolewa hoja kwamba miradi ya Serikali inakwama, ndiyo, tumelizungumza hapa suala la *PPP,* tumezungumza hapa suala la hizi sheria kuna upungufu na hayo yote hayo tumeyaona na tunayafanyia kazi. Kwa sababu tukienda bila kuyarekebisha haya na kuyaleta mbele ya Bunge tutakuja kuulizwa tulifanya nini. Tunayafahamu haya, tutayarekebisha ikiwemo suala la *Kurasini Logistics Centre* na *General Tyre.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *General Tyre* tunajua tunataka kufanya nini, lakini sheria sasa inayokuwezesha namna ya kushirikiana na yule *private* sekta ndipo inapokuja ngoma. Taasisi zinazohusika, watendaji wa Serikali wanashughulikia suala hili ili tuwe na mwendelezo mzuri wa kuweza kufanya shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda siyo rafiki, nakushuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, dakika saba.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kumshukuru Mungu kwa kuniruhusu kusimama tena, lakini pia niwashukuru Wenyeviti wote watatu kwa taarifa nzuri za kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa yetu ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali tulilitaarifu Bunge lako kwamba tumekamilisha majadiliano na taasisi mbalimbali za kifedha ili tuweze kukopa takribani Dola 1,460,000,000 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa reli ya kati na hususani kile kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutopora. Naona mdogo wangu alipandisha *BP* hapa ingawa amenikimbia, anasema sijapata ruhusa ya kwenda kukopa kiasi hicho cha pesa nimeipata wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya Bunge ni kwamba tunatafuta fedha hizi kutoka kwenye vyanzo viwili

vikubwa, kimoja ni *Export Credit Agency (ECA*) ambapo tunatarajia tutapata Dola za Kimarekani 990,000,000 lakini zilizobaki takribani Dola 470,000,000 tutakwenda kukopa kwenye vyanzo vya kibiashara na hususani *Standard Chartered* ambayo imepewa jukumu la kuratibu upatikanaji wa hizo fedha baada ya kukubaliana masharti ya mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa mkopo wa *Export Credit Agency* ni miaka 18 wakati kwa mikopo ya kibiashara ni miaka 10 na *disbursement* ni miaka minne na urejeshaji wake ni kwa miaka 14 kwa upande wa *ECA* na miaka sita kwa ile mikopo ya kibiashara. Riba unganishi tunaita *all cost margin* ni asilimia 2.77. Mikopo hii itapatikana ndani ya miaka minne ambayo ni takribani Dola 365 kwa kila mwaka. Kwa hiyo, ule ukomo wa Dola za Marekani milioni 700 ambazo ziko kwenye bajeti hazitavukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo nazingatia sana ni Sheria ile ya Mikopo ndiyo inaniongoza kukopa na sheria zake, hakuna kuvuka. Isitoshe kwa mwaka huu fedha Bunge hili liliridhia bilioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ambayo ni karibu shilingi milioni 800 bila *VAT* na gharama nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na maneno kwamba kuna trilioni mbili ambazo hazikujumuishwa kwenye Deni la Taifa. Hazikuwekwa huko kwenye kanzidata ya madeni kwa sababu wakati ule tulikuwa bado tunahakiki yale madeni ya mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulielezea na hili niliseme na hususani kwa Kamati ile ya Viwanda na Biashara, la Benki Kuu kwamba ile *structure* yake imepitwa na wakati na sasa tufike mahali ambapo Gavana hawi pia Mwenyekiti wa Bodi. Hili nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge tuwe waangalifu sana. Tumeangalia nchi nyingine ulimwenguni takribani asilimia 90 ya nchi ambazo zina *structure* na majukumu ya Benki Kuu kama ilivyo kwetu hapa wana utaratibu kama huu wa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya msingi kama mnafahamu, Bodi ya Benki Kuu kazi yake ni sera na *supervision*, kwa hiyo, wao wanapitisha (*approve) broad strategies* wakati Gavana anasimamia shughuli za kila siku za Benki Kuu na kama mnavyojua sekta ya kibenki ni *hypersensitive*. Kwa hiyo, ni muhimu sana tukahakikisha kwamba tunaunganisha hizi shughuli za Gavana ili kuhakikisha kwamba Benki inabakia kuwa *strong* lakini pia Gavana hawezi ku-*provide central leadership* na *independence* ya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua unapocheza na *exchange rate na interest rate, foreign reserves, money supply,* nchi nyingine Gavana akiugua, akipata mafua unaona kule *interest rate* zinavyoitika. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuwe waangalifu tusikimbilie kusema tu-*separate* hizi nafasi mbili itatugharimu sana, ndiyo uzoefu wa ulimwengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la utegemezi wa ruzuku ambao umekithiri katika Mashirika ya Umma. Tulipoanzisha haya mashirika shida yetu kubwa ilikuwa ni kutoa huduma kwa jamii kwa urahisi na hususani shughuli zile ambazo hazifanywi na sekta binafsi au kama wanafanya sekta binafsi wanazifanya kwa bei kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kuhakikisha hizo huduma na hususani upande wa afya, elimu na utafiti zinawafika Watanzania walio wengi, Serikali inatoa ruzuku kwa haya mashirika. Kwa sasa hivi, mashirika ambayo yanapata ruzuku yako takribani 175 ukilinganisha na idadi ya taasisi zote ambazo zipo takribani 269. Kwa hiyo, *logic* ni ile tu kwamba mashirika haya yanafanya shughuli ambazo *private sector* haiko kule na kama ipo basi wanafanya kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulisemea ni juu ya *fees* ambazo zinakua *charged* na *Regulatory Authorities.* Hili nadhani wote tunakubaliana na mnaona juhudi za Serikali ambazo tumefanya katika hotuba ya bajeti ili tuanze kuzi-*rationalize* na hii ni *continuous process* tutaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni bajeti ya viwanda, limesemwasemwa sana hapa, nataka tu kuomba, taarifa tulizotoa ndizo taarifa rasmi za Serikali. Sasa nimwombe sana Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara na Viwanda kama ana taarifa tofauti na takwimu ambazo sisi tumetoa kwenye taarifa rasmi tuliyowasilisha Bungeni, aziwasilishe kwangu kupitia Meza yako Mheshimiwa ili tuweze kuona shida ipo wapi kwenye hizi takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu la mwisho, yako mengi muda kidogo, hili la *conduct* ya Sera za Fedha na Sera za Kibajeti, *conduct* ya *monetary* na *fiscal policy*. Ningefurahi sana ningepata muda wa kulieleza vizuri ili tuelewane hususani Mheshimiwa Bashe. Sisi tunavyoliona haziko *contradictory* kama zinavyowekwa hata kidogo. Tofauti ya kwanza mimi ninayoona ni kwamba ni muhimu kujua hatua ambazo zinachukuliwa hivi sasa baadhi zina matokeo ya mara moja lakini nyingi zinachukua muda ndiyo uweze kuona tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hivi sasa, tulichokuwa tunafanya tunaita ni *Expansionary Monitory Policy*. Kwa lugha nyepesi *Expansionary Policy* ni pale ambapo tunatumia fedha za kibajeti kuongeza zaidi, kuchachua uchumi kwa kuwekeza kwenye miundombinu, tunalipa madai ambayo yamehakikiwa lakini pia kushusha viwango vya kodi kwenye maeneo ambayo tunataka ku-*promote* kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hiyo unakuwa pia na *Expansionary Monitory Policy* (Sera za Fedha) ambazo Serikali kama ilivyofanya kupunguza *statutory minimum reserve requirement* lakini saa nyingine inatumia soko lenyewe la fedha (*open market operations*) lakini pia kujaribu kucheza na riba za aina mbalimbali. Tunavyoziona sisi zipo *complimentary* tofauti ni muda ambao tunatarajia kwamba tutaona hizo *effects* tarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la muhimu sana, *the captains of industry*, kama mnasoma magazeti *CEO* wa *NMB*

ameliweka wazi, *CEO* wa *CRDB* ameliweka wazi, nimefanya mazungumzo na zaidi ya benki 12 zote wameweka wazi kwamba wanavyoona wao sekta ya kibenki sasa imeanza kuimarika *the worst is over*. Sasa tumuamini nani kuliko *the captains of industry* wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *VAT* kwenye bidhaa za maziwa na mafuta ghafi, naomba tu niweke tu *on record,* haya ni mambo ambayo tayari yamepokelewa na yanapelekwa kwenye Kamati za Kitaalam (*Think Tank)* kwa ajili ya kuchambuliwa. Namwalika Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye atapenda tutatangaza siku ambazo tutakuwa na ile mikutano akitaka aje ashiriki pia yale majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tena juu ya upitishaji wa shehena kule bandarini. Nafikiri ni vizuri tupanuke kidogo mawazo, mwenendo wa shehena kwenye bandari zetu hautegemei tu hizi *fiscal policies* hata kidogo. Ni muhimu kuangalia *trends* za biashara ulimwenguni zinakwendaje, kwa sababu na bandari zingine ukizitazama *the volumes of trade, imports and exports* zimekwenda chini siyo kwa Tanzania peke yake. Sasa ukiangalia Tanzania peke yake umefumba macho mno, hebu panua wigo kidogo. Kuna vitu vingi ambavyo inabidi kuviangalia, lazima kuangalia uwezo wa bandari yetu kwa maana ya *equipments,* lazima pia kuangalia *in terms of efficiency* hata *the way we are organize*, kwa maana ya watendaji wa mabenki...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Naelewa muda wetu sio rafiki. Sasa tunaanza kuwaita Wenyeviti waweze kuhitimisha hoja zao. Tuanze na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Ghasia, utakuwa na dakika zako 20.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutolea ufafanuzi hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, ambao baadhi yao wamezileta kwa maandishi idadi yao ni nane na baadhi yao wametoa kwa kuzungumza ambao idadi yao inafikia 14 ikiwa na pamoja Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna tatizo la muda, naomba niende moja kwa moja katika hoja ambazo zimezungumzwa. Nianze na Mheshimiwa Riziki Lulida ambaye amezungumzia uwepo wa rasilimali na akaomba kwamba Serikali izisimamie rasilimali hizo ili kuhakikisha kwamba zinaleta tija katika Taifa letu. Nakubaliana naye na sina haja ya kuendelea kuijadili hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Riziki Lulida pia aligusia pia suala la zao la korosho haswa akijikita katika eneo la uhujumu wa zao hilo, kwa kile kitendo ambacho korosho zetu zilizokwenda Vietnam kugundulika kuwa na mawe na masuala mengine. Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Mary Mwanjelwa amelitolea ufafanuzi lakini bado tunaendelea kusisitiza, naungana na Mheshimiwa Riziki Lulida kwamba bado Serikali inatakiwa ichukue hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba suala hilo halijotokezi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tunatoka katika maeneo ya korosho tunaona kitendo hiki kama hujuma kwa wale wanunuzi wapya ambao wamejitokeza katika zao hili na kuwezesha kupandisha bei na hata kufikia Sh. 4,000/= kwa kilo. Kwa sababu wapo ambao walikuwa wananufaika na bei zile za chini ambazo zilikuwa zinawanyonya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahisi kuongezeka kwa bei za korosho ambako kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa wanunuzi kutoka nchi za Vietnam, Uturuki na China kunaweza kukawa ni sababu ya kuwafanyia hizi hujuma ili kuwakatisha tamaa wasiweze kuja

kununua korosho zetu na hivyo kushusha bei za korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasisitiza suala la kuchukua hatua thabiti kwa wale waliohusika lakini pia kama Serikali iwekeze kwa kujenga maghala ambayo yataweza kuhakikisha kwamba muuzaji wa korosho anavyopeleka pale, tukiwa na maghala yanayokubalika, kwa utaratibu wa ununuzi wa korosho huwa zinamwagwa na hivyo kuhakikisha kwamba zinakaguliwa kabla ya kusafirishwa kwenda kule kwa wanunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukiwa na viwanda ambapo wale wawekezaji watakuja kubangua hapa hayo masuala mengine nadhani yataweza kuthibitiwa. Pia kwa upande wa Mkoa wa Mtwara, ilishapendekezwa kwamba korosho zote zinazozalishwa Mtwara na Lindi zitumie bandari ya Mtwara ili kuweza kudhibiti suala hili la kuziharibu korosho zetu zikiwa njiani zikielekea bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hizi korosho ambazo zimeonekana kuwa na mawe, baada ya kuzifuatilia ni zile korosho ambazo zimesafirishwa kupitia bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunarudia tena kusema kwamba hatua sahihi zichukuliwe kwa wale wote waliohusika kuharibu ubora wa korosho zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji wa pili ni Mheshimwa Balozi Diodorus Kamala ambaye aliomba suala la 10% kwenye mafuta ya kula kutoka nje liendelee na pia kusaidia sekta ya ngozi kama ambavyo wenzetu Ethiopia wanavyofanya. Tunaungana naye mkono hakuna haja ya kubishana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji mwingine ambaye alichangia kuhusu Kamati yetu ni Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambaye alisisitiza suala la Serikali kulipa madeni yote ya ndani na pia kufanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi na pia kuziwezesha taasisi kimitaji ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Naungana naye mkono katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Jitu Soni aliiomba Serikali kufanya tathmini ya gharama za uzalishaji ikiwemo tozo zinazotozwa na Mamlaka zetu za Udhibiti nadhani Mheshimiwa Waziri amelijibu, kwa hiyo, sina haja ya kulirudia. Pia mifumo ya malipo iendelee kuimarishwa ambalo pia Kamati tumelishalisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa David Silinde alizungumzia suala la urahisi wa ufanyaji wa biashara na uwekezaji. Pia alizungumzia kwamba tumeporomoka katika maeneo saba. Katika taarifa yangu nilisema tunaipongeza TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi, walikuja na maeneo ambayo yamewasababishia kuporomoka na wakaja pia na mikakati thabiti waliyoiweka na ambayo sisi kama Kamati tuliridhika. Bado tunaendelea kuisisitiza Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka mikakati thabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wanayo *Blue Print* lakini *Blue Print* ni maandishi yaliyopo na tumekuwa nayo muda mrefu. Tunaomba hiyo *Blue Print* ifanyiwe kazi kuhakikisha inaleta tija. Kwa hiyo, nimwombe shemeji yangu Mheshimiwa Mwijage apunguze maneno aongeze vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Janet Mbene alizungumzia suala la magogo kutoka Congo na pia tupate mikakati ya kuinua uchumi wetu na pia pongezi ambazo alizitoa kwenye Mfuko ya Kahawa katika kuondoa tozo za Kahawa na pia kupendekeza tozo zingine ambazo zitawalenga wakulima wetu. Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana naye sana kwa hayo aliyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzanite* yetu inasafirishwa kwa wingi na nchi jirani lakini sisi nchi jirani zikitaka kuleta biashara zao kama magogo au korosho kutoka Mozambique kuleta Tanzania wauze huku kwetu tunakuwa na vikwazo vingi. Kwa hiyo, tuiombe Serikali iondoe vikwazo, hivi korosho ya kutoka Kaskazini Mozambique ikiuzwa Mtwara na Mtwara ndiyo wakasafirisha kwenda nje, kuna tatizo gani?

Magogo kutoka Congo yakisafirishwa kupitia bandari ya Tanzania au yakiuzwa Tanzania kuna tatizo gani? Kwa hiyo, tuangalie uwezekano wa kuondoa hivyo vikwazo ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hussein Bashe alitoa mapendekezo yake na pia alisisitiza suala la viwanda vyetu pia kuoanishwa na sekta ya kilimo ambayo inaajiri kwa kiasi kikubwa Watanzania. Tunaomba Serikali hilo ilifanyie kazi. Pia aliongelea kuweka vivutio ambavyo vitasaidia viwanda vilivyoko nje kuja kuwekwa huku ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Mdee alizungumzia suala la kunyang'anya vyanzo vya mapato vya Halmashauri na kwamba pesa nyingi zilizoenda katika Halmashauri zimeenda kulipa madeni. Serikali eneo hili imelijibia lakini pia tukumbuke tunavyoandaa bajeti zetu huwa tunaweka na bajeti ya kulipa madeni na wazabuni. Kwa hiyo, sioni tatizo tukisema kwamba pesa zilizokwenda zimeenda kulipa madeni zaidi kwa sababu bajeti pia ilikuwa inasema hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Sixtus Mapunda kwamba *ATCL* itazamwe na iwezeshwe, tusiangalie tu suala kwamba inaleta faida kiasi gani kwa maana ya pesa ile ya kuiona moja kwa moja, hapana, tuangalie faida za ujumla. Kwa kweli *ATCL* ina mchango mkubwa sana katika kuinua uchumi wetu na hasa katika sekta za utalii lakini pia hata kuharakisha usafirishaji na kuwezesha uwekezaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na wale wanaosema kwamba tuziangalie taasisi zile ambazo zina mwingiliano ili kuondoa kero za kikodi na zisizo za kikodi kama vile *TFDA* na *TBS* ikiwezekana iunganishwe na iwe taasisi moja ambayo inatoa huduma zote hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa zile ahadi alizoahidi tunaomba basi ziharakishwe na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Ashantu Kijaji, tunakubaliana naye, sina haja ya kurudia kule lakini nirudie kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwamba viwanda vyote vilivyobinafsishwa na ambavyo havifanyi kazi yake iliyokusudiwa virudishwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya korosho karibu vyote, vingi viliuzwa kwa milioni 50 na vingine waliouziwa hawakutoa hata senti tano. Sasa hivi viwanda vile vimegeuzwa kuwa maghala wanawakodisha wakulima kwa kuhifadhi korosho zao mle ndani. Nimwombe Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda na Biashara atekeleze agizo la Mheshimiwa Rais, la kuhakikisha viwanda vile ambavyo vilibinafsishwa kwa bei nafuu zaidi ambapo wale wawekezaji wameacha kufanya yale majukumu ambayo waliagizwa basi vinarejeshwa kama Mheshimiwa Rais alivyoagiza. Kama Rais alimeshaagiza kigugumizi ni cha nini ndugu zangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tena kwa wenzetu Wizara ya Fedha waangalie zile tozo ambazo wamepunguza lakini kama zipo tozo ambazo wanaziona ni kwa manufaa ya nchi yetu na Serikali yetu basi pia tuendelee kuzipunguza ili kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira bora ya kufanyia biashara na kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tena kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi kuja kutoa ufafanuzi katika hoja zile ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge na pia niishukuru sana Kamati yangu ya Bajeti kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Niishukuru pia Sekretarieti, nimshukuru Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja sasa kwamba mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati yakubaliwe ili yaweze kutekelezwa na Serikali iyafanyie kazi pia na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono na Wabunge zaidi ya 10. Kabla sijaitoa kwenu hoja hiyo, kuna Jedwali la Mabadiliko limetolewa na Mheshimiwa Halima Mdee, nitamwita sasa Mheshimiwa Halima Mdee awasilishe hoja yake, karibu Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mabadiliko yangu, mosi kutokana na pendekezo la 3.8 la Kamati ya Bajeti ambalo linakiri kwamba Serikali ilihamisha ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kutoka Serikali za Mitaa na kupeleka Serikali Kuu ili *TRA* ikusanye kwa ajili ya kuongeza ufanisi. Vilevile imesema kabisa wazi kwamba walikubaliana na hoja kwa sababu tulikuwa tunafahamu kwamba wao walikuwa wanakusanya ili warejeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu imeendana tu na matakwa ya kisheria, sheria kama ambavyo nilisema pale mwanzo, kifungu cha 65 cha Sheria ya Fedha mwaka jana, kifungu kidogo cha (2)(a). Mapendekezo yangu kutokana na tafsiri hii ya kisheria ambayo niliizungumza wakati nachangia yanasomeka ifuatavyo:-

KWA KUWA katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilihamisha ukusanyaji wa Kodi ya Majengo kutoka Serikali za Mitaa na kupeleka Serikali Kuu, *TRA* ikipewa jukumu la kukusanya kwa niaba ya Halmashauri kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji;

NA KWA KUWA Kamati ilikubaliana na pendekezo hili kwa makubaliano kwamba chanzo hiki cha mapato ni cha Serikali za Mitaa na fedha zitarejeshwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo;

NA KWA KUWA kifungu cha 65(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 ambayo ni Sheria Na. 4, kimetamka bayana

kwamba Kodi ya Majengo itakayokusanywa itapelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina;

NA KWA KUWA kifungu cha 65(2)(a) cha sheria husika kinaendelea kuainisha kwamba ugawaji na usambazaji wa fedha husika zilizokusanywa zitapelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutokana na bajeti zake;

NA KWA KUWA bajeti za Serikali za Mitaa zinatambulika kwa kuwa mchakato wake ulishafanyika chini ya usimamizi wa Hazina na Bunge likaridhia;

HIVYO BASI Kamati inaitaka Serikali kuzirejesha fedha husika Halmashauri ili zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mapendekezo haya kwa nia njema tu, mosi, kusisitiza utekelezaji wa sheria lakini pili kuzisaidia Halmashauri zetu ziweze kupata mapato yake halali kwa sababu vyanzo hivi ni vyanzo halali vya Halmashauri ili waweze kufanya shughuli za maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na wewe tunafahamu kwamba Serikali Kuu, ukiacha miradi mikubwa mikubwa ambayo huwa ni michache fedha zinazokuja Halmashauri ni fedha za mishahara na matumizi tu ya kawaida lakini fedha za miradi ya maendeleo iwe kujenga zahanati, shule, hospitali, au kuboresha barabara zetu za ndani inategemea *own source*. Sasa *own source* zinapochukuliwa halafu hazirudishwi wakati sheria inaelekeza, wakati bajeti imepita tunakuwa hatuzitendei haki hizi Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wabunge wenzangu, kwa sababu tokea jana tumekuwa tukilalamikia hili waweze kuniunga mkono kwa nia njema tu ya kuzisaidia Halmashauri zetu na Serikali ina jukumu ya kusimamia. Kwa hiyo, kama inaona kwamba tumepitisha bajeti, Halmashauri kuna Watendaji ambao wanaenda kinyume na utaratibu ni jukumu la Serikali Kuu na vyombo

vyake kuwashughulikia hawa watu. Kwa hiyo, naomba isitumike kigezo cha upungufu wa watumishi wachache kuumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba kuwasilisha hoja yangu na naomba kutoa hoja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaaa. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, ahsante. Nitamwita kwanza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu halafu tuone tunaendeleaje kwa sababu ya muda.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuelewa na tunakwenda kikanuni vizuri na hasa unapoitizama kanuni ya 57(3),(4) na (5) ya kwamba baada ya hoja hii kutolewa basi inatupasa sisi wengine ambao hatukubaliani na hoja hiyo na sisi pia tutapata nafasi ya kuzungumza kama tulivyoanza kujieleza mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natizama hoja ya Mheshimiwa Halima, sitaki kwenda kwenye yale maelezo yake mengi ya utangulizi, lakini nataka tu kuishia pale ambapo anajenga hoja yake baada yale maneno mengi ya utangulizi. Mheshimiwa Halima yeye anataka kulishawishi Bunge hili kwamba liitake Serikali kuzirejesha fedha husika Halmashauri ili zitumike kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno mazuri ambayo yameelezwa hapa na Serikali ndani ya Bunge hili leo wakati wa kuchangia hoja hii, kwamba Serikali imekuwa ikifanya hicho ambacho Mheshimiwa Halima anakizungumza hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ametoa

maelezo kwa *data* kamili ambazo Serikali tunazo. Kwa sababu kwenye hoja ya msingi kwa maana ya mtoa hoja ya msingi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yeye amemalizia hoja hiyo ambayo Halima anataka kuibadilisha kwa kusema kwamba anachoomba kwa Serikali ni kutafuta utaratibu rahisi zaidi wa kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa na kuzifikia Halmashauri zinazohusika na ndicho kitu ambacho Serikali imekuwa ikikifanya na imekuwa ikiweka utaratibu huo wa kurejesha hizo fedha katika Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo na kwa kutumia hizo Kanuni ambazo nimezisema na kwa msingi wa majadilianao haya, naomba kulishawishi Bunge tubaki na mapendekezo ya Kamati kwa sababu mapendekezo ya Mheshimiwa Halima aliyoyatoa ni maelezo ambayo yapo *too general,* lakini ukienda kwa mapendekezo ya msingi ya Kamati yanataka kuendelea kuirahisishia Serikali kufanya kazi ambayo imekuwa ikifanywa na *data* za kufanya kazi hiyo zimeshasemwa na Naibu Waziri wakati anachangia hotuba hii. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima baada ya maelezo hayo unasemaje?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, sheria inasema fedha zitarudishwa kutokana na bajeti, mimi nimetoa *practical example* ya Kinondoni, kama ambavyo Wabunge wengi jana wamezungumza hali za Halmashauri zao zikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu kwanza limekuwa *straight* kuliko kuzunguka kwa sababu kwa mujibu wa sheria hii, hiki chanzo hakijawahi kuhama kutoka kwenye Halmashauri kwenda Serikali Kuu, Serikali Kuu walikuwa wanakusanya kwa niaba yetu na kama umefanikiwa kukusanya kama ambavyo Waziri na Naibu Waziri wanasema kwamba tumekusanya vizuri sana, hivi kweli mantiki inaingia akilini, mimi kwa sababu hiki chanzo ni changu, kwenye mpango wangu wa bajeti, pamoja na mipango yangu ya maendeleo nilijumuisha milioni 10, kwa mfano, za *property*

kwa ajili ya kujenga madarasa ama zahanati. Ikapitishwa na wataalam wa Hazina ikaja Bungeni, kama umekusanya zaidi, kwa nini usinirudishie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina pingamizi kabisa Serikali kupitia *TRA* kukusanya, sina. Shida yangu hapa, wanatuvunja miguu Halmashauri tunashindwa kufanya kazi kwa sababu tunawekea mipango vyanzo ambavyo tunajua ni vyetu halafu fedha haziji, hicho tu. Kwa hiyo, Serikali inaweza ikaamua ikasema kwa sababu sisi tunapenda sana kukusanya, tunakichukua chanzo cha *property,* tunachukua chanzo cha majengo, kinaenda kwenye Serikali Kuu, Halmashauri shughulikeni na masoko yenu, tusipangilie mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasisitiza kwamba kwanza hoja yangu na ya Kamati hazitofautiani kabisa, Kamati wameweka tu maneno malaini wakapanua vizuri na kuweka maneno matamu kidogo, lakini mimi nimesema *straight* kwa sababu sheria inasema mnakusanya kwa niaba yetu, basi mkishakusanya turudishieni. Kama mnaona kwenye Halmashauri kuna mafisadi hivi vyombo Polisi, *PCCB* vimewekwa kwa sababu gani? Hivi *CAG* amewekwa kwa sababu gani? Kwa hiyo, tusitumie kigezo cha nyie kupoka pesa zetu, tunashindwa kufanya miradi ya maendeleo kwa wananchi wetu kwa kusema kwamba kila mtu ni mwizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimamia hoja yangu, naomba Bunge lako Tukufu liamue na rekodi zitatuhukumu kwa sababu tupo hapa miaka mitatu imebaki, kilio kitabaki hiki hiki. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nataka niwahoji, ningependa niitoe mjadili, lakini mimi niwahoji tu twende mbele.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Halima J. Mdee ilikataliwa na Bunge)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Wasioafiki wameshinda. Kwa hiyo, sasa naitoa ile hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambayo mliiunga mkono sasa muiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017 Iliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na uwasilishaji wa Kamati ya Pili, Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kufika muda huu lakini kipekee nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi asubuhi hii kuweza kuwasilisha taarifa ya Kamati. Kipekee niwashukuru Wabunge wote kwanza kwa kusikiliza taarifa yenyewe na pili kwa kuweza kuisoma na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi niende kuwashukuru waliochangia taarifa hii. Taarifa hii imechangiwa na watu wengi, nitaenda mmoja baada ya mwingine. Naomba nianze kipekee kuwashukuru Serikali kwa *response* yao ya hotuba yetu na michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, naomba nianze na hoja za Serikali na nianze na hoja aliyowasilisha Waziri wa Fedha kwenye majibu yake, pale Kamati tulipoomba kwamba Gavana asiwe Mwenyekiti wa Bodi na tukawa tumependekeza kwamba kwa sababu ya *good governance* zitenganishwe hizi *pillar* mbili lakini kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameonesha kwamba ni vizuri iendelee kuwa hivyo kama ilivyo na ame-*cite* kwamba *90%* ya *survey* waliyoifanya Gavana ndiyo Mwenyekiti wa Bodi.

Kwa mtazamo wa Kamati tuliona kwamba huenda vingetenganishwa vingeweza kuleta ufanisi lakini naomba nikubaliane na majibu ya Serikali kwamba kama wataendelea kuifikiria na kuiona hivyo bado inaleta ufanisi, basi tunaiomba tuiache hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kabisa nimpongeze Profesa Luoga, tulipoita Benki Kuu kuja kwenye Kamati yetu hakuweza kufika lakini kwa kweli alionesha *concern* kwa nini hakufika na akawa amesikitika kwa nini hakufika, aliwatuma Magavana wake. Tunaomba tumpongeze kwa sababau alionesha *concern* kubwa ya kuheshimu Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la pili ambalo Mheshimiwa Waziri amesema ni huduma za mashirika kwamba mashirika mengine ni kwa ajili ya ruzuku. Kama Kamati tunakubaliana na majibu ya Serikali *issue* yetu ni kwamba kama mmesema kwamba mtaipa ruzuku na yanasaidia, kwa nini hampeleki fedha? Ndiyo hoja yetu. Tunajua mashirika 175 kati ya 269 yanapewa ruzuku lakini kwa nini Mheshimiwa Waziri fedha za kuendesha mashirika haya haziendi kwa wakati? Hiyo ndiyo hoja yetu, kwa hiyo, tunaomba mwendelee kuifanyia kazi ili muweze kui-*solve* hii changamoto ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngoja kidogo tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyonayo naongeza muda usiozidi dakika thelathini ili tuendelee na shughuli iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa endelea.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Sixtus Mapunda aliyejaribu kuelezea

vigezo na kwa nini *ATCL.* Sisi tumesema kwenye ripoti yetu *ATCL* ni kampuni ambayo ina umuhimu mkubwa lakini katika miaka mitatu imeendelea kupata hasara. Hata kama itakuwa na faida nyingine kwa sekta nyingine lakini kama shirika na sisi kama Kamati ya Uwekezaji ni lazima tui-*task management* na bodi ihakikishe kwamba inaleta faida ina-*turn out* hizi *loss* ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakubaliana na mawazo ya mchangiaji kwamba inazo faida nyingine kwa sekta nyingine, hizo hatukatai tunajua kwamba *intention* ya Rais ya kununua ndege na ataendelea kununua ndege na sisi tunaunga mkono katika ku-*boost* utalii lakini tunapokuja kwenye shirika lenyewe lile nalo tunalitaka liweze kuwa na faida. Tunapoangalia mizania yake tunataka na lenyewe shirika liwe na faida pamoja na kwamba lina *other profits* kwenye sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ameongelea mitaji, nipongeze nia nzuri ya Serikali, 2016 Serikali hii ilikuwa imewekeza trilioni 23 ambapo mwaka jana tulipata faida ya bilioni 422.9 lakini kwa 2017 mtaji umeweza kuongezeka mpaka kuwa trilioni 47.8 ambapo tumeweza ku-*realize* gawio la bilioni 845. Kwa hiyo, hii ni *achievement* kubwa, lakini tunaposema *generally* faida bado ni 1.9% ambayo ni ndogo. Kwa hiyo, bado ni wito wetu kuhakikisha kwamba wanaoendesha mashirika wana-*task* ya kuhakikisha faida ya mashirika hayo inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine aliyechangia ni Mheshimiwa Mary Deo Muro, yeye alikuwa anaongelea Bodi ya mashirika hasa aliongelea *RAHCO* na Elimu Kibaha. Kwenye ripoti yetu tumesema vizuri na ukiangalia kwenye bodi bado tunai-*task* Serikali, mfano, *MSD* ina miaka karibu miwili haina Bodi na sasa hivi nia njema ya Mheshimiwa Magufuli, Rais wetu ya kupeleka fedha ya kununulia dawa, nia njema aliyonayo Waziri wa Afya na Serikali nzima inapeleka fedha nyingi lakini hamna bodi iliyopo pale. Ni wajibu wetu kuwakumbusha kwamba bodi ya *MSD* iweze kuteuliwa. Wanashindwa kufanya *investment* kwa sababu

*decision* zingine za *investment* zinahitaji *endorsement* ya bodi. Sasa bodi hamna tunashangaa kwa nini uteuzi haufanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Juma Hija wameongelea mambo ya madeni makubwa ambayo Serikali inadaiwa. Kwa hiyo, tunawakumbusha, kwenye ripoti yetu tuko *so clear* kwamba Serikali iweze kuanza kuchukua hatua za kuyalipa madeni hayo kwa mpangilio ambao inaona inaweza kuanza kuyalipa. Madeni yamekuwa makubwa, yanafanya makampuni, mashirika na taasisi zetu zishindwe kujiendesha na ku-*meet target* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mashirika ya umma ya Serikali ambayo ni wakandarasi lakini Sheria ya Manunuzi iliyopo inawaona kama ni mashirika au taasisi wanaonunua lakini kumbe ni wakandarasi. Tunayo *TBA*, *DDCA*, JKT, haya yote ni makampuni makandarasi, lakini kulingana na Sheria ya Manunuzi wanaonekana kama ni wanunuzi. Kwa hiyo, tunaomba kupitia Ofisi ya *TR* iweze kuandaa mapendekezo mazuri ambayo yataendana na mashirika haya kwani yanakosa biashara nyingi kwa sababu sheria inawabana na shughuli zinakuwa za muda mfupi. Kwa hiyo, Kamati bado inasisitiza hilo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mashirika au kampuni ambazo hazijamtambua Msajili wa Hazina. Hapa ni msisitizo kwamba kupitia Ofisi ya *TR* basi aweze kuzikumbusha kwa sababu sheria zilizoanzisha mashirika haya nyingine ni za muda mrefu na *TR* ameanza kupewa uwezo muda siyo mrefu. Kwa hiyo, tungependa zile sheria ziweze kuwa *reviewed* iweze kuwekwa *addendum* ya sheria nyingine ili iweze kuzitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wito wetu kwa Wizara ya Fedha kwani haitendi haki kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kwanza hawana *manpower*, hawana watu wengi wenye weledi wa kuweza kuchambua mambo yote yaliyopo kwenye uwekezaji wa mitaji ya umma. Tuisihi Wizara ya Fedha iweze ku-*empower* Ofisi hii na iweze kuipa bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Ofisi ya *TR* ilitakiwa iwe imetupa ripoti ya mwaka na hiyo ripoti ingeweza kuletwa kwa Waziri wa Fedha ambaye angeileta Bungeni na baadaye Kamati kupewa, lakini sasa ni miaka miwili na nusu hatujapokea ripoti hii. Sasa tunaiomba Wizara ya Fedha iweze kuijali na kuipa kipaumbele Ofisi ya *TR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine makubwa yaliyoongelewa ni madeni, mambo ya ndege, Bodi za Wakurugenzi tumeiongelea, iko kwenye ripoti yetu, Sheria ya Manunuzi tumeisema iko *so clear* na iko kwenye ripoti yetu. Kwa hiyo, nawashukuru hawa walioboresha ripoti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rhoda Kunchela amezungumzia Serikali kutolipa madeni kwa wakati, ni kweli, yako mashirika madeni ya *DAWASCO, DUWASA* na umeme. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo yanaweza yakazungumzwa ndani ya Serikali na tukaondokana na hizi *embarrassment*. Wananchi wanakatiwa huduma za maji kwenye visima, wanakuta kuna mgogoro Serikali haijalipa umeme, ni mambo ambayo mnaweza mkayaongelea ndani ya Serikali ili wananchi wasiweze kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Janet Mbene ameongelea mashirika yaendeshwe kibiashara, ni kweli na sisi tunasisitiza hilo na ndiyo maana ya kuanzisha Kamati hii ili iweze kuangalia mujarabu wa biashara kwenye mashirika haya. Kuhusu vigezo vya *appointment,* kuona mtu mwenye uwezo wa kuongoza shirika, nafikiri hilo nalo liendelee kuzingatiwa kama ulivyolitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengine ni ya jumla ambayo kwa kweli tunashukuru kwamba yameweza kuboreshwa, mengine wote walikuwa wanarudia karibu maeneo yaleyale. Kitu muhimu tunachosisitiza kama Mitaji ya Umma tunaomba mapendekezo tuliyoyatoa kwenye ripoti yetu Bunge iyaazimie, iyachukue na yawe ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liweze kukubali

mapendekezo yetu na hoja zetu ambazo zimetolewa ndani ya ripoti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, naomba kutoa hoja.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017 iliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uwasilishaji wa taarifa yetu ya tatu, Mwenyekiti ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa Murad.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niwashukuru sana wachangiaji wote waliochangia hoja hii, wale ambao wamechangia kwa maandishi na wale ambao wamechangia kwa kuzungumza Bungeni. Waliochangia kwa kuzungumza Bungeni ni wanane na naomba kwa haraka haraka niwatambue, Mheshimiwa Lulida, Mheshimiwa Kamala, Mheshimiwa Jitu, Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao wamechangia kwa maandishi ni 11, naomba nao niwatambue; Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Zainabu Amiri, Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mheshimiwa Suzana Chogisasi na Mheshimiwa Juma Othman Hija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua niwatambue hawa kwa sababu wengi wamezungumza hoja ambazo zinafananafanana, wale ambao wameleta kwa maandishi na wale ambao wamezungumza hapa Bungeni. Pia naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa ufafanuzi wa hoja mbalimbali. Naomba niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri January Makamba, Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Dkt. Mpango, nawashukuru sana kwa ufafanuzi wa hoja mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi ambazo zimezungumzwa ziko katika maeneo tofauti tofauti. Kuna hoja ambayo imezungumzwa sana na Wabunge wengi ni kuhusu Mamlaka nyingi za Udhibiti. Wabunge wametoa michango yao, wametoa ushauri wao lakini na sisi kama Kamati tulishayaeleza haya na ni matumaini yetu kwamba Serikali itayafanyia kazi haya masuala ili kupunguza utitiri huu wa mamlaka na kuleta utaratibu mzuri wa uzalishaji katika viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezitaja zile mamlaka zote ambazo zinaingiliana katika usimamizi wa viwanda, mfano *OSHA, NEMC, TFDA, TBS* na wengine wengi. Kwa hiyo, ni hoja ambazo zimekuja lakini na sisi kama Kamati tulishapendekeza nini kifanyike, ni matumaini yetu Serikali itakuwa imepokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala lingine la ubinafsishaji wa viwanda. Katika hotuba yangu ukurasa wa 33 na 63 tumelizungumza kwa kina. Viwanda ambavyo taarifa tumeletewa kwenye Kamati viko 156 vimebinafsishwa

na Serikali inaendelea kuvifanyia kazi vile viwanda lakini Wabunge wameeleza kwa masikitiko makubwa na wengine wamediriki kusema kwamba hatua kali zichukuliwe kwa wale ambao wamepewa viwanda vile lakini havizalishi, Serikali imekosa mapato kwa kipindi chote cha miaka ambayo viwanda vile vimebinafsishwa. Viwanda vingi vimebinafsishwa kati ya mwaka 1997, 1998, 1999 mpaka 2000, utaona ni miaka mingi sasa Serikali imepoteza mapato mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili wapo Wabunge wamesema kwamba hatua ambazo zitachukuliwa ni pamoja na kulipa kodi kwa miaka yote ambayo viwanda vile havikufanya kazi. Wapo Wabunge wameshauri kwamba lipo suala la viwanda hivi vilivyobinafsishwa, wawekezaji wale wamechukua hati wamezipeleka benki, wamekopa na matokeo yake hati zile zimekaa benki lakini viwanda vile havikupata fedha zile, fedha zimeingia kwenye biashara zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo Kamati ilishayapendekeza, ni matumaini yangu kwamba Serikali itayafanyia kazi. Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba hili jambo lipo katika hatua za utekelezaji, Kamati inasisitiza utekelezaji ufanyike kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la Mradi wa Kurasini *(Kurasini Business Park),* Kamati imezungumza muda mrefu na Mheshimiwa Waziri amelijibu. Ni matumaini yetu kwamba jambo hili sasa litashughulikiwa kwa uharaka mkubwa ili eneo lile sasa lianze kuzalisha Watanzania wapate ajira, Serikali ipate mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni suala la Kiwanda cha *General Tyre. General Tyre* ya Arusha Kamati tumeizungumza sana, tumetoa ushauri wetu, Serikali imesikia na leo hoja hii imejibiwa ni matumaini sasa msukumo mkubwa utaanza. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, katika hili la

*General Tyre* na yeye aweke mkono wake kwani Wizara ya Viwanda peke yake hawataweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha suala la *General Tyre* liwe ni suala la umoja wote Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Wizara nyingine tushirikiane. Zipo hatua ambazo zimechukuliwa na tunaomba Serikali iandae mazingira rafiki ya uwekezaji katika *General Tyre*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la bidhaa feki za pombe na *sticker fake*, hili limepokelewa na Kamati yetu na Serikali itakuwa imelisikia, imelipokea litafanyiwa kazi. Eneo hili linapoteza sana mapato. Bidhaa feki kwanza zinaharibu afya za Watanzania, lakini pia Serikali inakosa mapato. Hili limechukuliwa na litafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo suala la *TBS* na *TFDA,* Wabunge wamelizungumza sana. Naomba niseme kwa kifupi sana, *TBS* wao kazi yao ni bidhaa za viwandani, *TFDA* wao kazi yao ni bidhaa ambazo zinakwenda moja kwa moja kwenye madawa na vyakula. Kwa hiyo, pale kuna utaratibu tofauti kabisa, sasa wanapoingiliana wale hatujui ni kwa nini wanaingiliana. Kila mmoja ana eneo lake, kuna bidhaa za madawa na bidhaa za chakula na yule ana bidhaa za viwandani. Tunaomba Mamlaka hizi zipewe eneo la mipaka ya kazi ili kupunguza urasimu ambao wafanyabiashara wanaulalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilipongeze suala la umeme. Leo asubuhi tumezungumza kwamba Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Morogoro walikuwa wana *ration* ya umeme, wanaambiwa viwanda vizalishe usiku na mchana wasizalishe. Kwa taarifa niliyoipata leo kupitia kwa Waziri kwamba lile zoezi lilikuwa ni la muda, ukarabati umeshafanyika, sasa hivi viwanda vinazalisha usiku na mchana. Hili nalipongeza sana Serikali na Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Wakala wa Vipimo, Wabunge wameshauri Wakala huyu ashuke chini ili mazao ambayo yanakwenda sokoni wale wakulima na wazalishaji wapate haki yao ya vipimo. Vipimo viende sambamba na uzalishaji. Tunaiomba Serikali ilifanyie kazi hili na Wakala huyu aongeze nguvu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala limezungumzwa la utitiri wa kodi. Suala hili nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Kamati yetu kupitia *CTI* ambayo walikuja wametuletea orodha ndefu ya utitiri wa kodi. Kodi nyingine zinarudiarudia, wafanyabiashara wanapata shida na wakati mwingine wanapata matatizo jinsi ya kulipa zile kodi. Tunaomba Serikali ilifikirie jambo hili na wafike mahali waanze kukaa na Kamati ya Bajeti, Kamati ya Viwanda na Kamati zingine ili walifanyie kazi kwa ndani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la mifuko ya plastiki, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri January Makamba amelisemea vizuri na Kamati imependekeza lazima tufike mahali sasa mifuko ya plastiki iwe basi. Kamati katika eneo hili imependekeza Wizara itafute namna nyingine, tupate viwanda mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zingine zinazobebwa zinahitaji mifuko, kwa hiyo, Wizara iharakishe kutafuta viwanda mbadala au wenye viwanda hivyo ambavyo wapo wapewe teknolojia ambayo itawasaidia kuzalisha mifuko mbadala ikiwemo mifuko ya karatasi, nguo, majani na mifuko mingine ili tunapoondoa mifuko tuweke mifuko mbadala. Kamati imependekeza hilo, ni matumaini yetu Wizara imesikia na Wizara ya Viwanda nao watakuwa wamelisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunapenda sana kuliunga mkono ni suala la uchafuzi wa mazingira. Kuna viwanda kwa makusudi wanachafua mazingira kwa kutumia Tanzania ya Viwanda. Hii dhana hii wanaitumia vibaya. Tunaomba Wizara hii, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira

kazeni buti wale wanaochafua mazingira sheria ichukue mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi na sisi tunasema tumeyapokea kama Kamati lakini Kamati nayo asubuhi wakati tunawasilisha taarifa yetu tulitoa maoni na mapendekezo yetu. Naomba Waheshimiwa Wabunge mapendekezo yetu yale tutayachukua pamoja na ya kwenu mliyotuletea leo kwa maandishi pamoja na kwa kuzungumza tutayachanganya pamoja ili tuyapeleke katika taasisi zinazohusika yafanyiwe kazi kwa faida ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kuchelewesha muda, naomba sasa nikushukuru wewe, niwashukuru Mawaziri wote waliochangia, lakini pia niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu kwa jinsi ambavyo tumekwenda pamoja katika suala hili. Maoni yetu ya mwisho na maazimio yetu, wawekezaji wawe wakweli kwa Taifa lao. Wawekezaji watoe taarifa sahihi Serikali iweze kuwasaidia na walipe kodi Serikali iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tunawashauri wawekezaji wawe wakweli kwa Serikali, watoe taarifa sahihi na sisi kama Kamati tutawalinda na tutawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ombi letu la pili tunaomba Watanzania wapende bidhaa za Tanzania. Unapopenda bidhaa za Tanzania, unaunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania ya Viwanda lakini tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu. Kwa hiyo, tunaomba Watanzania wapende bidhaa za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba Serikali iendelee kuboresha mazingira mazuri kwa wafanyabiashara, mazingira rafiki kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nihitimishe hoja yangu kwa kuwaahidi kwamba

Kamati yetu imeyapokea masuala mbalimbali na yale ambayo tumeyatoa asubuhi pamoja na haya ya jioni ya leo tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja, mapendekezo yote ya Kamati yapokelewe na yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono na Wabunge zaidi ya 10. Sasa nitaitoa muiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 Iliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kama yalivyowasilishwa mbele ya Bunge hili yamekubaliwa rasmi na hapo ndiyo tunafika mwisho wa shughuli zetu hizi.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Tulia tu Mheshimiwa. Kabla sijafika huko nilikuwa na ombi la mwongozo ambao ndiyo mwenzangu ameanza, tuna muda kidogo. Karibu Mheshimiwa Kangi Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Kijaji anachangia hoja ya Kamati, Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani walikuwa wanapiga makelele ambayo kwa kiwango chake, wewe Kiti baada ya kuona yamezidi ulilazimika kusimama na kutuliza hali hiyo. Pia Mheshimiwa January Makamba alipotaka kuanza kuzungumza hali hiyo iliendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kupiga makelele, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya mwaka 2004, kifungu namba 106(5) ambacho naomba ruhusa yako nikisome, kinasema:-

*"Si ruhusa kwa mtu yeyote kupiga kelele au kusababisha kupiga kelele kuzidi kiwango kilichoainishwa au kitakachobainishwa kuhusiana na upigaji kelele". (Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upigaji wa kelele ni sehemu ya uchafuzi wa mazingira chini ya sheria hii na kwa kuwa uchafuzi huu wa mazingira umefanyika mbele yangu ambaye nina dhamana ya kusimamia mazingira yasichafuliwe kwa namna yoyote na kwa kuwa ukikiuka kifungu hiki lazima unapigwa faini, naomba mwongozo wako katika mazingira haya ambapo makelele haya ambayo yametokea humu Bungeni na ambayo si sehemu ya uhuru wa mawazo kwa mujibu wa Ibara ya 100 ya Katiba, kwa nini usiwe unaandaa orodha ya wale ambao wanachafua mazingira kwa kukiuka kifungu hiki ili baadaye tuwatoze faini kwa ajili ya kutunisha dhamana ya Mfuko wa Mazingira ambayo ilikuwa inalalamikiwa hapa kwamba hatuna fedha ili chanzo cha fedha hizo kianzie kwa Wabunge hawa ambao wanapiga makelele. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kangi Lugola, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Nadhani lazima tuwe na *light touch* lakini nimeombwa mwongozo. Yeye ni Naibu Waziri ndiyo lakini Kanuni ya 68 yote iwe ni kwa utaratibu, taarifa au mwongozo ni *neutral,* inaongelea Mbunge na Waziri ni Mbunge.

Ukikiuka Kanuni na Naibu Waziri au Waziri anaona Kanuni imekiukwa na Mbunge mwingine hawezi akakaa tu eti kwa sababu yeye ni Waziri amwachie Mbunge mwingine aseme, hapana. Hivyo ndivyo ilivyo niwaambie Waheshimiwa, Kanuni ya 68 ni utaratibu ambao tunapaswa kuuzingatia *regardless whether* umepewa wadhifa mwingine, kwa hiyo tulielewe hilo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa yeye kaomba *specifically* kwa hilo, tumefanya kazi nzuri kwa leo, mimi nadhani hili linaeleweka kwa sababu sisi tunasimamia Kanuni hizi, yeye naye amekabidhiwa kusimamia ile sheria ile katika maeneo husika kuwashughulikia wale ambao wanayafanya yale. Humu ndani mniache mimi nihangaike nao kwa mujibu wa Kanuni na ndiyo maana nilisimama na nashukuru wote waliitikia maelekezo ya Kiti. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumesemea sana suala la muda na nilianza nalo kujaribu kusaidia, kwa binadamu hakuna kitu ambacho kinakuwa *perfect*. Mimi nilisema tungeenda kwa dakika 15 tungeishia na wachangiaji sita tu. Tukajaribu hata 10, wamecheza sana wataalam hapa wakasema tuje na dakika saba. Naelewa siyo muda mwingi lakini angalieni mliochangia mmejielekeza kwenye hoja na nadhani tuendelee kujifunza hivyo. Haya mambwembwe na kuzunguka kwenda Bariadi na kurudi na nini muda kama unajua hautoshi usiende huko*, be specific* na mmefanya vizuri tu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja ninayoiona, nadhani tulione hili, tulichukue maana sote ni viongozi. Kipindi hiki

ndiyo tunaisimamia tena Serikali yetu kupitia taarifa za Kamati katika kila sekta. Najua tatizo la muda siyo la Tanzania tu, changamoto kubwa ya dunia ni muda, sasa ni *how* tunavyotumia muda huu. Kwa mujibu wa Kanuni hizi Mkutano huu wa Bunge hazisemi kwamba zitakuwa ni shughuli za Kamati tu, *no*, Serikali na yenyewe ina shughuli na ndiyo maana tulianza na Miswada ile ya Serikali. Tuna maswali, mmeuliza maswali, mmejibiwa na mtaendelea kuuliza na mtajibiwa na Serikali. Sasa tuone, je, huko mbele tunaweza tukaboresha kivipi ili kuongeza muda kidogo ili Wabunge wengi wachangie hoja hizi. Hiyo ndiyo hoja yangu nimeliona hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilijaribu leo hapa ku-*manage* muda tu ili tuweze kwenda vizuri, imetulazimu kuingia katika nusu saa ambayo ndiyo tunaitumia sasa, Wenyeviti wametumia muda huo vizuri *otherwise* kama tungechelewa na hoja ya Mheshimiwa Mdee ingebidi tuombe itolewe hoja kutengua Kanuni tuendelee mpaka tutakapomaliza. Yote haya ni maamuzi ya Bunge.

Hata hivyo, naamini taarifa hizi ni nzuri, Bunge limeridhia maazimio haya, kwa taratibu zilizopo yatapelekwa Serikalini na Serikali itayafanyia kazi tuwe sasa na *platform* ya kujua haya yaliyowasilishwa yametekelezwa vipi. Maana haiwezekani tukawa na *platform* ya kuja kuongea tu tunamalizana, tunashikana mikono tunaondoka, hapana! Lazima utekelezaji uonekane na watatoa taarifa. Nadhani hilo limekaa vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nina tangazo. Nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Wabunge wote wanaotoka Mikoa ya Pwani, Morogoro na Iringa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 3 Februari, 2018 yaani kesho kuanzia saa 8.00 mchana katika Ukumbi wa Hazina kutakuwa na semina kuhusu Mradi wa Kufua Umeme wa Rufiji wa *Stieglers Gorge* pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta

Ghafi la Afrika Mashariki *(East African Crude Oil Pipeline - EACOP)*.

Semina hii imeandaliwa na Wizara ya Nishati ili kuwajengea uelewa wa miradi hiyo Wajumbe wa Kamati hiyo. Mnaombwa wahusika wote kuhudhuria bila kukosa. Hilo ndiyo tangazo nililoletewa.

Waheshimiwa Wabunge, nirudie tu kwa kukumbushana yale niliyosema mchana, tangazo la semina ya *compensation* ya wafanyakazi ambayo itaanza saa 4.00 kamili katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Tuhudhurie kwa wingi ni semina muhimu sana, itatupa uelewa mzuri wa masuala haya na naamini Mwenyezi Mungu atatujalia tuamke wote salama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.07 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 5 Februari, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*